

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 23 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza kikao cha leo ningependa kutoa maelezo yafuatayo kwa wananchi wanaosikiliza mijadala ya Bunge.

Nataka waelewe kwamba, kila hoja inayowasilishwa hapa Bungeni, imetengewa muda maalum wa kujadiliwa. Kwa mfano, hivi sasa tunajadili hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hoja hii ilitengewa siku tatu na leo ndiyo siku ya mwisho, ambapo mijadala wa hoja hiyo lazima umalizike. Kutokana na utaratibu huo basi wa kutenga muda maalum kwa kila hoja, haiwezekani kwa kila Mbunge anayependa kuchangia mawazo yake, apate nafasi ya kufanya hivyo, inabidi baadhi yao wakose nafasi. Kwa hiyo, mpiga kura anayehusika asipomsikia Mbunge wake katika redio akichangia mawazo yake asifikiri kwamba Mbunge huyo hana mchango wa kutoa hapana, inawezekana tu kwamba amekosa nafasi ndiyo sababu tumeweka kanuni nyingine inayowawezesha Waheshimiwa Wabunge, kuchangia mawazo yao kwa maandishi na kuyawasilisha kwa Mheshimiwa Waziri anayehusika ili yakafanyiwe kazi.

Nimeona nitoe maelezo haya ili baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wanaokosa nafasi ya kuchangia kwa mdomo wasilaulumiwe kwamba wamekuwa bubu wakati kumbe wamekosa nafasi kwa mujibu wa taratibu za Bunge. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 99

**Miradi ya TASAF**

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa miradi ya *TASAF* inacheleweshwa sana kuanzishwa na kumalizika kama ilivyopangwa:-

(a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha hali hiyo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tatizo hilo la ucheleweshwaji?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA - MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi kwa maelezo yako mazuri ulistahili kura zetu, ninakupongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Miradi ambayo Mheshimiwa Mbunge, ameiita kuwa miradi ya *TASAF* ni ile miradi ya wananchi ambayo huibuliwa kutokana na upembuzi shirikishi jamii na kutekelezwa na wananchi wenyewe. Kwa miradi ya jamii *TASAF* huwawezesha wananchi kwa kuwachangia asilimia 20. Miradi hii imepangwa kutekelezwa katika kipindi cha miezi 12. Katika kutekeleza miradi ya *TASAF*, wananchi hupata nafasi ya kujifunza na kuwa na uzoefu wa kuibua, kupanga, kusimamia na kutekeleza miradi ya maendeleo yao kwa namna ambayo ni endelevu. Kwa miradi ya ujenzi yaani ya kujinusuwa wananchi ambao ni maskini zaidi kuliko wananchi wenzao katika jamii husika, hupewa ajira ya muda mfupi ili kuwavusha katika kipindi ambacho ni kigumu zaidi katika mwaka. Miradi hii imepangwa kukamilika katika kipindi cha miezi minne hadi miezi minane.

Baada ya maelezo haya napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mbunge wa Kiwani, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kasi ya utekelezaji wa miradi ya *TASAF* hutegemea wepesi wa utendaji wa wadau wote husika, yaani wananchi wenyewe, wataalam Wilayani, *TASAF* Makao Makuu na Benki ya Dunia. Kwa upande wa miradi ya Pemba, kinachoitwa ucheleweshaji ni ule muda ambao unatumika kuandaa miradi yenyewe na kupitisha katika vikao husika. Hatua hizi ni za muhimu na lazima zifuatwe.

(b) Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali haipendi kuchelewesha miradi ya wananchi. Pale inapoonekana kuwa na ucheleweshaji, Serikali huchukua hatua za kuchunguza tatizo ili kubaini chanzo na hivyo kuchukua hatua zinazofaa. (*Makofi*)

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Waziri napenda kumwuliza swali moja kama ifuatavyo: Baada ya wananchi kuibua miradi na *TASAF* kuweka mkono wake (*support*), je, Serikali haioni kuwa inawavunja moyo wananchi kwa kutekeleza kwa kusuasua mradi huo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLO - MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji ya miradi ya *TASAF*, kuna mambo mengi tumejifunza na ndiyo maana wiki iliyopita kulikuwa na mkutano mkubwa wa wadau wote wanaohusika na *TASAF* kujifunza matatizo yaliyojitokeza katika awamu ya kwanza ili tunapoingia awamu ya pili mwaka 2005 yasirudiwe, hii ni pamoja na ucheleweshaji ambao unasababisha miradi hiyo kusuasua. Jambo hilo tutalirekebisha na kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba, wakati mwingine ni suala la utaratibu tu lakini nina imani kwamba tutakuwa tumesahihisha matatizo ambayo yamejitokeza huko nyuma. (*Makofi*)

**MHE. KHADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza swali dogo kama ifuatavyo: Kwa kuwa *TASAF* imefanya vizuri katika Wilaya ambazo zilipewa kama majaribio ikiwemo Wilaya ya Temeke na imefanya vizuri sana; na kwa kuwa ilijitokeza katika utekelezaji wa miradi hii kuwa kuna ugumu wa kuibua miradi na hasa ukizingatia masharti yaliyowekwa ni kwamba kuwe na wahusika wengi wa kubuni hiyo miradi, lakini kule vijijini kunakuwa na matatizo ya mahudhurio katika mikutano; je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa wa kupunguza masharti hayo ili watu waweze kubuni miradi mingi na kuitekeleza kwa wakati uliopangwa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, misingi ya miradi hii shirikishi, miradi ya *TASAF*, ni kuwawezesha wananchi wenyewe kuona ni mradi gani ni kero kwao na hivyo kufanya washiriki katika kuhakikisha kwamba wanaiibua. Kwa kufanya hivyo maana yake ni sehemu wanajitolea, watahiriki kwa sababu wameanzisha wenyewe. Kitendo cha kusema tupunguze utaratibu huo wa ushirikishwaji katika kuibua kutafanya sasa miradi ibuniwe na viongozi, jambo ambalo halitakuwa zuri na hasa kama tulivyojifunza kwenye uzoefu uliojitokeza. Kwa hiyo, safari ijayo katika awamu ya pili, miradi itaenda zaidi kijijini na kuhamasisha wananchi wajue uzuri wa kuibua miradi yao na kuitekeleza kama ilivyofanyika huko nyuma. Tutazingatia pia ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Khadija Kusaga, pamoja na ule wa Mheshimiwa Zuhura Khamis Abdallah.

Na. 100

### **Kufungua Ofisi za Mkemia Mkuu Ki-Kanda**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua Ofisi za Mkemia Mkuu wa Serikali Ki-Kanda ili kurahisisha utendaji kazi wa kitengo hicho ambacho ni muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul N. Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, ili kurahisha kazi za Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kuna umuhimu wa kufungua ofisi zake kikanda. Kwa kuzingatia ukweli huo, Wizara yangu imeanza mpango wa kuanzisha Maabara za Kanda kwa kuanzia na Kanda ya Ziwa. Katika hilo, Wizara yangu tayari imeshapata kiwanja Mwanza chenye namba ya usajili 183271, Hati Miliki 13,774 kilichopo *Block A* Kiwanja Na. 107 na 109 katika maeneo ya Nyamhongolo. Kiwanja hicho kina ukubwa wa eneo la mraba wa mita 7.077. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na kupata kiwanja hicho, Wizara yangu imepata jengo lililokuwa karakana ya *HESAWA* katika Hospitali ya Mkoa wa Mwanza ambalo lilikuwa halitumiki. Jengo hilo limefanyiwa matengenezo ili litumike kama Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Kanda ya Ziwa wakati fedha za kujenga maabara huko Nyamhongolo zinatafutwa. Hivi sasa kazi ya ukarabati imekamilika na tupo katika maandalizi ya awali ya kufunga mitambo tayari kwa kuanza kazi. *(Makofi)*

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja kama ifuatavyo: Kwa kuwa kikwazo kikubwa cha ujenzi wa ofisi hizi za mkemia kwenye kanda ni fedha. Je, Serikali itakuwa tayari kukaribisha wakala ambao wanaweza wakaanzisha maabara kwenye mikoa na kanda ili kusaidiana na juhudi hizo za Mkemia Mkuu wa Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba, fedha hizo tayari zimeanza kupatikana kwa hiyo, hatuna mashaka kwamba tutashindwa kuanzisha maabara katika kanda zetu. Kama nilivyosema pale Mwanza tayari ile Karakana ya *HESAWA* imeshabadilishwa kuwa maabara na tutaendelea na kanda nyingine. Aidha, ofisi hii ya Mkemia Mkuu wa Serikali sasa hivi ni *executive agency* kwa maana inapata malipo kutokana na huduma wanazozitoa. Kwa hiyo, bila shaka hilo litasaidia katika kujenga uwezo wa ofisi hii kusambaza maabara. Kuhusu suala la wakala binafsi, bado uamuzi wa jambo hilo haujatolewa na sababu za msingi ni kwamba, kwa kiwango kikubwa, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pia huangalia kesi za jinai. Kwa hiyo, ni vema jambo hili libaki katika mikono ya Serikali.

Na. 101

### **Ujenzi wa Barabara za Mpakani**

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake iliyoitoa Bungeni katika Mkutano wake wa Kumi na Tatu Novemba, 2003 ya kuziimarisha barabara zote za mipakani kwa misingi ya Ulinzi na Usalama wa Taifa ikiwemo ujenzi wa Daraja la Mto Kahambwe?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Beatus Ruzuba Magayane, Mbunge wa Buyungu, kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda kufafanua kuwa Serikali ilichosema katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge ni kwamba, Serikali inao mkakati wa kuangalia ni kwa jinsi gani itashughulikia barabara za mipakani kutokana na umuhimu wake. Napenda pia nitoe ufafanuzi wa kwamba, barabara zote zipo katika madaraja (*classifications*) ya Barabara Kuu, Barabara za Mkoa, Barabara za Wilaya. Hivyo, uimarishwaji wa barabara zierendazo mipakani na matengenezo ya barabara hizo hufanywa chini ya uangalizi wa wakala wa barabara (*TANROADS*). Halmashauri za Wilaya huhudumia zile zilizo chini ya Wilaya. Matengenezo haya hufanyika kulingana na upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini na husimamiwa na Wizara husika. Aidha, Mto Kahambwe unakatisha Barabara ya Kibondo - Mabamba mpakani na Burundi ambayo ni barabara ya Mkoa iliyo chini ya uangalizi wa *TANROADS*. Mto huo pia hukatiza Barabara ya Nyange - Mabamba ambayo iko chini ya uangalizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo.

Mheshimiwa Spika, kwenye Barabara ya Mkoa, ambako mto huo umepita, daraja la chuma na zege (*Composite Bridge*) lenye upana wa mita 12.4 lilijengwa na *UNHCR* chini ya usimamizi wa *TANROADS* Mkoa wa Kigoma kuanzia tarehe 24 Oktoba, 2001 na kukamilika 26 Januari, 2002. Gharama ya ujenzi wa daraja hili ilikuwa shilingi 39.18 milioni. Daraja hili lipo na linaendelea kutumika kwa magari yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya Daraja la Mto Kahambwe katika barabara ya Wilaya ya Nyange - Mabamba na hali ya barabara hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge, apate maelezo kutoka kwenye Halmashauri husika kwa sababu barabara hii ni ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika kuiimarisha Barabara ya Kibondo - Mabamba iendayo mpakani mwa Burundi, matengenezo yafuatayo yamefanyika na mengine bado yanaendelea yanafanyika:-

(i) Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, matengenezo ya sehemu korofi ya km.5 kati ya Bonde la Luguzye na Mabamba yaliharimu shilingi 47.936 milioni;

(ii) Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, ujenzi wa madaraja mawili kwenye Bonde la Luguzye uliharimu jumla ya shilingi 31.546 milioni;

(iii) Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, ujenzi wa madaraja mawili kwenye Bonde la Luguzye uliharimu jumla ya shilingi 31.546 milioni; na

(iv) Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 matengenezo ya kawaida yatakayoharimu shilingi 12.197 milioni yanaendelea na matengenezo ya sehemu korofi ya km. 4.4 yatakayoharimu shilingi 41.152 milioni pia yanaendelea.

Matengenezo haya yamefanyika kwa kutumia bajeti ya Serikali kwa upande wa Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Wilaya ya Kibondo asilimia 70 ni hifadhi ya misitu na asilimia 17 ni maeneo chepechepe (*wetlands*), ambayo husababisha mgao wa Serikali Kuu kwenda kuhudumia *network* za barabara ambazo ni ndogo kuwa kidogo. Je, Serikali haioni kwamba ni vyema ikahudumia zaidi hizo barabara zinazoelekea mipakani ili kuongeza kiwango cha huduma kwa Wilaya ya Kibondo? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa vijiji vya mipakani katika Jimbo la Buyungu, vijiji kama vya Bukililo, Malenga na Kiga, mara nyingi hushambuliwa na majeshi ya kutoka Burundi na kwa kuwa ili Serikali iweze kutoa msaada inabidi kuzunguka kupita Kakonko kuja mpaka Kasuga badala ya kwenda moja kwa moja kutoka Bukililo kwenda Malenga na Kiga. Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara ya kutoka Bukililo, Malenga na Kiga ili iwe rahisi kutoa msaada wakati kunapotokea mashambulizi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Kibondo asilimia 87 ipo katika misitu na chepechepe kwa hiyo basi mgawanyo haulingani na Wilaya zingine, hili kwa kweli sina uhakika nalo. Nililokuwa na uhakika nalo ni kwamba, barabara za *TANROAD* katika Wilaya ile sisi tunazishughulikia kufuatana na makubaliano ya sheria ambayo ilipitishwa hapa mwaka 1967, barabara zipi zitakuwa za *TANROAD*, zipi zitakuwa za Wilaya na zipi zitakuwa *TRUNK ROAD*. Kwa sababu ni maliasili nina hakika Wilaya hii inapata asilimia 25 ya mavuno ya maliasili na kama haipati fuatilia Wizara ya Maliasili. Hiyo, wanaweza kuwekeza katika utengenezaji wa barabara zao.

Pia ameuliza kwamba vijiji vya mpakani hushambuliwa na majeshi kutoka nchi jirani na kwa hiyo barabara ya Bukililo, Malenga na Kiga ni muhimu kutengenezwa, hili nimelipokea na nitaangalia katika undani wake tuone kama barabara hii ni ya *TANROAD* ama ya Wilaya na tutashauriana na Wilaya kama ni yao. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maelezo ya nyongeza kutokana na swali la nyongeza la Mheshimiwa Beatus Magayane kama ifuatavyo: Majeshi ya Burudi hayajaivamia Tanzania. Hakuna jeshi lolote ama nchi yoyote itakayothubutu kuivamia Tanzania. Kama kwa bahati mbaya wanajeshi kutoka nchi jirani wameingia Tanzania, kwa bahati mbaya, mara nyingi tunawashika, tunachukua silaha, tunawauliza kwa sababu gani wameingia Tanzania na kama ni kwa sababu ya uchochezi wanashughulikiwa ipasavyo. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 102

**Barabara ya Galula - Namkukwe**

**MHE. PAUL E. Ntwina** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Galula hadi Namkukwe ni ya Mkoa na ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi na kwa kuwa nimekuwa naulizia maswali kuhusu barabara hiyo na majibu yake yamekuwa hayaridhishi:-

(a) Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha kokoto utaanza?

(b) Je, kwa kutotengenezwa barabara hiyo Serikali haioni kwamba haiwatendei haki wananchi wanaoitumia barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Paul E. Ntwina, Mbunge wa Songwe, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Barabara ya Galula - Namkukwe, yenye urefu wa kilometa 57 inanzia katika Kijiji cha Galula katika barabara ya Mbalizi - Mkwajuni, umbali wa kilometa 60 kutoka Mbalizi. Barabara hiyo inapita katika Vijiji vya Galula, Ilembo, Magamba, Malangali, Muheza na Namkukwe. Kihistoria barabara hii ilikuwa ni ya Halmashauri ya Wilaya, lakini katika mradi wa matengenezo ya barabara za Mkoa wa Mbeya, chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Norway (*NORAD*) uliotekelezwa kuanzia mwaka 1983 hadi mwaka 1985, barabara hii iliingizwa katika mtandao wa barabara za Mkoa ili iweze kufanyiwa ukarabati kwa msaada wa *NORAD*. Bahati mbaya kutokana na uhaba wa fedha, hadi mradi ulipokamilika barabara hii ilikuwa haijafanyiwa matengenezo yaliyokusudiwa.

Barabara hiyo iko kwenye bonde la Ziwa Rukwa na hufurika maji wakati wa masika. Barabara hiyo pia ina umbo la barabara katika kipande cha kilometa SITA tu za mwanzo kutoka Galula na baada ya hapo hakuna sura ya barabara iliyo wazi. Barabara hiyo inahitaji kutafutiwa *alignment* muafaka ambayo itapunguza athari za mafuriko.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul E. Ntwina, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Galula - Namkukwe imetengenezwa kwa kiwango cha changarawe (kokoto) kipande cha kilometa sita kutoka Galula hadi Ilembo. Kipande cha barabara kutoka Ilembo hadi Namkukwe, kinahitajika kufanyiwa upembuzi yakinifu utakaoainisha sehemu za kupita barabara (*Road Alignment*) na hatimaye kufanyika usanifu na ujenzi ama ukarabati wa barabara hiyo. Serikali inaendelea na jitihada zake za kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na ukarabati wa barabara hii. Aidha, barabara ya Galula - Namkukwe pamoja na barabara zingine nchini zitaendelea kufanyiwa matengenezo kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara (*Road Fund*), kulingana na upatikanaji wa fedha. Si nia ya Serikali

kutotengeneza barabara yeyote, bali tatizo ni upatikanaji wa fedha za kutosha kuzifanyia matengenezo yanayotakiwa barabara zote kwa wakati mmoja.

**MHE. PAUL E. Ntwina:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Waziri anakiri kuwa barabara ya Galula na Namkukwe na barabara nyingine nchini hazijapata *road funds* za kuweza kutengenezwa. Lakini hii barabara nimekuwa nikiiongelea kila mara hapa, je, haoni kuwa hizi barabara zinazosemwa na Wabunge mara kwa mara zingetiliwa mkazo hasa kwa kuwa tunakopa hela sasa hivi? (*Makofi*)

(b) Kwa kutengeneza hii barabara ingedumisha sana uzalishaji wa ufuta na mahindi ambayo yanazalishwa kule kwa wingi na kwa kuwa yeye mwenyewe amekiri kuwa haijatengenezwa sasa nashangaa jibu la pili anasema kuwa imewekewa changarawe wakati hakuna changarawe. Je, atakubaliani na mimi kwamba, Waziri mwenyewe au Naibu Waziri watembelee na kuiona ile barabara ili majibu haya yasiwe ya kubabaisha? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paul Ntwina, amekuwa akiizungumzia barabara hii mara nyingi sana karibu kila tukikutana atazungumza juu ya barabara hii. Naelewa umuhimu wake kwake sasa hivi. Lakini vile vile Mheshimiwa Mbunge akubali kwamba, tunajitahidi kwa dhati kabisa kupanga fedha kwa uwezo wetu wote kuona ni barabara zipi tuanze kupunguza, hatuwezi kutengeneza barabara zote nchini kwa mara moja.

Pamoja na hii tutajitahidi tuone, naomba nitamke lakini siyo ahadi kwamba, tutaipangia fedha barabara hii. Lakini nathibitisha tumetengeneza km. 6 za barabara hii kwa kiwango cha kokoto siyo tu changarawe. Tofauti ya kokoto na changarawe ni kwamba, changarawe zinaweza kuwa ndogo ndogo sana, lakini hapa tumetengeneza kwa kiwango cha kokoto kuweka kama *foundation* ya zege kwenye barabara hii. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Mbunge, ameuliza kuwa, je, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, watakuja waone wenyewe siyo tu kujibu maswali ya kubabaisha?

Mheshimiwa Mbunge kwanza nikuhakikishie kabisa hapa haparusiwi kubabaisha. Ukijibu hapa unajibu kwa niaba ya Serikali kwa hiyo, unajibu jambo la uhakika na wewe unajua Waziri wangu hababaishi, mimi sibabaishi. Kwa hiyo, tukipata nafasi mmoja wetu atakuja kutembelea siyo kuja kuona tunavyobabaisha ila kuja kuwaambia wananchi ukweli kwamba kuna upungufu wa fedha nchini. (*Makofi*)



**Kupeleka Trekta Mpya Gereza la Butundwe**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika Mkutano wa Bajeti iliyopita aliahidi kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004 Serikali itapeleka trekta mpya iliyo na vifaa kamili vya kulimia na kuvunia katika Gereza la Butundwe:-

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi yake?

(b) Kama trekta hiyo iko tayari, je, Serikali itakuwa tayari kumruhusu Mkuu wa Gereza hilo aichukue?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alitoa ahadi ya kupeleka trekta katika Gereza la Butundwe ili kuimarisha kilimo katika gereza hilo.

Katika kutekeleza ahadi hii, gereza hili limepatiwa trekta ambalo limesafirishwa kutoka Dar es Salaam tarehe 14 Juni, 2004. Trekta hii ni aina ya *Massey Ferguson 390* lenye namba ya usajili *CW 5510*. Japokuwa trekta hili siyo jipya lakini limekarabatiwa vizuri sana, hivyo ni zima kabisa na litasaidia sana shughuli za kilimo. Aidha, Mkuu wa Gereza amepelekewa Sh. 1,840,000/= kwa ajili ya kukarabati vifaa vya trekta hasa majembe mawili, *harrow* mbili na tela moja vilivyopo Gerezani Butundwe. (*Makofi*)

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kuniruhusu niulize swali moja dogo la nyongeza. Naanza kwanza kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jitihada aliyoifanya ya kunipatia trekta hilo na hizo shilingi milioni moja. Kwa niaba ya Gereza la Butundwe, napenda kushukuru kwa msaada huo.

Lakini swali, wakati naomba hapa niliahidiwa kununuliwa trekta jipya na matrekta 10 yalinunuliwa. Kwa bahati mzuri au mbaya wakati wa kugawa Watendaji wakawa wamekiuka kauli ya Mheshimiwa Waziri, aliyoahidi kwamba, atanipa trekta mpya. Je, Mheshimiwa Waziri hawa Watendaji ambao hawawezi kutii amri yako bado unao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Waziri ilikuwa ni kupeleka trekta la kusaidia kilimo, kwa sababu Gereza la Butundwe kati ya hekta 1,000 sasa hivi linalima hekta 250 tu. Kwa hiyo, nia ya

Mheshimiwa Waziri ilikuwa ni kusaidia Gereza lile lilime hekta nyingi zaidi na utekelezaji wake katika kutekeleza hilo Mkuu wa Magereza amepoleka trekta, Magereza mengi sana yanahitaji matrekta, hayakupata matrekta. Kwa hiyo, Gereza la Butundwe ni katika hayo machache yaliyobahatika. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyosimamia suala la kilimo katika Gereza la Butundwe.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Gereza la Liwale lilianzishwa kwa msingi kwamba liwe gereza la kilimo. Je, Serikali imechukuwa hatua gani za dhati za kuweza kuboresha kilimo katika gereza hilo hasa ukitilia maanani kwamba halina gari wala trekta mpaka hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Jeshi la Magereza, tunao mpango kamambe wa kuboresha magereza yote nchini, kuyaboresha kimajengo, kuyaboresha kwa nyumba za kuishi askari, kuyaboresha kwa kilimo na viwanda. Lakini mpango huu tunakwenda nao, tunautekeleza kwa kadri bajeti inavyoruhusu. Hivyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika programu yetu tutafika katika Gereza la Liwale ili kuliboresha kama tunavyoiboresha magereza mengine, lakini hatua kwa hatua kwa kadri bajeti inavyoturuhusu.

Na. 104

### **Simu za TTCL Wingwi**

**MHE. MOHAMMED ALI SAID** aliuliza:-

Kwa kuwa mawasiliano ni muhimu kwa maendeleo na kwa kuwa huduma ya mawasiliano ya simu za *TTCL* imechukua nafasi kubwa katika kurahisisha mawasiliano katika maeneo kadhaa nchini. Je, ni lini mtandao wa mawasiliano ya simu za *TTCL* utafikishwa Jimboni Wingwi ili wananchi wa huko waweze kufaidika na huduma hiyo?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Ali Said, Mbunge wa Wingwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kuanzisha na kuendeleza Mfuko Maalum (*Rural Telecommunications Fund*), kwa ajili ya kupeleka huduma za mawasiliano ya simu vijijini. Mtaalam Mwelekezi ambaye ni Kampuni ya Apoyo kutoka Peru amekamilisha mapendekezo yake mwezi huu wa Juni, 2004.

Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi inaifanyia kazi ripoti ya Mtaalam, kuhusu vianzio vya fedha kwa ajili ya Mfuko, uendeshaji wa Mfuko, viashiria kuhusu kipaumbele na masuala ya kisheria. Ni mategemeo yetu kwamba, mara Mfuko huo

utakapoanza kufanya kazi, maeneo mengi nchini, ikiwa ni pamoja na Jimbo la Wingwi, yatapata huduma za *TTCL* na zile za kampuni nyingine.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baadhi ya wananchi wa Jimbo la Wingwi hususan maeneo ya Wingwi, Dodeyani, Wingwi Mapofu na baadhi ya Vitongoji vya Wingwi, wanapata mawasiliano kupitia mtandao wa *ZANTEL*. Wananchi wote wa jimbo hilo watapata mawasiliano ya kuridhisha kupitia mtandao huo baada ya kumalizika kujengwa kwa kituo cha simu cha Zantel (*Zantel Base Station*) katika Kijiji cha Madenjani. Kituo hiki kitamalizika kujengwa kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuhusu maendeleo makubwa ya Sekta ya Mawasiliano ya Simu Zanzibar. Wastani wa matumizi ya simu nchini yaani Tanzania nzima ni simu 2.5 kwa watu 100. Lengo la Sera ya Mawasiliano ya simu ni kuwa na simu 6 kwa watu 100 ifikapo mwaka 2010. Hivi sasa Zanzibar kuna simu 8.15 kwa kila watu 100.

Mheshimiwa Spika, hatua hii kubwa inatokana na na misingi imara ya maendeleo iliyowekwa na Chama Cha Mapinduzi na kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. (*Makofi*)

Na. 105

### **Kituo cha Reli - Igusule**

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa boma wa jengo la Kituo cha Reli (*Railway Station*) cha Igusule ulisitishwa kwa dhana ya kupunguza idadi ya vituo hata vilivyokuwepo tayari kwa kulifanya Shirika la Reli kufanya shughuli zake kibiashara zaidi ya kutoa huduma kwa umma na kwa kuwa hivi sasa hata vituo vidogo yaani *HALTS* vimeanzishwa mahali pengine katika reli ya Kati. Je, ni nini hatma ya jengo la Kituo cha Igusule?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa jengo la kituo cha reli cha Igusule ulisitishwa kwa dhana ya kupunguza idadi ya vituo kuzingatia ukweli kwamba, Igusule ambayo ipo kati ya Mahene na Isaka ipo umbali wa takribani kilomita 7 kutoka Stesheni kubwa ya Isaka.

Hata hivyo, treni za abiria husimama pale kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa maeneo hayo. Iwapo wananchi wa Igusule na Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, wana mapendekezo yoyote kuhusu kumalizia na hatimaye matumizi mbadala ya jengo la kituo cha Igusule, Shirika la Reli Tanzania litakuwa tayari kuyapokea.

Mheshimiwa Spika, huduma za Shirika la Reli linapohusika Mheshimiwa Stephen Kahumbi, amekuwa mstari wa mbele kuzisimamia na kuzisemea hasa zinapowahusu wananchi wa Bukene na watumiaji wa Reli ya Kati kwa ujumla.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Stesheni ya Igusule ni kweli iko karibu na Isaka lakini ina abiria wengi sana. Ukaribu pekee hausababishi kuzuia kuwa na Stesheni kwa sababu Mwanza kuna *Mwanza South*, Dar es Salaam kuna Ilala, Dodoma kuna Zuzu. Je, hizi haziko karibu na Stesheni nyingine? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Stesheni alizozitaja ziko karibu sana na Stesheni nyingine. Lakini Stesheni hizi atakubaliana na mimi ziko mijini. Kwa hiyo, watu ni wengi zaidi ya eneo la Igusule. Lakini kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, tuko tayari kusikiliza maoni yoyote kutoka kwa Mheshimiwa Stephen Kahumbi, kuhusu jinsi gani tunaweza kulikamilisha jengo la Boma la pale Igusule ili liweze kutumika kwa maendeleo ya wananchi kama vile zahanati au shughuli nyingine za kimaendeleo.

Na. 106

### **Kilimo cha Umwagiliaji Wilayani Same**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Wilaya ya Same lipo bonde zuri linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Mto Pangani na kwa kuwa wananchi kwa nguvu zao wenyewe wamechimba mifereji ya umwagiliaji ya Naururu, Kwa Sita, RC, Gunge, Kirua na Ruvu-kwa Mporomoko na kwa kuwa mifereji hiyo inatumika kumwagilia eneo lenye zaidi ya ekari 90,000.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mifereji hiyo kwa kuiwekea kingo za saruji ikiwa ni pamoja na kustawisha kilimo hicho cha umwagiliaji kwa teknolojia ya kisasa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mwaka wa 1995, Serikali ilifanya uchunguzi na kubaini kuwa Bonde la Mto Pangani katika Wilaya ya Same, lina eneo la hekta 6,960 (ekari 17,400) linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Kati ya hizo, ni hekta 810 (ekari 2,025) zinazomwagiliwa hivi sasa na zinajumuisha mfereji wa Naururu, Kwasita, RC, Gunge, Kirua na Ruvu-kwa Mporomoko. Kila mfereji una matatizo na mahitaji yanatofautiana na mwingine. Ili kupunguza gharama za ukarabati, umuhimu umewekwa katika kusakafia

sehemu korofi za mifereji. Maelezo na gharama za kusakafia mifereji hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mfereji wa Naururu, gharama za kusakafia mfereji huo zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 20 na umejumuishwa katika mpango wa maendeleo ya kilimo wa Wilaya ya Same wa mwaka 2004/2005 kwa ajili ya kuombewa fedha. Ukarabati huo utawezesha kupanuliwa kwa eneo linalomwagiliwa kutoka hekta 80 za sasa hadi hekta 380 ambalo ni eneo lote la skimu;

(ii) Mfereji wa Gunge una uwezo wa kumwagilia hekta 280 ambalo ni eneo lote la skimu. Gharama za kusakafia mfereji huo zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 13. Shirika lisilokuwa la Kiserikali la *Same Agricultural Improvement Programme (SAIPRO)*, liko tayari kusaidia ujenzi na kusakafia sehemu korofi kwa kushirikiana na wananchi wa eneo hilo. Kazi inayofanyika sasa ni uhamasishaji wa wakulima kukusanya vifaa vya ujenzi kama mawe na mchanga;

(iii) Mfereji wa Kwa Sita, gharama za kusakafia mfereji huo zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 18 na umejumuishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya ya Same wa mwaka 2004/2005 ili uombewe fedha za utekelezaji. Ukarabati huo utawezesha kupanuliwa kwa eneo linalomwagiliwa kutoka hekta 50 za sasa hadi hekta 180;

(iv) Mifereji ya RC na Ruvu-kwa Mporomoko, eneo linalomwagiliwa sasa ni hekta 55 kati ya hekta 230 zilizopo katika skimu hizo. Gharama za kusakafia mifereji hiyo zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 45. Halmashauri ya Wilaya ya Same, inashauriwa kujumuisha mifereji hiyo kwenye Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya ili iombewe fedha za utekelezaji; na

(v) Mfereji wa Kirua una sehemu mbili, Kirua Ndogo na Kirua Kubwa. Sehemu ya Kirua Ndogo inamwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 21.5 baada ya kukarabatiwa na Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Jamii mwaka 1993, kwa gharama ya shilingi milioni 13.7. Sehemu ya Kirua Kubwa ilishindikana kuendelezwa kutokana na kuwepo kwa magadi katika udongo, kina kifupi cha udongo kutokana na miamba, makorongo makubwa, kuingiliana na Hifadhi ya Wanyamapori ya Ruvu, pamoja na eneo la Wafugaji.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutoa maelezo mazuri yanayohusu kilimo cha umwagiliaji kule Same. Lakini kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametaja kwamba baadhi ya mifereji imewekwa katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo cha Umwagiliaji wa mwaka 2004/2005 na kwa kuwa ndiyo sera ya Wizara ya Kilimo na Chakula sasa. Je, Mheshimiwa Waziri anasema nini kuhusu maombi yao ya fedha, je, yamekubaliwa?

Pili, kwa kuwa Serikali ilitoa ahadi ya muda mrefu ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kule katika eneo la Kiurio Kisiwani na mradi wa kilimo cha mpunga kule Gonja Maore. Je, Serikali inasema nini kuhusu kilimo hicho sasa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa John Singo, kwa kufuatilia maendeleo ya umwagiliaji katika jimbo lake la uchaguzi. Pongezi sana. *(Makofi)*

Pili, ningependa kumhakikishia chochote kilichowekwa kwenye mpango ulioibuka kutoka Wilayani tunaheshimu sana na itakuwa bahati mbaya sana kama haitawezekana katika bajeti hii tutakayoomba na kupitishwa na Bunge letu hili Tukufu. Kwa hiyo, namwomba awe na imani, mambo haya yatatekelezeka mwaka huu.

Mwisho, hizo ahadi hazikuunganishwa na hii kwenye swali. Naomba tu Mheshimiwa Spika, liletwe kwa utaratibu wa kawaida tutalipa jibu barabara. *(Makofi)*

Na. 107

### **Fedha za *STABEX* kwa Ujenzi wa Barabara**

**MHE. MEJA JESSE J. MAKUNDI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika semina ya *TANROAD* iliyofanyika wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Waziri wa Ujenzi aliulizwa ni kwa nini sehemu ya fedha za *STABEX* - Sh.42 bilioni zilizotolewa na Jumuiya ya Ulaya (*European Union*) zisitumike kuboresha barabara zinazosafirisha mazao ya kahawa kupeleka kwenye kiwanda cha kukoboa kahawa alisema hajui ziliko aulizwe Waziri wa Fedha ambaye naye alijibu hajui ziliko bali aulizwe Waziri wa Kilimo na Chakula, ndipo Naibu Waziri wa Kilimo na chakula alijibu kuwa fedha hizo ziko Serikalini:-

(a) Je, huo ndio utaratibu unaofaa wa kujibizana Bungeni?

(b) Je, fedha hizo ziko wapi, zimepangiwa kufanya nini na ni nani awajibike kwa suala hilo au utandawazi utumike kuiuliza Jumuiya ya Ulaya ili itoe matumizi sahihi ya fedha hizo?

(c) Je, kama Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi imekwepa kujenga barabara hizo za kusafirishia kahawa hasa zile za Vunjo, watatumia barabara zipi ili kurahisisha kazi ya mawasiliano na uchukuzi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meja Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kipindi kilichopita fedha za *STABEX* zimekuwa zikisimamiwa na Wizara za Fedha na Kilimo na Chakula na mazungumzo na Jumuiya ya Ulaya yalifanywa na Wizara hizo mbili. Wakati wa Semina ya Wabunge iliyofanyika tarehe 14 Februari, 2004, Wizara ya Ujenzi ilikuwa haijapata maelezo juu ya fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara muhimu mikoani, kwa hiyo, majibu yaliyotolewa wakati ule yalikuwa sahihi.

(b) Makubaliano kati ya *EU* na Serikali ya Tanzania ni kwamba, ujenzi wa barabara hizo utasimamiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ambao wako chini ya Wizara ya Ujenzi. Aidha, *Euro* milioni kumi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ziko kwenye akaunti ya pamoja ya *EU* na Serikali ya Tanzania na zitatolewa pindi maandalizi ya ujenzi wa barabara hizo yatakapokamilika.

(c) Serikali haijakwepa kujenga barabara chini ya fedha za *STABEX* na Waziri wa Ujenzi amethibitisha hivyo kwa maandishi. Kinachofanyika ni kwamba, Serikali kwa kushirikiana na *EU* imemwajiri mtaalam mwelekezi (*Consultant*) ambaye anashirikiana na Halmashauri za Wilaya zinazohusika kuainisha barabara muhimu zitakazojengwa na viwango vya ujenzi. Kazi ya kuainisha barabara hizo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Julai, 2004 na ujenzi utanza mwaka 2004/2005.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa *STABEX* ilitolewa kwa ajili ya kuboresha kahawa na kwa kuwa matatizo makubwa ya kahawa ni wadudu visumbufu ambavyo vinafanya ile kahawa isikue na saa nyingine kahawa iliyokwishazaa kupotea. Ni kwa nini Serikali haitumii hela hizi za *STABEX* kuwanunulia dawa hizi wakulima wa kahawa na kuwapa bure kama unavyoelekeza mpango mzima wa *STABEX*? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli *STABEX* inahusu masuala ya kahawa. Kwa sababu kuna *STABEX* inashughulikia vile vile utafiti wa chai na pamba na vile vile *STABEX* ina shughuli nyingine zaidi ya utafiti tu hata shughuli za ugavi. Sasa kuhusu swali lake naomba nieleze kuwa, katika utafiti jambo ambalo tumeliona lilitiwe maanani zaidi siyo tu kumwagia madawa kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, lakini vile vile kuzalisha kahawa kwa njia ya vikonyo ambavyo vinazuia kasi ya mashambulizi ya kahawa. Kwa hiyo, tunafanya hilo analopendekeza Mheshimiwa Mbunge, lakini tumeenda mbele zaidi kwa kushughulikia na vikonyo ambavyo tunafikiri ni uamuzi wa busara.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuniruhusu. Kama ilivyo kwenye swali la msingi, kwa kweli maelezo ya Serikali hayajitoshelezi kwa sababu mwaka wa fedha umeshakwisha na kwenye Wilaya yangu sijamwona Mtaalam anayemsema Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa Waziri wa Ujenzi yuko hapa ningependa asimame atuhakikishie kwamba ni ukweli ujenzi wa kutumia hela utanza mwezi wa saba? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi anafahamu kwamba, kuna makubaliano kati ya Serikali na *EU*

kwamba, *Euro* milioni 10 zimetengwa kwa ajili ya barabara muhimu katika Mikoa na nimeshatoa taarifa hapa Bungeni juu ya suala hilo na nitarudia tena kutoa maelezo juu ya suala hilo wakati nitakapowasilisha hotuba yangu hapa Bungeni. Naomba awe na imani na kama anahitaji kuona makaratasi hayo atuambie tumtafutie ili na yeye ayasome aelewe yaliyomo. (*Makofi*)

Na. 108

### **Mashine za Kusukuma Maji**

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA** aliuliza:-

Kwa kuwa pamoja na juhudi za kutafuta mashine za kusukuma maji zilizoibiwa katika Kata ya Iramba, Jimbo la Mwibara, mashine hizo hazijapatikana na kwa kuwa Serikali ilitoa ahadi kuwa ingetoa mashine nyingine badala ya hizo zilizoibiwa.

Je, ni lini mashine hizo zilizoahidiwa na Serikali zitatolewa ili kutatua tatizo la maji katika Vijiji vya Kata ya Iramba, Karukekere, Muranda, Namhura na ni lini Serikali itachimba visima katika Vijiji vya Ragata, Kabainja, Buzimbwe na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mutamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mradi wa maji wa Iramba ulikuwa na mitambo mitatu ambayo ilikuwa inafanya kazi hadi mwaka 1978 ambapo mashine zote tatu za kusukuma maji ziliibiwa na kusababisha kituo kusimama kabisa kufanya kazi. Mpango wa *HESAWA* uliokuwa unatekelezwa katika Mkoa wa Mara ulikuwa tayari kununua mitambo mitatu ya maji kwa ajili ya kituo cha Iramba ili itumike badala ya ile iliyoibiwa. Lakini, kutokana na wananchi kutoitika wito wa kuchangia sehemu ya gharama ya ukarabati wa mitambo hiyo, ununuzi wa pampu hizo haukufanyika.

Mheshimiwa Spika, ili kurudisha huduma ya maji katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, imenunua mashine moja mpya na kukarabati pampu ya maji iliyokuwepo, kazi zilizobaki ni kukamilisha ufungaji wa mitambo hiyo ili ununuzi wa *foot valve* na matengenezo madogo ya nyumba itakamowekwa mashine ufanyike. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Juni, 2004 ili mradi uanze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, chanzo cha maji kwa ajili ya vijiji vya Karukekere na Muranda ni bwawa la Karukekere. Aidha, Kijiji cha Kabainja kimeendelea kupata huduma ya maji kutoka bwawa lililokarabatiwa na Serikali kupitia Mradi wa *Mara Farmers Initiative Project* uliokuwa unafadhiliwa na *IFAD*.



Serikali kupitia Mradi wa *Mara Farmers Initiative Project* ilijenga kingamaji ya bwawa la maji la Namhura. Bwawa hilo halikukamilika na hivi sasa linakamilishwa kwa fedha kutoka Programu ya kuendeleza Sekta za Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme - ASDP*). Vifaa vyote vinavyohitajika katika kukamilisha kazi hiyo vimeshakusanywa katika eneo la kazi. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha muda mfupi kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali vile vile kupitia Mradi wa *Tanzania Social Action Fund (TASAF)*, imechimba visima viwili katika Kata ya Namhura na kuvifungia pampu za mkono. Visima hivyo vinafanya kazi kama tunavyofahamu. Serikali pia kupitia Mradi wa *Lake Victoria Environmental Management Project* imechimba visima viwili katika Kijiji cha Ragate. Visima hivyo vimewekewa pampu za mkono na vinafanya kazi. Aidha, uchimbaji wa kisima cha tatu ambacho pampu yake ipo, upo katika hatua za mwisho ili kukamilika.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pia ninaomba nishukuru kwa juhudi za Wizara hii. Lakini ninaomba tu kumtaarifu Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, Bwawa la Karukekere mara nyingi limekuwa haliweki maji kwa muda mrefu, lina tabia ya kukauka, sasa nikadhani kwamba Waziri au Wizara iangalie njia mbadala ya kutatua matatizo ya maji katika Kata hizi badala ya kutegemea Bwawa hili. Je, Mheshimiwa Waziri unaweza ukawa na njia mbadala ya kutatua tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, njia mbadala ni kumwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wanaoishi maeneo hayo, kutunza vyanzo vinavyoingiza maji kwenye bwawa analolisema. Hiyo ikiwa ni pamoja na kupanda miti kando kando ya hilo bwawa na kuhakikisha kwamba, inatunzwa na haiingizwi mifugo sehemu ambayo haitumiki kwa ajili ya kunyweshea mifugo.

Kwa namna hiyo, nina hakika kwamba, bwawa hili litaanza kutunza maji tena na litasaidia wananchi, kwa sababu hata kama tungeweka visima bado vitakauka, bado pampu zake zitaibiwa, kitu ambacho ningeomba kupitia Bunge lako Tukufu ni kwamba, kwa sasa hivi kulingana na mahitaji ambayo wananchi wengi wana shida ya maji, sehemu ambako vyombo au vifaa vya miradi yetu vinaibiwa ni juu ya Halmashauri husika na wananchi husika kuvirudishia. Ninapenda kutoa mfano wa Handeni ambako kuna vifaa vingi vimeibiwa, wafanye hivyo, Halmashauri yao na wananchi ili fedha zinazobaki za Serikali ziweze kutumika maeneo mengine ambako wana uwezo wa kutunza miradi hiyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamejibiwa. Sasa matangazo ya vikao vya leo ni kama ifuatavyo: Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mwenyekiti wake anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 5.00 asubuhi hii kwenye Ukumbi Na. 133 ghorofa ya kwanza. Kamati ya pili, ni Kamati ya Hesabu za Serikali, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*) wakutane mara baada ya kipindi hiki cha maswali chumba Na. 227 ghorofa ya pili.

Kamati za Vyama vya Siasa vile vile vinatambuliwa na Kanuni za Bunge, kwa hiyo, natangaza kikao cha Kamati ya Wabunge wote wa CCM kwamba, watakuwa na Kikao leo jioni baada ya kuahirisha shughuli za Bunge hapa hapa ndani ya Ukumbi huu. Mwisho, orodha ya wachangiaji wa leo imeshawekwa kwenye ubao wa matangazo.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005 Ofisi ya Waziri Mkuu

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kwa siku ya leo ili niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nami napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa Waheshimiwa Wabunge wote, waliofiwa pamoja na waliopata matatizo mbalimbali wakati wakijiandaa kuja kwenye shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo, napenda kutumia nafasi hii kwanza kuipongeza Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi ilivyoandaliwa, kwa kweli ni nzuri. Ninawapongeza Mawaziri wote wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu Mkuu na Wasaidizi wake wote. Kwa kweli wamejiandaa vizuri, kwa kweli hotuba hii imeonyesha Dira ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuchangia suala la ujenzi wa barabara. Katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000, kulikuwa na ujenzi wa barabara nyingi nitataja baadhi tu ya barabara na ile ambayo nataka kuichangia. Kwanza, kulikuwa na barabara ya Kibiti - Somanga - Lindi - Mingoyo, ilipewa kipaumbele kwamba kwa kipindi hiki itajengwa. Ya pili ni Ubungo - Mlandizi. Tatu ni Dodoma - Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kulikuwa na barabara nyingine ambayo ilikuwa imetajwa katika ukurasa wa 44, katika Kitabu cha Ilani ya Uchaguzi nayo ni barabara inayotoka Makuyuni - Oldieni - Lalago. Ni barabara ya *corridor* ya Kaskazini inayounganisha Mikoa ya Arusha, Manyara, Singida, Shinyanga, Mwanza na Mara. Barabara hii ni muhimu na imefanyiwa upembuzi yakinifu kwa miaka ya 1997/1998 na ilipangwa kwa kipindi hiki ikamilike na tayari imeanza kujengwa lakini imetengenezwa kwa sehemu fupi kutoka Makuyuni mpaka kwenye lango la Hifadhi ya Ngorongoro. Barabara hiyo ni muhimu na imejengwa kwa kiwango cha lami ni kilomita 77 lakini bado kuna ujenzi wa barabara hiyo kutoka lile lango la Hifadhi ya Ngorongoro kupitia Oldieni - Wilaya ya Meatu - Wilaya ya Maswa Lalago - sehemu ya Bariadi na kwenda Ramadi. Barabara hii ni muhimu sana.

Kwa sababu imebaki sehemu kubwa na Serikali imefanya kazi nzuri, naamini sio rahisi kujenga tena kipande kilichobaki lakini naleta ombi maalum sehemu ya kiungo cha Mkoa wa Shinyanga na Singida kuna mto Sibiti ni mkubwa wananchi wa Mikoa hii miwili wanapata shida sana kuwasiliana, kuna haja ya kujenga daraja lile. Naomba kwa wakati huu kabla hawajapata pesa nyingi daraja hilo lijengwe ili kuwasiliana na Mikoa hii ya Shinyanga na Singida. Nalileta hili kama ombi maalum ili kuwasiliana wakati bado wanajiandaa kujenga barabara nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya ombi hilo, napenda nichangie jambo ambalo limezungumziwa na Wabunge wengi. Suala la Walimu ni muhimu sana. Mtumishi wa Serikali anapokubali kuajiriwa anaweka mkataba wake na mwajiri wake kwamba atatimiza masharti yote ambayo mwajiri amemwelekeza atimize na mwajiri lazima awajibike kumlipa mahitaji yake yote ambayo yako kwenye utaratibu. Inapotokea Serikali imeshindwa kufanya hivyo inakuwa ni tatizo na kero kwa yule mwajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe mfano kwa Mkoa wa Shinyanga. Mkoa huu una jumla ya Shule za Msingi 976 lakini madai ya Walimu wa Shule za Msingi kuanzia mwaka 1995 - 2003 yamegawanyika katika sehemu sita nazo ni uhamisho, masomo yaani mafunzo ya Walimu, likizo, matibabu, ajira mpya na malimbikizo ya mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, kwa vifungu hivi sita, uhamisho tu peke yake unagharimu shilingi 959,512,000, upande wa masomo unagharimu shilingi 49,302,000, upande wa likizo shilingi 55,000,000, upande wa matibabu shilingi 24,000,000, ajira mpya shilingi 193,000,000, malimbikizo ya mishahara shilingi 52,000,000, jumla yote Mkoa wa Shinyanga peke yake ni shilingi 1,335,204,104. Hela hii ni nyingi lakini wanaodai lazima waipate na kama ni deni ni lazima Serikali iwajibike kulipa deni hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi karibu tutaingia kwenye mahesabu ya mwaka 2004/2005, hesabu hii ninayoizungumzia ni kuanzia mwaka 1995 - 2003. Kwa hiyo, tunapofunga mahesabu ya mwaka huu hesabu nyingine itaongezeka kwa mwaka huu tunaouzungumzia. Serikali ione umuhimu wa kuwalipa Walimu hawa, kwa kweli inawavunja moyo na dawa ya deni ni kulipa tu hakuna njia nyingine itakayofanyika isipokuwa kuwalipa Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ilione suala hili kama ni tatizo na kero kwa Walimu. Tafadhali sana Serikali naomba suala hili mlipe kipaumbele, wenzangu wameshazungumza lakini na mimi naongeza kusema kwamba, kwa kweli ni tatizo. Shilingi bilioni 1.3 kwa Mkoa mmoja ukichukua Mikoa yote kutokana na jinsi Waheshimiwa Wabunge wote walivyopiga kelele hapa nadhani kuna haja ya kulifanyia kazi suala hili kikamilifu. Hilo naomba niliachie hapo nadhani Serikali imesikia.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo jingine ambalo nalo linatupa shida sana, Mheshimiwa Jacob Makolo amelizungumzia. Ugawaji wa Pato la Taifa ni tatizo. Bado tunalichukulia kama upendeleo Mkoa fulani tuupe hela za maendeleo kiasi fulani, ni

tatizo sana. Lakini tungekuwa na *formula* au *ratio* fulani ambayo itakuwa na uhakika wa ugawaji wa Pato hili la Taifa, ndiyo ni ndogo tunakubali lakini kuwe angalau na kitu ambacho kitatuongoza namna ya kugawa Pato hilo la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Paul Makolo na mimi ninarudia, Mwanza imepewa fedha nyingi, ni sawa kwa sababu Mkoa wa Mwanza kwenye sensa iliyopita ya mwaka 2002 kulikuwa na idadi ya watu milioni tatu na inaongoza Kitaifa kwa kuwa na *population* kubwa. Mkoa wa pili ni Shinyanga una watu milioni 2.9, watu hao ni wengi. Dar es Salaam ni Mkoa wa tatu ambao una watu milioni 2.5. Mkoa wa Mbeya una watu milioni 2.4. Lakini unakuta Mkoa mdogo kabisa umepewa hela za maendeleo nyingi zaidi kuliko Mikoa hii minne niliyoitaja. Unajiuliza tunatumia vigezo gani kugawana Pato hilo la Taifa? Kama watu walio wengi hawakupewa fedha nyingi za maendeleo ina maana kwamba, hawa walio wengi wanapunjwa. Naomba kuishauri Serikali izingatie suala hili. Hatuna malalamiko kama kutakuwa na mgawanyo mzuri wa Pato la Taifa lakini kama hali ni hii, inaonyesha kuna upendeleo fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwe muwazi, sijui bahati nzuri au bahati gani, Mkoa unaopendelewa kupata Mawaziri wa Fedha ni wa Kilimanjaro na kila wakati *trend* ni hiyo hata miaka ya nyuma kama sio Mkoa wa Kilimanjaro kuongoza kupata fedha nyingi za maendeleo basi Mkoa wa Tanga unaongoza, wakati mwingine Mkoa wa Arusha unaongoza, Mkoa wa Kilimanjaro unakuwa wa pili. Sasa unashindwa kuelewa kwa nini wanafanya hivyo na Mikoa hiyo yote ina idadi ndogo ya watu kuliko ile Mikoa niliyoitaja. Hata kama wanagawa Kikanda, Kanda ya Ziwa ndio yenye watu wengi ya pili ni Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wanapokuwa wanapanga Kanda hii inapewa pesa nyingi zaidi kuliko Kanda nyingine, hutuelewi! Kama tungekuwa na utaratibu mzuri wa kugawana Pato la Taifa hatutakuwa na malalamiko kama haya lakini sasa inapotokea kule ambako Waziri wa Fedha anatoka na pesa kule inakuwa nyingi basi tunakuwa na wasiwasi hivi kulikoni? Hii inaonyesha kwamba kuna tatizo, wanapendelea. Ili Pato la Taifa lisiwe na upendeleo tupewe kwa kufuata *formula* ambayo inaweza kutusaidia wote tuamini kwamba, Pato la Taifa linagawanywa vizuri. Naamini tukiwa na kigezo kizuri nadhani wote tutaelewa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine napenda nizungumzie suala la njaa. Ni kwa bahati mbaya sana mwaka huu kwa kweli tumekuwa na tatizo la njaa. Bahati mbaya msimu wa mvua uliopita tumepata mvua kama mara tatu, nne, mwaka ukaisha, mazao hayakukomaa, sehemu nyingine hawakupata chochote kwa hiyo tunaendelea na njaa. Lakini naipongeza sana Serikali kwa suala la njaa imejitahidi sana kwa sababu Mkoa wa Shinyanga tumepata tani 4,061 ambapo ni Wilaya tatu au nne zimepata chakula hicho, tusingepata chakula hicho watu wangekufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mashirika haya ya *World Food Programme*, yamesaidia sana tena wakati mgumu wa shida tukapewa chakula Wilaya tatu za Kishapu, Meatu na Maswa na ndiyo sehemu ambazo tumeathirika sana. Shirika hili kwa kupitia *World Vision* wametupa tani 3,874 na ndio ulikuwa wakati mgumu, wa shida, watu wanakula mlo mmoja, wanakunywa uji au wanakula mboga za majani tu yaani ilikuwa shida kubwa

sana lakini tukabahatika kupata nafasi hiyo kwa kweli wananchi wanashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya hizi tatu, napenda kutumia nafasi hii kuishukuru Serikali na kuipongeza kwa juhudi ambazo imezifanya vinginevyo tungekuwa tunasema maneno mengine. Mheshimiwa Lukuvi amefanya kazi nzuri sana ya kutembelea na kuona maeneo hayo, kwa kweli nimeridhika na huduma hizo ambazo zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nitumie nafasi hii ya pekee, niishukuru Serikali kwa Awamu hii ya Tatu, imefanya kazi kubwa sana hasa kwa Kanda yetu ya Ziwa. Suala la maji kutoka Ziwa Victoria lilikuwa ni kero kubwa sana, maji tunayaona lakini hatuyatumii. Kwa kupitia Serikali, Rais mwenyewe, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, namshukuru sana na Wizara ya Maji imefanya kazi nzuri sana, naipongeza sana kwa suala hili. Tulikuwa hatuna njia nyingine na pengine tukipata maji haya ni ukombozi Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kusema kwamba, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuungana na Wabunge wenzangu, kuwapa pole waliopata misiba na wale waliopata ajali pamoja na jirani yangu hapa, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela aliyevamiwa na majambazi.

Napenda nianze mchango wangu kwa kuzungumzia suala la umaskini. Suala la umaskini ni kubwa na baya sana hapa kwetu Tanzania. Nadhani umaskini ni mkubwa sana huko vijijini na sijui Serikali imeandaa vipi suala la kupunguza huu umaskini. Sijui tumeandika tu tukaacha kwenye vitabu kwa sababu hakuna kinachofanyika vijijini ambacho tunaweza kusema kwamba tumeweka mikakati.

Mheshimiwa Spika, niwazungumzie wafugaji, zamani walikuwa matajiri sana lakini siku hizi ni maskini sana kwa sababu wamehamia mijini, kilichowafukuza kule ni umaskini. Watu wengi sana wanadhani kwamba kila mfugaji ana ng'ombe, sio kweli. Kuna watu waliosahaulika, Tanzania ina matabaka ya watu kuna tabaka la watu ambao hawana elimu na kuna tabaka la watu ambao wana elimu. Hata ukiangalia sekondari katika maeneo ya wafugaji, Jimbo moja lina sekondari moja katika maeneo mengine kila kijiji kina sekondari, kila Kata ina sekondari, hii inaonyesha kwamba, elimu katika maeneo haya ya wafugaji ni duni. Naomba Serikali itambue hilo na iweke mikakati ya kujaribu kunyanyua elimu katika maeneo ambayo hayana elimu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la kilimo na mifugo, nianze na kilimo. Sijui imesahaulika kwamba katika maeneo yale pia kuna wakulima wanadhani kilimo kiko Kusini tu maeneo mengine hakuna kilimo? Juzi Mheshimiwa Benedict Losurutia, alisema kwamba, hajawahi kupata pembejeo, hivi ina maana kwamba wakulima hawako Kiteto na Monduli, kwa nini kunakuwa na matabaka ya kugawa huduma? Mkulima ni mkulima kama wa Kusini anahitaji pembejeo hata aliyepo Longido anahitaji pembejeo.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye mifugo, nadhani kuna watu wanaipenda nyama lakini hawapendi mifugo. Suala la mifugo halitiliwi maanani kabisa kana kwamba kuna mifugo Tanzania. Kila siku tunachozungumzia ni pembejeo lakini hatuzungumzii madawa ya mifugo. Hapa nchini mifugo wanakufa kutokana na magonjwa lakini sijawahi kuona kwenye bajeti fedha zilizotengwa kwa ajili ya dawa za mifugo, hivi ni kwa nini Serikali haitambui kwamba mifugo inahitaji dawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, anatoka kwenye jamii ya wafugaji, ana wafugaji wengi sana ambao ni maskini. Waziri wa Mifugo naye ni mfugaji na anajua mifugo inakufa. Leo naomba Serikali itenge kwenye bajeti itafute popote fedha kwa ajili ya dawa za mifugo. Nadhani wafugaji popote walipo wanasikia mpaka kule Mbeya wafugaji hawataiunga Serikali mkono kama hawapati madawa. Naomba Serikali iwasikilize Wabunge, mimi nimezungumzia dawa za mifugo, wengine wamezungumzia fedha za Walimu zilizoliwa, kama mnataka sasa kuanza kupambana na rushwa anzeni kwenye hizi fedha za Walimu zilizoliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la mikopo. Bajeti iliyopita (2003/2004) tumetenga shilingi bilioni moja mwaka huu (2004/2005) sijui itatengwa bilioni ngapi hatuna hakika hiyo shilingi bilioni moja tuliyotenga nani kapata na imebaki kiasi gani. Hizo fedha zilizopelekwa *Exim Bank*, Mheshimiwa Maria Watondoha aliuliza hii Benki ni ya nani na mimi nataka kuuliza tena hii Benki ni ya nani kwa sababu kila siku neno linalotumika ni ya vigogo sasa kama ni ya vigogo tujue vigogo hao ni akina nani kwa sababu hatujui hizi fedha zimetumikaje na yamewekwa masharti magumu ili tusizipate fedha hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile nataka kujua wafugaji wamo katika mkopo huu au ni wakulima tu mnasema wakulima, wakulima hivi wafugaji watapata wapi mikopo? Hizi fedha kuna walakini, inafaa Serikali ikae na kuangalia kwa sababu Mabenki tunayoyajua mmekwepesha fedha hizi zisiende huko kwa mfano, *CRDB*, *NMB*, mnakwenda kuweka kwenye Benki za vichochozoni kwa nini mnaweka kwenye Benki za vichochozoni ambazo hazitambuliki? Kwa hiyo, tunakata hizi pesa za mwaka huu zisiingie katika hii Benki inayoitwa *Exim Bank* ni watu wenye masharti magumu ili tusizipate mkopo huo waendele kufanyia biashara pesa hizo, pesa za wananchi mnapeleka kwa watu zikafanye biashara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la umeme. Tulipokuwa kwenye kampeni ya Rais mwaka 1995 - 2000, Serikali ilitoa ahadi kuupatia Mji wa Namanga umeme, tunaingia 2005 wananchi wa Namanga na Longido wanasubiri umeme, sijui kuna tatizo gani. Kila Waziri wa Nishati na Madini anatoa ahadi kwenye kila bajeti

kwamba umeme utafika Namanga mpaka leo haujafika, nataka nijue kuna matatizo gani?  
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la barabara. Suala hili nataka niliweke vizuri, siku moja nilizungumza kidogo lakini nataka niliweke vizuri kwamba, barabara ya lami inayojengwa kutoka Rombo - Kamangwa ni barabara moja ambayo inazunguka Mlima Kilimanjaro mpaka inakuja kutokea Hai. Nisingependa waipindishe, nasikia Waziri wa Ujenzi aliambiwa kwamba, hiyo barabara ilitengenezwa kwa ajili ya kwenda Nairobi, hivi mtu ambaye anaelewa ramani ya Rombo na Nairobi inatoka wapi, ni tofauti kabisa. Barabara inayotoka Holili haiendi Nairobi inakwenda Mombasa kwa hiyo, barabara inayotoka Arusha kwenda Nairobi ndio barabara ya Nairobi, wanasema eti wamezungusha ili iende Nairobi, hapana. Naomba Serikali ikae na kumalizia hiyo barabara na izunguke kama walivyoifikisha Kamwangwa iende Kitenden - Learang'wa - Olmoluk - Ngaranairobi, ikutane na barabara iliyoachwa porini, kuna lami imefika Sanya Juu ikaachwa porini iunganishwe hapa. Barabara hiyo naiunga mkono kabisa, lakini Serikali wamalizie isipomalizika mimi na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, tutakuwa hatarini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono *TASAF* pamoja na kuwa bado haijafika Wilayani kwangu. Kwa kweli nawashukuru sana kwa miradi waliyoifanya maeneo mengine lakini naomba ifike katika maeneo mengine kwa sababu umaskini umekithiri sana. Monduli watu wengi wamehama wamekwenda Mererani, wako Nairobi umaskini ndio unaowafukuza. Naomba Mradi wa *TASAF* ufike katika maeneo ambayo haujafika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kurudia kuiomba Serikali na naomba sana suala hili la dawa za mifugo lizingatiwe, tuokoe mifugo kwa sababu tusipoiokoa umaskini utakithiri zaidi. Kama tunataka kupunguza umaskini sio kilimo tu ndicho kinapunguza umaskini, tuna watu wengi sana wanategemea mifugo na mifugo inaangamia kila siku na kila siku nalia hapa kwamba, tunataka dawa ya kinga ya ugonjwa wa miguu na midomo, Serikali mkinisikia nawashukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. ALHAJI AHAMAD H. MPEME:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kabla ya yote nianze kutoa pole kwa Rais wetu mpenzi, Mheshimiwa Benjamin William Mka. Namtakia kheri kwa Mwenyezi Mungu, amrejeshee afya ili aweze kuwatumikia Watanzania vizuri.

Ninatoa pole kwa Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda pamoja na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kuondokewa na mzazi wao. Pia ninampa pole Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa kuvamiwa na majambazi. Vile vile ninampa pole Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere kwa kupata ajali, namtakia Mwenyezi Mungu ampe nafuu apone.

Mheshimiwa Spika, labda nianze kwa kuipongeza bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kweli bajeti ni nzuri, yenye mwelekeo na iliyo na makusudio ya kupambana

na umaskini. Lakini nichukue nafasi hii pia niipongeze Serikali, kwa kweli Rais alivyotamka kwamba, anachagua askari wa miamvuli ili waweze kuhakikisha kwamba wanaitumikia nchi hii kwa makini na kwa umahiri mkubwa, imeonyesha kwamba hali hiyo kweli imeanza kujitokeza. Karibu Wizara zote zimefanya kazi vizuri sana ya kuhakikisha kwamba, wanatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2000. Isipokuwa tupo hapa kwa ajili ya kuishauri Serikali katika yale maeneo ambayo bado yanahitaji marekebisho (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya akiwemo Waziri Mkuu, ya kutembelea Mikoani mara kwa mara. Kwa kweli hali hiyo inatoa changamoto kwa kuwahamasisha wananchi kushughulika na shughuli za maendeleo ili kuondoa umaskini. Isipokuwa ninachoomba ahadi wanazozitoa katika ziara zao hizo basi zitekelezwe. Nisingependa nieleze kwamba ni yupi alikuja kwenye Jimbo langu, alitoa ahadi gani na hajatekeleza. Nadhani kwa jumla niseme tu kwamba, naomba ahadi zinazotolewa na Mawaziri kwenye Majimbo wanapokuja basi wazitekeleze na zile ahadi ambazo wanawapa Waheshimiwa Wabunge tunapowaomba kwamba kwenye Majimbo yetu kuna hili na hili basi wakiwa wanaahidi kwamba watatekeleza, naomba zitekelezwe kwa sababu Mbunge anapokwenda kwenye Jimbo lake anaeleza kwamba hili jambo litatekelezeka, matokeo yake baadaye likawa halitekelezeki anapata matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Kanda ya Mtwara. Mpango huu wa Kanda ya Mtwara ulipoanzishwa ulijenga matumaini makubwa kwetu sisi wa Mikoa ya Kusini kwamba sasa tutakomboka hasa kiuchumi. Lakini inaonyesha ni kwamba, mpango mzima huu umebaki katika maandishi, utekelezaji wake umekuwa ni mgumu sana. Kwa hiyo, tumefika mahali tunakata tamaa kwa sababu mipango mingi iliyopangwa kutekelezwa katika Mpango huu wa Maendeleo ya Kanda ya Mtwara bado haionyeshi kutekelezwa. Kwa mfano, kuna ujenzi wa barabara ya Mtwara - Masasi - *Mbamba Bay* hatuelewi imefikia wapi, kuna mpango wa ujenzi wa daraja la pamoja la Tanzania na Msumbiji, bado haieleweki umefikia wapi, kuna upanuzi wa bandari ya Mtwara haijaleweka vizuri, kuna kupatiwa umeme wa kudumu aidha unaotokana na makaa ya mawe au unaotokana na gesi zetu tulizokuwa nazo, pamoja na kwamba katika Kitabu hiki cha Bajeti ya Waziri Mkuu imetajwa kwamba kutakuwepo na *grid* ndogo kati ya Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, lakini kilichokatisha tamaa zaidi ni kile kitendo cha kuuchukua Mradi mzima wa gesi ya Songosongo ukanufaishe maeneo mengine wakati ile gesi inatoka Kusini na kule kuna matatizo ya umeme na Mpango wa Maendeleo ya Kanda ya Mtwara upo kule. Nilifikiria kwamba ile gesi ya Songosongo ingepewa kipaumbele kupelekwa Mikoa ya Kusini ili kutekeleza ule Mpango wa Maendeleo ya Kanda ya Mtwara. Lakini inasikitisha sana kwa sababu kwanza ilitokea bahati kwamba katika Mradi ule ilikadiriwa kutumika Sh. 174bn/=. Lakini pesa zinazokadiriwa kutumika ni Sh. 114bn/=, kwa hiyo, kuna kubakia kwa Sh. 60bn/=. Sasa hizi Sh. 60bn/= kwa sababu gharama ya kuondoa gesi ile kuipeleka Mikoa ya Lindi na Mtwara ni Sh. 34bn/=, tungetegemea kwamba hizi pesa zinazobaki zingeweza kutoa ile gesi kupeleka Mikoa ya Lindi na Mtwara.



Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya pesa hizi zote zimewekwa kukarabati nyaya za umeme, yaani ufanyiwe ukarabati mpya kuwa nyaya za umeme kutoka Dar es Salaam labda kwenda Kilimanjaro au kwenda Tanga. Sasa huku kunakarabatiwa nyaya huku watu hawana umeme kabisa wa uhakika. Sasa kitendo hiki kwa kweli kinatukatisha tamaa. Lakini lingine kitendo cha kuchukua zile bilioni 15 ambazo sasa hivi utekelezaji wa gesi ya *Mnazi Bay* ungekuwa umeshakamilika, zikapelekwa kununua majenereta ambayo sasa hivi yapo Ubungo, pia kwa kweli inatukatisha tamaa. Sasa ningeiomba basi Serikali, maadam inayo makusudio ya kupambana na kuondoa umaskini ni vema miundombinu ipelekwe katika maeneo yote kwa uwiano maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama miundombinu ikielekezwa upande mmoja tu maana yake ni kwamba, utakuwa kama unaigawa nchi kwamba upande mwingine waneemeke na upande mwingine waendeleo kuathirika. Sasa tuna mategemeo makubwa, naomba niishauri Serikali kwamba, ule Mradi sasa wa gesi ya *Mnazi Bay* ambao sasa ndiyo tuna mategemeo kwa *grid* ile ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameitaja kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara kupitia hii Kampuni ya *Atmus Group*, Serikali iwasukume ili ule Mradi utekelezeke ili kuondoa hii dhana tuliyokuwa nayo sasa hivi kwamba, Serikali inaelelea upande mmoja, hiyo dhana iondoke. Kwa hiyo, wajitahidi kusukuma ule Mradi wa gesi ya *Mnazi Bay* ili kutengeneza ile *grid* ya Mtwara na Lindi ili angalau Mikoa hiyo ya Kusini iondokane na dhana hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende katika upande wa kupambana na umaskini. Kwa upande wa kupambana na umaskini, naomba Serikali ijishughulisha sana katika shughuli za kuwaondolea wakulima au kuwapa uwezo wakulima kwa sababu karibu asilimia 80 ya uchumi wetu unategemea sana kilimo na karibu watu wengi katika nchi yetu wanajishughulisha na masuala ya kilimo katika kuondoa umaskini. Sasa kama kilimo kitakuwa legelege basi hali ya umaskini kuondoka itakuwa ni vigumu. Mara nyingi sana kwenye bajeti imekusudiwa mambo mengi kwamba wataelimishwa wakulima kilimo cha kisasa ili kutoa mazao bora yatakayoleta ushindani kwenye soko, kuvifufua viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, itatolewa mikopo kwa wakulima, lakini utekelezaji wake umekuwa mdogo. Mpaka sasa hivi viwanda vya korosho vinaoza. Korosho tunazouza nje ni korosho ghafi kiasi ambapo soko lake ni gumu, wakulima wa korosho kuna wakati wanapata tabu, viwanda vipo kwa nini Serikali haitilii mkazo kuvifufua vile viwanda vikaweza kufanya kazi ya kusindika korosho ili tukauze korosho zilizobanguliwa ili mkulima wa korosho apate tija nzuri? Sasa naiomba Serikali iangalie kwa kiwango kikubwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba nizungumzie kuhusu barabara ya Dar es Salaam - Kibiti - Lindi - Mingoyo. Kwa kweli tunashukuru sana, hatukutegemea kabisa, ilikuwa ni ndoto, tangu Uhuru Wabunge hapa walikuwa wanazungumzia habari ya barabara ya Dar es Salaam - Kibiti - Lindi - Mingoyo. Leo hii Daraja la Rufiji limejengwa na limemalizika na linatumika. Kwa kweli hali ya maendeleo imeanza kujionyesha kabisa, tunaishukuru sana Serikali kwani Serikali haiwezi kufanya mambo yote kwa mara moja kutokana na hali ya kipato tulichokuwa nacho, lakini lile

linalowezekana likifanywa lazima tuishukuru kwa kiwango kikubwa sana. Inaonyesha kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inajali sana malalamiko ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi aliahidi kwamba, kipande cha kutoka Nyamwage na Somanga kitapatiwa Mkandarasi kabla ya bajeti hii, tungeomba katika bajeti atueleze kwamba kipande hicho kimepatiwa Mkandarasi kwa sababu vipande vingine vyote vinavyobakia tayari kazi imeshaanza, kipande cha kutoka Lindi - Mbwemkulu, Mbwemkulu - Nangurukuru na kutoka Matandu kuja Somanga vipande hivi vyote vina Wakandarasi wanafanya kazi vizuri. Sasa kipande cha Somanga kuja Nyamwage basi tunaomba apatiwe Mkandarasi ili aweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo, naomba kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri Mkuu. Nami nataka nitamke mwanzo kabisa, naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia maeneo makubwa mawili. La kwanza, kuhusu utawala na uongozi na vile vile suala zima la rushwa. Utawala na uongozi bora kwa mtumishi yeyote yule wa umma ni pamoja na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazotawala utumishi wake. Iwe ni Mhudumu wa Ofisi, iwe ni Msimamizi wa Ofisi, Katibu Tarafa, DC, wote sawia. Lakini vile vile sheria na kanuni au taratibu hazibagui. Hata kama ukiwa Mkuu wa Mkoa, vile vile unatawaliwa na sheria, kanuni na taratibu hizo. Sote tunafahamu Mkuu wa Mkoa ni nafasi ya ngazi ya juu sana katika Taifa letu na kwa maana hiyo ni nafasi ya uongozi ambayo kwa kweli haihitaji Utoto wa Mjini. Ni nafasi ya uongozi ambayo inahitaji busara, hekima na uwezo mkubwa wa kuona mbali. Mathalan, kaka yangu, Mheshimiwa Philip Magani, kama akipewa Ukuu wa Mkoa na namwombea apate huo Ukuu wa Mkoa, haitampa heshima kujiona kwamba yeye ni bora kuliko wote Mkoani na kwamba anajua kila kitu na hata pengine kupelekea kudharau viongozi wenzake Mkoani. Lakini vile vile haitampa fahari yoyote kugombanisha ma-DC na Wabunge katika Mkoa wake. Lakini vile vile haitakuwa jukumu lake Mheshimiwa Philip Magani kupanga nani awe na nani asiwe Mbunge katika Mkoa huo na pengine hata kuwapigia debe maswahiba wake ambao anataka wawe Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aisadie sana Mikoa ile ambayo badala ya viongozi kuhimiza maendeleo, wanafarakanisha viongozi na kuwaimbisha taarabu na ngonjera wananchi. Mikoa hiyo itaendelea kuwa duni kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumepata maendeleo hasa katika sekta ya elimu, maji, barabara, afya, utalii na mengineyo. Ni dalili ya wazi kwamba uwajibikaji ndani ya Serikali umeongezeka na pengine kwa kiwango fulani rushwa imeanza kupungua. Lakini ni kweli vile vile kwamba vita yetu dhidi ya rushwa bado ni ngumu na ndefu. Takwimu nilizozipata jana tu kwenye mtandao kupitia *Transparency International* imetoa tathmini

ya hali ya rushwa katika kila nchi hapa duniani. Wao wanatoa alama sifuri kwa nchi ambazo rushwa imekithiri na alama kumi kwa nchi ambazo rushwa haipo kabisa. Kwa mwaka 2002, Tanzania tulikuwa nchi ya 71 kati ya nchi 102 zilizofanyiwa tathmini na sisi tulipata alama 2.7. Mwaka 2003, Tanzania tulikuwa nchi ya 92 kati ya nchi 133 zilizofanyiwa tathmini na tulipata alama 2.5 chini ya kumi. Ukilinganisha na nchi kama Finland ambayo yenyewe ilikuwa ya kwanza na ilipata alama 9.7 chini ya kumi. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba, bado vita yetu ni kali na inabidi tujizatiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ni kweli vile vile kwamba, zipo dalili za baadhi ya viongozi kufumbiana macho na kulindana linapokuja suala zima la rushwa hata pale ambapo ushahidi ni wa wazi kabisa. Kuna mifano mingi tu lakini nitatoa mfano mmoja na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, mkarejee taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi kilichoishia 30 Juni, 2001, katika Wizara ya Maji ya wakati ule siyo ya sasa ambayo imeunganishwa na Mifugo. Kutokana na vitendo vya hujuma vilivyofanywa na Afisa Mhasibu wa Wizara hiyo, Serikali ilipata hasara ya Sh. 716,390,650/= . Hasara hii ilitokana na manunuzi ya *compressor* tatu. Katika taarifa yake Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, alibaini mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, alibaini kwamba Afisa Mhasibu hakufuata taratibu za manunuzi na hata Bodi Kuu ya Zabuni haikuhusishwa hata kidogo. Hata *Memorandum of Understanding* ambayo imesainiwa kati ya Katibu Mkuu wa Wizara na Kampuni ya *Soft Trade* ya Canada ilikosa kile ambacho Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alichokiita *detailed specification for machinery and equipment*. Lakini baya zaidi ni kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amebaini kwamba, bei halisi ya *compressor* hizo tatu ilikuwa ni Sh. 164,144,700/= badala ya malipo ya Sh. 880,535,900/=.

**MBUNGE FULANI:** Maneno hayo.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Hivyo, kulipa Taifa hili hasara ya shilingi hizo 716,399,650/= . Sasa nilikuwa napenda niulize, viongozi wamekuwa wakisitiza lazima pawepo na ushahidi, je, hii taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali siyo ushahidi tosha tena wa uhakika?

**MBUNGE FULANI:** Maneno hayo.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, ili twende vizuri wakati wa kupitisha vifungu vya matumizi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, nataka Serikali ifanye yafuatayo:-

**MBUNGE FULANI:** Lete maneno.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Kwanza, kama taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali siyo ya kweli maana yake amelidanganya Bunge hili kwa sababu taarifa hiyo imeletwa hapa ndani ya Bunge na kama ni hivyo basi, Kamati ya

Maadili ya Bunge imchukulie hatua Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kama taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni sahihi, basi huo ni ushahidi tosha kwamba, Afisa huyo Mhasibu achukuliwe hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuitahadharisha Serikali kwamba, wakati mwingine lazima iwe makini inapowapa ajira kwa Mkataba watumishi ambao wamestaafu na matokeo yake ndiyo haya ambayo yamebainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kushukuru kwa mambo mawili. Kwanza, niishukuru Serikali na hasa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa msaada wa chakula cha njaa ambacho wananchi wa Rufiji wamepata. Lakini nataka niseme awali tu kwamba, kuna baadhi ya Vijiji vitaendelea kuwa na upungufu wa chakula na hasa katika Vijiji vya Kata ya Chumbi, ambako mvua zilikatika mapema na vile vile katika Vijiji vya Kata ya Mwaseni na Ngorongo ambapo wananchi walikimbia mashamba yao kutokana na matatizo ya simba. Lakini vile vile katika baadhi ya Vijiji vya Mbunju na Mbambe katika Kata ya Mkongo vilivyopatwa na mafuriko na mazao yao kwa kweli yameharibiwa na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kuchukua nafasi hii maalum kabisa kuwapongeza Kampuni ya *CelTel* kwa kuwa kampuni ya kwanza kabisa kufikisha huduma ya simu za mkononi Wilayani Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo mimi naamini kabisa kwamba, ndugu zangu Wamakonde, Wasukuma, Wanyamwezi, Wanyalukolo, pamoja na hata rafiki zangu Wamasai, katika kipindi kifupi kijacho watakuwa na uwezo wa kuwasiliana na baba zao Wandengereko kwa kutumia mtandao wa *CelTel*. Lakini vile vile naomba nimshukuru Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, ametuahidi kwamba, huduma za *TTCL* nazo zitaboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MWANAMKUU MAKAME KOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuzungumza machache niliyo nayo juu ya hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea napenda niungane na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu, waliopata misiba mbalimbali kuanzia Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafisishaji, pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na mtoto wake.

Nawaombea dua Mwenyezi Mungu, awape nyoyo za uvumilivu na pia nawaombea marehemu walazwe mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, pia napenda nitoe pole kwa wenzetu waliofikwa na matatizo wakati wa safari zao za kuja huku Bungeni. *Inshallah* Mwenyezi Mungu atawalinda na atazidi kutulinda sote na matatizo haya na mengine Mwenyezi Mungu atuepushe na mwenzetu aliyekuwa bado hajatolewa hospitali Mwenyezi Mungu atamsaidia.

Mheshimiwa Spika, pia baada ya rambirambi hizo na pole napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kushinda katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Bariadi Mashariki pamoja na Madiwani wake saba kati ya wanane. Kwa kweli ni kitendo cha kufurahisha sana. Mheshimiwa Danhi Makanga baada ya kuona hali mbaya na njia aliyopita siyo akaona bora apite njia ya CCM ambayo haina matatizo na kwa kweli tunamkaribisha sana na pia amewazindua macho watu wake wa Bariadi wakaona ukitaka maendeleo upitie CCM, ukitaka amani na utulivu upitie CCM. Kwa hiyo, pia nawaomba wale wenzetu ambao bado hawajafungua macho yao wakaona matatizo humo walimo ingawa wameshaanza kuona, waje CCM tuungane ili tuweze kudumisha maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda pia niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri, waliotangulia kutoa hotuba zao hapa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa hotuba yake na Waziri wa Fedha kwa hotuba yake ya Bajeti. Kwa kweli hotuba ilikuwa ni nzuri, ya kimaendeleo na pia Serikali inastahili kupongezwa sana kwa kupunguza utegemezi kutoka asilimia arobaini na saba mwaka 2002, mwaka 2003 ikaja asilimia arobaini na tano na mwaka huu wa 2004 tukafikia asilimia arobaini na moja. Kwa hiyo, ni jambo la kuipongeza sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Kama mwenyewe Waziri wa Fedha alivyosema hii ni bajeti ya mwenye macho haonyeshwi njia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nikija kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye yeye ni kiongozi wa shughuli zote za Serikali, napenda kwanza nimpongeze yeye binafsi, kwa hotuba yake pamoja na Makatibu wake Wakuu na Mawaziri wake wa Nchi, kwa namna bajeti hii ilivyotufikisha hatua ya kuona mwanga mkubwa sana wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ina mipango mizuri sana yenye lengo la kuimarisha ukuaji wa uchumi wetu na vile vile kutaka kuwaondolea hali mbaya ya kipato wananchi wetu. Lakini hapo hapo tunakosa usimamizi wa uhakika katika shughuli zetu za maendeleo. Hatuna usimamizi, ufuatiliaji wala tathmini ya mipango wala ya maendeleo yetu tunayoyafanya. Naomba nikumbushe vile vile katika nchi yetu na nchi nyingine, lakini katika nchi yetu kuna wale ambao ni wapinga maendeleo waliokuwa hawaitakii mema Serikali yetu hii ya Chama cha Mapinduzi, hufanya hujuma mbalimbali dhidi ya huduma nzuri zilizofanywa na Serikali yetu. Kwa hiyo basi, ningomba nimshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali, tuimarisha sana na tuweka utaratibu madhubuti kabisa katika usimamizi na ufuatiliaji na hata kufanya tathmini ya mipango yetu. Vilevile hata

kufanya tathmini ya maendeleo tunayoyaweka katika Mikoa yetu na katika sehemu zetu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu kuna mifano chungu nzima ya hujuma zinazotokea dhidi ya juhudi nzuri sana zinazofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Mfano wa kwanza, Mbunge mmoja alipokuwa akichangia hapa aliwahi kusema kwamba, yeye alikuwa mmojawapo katika walioshiriki kujenga daraja huko kwenye Jimbo lake kwa shilingi milioni 16. Lakini baada ya muda kidogo likajengwa tena daraja kama lile kwa shilingi milioni 100 na sasa haya ni mambo ya ubadhirifu ambayo ndiyo nataka kusisitizia, usimamizi, ufuatiliaji na kufanyike tathmini ya mambo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Mheshimiwa Mbunge hapa amezungumza akasema habari ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mambo haya kama hatukuyafuatilia yatatuweka mahali pabaya. Jambo la pili, kuna huduma nzuri sana kwa sababu kama tulivyosema kwamba tunakwenda kwa mujibu wa miongozo tuliojiwekea, tunakwenda kwa mujibu wa Ilani yetu ya CCM, tunakwenda kwa mujibu wa Dira ya Taifa ya Maendeleo na tuna mikakati yetu mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa na ni sera zetu zimefanya tuweze kuboresha huduma mbalimbali za kijamii kama afya, elimu, miundombinu, maji na mambo chungu nzima. Hata Serikali imeweza kuondoa kodi pia ambazo zilikuwa kero kwa wananchi.

Vilevile kuna Mifuko mbalimbali ilioundwa ya wafanyabiashara wadogo wadogo, hizi zote ni bidii zilizowekwa na Serikali ya Tanzania. Lakini kutokana na vitendo vibaya vya wenzetu wanajaribu kurudisha nyuma juhudi hizi ili ionekane hakuna juhudi yoyote wala hakuna lolote linalofanyika, lakini ukweli ukidhihiri uongo hujitenga. Sasa hivi juhudi hizi zimeanza kuonekana na Wapinzani walijaribu kusema bajeti hii inafagilia uchaguzi, lakini hata hivyo siyo ya kufagilia uchaguzi kwa sababu bidii zote hizi zinazoonekana zimeanza muda mrefu sana. Kwa mfano, katika elimu zamani ilikuwa mtoto wako haingii darasani kama huna ada ya kumlipia kwanza, lakini sasa hivi watoto wetu wote wenye umri wa kwenda shule wanakwenda shule bila matatizo na vilevile kuwafikiria ambao wako katika hali ya umaskini. Kwa hiyo, hizi ni juhudi na mambo mbalimbali yaliyofanywa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kutokana na matatizo hayo ya wenzetu waliokuwa hawaipendelei Serikali yetu, basi Serikali ijaribu kuweka ufuatiliaji imara na kufanya tathmini katika shughuli hizi. Kwa mfano, kuhusu Hospitali ya Muhimbili iliporudishiwa uwezo wake wa kuwa Hospitali ya Rufaa, hapa kama sikosei na niko tayari kusahihishwa. Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa akieleza hapa alieleza kuwa, baada ya kutoa hizo shilingi 10,000 kwenye mapokezi pale basi tiba na dawa na mambo mengine tena itakuwa ndiyo zile zile shilingi 10,000/= lakini sivyo ilivyo. Kwa hiyo, kama nimekosea niko tayari kusahihishwa lakini namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kulieleza hili ili wananchi waweze kufahamu na haya mambo yakomeshwe ya kurudisha nyuma maendeleo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze upesi upesi habari ya shughuli za kilimo, mambo ya ukame na ukosefu wa chakula. Kwa kweli suala hili la kilimo kwa hapa nchini kwetu naliona bado halijapewa uzito wa kutosha hakuna mpango katika kilimo. Mipango iko kwenye makaratasi lakini bado hatujaweza kusukuma mbele kwa sababu toka niingie mimi Ubunge miaka ya 80 kilimo hakijapewa msukumo. Tulianza na kilimo cha bega kwa bega mpaka kikaja kilimo cha kufa na kupona afadhali hiki kilimo cha kufa na kupona walichukuliwa watu kutoka Mikoani sijui kama ilikuwa katika Mikoa yote au vipi, lakini kwangu Pemba walichukuliwa watu wakapelekwa Mikoani sijui kama Iringa au Mbeya, wakaenda wakafundishwa kilimo cha ngoro angalau hiki kilimo cha kufa na kupona na ilikuwa kufa na kupona kweli kwa sababu matuta ya ngoro ni matuta makubwa sana.

Lakini hata hivyo, waliweza kurudi nyumbani na wakafundisha wenzao na kilimo kile kikaimarishwa. Lakini baada ya hapo tukasema kilimo ni uti wa mgongo kikaanza kudidimia na sasa hivi kilimo ni sekta kiongozi. Nasema hivi kwa masikitiko kwa sababu juzi nilimsikia mwenzangu mmoja ambaye walikwenda safarini huko hivi karibuni, akasema sisi kwetu tukisema kwamba tuna njaa hapa kwa kweli ni jambo kama la kukufuru, kwa sababu wenzetu wana jangwa kule na wameweza kuimarisha kilimo na wameweza kupanda mazao yao vizuri sana, sisi hapa tuna mvua, tuna maziwa makubwa makubwa, tuna mito na mambo chungu nzima lakini bado kilimo chetu ni kilimo kinachosuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye ndiye Kiongozi wa Serikali hili suala la kilimo ambayo ndiyo sehemu kubwa ya ajira ya Watanzania iimarishwe watu wetu wapumzike kutumia majembe madogo madogo ya mikono, wanaanze kutumia zana za kisasa angalau hata kama matrekta na vilevile pembejeo. Kwa hapa pembejeo zinagawiwa lakini utaona inafika wakati wa kutumia zile pembejeo zenyewe hazijafika Mikoani kunakohusika. Kwa hiyo, mambo haya lazima kwa sababu ni mambo ya msimu tuweze kuyapeleka kule kwa muda unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna hii tu kilimo hakiwezi kuimarika na tutakuwa tukizungumza kilimo kwa muda mrefu. Sasa hivi ni miaka mingi sana tunazungumzia habari ya maendeleo ya kilimo na kila mwaka tunaongeza bajeti katika Wizara ya Kilimo na Chakula lakini bado tukitazama kilimo kiko vilevile, wanaolima ni wale wale wanawake na majembe wanayotumia ni yale yale ya mikono, hakuna maendeleo katika kilimo ambacho ndiyo Sekta muhimu kuliko sekta zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi kazi yangu ni kusisitiza tu kwamba, sasa tuache kufikiria mambo au mipango kwenye karatasi hasa mipango muhimu kama hii sasa tufanye mambo haya kwa vitendo ili tuweze kujiimarisha kama wenzetu walivyoimarika hao tunaowasikia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kwanza nami nitoe pole kwa wenzetu waliopata msiba, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mpendwa, Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, *Amina*.

Mheshimiwa Spika, pili naomba nitoe pole kwa wale wote waliopata matatizo, Mheshimiwa Anne Kilango, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, akiwa hospitali pole zangu naomba zimfikie sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri, yenye kina cha kueleweka kwa kila mmoja. Pili, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kufanya ziara katika Mkoa wa Tabora. Nampongeza sana ziara yake ilikuwa ni nzuri ambayo ilileta chachu ya maendeleo katika Mkoa wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nichangie kwanza katika sehemu ya kilimo cha tumbaku Mkoani Tabora. Waziri wa Kilimo na Chakula, alikuja kufungua soko letu la tumbaku Wilaya ya Urambo Kaliuwa na aliona jinsi wakulima wa tumbaku wa Tabora walivyojitahidi kwa kilimo hicho na mafanikio yaliyopatikana kwani katika soko lile wakati huu soko limepanda au bei ya tumbaku imepanda zaidi. Lakini kitu kimoja tu ambacho bado kinatusikitikisha katika Mkoa wa Tabora ni kutokuwa na kiwanda cha tumbaku katika Mkoa wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala hilo linatusikitisha sana kwa sababu ni sawa na Mkoa wa Mwanza kuwa na Ziwa wakawa na kiwanda cha samaki pale, lakini huwezi kukitua Mwanza kiwanda cha samaki ukakiweka Tabora, ni sawa na Tabora kutunyima kiwanda cha tumbaku kwa sababu Tabora ni wakulima wanaolima tumbaku kwa wingi sana. Kiwanda kimeenda Morogoro sisemi kama kihame Morogoro angalau na Tabora kiwepo kiwanda kingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kutuangalia kwa macho mawili Mkoa wa Tabora, atuwekee kiwanda kwa sababu sisi tunalima tumbaku na pale kitakapojengwa kiwanda cha tumbaku vijana wetu waweze kupata ajira katika kiwanda kile cha tumbaku ili kiweze kusaidia wananchi wa Mkoa wa Tabora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza kabisa nilipoingia katika Bunge hili mwaka 2000 niliuliza kuhusu kufungwa kwa kiwanda cha nyuzi Tabora. Namshukuru Naibu Waziri wakati ule alikuwa Mheshimiwa Anthony Diallo, alinijibu vizuri na nikapata matumaini kuwa kiwanda kile yule mwekezaji aliyekichukua ametoa *ten percent* amefutiwa *ten percent* yake na kiwanda hakijapata mtu kinatangazwa upya. Lakini mpaka sasa kiwanda kile bado hakijafunguliwa na sisi wananchi wa Tabora hatujajua hatma ya kiwanda kile. Lakini bahati nzuri katika utaratibu wa kuchangia kwa



maandishi kwenye bajeti, nami nilichangia na ninashukuru Mheshimiwa Waziri alinijibu kwa maandishi. Nina imani kuwa utaratibu huo ni mzuri sana na ninakupongeza sana Mheshimiwa Spika. Baada ya kunijibu kwa maandishi walisema kuwa kiwanda hicho kimeenda *LART* kwa ajili ya mfilisi, ambayo majibu yake ninayo hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini bado napata wasiwasi mkubwa, *LART* yenyewe muda wake unakwisha, kama muda unakwisha hiki kiwanda hatma yake itakuwa mpaka wakati gani, kwa maana hiyo utaratibu wa mfilisi utachukua kama mwaka mzima na hiyo itatuletea matatizo sana kwetu, maana mpaka hivi sasa tuna miaka karibu mitano au zaidi ya miaka saba kiwanda kile hakijafanya kazi. Kwa hiyo, tunaomba sana wananchi wa Tabora kiwanda kile kiweze kufanyiwa utaratibu nasi wananchi wetu na vijana waweze kupata ajira kwa sababu hatuna kiwanda hata kimoja, basi angalau hata hiki kimoja kiwepo na kiweze kufanya kazi ili wananchi waweze kupata ajira na kiweze kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, sisi Waheshimiwa Wabunge tunapata matatizo sana kwa kiwanda hiki. Kwa sababu wananchi wao wanajua kuwa hatukisemei kiwanda hiki wala hatukishughulikii, kwa hiyo, tunaomba sana sana kiwanda hiki Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kukisemea na kukitolea tamko ili kilete mafanikio katika Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kwanza naomba nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa wa Tabora. Mkuu wa Mkoa wa Tabora kwa kweli mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Amejitahidi sana katika kufungua barabara yetu ya Dodoma - Itigi - Tabora, ambayo ni barabara fupi sana. Hivi sasa ninavyoongea najua saa hizi mabasi yapo barabarani yanatoka Dar es Salaam kwenda Tabora na yanasafiri kwa siku moja tu na mabasi mengine yanatoka Tabora kuja Dodoma mpaka Dar es Salaam. Lakini sasa Serikali inatusaidia vipi kututengea fedha kwa ajili ya barabara hii na sisi tunaomba Mkoa wetu ufunguke kwa barabara hii, hatukatai pia inaweza pengine ikawa ni uzito kwa sababu mnasema tuna reli, lakini matatizo ya reli wote tunayajua na tunaona mambo yanayofanyika. Wafanyabiashara wanapopata barabara ya kupitisha mabasi yao kwa ajili ya kuwasaidia wananchi ili waweze kupata usafiri kwa urahisi inakuwa ni bora zaidi kwa wananchi ambao wengine ni wafanyabiashara watakaokwenda Tabora kufanya biashara na watakaokwenda Dar es Salaam kufanya biashara, barabara ile inapotumika kiurahisi inakuwa ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu barabara hiyo saa 12.00 alfajiri ukitoka Dar es Salaam saa mbili za usiku unafika Tabora. Kwa kweli tumpongeza sana Mkuu wa Mkoa pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano wao ambapo wamejitahidi mpaka kufikia hapo. Lakini itakuwa na maana nzuri zaidi kama Serikali itatusaidia kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami hata muda wa saa nane au 12 nina imani utapungua zaidi ili wananchi waweze kupata usafiri kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nachukua nafasi hii kuwapongeza wale wenye mabasi wote ambao wamejitokeza kuweza kusaidia wananchi kuwasafirisha kutoka Dar es Salaam mpaka Tabora kwa sababu hiyo barabara bado haijawa kwenye hali nzuri pamoja

kwamba haijawa kwenye hali nzuri lakini wamejitahidi kutoa mabasi yao, hiyo yote ni moja ya upendo wa wananchi na kuweza kusaidia Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani hilo limeeleweka na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi atalielewa na kulifanyia kazi kwa sababu tunamwelewa uelewa wake na jitihada zake na Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Waziri Mkuu, akiwa ni kiongozi Mkuu wa Serikali, nina imani barabara hiyo itaweza kuangaliwa kwa macho yote ili tuweze kupewa fedha za kuitengeneza barabara ile kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilio changu kingine kitakuwa ni kilio cha mikopo kwa akinamana na vijana. Mikopo kwa vijana na akinamama, Halmashauri zinatenga asilimia 10 lakini Halmashauri hizo zinapata matatizo baada ya kuwa kuna kodi ambazo zimefutwa na kama kuna kodi ambazo zimefutwa bado wanasumbuka asilimia 10 wataitengaje kwa hiyo inakuwa ni ngumu kidogo. Lakini bado kuna uwezekano pia wa kutumia *PRIDE* ambayo kwa kweli ninaipongeza sana *PRIDE* kwa kujitahidi kusaidia wananchi wengi ambapo si wanawake peke yao wala si wanaume, tumeona maadhimisho ya miaka 10 ya *PRIDE* na Mheshimiwa Basil Mramba, alikuwa ni mgeni rasmi pale, tumeona ni nini ambacho wananchi wameendelea kwa kutumia *PRIDE*. Kwa hiyo basi, tunaweza tukatumia njia hiyo ya *PRIDE* hata wananchi wetu wakulima wadogo wadogo kupitisha fedha zao za pembejeo kwenye *PRIDE* kwa sababu wao wana utaratibu mzuri ambao wao wenyewe kwa wenyewe wanakabana huko na kuweza kulipa deni. Kwa hiyo, naomba sana hii *PRIDE* tuweze nayo kuiangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni matatizo ya walimu. Bunge lililopita la bajeti pia nililalamika kuhusu mishahara ya walimu. Mheshimiwa Said Juma Nkumba yeye alilia kuhusu Mwenge na mimi nililia kuhusu mishahara ya walimu na Mwenge, ukaenda kuwashwa Tabora ukafika mpaka Sikonge. Lakini mimi tatizo langu nililolisemea kuhusu mishahara ya walimu kwa kweli naona bado halijatekelezwa. Kwa hiyo, katika Bunge hili hicho pia nami ni kilio changu tena cha kulilia mishahara ya walimu waweze kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maswali mengi ya Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni yanayoulizwa ni kuhusu mishahara ya walimu na marupurupu yao na Waheshimiwa Mawaziri wamekuwa wakijibu vizuri sana kuhusu mishahara hiyo. Lakini tatizo liko sijui ni sehemu gani, ikiwa fedha hizo zinatoka Hazina utaambiwa zinatoka Wizara ya TAMISEMI, utaambiwa tatizo liko Utumishi au kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu au Wizara ya Elimu na Utamaduni. Naomba nikushauri Mheshimiwa Waziri Mkuu sisi tunapenda au mimi ninapenda miaka yako 10 uliyokuwa kwenye Uwaziri Mkuu usiondoke na dosari ya aina yoyote. Kwa hiyo, kama kuna sehemu ambayo ina tatizo naomba hili la mishahara ya walimu ulifuatilie zaidi ili liweze kukukosha wewe au pia ikiwezekana uunde Kamati au Tume itakayokwenda kusimamia tatizo hili liishe. Wako ambao wanashindwa kukueleza hili lakini mimi nimeona bora nikueleze kusudi uwe safi, watasubiri wakati unaondoka waanze kutoa kasoro na sisi vijana wako wa Chama cha Mapinduzi hatutopenda kasoro hizo ziwepo. Tunajua Mheshimiwa Waziri

Mkuu wetu ni safi, kwa hiyo, tunapenda uendelee kuondoka katika hali nzuri ya usafi bila tatizo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu suala la UKIMWI. Suala la UKIMWI ni tatizo kubwa katika maisha yetu, lakini katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ukurasa wa 78 na 79 imeorodheshwa Mikoa yote ambayo inapata fedha za uhamasishaji kuhusu UKIMWI kwenye Wilaya, lakini kwa nini kuna Wilaya nyingine zimepata fedha zote na Mikoa mingine ni Wilaya mbili tu zimepata, kwa mfano, Mkoa wa Iringa kwenye Wilaya kuna fedha nyingi zaidi kuliko Wilaya zote ambazo zimeorodheshwa?

Pamoja na kuwa wanasema sehemu hizo zina UKIMWI mwingi lakini naona takwimu pia zina matatizo yake, pamoja na kuwa sehemu hizo zina UKIMWI lakini naomba fedha hizi ziweze kufuatiliwa na kujua kwa nini Mikoa mingine mfano Mkoa wetu wa Tabora zimepewa Wilaya mbili tu. Kwa hiyo, basi tunaomba Wilaya zote za Mkoa wa Tabora ziweze kupata fedha na sisi tuweze kwenda kuhamasisha katika Mkoa wetu matatizo yaliyokuwepo ni ya wote na ni janga la dunia nzima si ya sehemu moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niwe miongoni mwa wale ambao wamechangia hotuba hii ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia hotuba hii, naomba nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kuchangia kwa kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kufiwa baba yao mpendwa, kwa kweli tunatoa pole sana na naomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba pia nitoe pole kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu, waliopata matatizo mbalimbali akiwemo Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Estherina Kilasi na kaka yetu, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa matatizo yaliyowapata.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi mkubwa alioupata, sisi tunasema ni ushindi wa kishindo, kwa kweli tunampongeza sana. *(Makofi)*

Sasa baada ya kusema hayo, naomba nianze kuchangia hotuba hii. Lakini kabla sijaanza kuchangia nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri. Nilikuwa nakipitia kitabu hiki na nikawa najaribu kubadilishana mawazo na baadhi ya wageni wetu wanaotutembelea hapa kuja kusikiliza Bunge hili kwamba wenzetu mnaionaje bajeti hii, kwa kwa kweli wanasema ni nzuri. Sasa nachukua nafasi hii ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini pia ninawapongeza sana watendaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu wakiongozwa dada yangu

mpendwa, Ndugu Rose Rugembe. Ndugu Rose Rugembe anafahamika kwamba yeye ni mchapakazi maana tulikuwa naye wakati akiwa Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana kwa kweli mimi ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwa ujumla niwatoe wasiwasi kabisa Waheshimiwa Mawaziri wote kwamba, mwaka huu bajeti zenu zote mlizomba zitapita bila kupingwa tena kwa asilimia kubwa kabisa. Kwa nini zitapita bila kupingwa? Mimi ninakumbuka tulipoingia hapa mwaka 2001, tulikuwa na kiu kubwa ya maendeleo. Kwa hiyo, kuanzia mwaka 2001 michango ambayo Waheshimiwa Wabunge tulikuwa tukiichangia hapa ilikuwa ni ya kulalamika na ilikuwa ni ya kuelezea yale ambayo tumetumwa na wananchi wetu. Lakini kuanzia mwaka 2001 mambo yamefanyika, mwaka 2002 mambo yameongezeka na mwaka 2003 hivyo hivyo. Sasa kwa mwaka huu tuko katika ukingo wa kuhitimisha katika kutekeleza Ilani ya Chama Tawala na yamefanyika kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, wenzangu waliochangia sipendi nirudie, wamezungumzia mambo ambayo yamefanyika Majimboni kwao na mimi hivyo hivyo Temeke na mwaka 2003 nilichangia kwamba, kuna vitu vinaoteshwa kule kama uyoga unavyoota porini, majengo mazuri yamejengwa kule Temeke ikiwemo Manispaa yetu ya Temeke kwa kweli kwa nchi nzima niliwahi kupongezwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, hakuna Halmashauri ambayo imejenga jengo zuri kama Manispaa ya Temeke. Hizi zote ni kazi na tulikuwa tukitekeleza Ilani ya Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, sasa ndiyo maana nimesema kwamba, Waheshimiwa Mawaziri wasiwe na wasiwasi, kwa mwaka huu bajeti hizi tunazipitisha bila matatizo kwa sababu tayari tunajiandaa kuja kusimama tena mwaka kesho kwa ajili ya kuwamba wenzetu wakipe mamlaka ya kuendelea kutawala Chama hiki.

Baada ya pongezi hizi, leo nina jambo moja tu la kuzungumza. Kwa nini ninasema nina jambo moja, mambo mengi yameshafanyika na jambo lenyewe si lingine bali ni suala la Uwanja wa Taifa. Umekuwa ukitania kwamba kila nikisimama, unaniambia usije ukasema Uwanja wa Taifa ni kweli. Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakuwa mashahidi kwamba toka nimeingia hapa Bungeni nimekuwa nikiimba wimbo wa kuzungumzia suala la Uwanja wa Taifa. Sasa naomba nichukue nafasi hii kurudia tena na tena kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa busara wa kutoa ahadi ya kwamba kabla hajamaliza muda wake wa uongozi atahakikisha uwanja mzuri na wa kisasa unajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naomba leo niseme siri moja kwa sababu tunakwenda ukingoni. Sisi Temeke tuliposikia maneno hayo yametamkwa na wananchi wangu wakiwa wamenichagua mimi kuwa Mbunge wao wazee wa Temeke walinituma wakaniambia Mheshimiwa Mbunge tumesikia Rais ameahidi kujenga uwanja. Walinituma mambo mawili na kwa kweli niliyafikisha kwa Rais Mheshimiwa Sarungi atakuwa shahidi siku ya kwanza kabisa kumfikishia ujumbe huu Mheshimiwa Rais. Jambo la kwanza lilikuwa ni suala la Uwanja wa Taifa. Waliniomba wazee wa Temeke kwamba utakapokutana na Mheshimiwa Rais jambo la kwanza nenda umuombe kwamba

wazee wa Temeke wanaomba ahadi yake ya Uwanja wa Taifa wa kisasa uyoga huu uote ndani ya Temeke. Kwa kweli nilifanya hivyo. *(Makofi)*

La pili walinituma kwamba Mheshimiwa Rais ameamua kwa makusudi kila mwezi atoe hotuba yake kupitia vyombo vya habari wakasema wanaunga mkono sana maamuzi hayo. Lakini waliniomba sisi kama wazee mara nyingi tunapenda kukaa na viongozi wetu ili tuweze kutoa ushauri mbalimbali. Kwa hiyo, tungemshauri Mheshimiwa Rais kwamba baada ya kutoa hotuba zake kwenye vyombo vya habari wengine hatuna vyombo hivyo ila tunavyo tunaweza tukawa na tatizo la umeme ama betri. Kwa hiyo tulimwomba apate muda wa kukutana na wazee kwa kubadilishana nao mawazo. Maneno haya niliyafikisha kwa mara ya kwanza kwa Mheshimiwa Rais. Kwanza niliandika barua ya kumpongeza kwa uamuzi wake wa busara na nikapeleka mawazo niliyokuwa nimetumwa na wazee wangu kutoka Temeke. Mheshimiwa Rais aliipokea barua hiyo na anayo ofisini kwake mpaka hivi sasa. *(Makofi)*

Lakini kwa mara ya pili nilikutana naye katika ukumbi wa Karimjee siku hiyo tulikuwa na kikao cha chama. Pale niliongea kumueleza nimetumwa na watu wa Temeke kuhusu suala la Uwanja wa Taifa. Haya yalikubalika. Lakini lingine nilifanya kazi ya kukutana na Waziri Mkuu na ndiyo maana nimesema mimi katika hotuba yake mambo yote yaliyomo humu ninayaunga mkono lakini bado nimeona nizungumzie suala la Uwanja wa Taifa kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu amenipa ushirikiano mkubwa sana katika kuhakikisha suala hili linakubalika uwanja huu uoteshwe ndani ya jimbo la Temeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu mniunge mkono katika hili ndugu zangu ili uwanja huu uendeleekubakia pale. Imenibidi niseme leo ni juzi juzi tu kuna mwenzangu mmoja nisingependa kumtaja amezungumzia kwamba anashangazwa kusikia uwanja unajengwa tena pale mbona pale uko mwingine upelekwe Kibaha. Nikasema duu!!! Kwa kweli ninamsikitikia kwa sababu amechelewa.

Ameshachelewa huwezi ukatenga fedha bila kujua mahali gani unataka kwenda kujenga uwanja haya mambo yalishafanyika siku nyingi. Juzi Mheshimiwa Rais amepokea fedha Dola za Kimarekani 56.4 milioni kwa ajili ya kujenga uwanja huu. Sasa asingeweza kuzipokea fedha hizi bila ya kuwa na michoro. Michoro huwezi kuipata bila ya kujua kwamba uwanja huu unaoteshwa wapi, uwanja unajengwa Temeke. Kwa hiyo nilikuwa naomba wazo la kuhamisha uwanja huu halipo Rais alishakubali kwamba utajengwa pale. *(Makofi)*

Mimi naomba niseme kama Mkuu wangu Mkoa Mzee Makamba leo yuko hapa huwa ana usemi mmoja anasema: “Tusigombanie kito wakati tunajenga nyumba moja”. Yuko pale. Kwa hiyo katika suala la uwanja hili, uwanja unajengwa Tanzania na sio Kenya wala Uganda. Kwa hiyo tukubaliane na mimi uwanja ule uote pale kama kutakuwa na mafungu mengine basi tutajenga Mwanza, Tabora, Lushoto huko kwa Mheshimiwa Makamba na kila sehemu tutajenga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nilikuwa na hilo la kusema lakini naomba nirudie kusema naunga mkono hoja bajeti hii ipite kwa asilimia mia moja na bajeti za Mawaziri wote zitapita kazi nzuri inafanyika. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikushukuru kwa kuniwezesha niweze kusema machache ambayo nimejiandaa. Nayo yatahusu sehemu ya mbolea, Walimu na majengo ya nyumba zilizowekwa X Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kutoa salamu zangu za pole kwa wenzetu waliofiwa na ndugu zao hasa wazazi. Pia naomba niwape pole jamaa zangu waliopata mikasa ya ajali na pia kuvamiwa na majambazi na pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kurudi tena Bungeni nafahamu ubora wake wa kazi kwa hiyo CCM tumefaidika pia. Lakini pia naomba nimpongeze Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na nampongeza yeye pamoja na Ofisi yake wakiwemo Mawaziri wa Nchi, pamoja na Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ningependa kueleza yafuatayo. Mwaka jana Serikali ilitangaza bayana na uzuri wananchi wanasikiliza sana vyombo vya habari. Ilitangaza kwamba mikoa minne ya Kusini itapewa mbolea ambayo itakuwa na ruzuku. Watu tumeshangilia humu ndani nadhani tulipiga na vigelegele. Tulipokwenda kwenye ziara katika eneo lile tulikwenda kuwaeleza wananchi lakini tulikuwa tunaeleza tu kwa sababu na wao pia walikuwa na shauku kubwa sana ya uamuzi mzuri wa Serikali kupeleka mbolea yenye ruzuku. Tulijieleza lakini maswali waliyokuwa wanatuuliza:“Mheshimiwa Mbunge mbolea itakuja lini”. Unawaambia aah hili ni la utendaji. Mheshimiwa Mbunge mbolea itauzwa kwa bei gani? Unawaambia na hili pia ni la utendaji. Mheshimiwa Mbunge utaratibu utakuwaje wa kupeleka mbolea hiyo. Nayo unawaambia aah hayo ni ya utendaji, nyie mlivyosikia kwenye redio na mimi ndiyo hivyo nasema.

Kwa hiyo, wakatusikiliza, wakatuheshimu, wakaiheshimu Serikali wakaona sasa mambo yote yamekuwa salama. Bahati nzuri Mwenyezi Mungu wenzangu wanalia njaa sisi tulipata mvua nzuri sana. Watu wakalima sana, walilima sana wakijua kwamba tutakuwa na mbolea ambaye ina ruzuku. Huo ulikuwa mwezi Agosti, Septemba ukapita na kule kwetu usipoweka mbolea mwezi Septemba na Oktoba mambo mengine yote inakuwa kama umefanya kazi ya bure. Ukafika mwezi wa Septemba, Oktoba, Novemba na Desemba. Wale wauzaji wa mbolea walikuwa wana wasi wasi kwamba itakuweco mbolea nyingi sana yenye ruzuku na watakosa soko. Bahati mbaya kwetu sisi lakini ni nzuri kwao walifanikiwa wakauza yote ikaisha. Ilipofika Februari ndiyo mbolea ya Serikali yenye ruzuku ndiyo ikaanza kufika na ilifika chini ya tani 20,000. Tani 20,000 Wilaya ya Njombe peke yake haitoshi. Sasa mbolea hii ilikuwa kwa mikoa yote minne. Kwa hiyo, huu ukawa utani wa kwanza ndio huo. Ilikuwa utani kwa sababu wakulima waliwekewa matumaini lakini hakukuweco mbolea tani 20,000 kwa mikoa minne ni kama utani kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Njombe wanakotumia mbolea kwa wingi sana ni jimboni kwangu Njombe Kusini lakini mbolea ikawekwa Makambako kwa hiyo wale wanawaita mawakala wanachukua mbolea kutoka Makambako kupeleka kule Njombe Kusini haikuwezekana gharama zake zilikuwa zimerudi pale pale. Sio siri mimi Mbunge ilinibidi nikope mafuta ya kumwezesha huyo aliyekuwa Muwakala asambaze Kata sijui mbili na ingawa hawakupewa ya kutosha. Kwa hiyo ziara yangu ya safari hii kabla ya kuja huku maana yake ni lawama lawama. Mkuu wa Wilaya akaenda kuomba radhi kwa wananchi kwa niaba ya Serikali. Jamani Serikali ilikuwa na nia njema lakini ndio Wananchi hawakupata mbolea, hawakupata mbolea.

Kwa hiyo, wale ambao walilima hawakupata mazao kwa sababu walikosa mbolea. Bahati mbaya sana ile mbolea iliyokuja kidogo ilisambazwa kwa muda wa wiki moja tu. Kwa hiyo, wale wauzaji wa mbolea wakaona kabisa kulikuwa na vacuum ya mbolea, hakukuwa na mbolea. Nakwambia ninavyozungumza leo Njombe mbolea mfuko mmoja unakwenda mpaka shilingi 30,000 wakati kabla ya tangazo la Serikali tulikuwa tuna-range kati ya shilingi 9,000 mpaka 12,000. Sasa shilingi 30,000 mpaka 35,000. Kwa sababu kulikuwa na vacuum wale wauzaji wa kawaida waliileta mbolea kwa haraka express kwa hiyo wakapandisha bei mara tatu.

Juzi Waziri wa Fedha tena ametangaza kwamba Serikali itakuwa ina-subsidize mbolea usafirishaji. Jamani tusifanye utani. Ku-subsidize usafiri wa mbolea ni tani ngapi mnazozitungumza. Ni tani ngapi mnazozitungumza mpaka ku-subsidize usafiri. Mimi nina uhakika kwamba mbolea kule haitashuka tena. Wakati kumbe tungeacha ile market force ipambane yenyewe na kutoa fedha nyingi kwenye hizi mnazoita fedha za kununulia mbolea.

Mimi nadhani ingekuwa vizuri zaidi watu wangekopa na watu wanashindana wenyewe na *market force* ingekuwa ina *balance price*. Sijaelewa hiyo mnayosema na sasa mtaitoa ni tani ngapi na mtakwenda wapi, mtaigawa vipi? Maana nazungumza kutokana na experience sizungumzii hadithi. Tunalo tatizo mimi sielewi kama ni bilioni 2 mnayosema basi mmefanya utani mwingine. Kama ni shilingi bilioni 2 ku-subsidize usafiri kwa mbolea zote mnazotazamia mikoa hiyo minne mimi nakwambieni tumefanya utani mwingine.

Kwa hiyo mimi napendekeza kwamba mradi nyie mmewaleta Wakuu wa Mikoa wako hapa hawa Wakuu wa Mikoa hiyo watakaopewa subsidize wakae na Waziri Mkuu wakwambie ukweli kama wao watakuogopa kusema ukweli mimi kama mwanasiasa nabeba lawama hii haiwezekani na mmefanya kitu kisichowezekana wakae hapa basi wakuambie ukweli itawezekana vipi na watuambie nini tukawaambie wananchi nini cha kusema tena safari hii ya pili. Sina cha kusema. Nitakwenda kuwaambia nini kwa sababu hali iliyokuwa ya mwaka jana ni aibu. Kwa hiyo, mimi nafikiri hilo ndilo pendekezo langu Waziri Mkuu ukae na Wakuu wako wa Mikoa wakwambia hiyo subsidize waliyopewa ya usafiri kweli itakuwa na kitu chochote cha maana ama ni tatizo tupu lingine.

La pili ningependa kusema hata haidhuru wenzangu wamesema lakini mimi nasema safari hii kwa sababu nilipokuwa nafanya ziara nimeishi kwenye nyumba za Walimu wa Sekondari wengine Walimu wa Msingi nikienda kukaa kule huwa nalala huko. Nimefanikiwa kila ninapomaliza mikutano mikubwa ya hadhara nimekaa jioni na Walimu. Hivi ninavyozungumza nina makabrasha yote ya mishahara ya Walimu ambayo hawajapewa mpaka leo toka wengine wameajiriwa inafikia kutetemeka kwa sababu siwezi kuelewa. Nimewaona kabisa wasichana hawa wamekaa hao wanaoelezwa wasichana, mtoto wa kike ameajiriwa kule toka mwezi Januari hana mishahara wowote shuleni kule sekondari, jamani. Jamani nafikia kutetemeka. Alikuwa anaishije miezi yote toka alivyoajiriwa. Yaani nazungumza siyo makabrasha yote tuliyonayo hapa ninayo kule kwenye gari yangu nina bahasha mtawapelekea wanaohusika sasa sijui nani. Nimepata faida hapa kwamba Serikali ilikuwa inapeleka fedha lakini zilikuwa zinaliwa huku na sijui na Wakurugenzi na nani! Ndiyo nimesema kuna barua hizi hapa kuna barua hii moja hapa. Katibu Mkuu wa Fedha anaeleza kwenye kabisa majedwali jinsi walivyopeleka hizo fedha zimekwenda wapi sasa! Jamani sio kama nasimulia hadithi haya ndiyo niliyosikia mwenyewe. Katika ziara yangu nafanya ziara zangu na mikutano, jioni nakwenda shuleni tunaongea mpaka usiku wa saa sita na wamenipa yote. Wale waliopandishwa vyeo hakuna chochote. Wamepewa cheo toka wamepewa cheo hawakupewa mishahara ninayo mafaili kule. Ninazo barua zao. (*Makofi*)

Sasa jamani mimi nasema tuko makini sana tunasema Utawala Bora. Mimi najua Utawala Bora ni kuzingatia sheria zote tulizotunga wenyewe na kuzifuata. Kwa upande wa Serikali na kwa upande wa raia. Haiwezekani Utawala Bora maana yake raia wenyewe wasitendewe haki ya Serikali hapa hakuna. Utawala Bora. Hakuna Utawala Bora kama watu wasipewe fedha zao wanapandishwa vyeo hawajapata kitu. Sio Utawala Bora jamani. Na inatisha sana. Kwa hiyo mimi ninayo mafaili naweza kukupa. Waziri Mkuu naungana na Mheshimiwa Aziza kila mtu katika maisha yake alipopata madaraka afanye jambo moja tu ambalo watu watakumbukwa nalo. Waziri Mkuu ukumbuke kwa kumaliza matatizo ya Walimu. Ukumbukwe kwa hili walipwe lumpsum fedha zao zitoke ni haki yao, sio waanze kusema sijui watapewa watapewa zote wanazodai huko walikopa hata watalipa lini mkiwapa kidogo kidogo wapate fedha zao zote ni haki yao wala sio kitu kingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nilitaka kusema nashukuru Serikali kwa kuamua kwamba zile nyumba zilizowekewa X ni kama hakuna barabara inayojengwa basi watatumia muda wao kujaribu kujenga nyumba nyingine mahali pengine. Waziri Mkuu naye amelisema hili. Lakini kwa Njombe naomba tulishughulikie hili suala kinamna yake. Sio kwamba walijenga kinyume na sheria. Nyumba zile zilijengwa katika Mtaa wa Njombe kabla mimi sijazaliwa. Wakaja hawa wakoloni wakatathmini barabara. Wakazisogeza zile nyumba pembeni mwa barabara mwaka 1947. Mwaka 1956 tena Serikali ikaja hiyo hiyo ya wakoloni ikachora ramani nyingine hapa zilipojengwa nyumba za sasa. Nyumba nyingine zilizojengwa kabla mimi sijazaliwa. Sasa wamewekewa X. Mimi nakubaliana na uamuzi ni kwamba waweze kupata muda wajenge nyumba nyingine na wenyewe wanasema hivyo hivyo. Lakini bado wale watu wana haki yao hiyo mnayoita *trunk road* haitakuwepo.



Kwa hiyo, naomba kwa hili niombe Waziri anayehusika kuna Kamati imeundwa tumwone na mimi nikiongoza ujumbe huo tueleze kwenye kesi yetu hiyo wakati tunakubaliana kwa sababu kikatiba tuna haki kwamba zile nyumba tulijenga kabla ya sheria zote hizi. Kwa hiyo, si suala la kusema kwamba itakapofika wakati basi watabomolewa. Haki yetu sasa hivi ipo tuliitumia sheria na *master plan* zote hizo zipo. Nyumba zile zilizokuwa nje ya sheria zilibomolewa mwaka 1956 zipo. Hiyo sheria mnayozungumza ya mwaka 1967 nimi nazungumzia ile ya mwaka 1956 zipo.

Kwa hiyo, *main road* haikuweko. Kwa hiyo mimi naomba kabisa hili suala tuwe na msimamo watu wajue kabisa wana haki yao ili sasa wajiandae kujenga huko kwingine. Tukifika hapo hakuna ugomvi lakini kwamba jumla tu wale hawana makosa kwani *main road* ya kwenda Songea haikuwepo mwaka 1956. Ni mwaka 1956 ndiyo mara ya mwisho *master plan* ya Njombe ilifanyika na nyumba zikatambuliwa zilizojengwa ndani ya barabara zikabomolewa sheria ya mwaka 1967 ni ya karibuni haihusiani na hawa. Kwa hiyo, naomba sana hapa msimamo wa Serikali ujulikane halafu wenyewe watakubali kuendelea kujenga huko nyumba za kwao lakini haki yao ipatikane.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia. Pia nimshukuru Waziri Mkuu na nimpongeze kwa hotuba yake nzuri yenye dira ya mwelekeo na yenye sura ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa kusimamia kikamilifu mradi wa gesi ya Songosongo na kuifikisha inakotakiwa. Niwashukuru Makampuni mbalimbali yaliyoshiriki katika kufanikisha mradi huu. Mengi yamezungumzwa kuhusu mradi huu wa gesi ya Songosongo.

Lakini mimi ni kama mwenye mtoto nina haki kuzungumzia zaidi. Mradi huu ni mradi mkubwa tumetegemea utatuondolea umaskini kwa sababu umeme ndio chanzo cha kuondoa umaskini hili halina ubishi. Lakini hakuna mahali popote nilipoona kama mimi mzazi nitafaidika na umeme unaotokana na gesi hii. Sasa ni vyema leo Waziri Mkuu akinihakikishia kwamba mimi nitapata umeme kutokana na gesi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna vitu ambavyo vimenishtua kwa sababu mradi huu ulikuwa na fedha shilingi 174 bilioni. Baada ya kufanya matumizi zilitumika shilingi 174 bilioni, zilibaki shilingi 60 bilioni nazo hizo nilitegemea hasa kama nitapata umeme kutokana na fedha hizo. Lakini kinyume chake fedha hizo zimepelekwa Tanga, Kilimanjaro kwenda kukarabati nyaya kule. Wao umeme tayari wanao, lakini imekwenda kukarabatiwa nyaya. Sisi wa Kilwa, Lindi na Mtwara tubaki solemba. Sasa naomba nielezwe tatizo ni nini. Kwa kuwa Lindi na Mtwara hakuna anayehusika. Kwa sababu inaonekana hapa ubinafsi dhahiri umetumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ubinafsi tumeuona hata katika madaraja. Tulipojengewa madaraja kule Mkwaya tuliambiwa Konoike waliacha vifaa pale wakasema wataendelea

kujenga madaraja ya Masasi. Lakini hatimaye vyombo vile vikaja vikachukuliwa bila taarifa na madaraja yale yameachwa mpaka leo na juzi daraja hilo moja limeua watu 11. Sasa hivi mikoa ya Kusini bado tunataka tuendelee kufa tu na tuendelee kuwa nyuma mpaka lini? Sisi hii ni haki yetu, gesi inatoka katika eneo letu ni haki yetu kupata kama walivyopata watu wa Mtera, kama walivyopata watu wa Kihansi kama walivyopata Shimo la Mungu na sisi tuna haki ya kupata hivyo hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili tunaomba tusije tukafikia mahali tukawa na mtafaruku. Maana tunakoelekea sasa tutakuwa na mtafaruku na mtafaruku si mzuri katika nchi. Mara nyingi mnasema tunaigawa nchi. Tunataka kugawa nchi, hatutaki kugawa nchi. Mnataka kusababisha tugawe nchi. Sisi hatukusudii kugawa nchi, lakini mnataka kusababisha kugawa nchi. Hili sisi tumechoka kabisa. Kwa sababu siku za nyuma mlikuwa mnatueleza kwamba ooh nyinyi mna harakati kule za ukombozi wa Kusini hamuwezi kupata maendeleo. Leo je, bado ukombozi upo? Haupo. Sasa kwa nini tusipewe haki yetu. Sasa hivi maendeleo yote yaelekezwe Kusini kwa sababu tunachukua nafasi hii ambayo tulikuwa hatujaitumia.

Mheshimiwa Spika, pia nimeona katika kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 47 kifungu cha 62 kinaeleza miradi mikuu ya maji Mkoa wa Lindi sikuona. Mkoa wa Lindi hakuna kabisa. Tatizo la maji katika Mkoa wa Lindi ni tatizo sugu. Hivi sasa tunaambiwa kwamba hatuzalishi, hatuzai, basi tatizo moja tusilozalisha na kuzaa ni maji. Kwa sababu wake zetu wanakesha visimani kucha kungojea maji, tutazaa vipi. Ndiyo katika sensa tumo kwamba Mkoa wa Lindi hatuzai, tena tatizo la kutokuzaa ni hilo. Lakini tatizo la pili tunaambiwa hatuzalishi. Sisi tunalima wanaume tu wanawake wanahemea maji, tutazalisha lini. Kwa hiyo, hapa haki za binadamu hazitendeki. Maana kama hatuzai haki zinatendeka hapo. Kwa hiyo, naomba Waziri Mkuu alione hili. Tupate maji sensa inayokuja ili muone idadi tutakuwa kiasi gani. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu suala la zao la korosho. Ndugu yangu hapa aliyemaliza kuchangia baada yangu yeye amezungumzia walau walipata mbolea kidogo. Lakini sisi nataka niseme Mkoa wa Lindi hatujapata ruzuku inayohusu pembejeo za kilimo. Kule ili korosho zizae lazima tupate *sulphur*. Leo hii nimepigiwa simu toka juzi kuulizwa suala hili majibu sina. Tuna mikorosho milioni 7 ambayo inahitaji kufufuliwa na zao hili tunapeleka nje Serikali inafaidika na wananchi wanafaidika. Lakini bado haijaitiliwa mkazo. Sasa walau hiyo kidogo kwa nini tusipewe. Mimi nataka Mheshimiwa Waziri Mkuu unieleze hasa kwa nini fedha za Serikali zilichukuliwa kwenda kupelekwa *Exim Bank* ili sisi tunapotaka pembejeo twende tukawasujudie wale. Mimi na Mheshimiwa Chubi tumekwenda kupiga magoti kwao mwenyewe Waziri wa Kilimo ni shahidi mpaka tumechoka. Tena tumewahi kuwasumbua Wakurugenzi wetu kuja kwamba watapata fedha hakuna kitu wanaweka masharti makubwa wakati sisi tuna Benki zetu *NMB* kwa nini tusipeleke huko au kuna chochote hapo. Maana inawezekana wale wanaelekeza kaweke hiki weka hiki na *NMB* hawaelezeki inawezekana. Sasa vizuri hili tukaelezana kwa sababu imefikia mahali limekuwa kero. Fedha zetu wenyewe tukawape watu ambao watu wanataka lazima lazima tuwapigie magoti maana yake nini.

Mheshimiwa Spika, niende katika wanyama waharibifu. Katika Mkoa wa Lindi hususan katika Wilaya yangu ya Kilwa kuna wanyama waharibifu wanyama hao wanasababisha Wananchi kukosa chakula. Ingawa wanalima kwa uchache lakini uchache huo huo wavunaji ni wanyama. Hii kila ninaposimama katika Bunge hili napiga sana kelele nasema pamoja na kwamba mmewapunguza Ma-game walikuwepo 40 Kilwa wamefika mpaka 10 na mmpunguza mpaka 4 hasa ningepomba tupate upendeleo maalum kwa sababu sisi tuko karibu na Mbuga ya Selous. Tupate basi walau ma-game 30.

Kuna kata yangu ya Kilanjelanjé walivuna mtama mwaka huu lakini mtama huo wote wamekula wanyama. Wamelima mtama wamepata lakini mtama huo wote umevunwa na wanyama. Sasa hivi wana tatizo la chakula. Ni maeneo mengi tu ya Kilwa wana tatizo la chakula ili hali watu walilima na mvua mwaka huu ilikuwa nzuri sasa wamebakiwa na zao la ufuta tu ambalo zao hili wanyama waharibifu hawalishambulii. Lakini nalo zao hilo la ufuta lina tatizo la bei. Kuna wafanyabiashara wanaojitahidi kuwakandamiza wakulima kwa makusudi lakini Waziri wa Ushirika na Masoko hataki kuliingilia kati suala hilo. Huko Dar es Salaam kilo moja ya ufuta shilingi 850/= kule wananunua kilo moja shilingi 620/- hivi jamani gharama hii ya shilingi 230/= ni gharama ya kiasi gani. Sasa hii Waziri wa Ushirika na Masoko aliingilie kati pamoja na kuwa ni soko huria lakini huria yenyewe ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie kwa kurudia suala la gesi ili tupate mrahaba kama mlivyoweka katika chokaa. Huu ni mradi mkubwa lazima tunataka tuelezwe Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa inafaidikaje na mradi huu. Kwa sababu sisi tunachangia kwa namna moja au nyingine, tunaulinda ule mradi. Tumeulinda toka mwaka 1974 mpaka hii leo. Hata kama mtaleta askari lakini askari hao bila msaada wetu hawawezi wakalinda. Kwa hiyo ili tuendeleo kulinda tunaomba mtupe moyo ili Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa inufaike.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja mia kwa mia.  
(Makofi)

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hotuba hii ya Mheshimwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, lakini nianze kwanza kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge wote waliopata misiba. Vile vile ninampongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga kwa ushindi mkubwa alioupata. Nasema karibu sana CCM ili tuimarisha sera za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Pia, nitoe wito kwa Waheshimiwa wengine ambao bado wameng'ang'ania mti ambao sasa karibu uvunjike waporomoke huko, utawaangusha.  
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Wananchi wa Mikoa ya Kusini, jana tulipata taarifa hapa kwamba wanaendelea kupokea Watanzania wenzao wa Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Mwanza wakiwa na makundi ya ng'ombe. Hao ni wawekezaji ninaomba muwapokee watawasaidia sana katika kuboresha mifugo yenu.  
(Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, naomba nipongeze sana hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hotuba nzuri ambayo inalenga utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2000. Toka tuanze kutekeleza Ilani ya Uchaguzi mwaka 2000 mpaka sasa ni miaka mitatu na nusu, yaliyotendeka ni makubwa sana na hasa nianze na Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa MEM umekuwa na mafanikio makubwa sana katika kuboresha Elimu ya Msingi. Hivi sasa hakuna shule ambayo utakuta wanafunzi wanakaa chini ya kivuli cha mti, lakini hii ni kwa sababu ya mikakati mizuri ambayo imeandaliwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Pamoja na mafanikio haya, kumejitokeza tatizo la watoto wetu kufanya vizuri lakini wanakosa nafasi kwenye Shule za Sekondari. Tatizo hili litapata majibu yake endapo mpango wa MEM utanzishwa. Nina imani mpango huu utakuwa ndiyo ufumbuzi wa tatizo la watoto wetu kukosa nafasi za Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, labda hapa nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Madiwani kote nchini kwa kusimamia vizuri mpango wa MEM kwa sababu Waheshimiwa Madiwani pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri na Kamati za Shule wasingemamia vizuri mabilioni ya fedha ambayo yalikuwa yanaenda Vijijini mpango huo usingefanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito kwa Serikali. Serikali haikuwatendea haki Waheshimiwa Madiwani kuwatoa kwenye *Tender Boards* za Halmashauri. Mwenye Halmashauri ni Diwani kwa niaba ya Wananchi, sasa unapomwambia akae pembeni halafu Mtendaji ndiyo ajadili maendeleo ya Halmashauri ni kutomtendea haki mwananchi ambaye amemchagua Diwani amwakilishe kwenye Halmashauri. Ninaomba Waheshimiwa Madiwani warudishwe kwenye *Tender Boards* za Halmashauri ili washirikiane na Watendaji kama washauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, naomba nitambue juhudi za Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kwa kazi kubwa ya kuhakikisha mawasiliano ya uhakika kuhusu barabara yanakuwepo nchini. Mfano hai ni ujenzi wa daraja la Mto Rufiji na kazi inayoendelea sasa ya ujenzi wa barabara ya Mwanza - Shinyanga - Dodoma. Barabara ya Mwanza - Shinyanga - Dodoma, itakapokamilika itakuwa ni ufumbuzi wa matatizo ya Wananchi wa Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Magufuli asichoke kutenda mema, lakini nimpongeze kipekee kwa jinsi alivyolivalia njuga tatizo la barabara ya Ushirombo - Bulembela mpaka Mto Nyikonga, barabara ambayo inatuunganisha na wenzetu wa Geita. Ninaomba utekelezaji wake uharakishwe ili kuokoa matatizo na maisha ya Wananchi wa Geita ambao kila mwaka walikuwa wanapoteza maisha yao kwa sababu ya daraja la Mto Nyikonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo ni Sekta Kiongozi katika Taifa letu. Asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo, lakini bila kuboresha kilimo hata Sera ya Kuondoa Umaskini haitafanikiwa. Umefika wakati sasa tuangalie uwezekano wa kuwakwamua

Watanzania wetu waondokane na jembe la mkono. Ili tuwasaidie Wananchi wetu kuondokana na jembe la mkono ni lazima tuandae mazingira ya kuwawezesha waeleweke na kutambulika na Vyombo vya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuwamilikisha Wananchi ardhi ni mkakati ambao utakuwa ni mkombozi kwa wakulima wetu kwani hati za ardhi zao watazitumia kama dhamana kwenye Vyombo vya Fedha na hivyo wataaminika kwenye Taasisi za Fedha kwa kupata nguvu ya kupata fedha ya kuendeshea shughuli zao za kilimo. Wapo watu wengine wamekaa Dar es Salaam hawana kazi wala hawana mashamba, hawa ni vizuri wakaenda Bukombe ambako kuna mashamba, wakaenda Mbarali kwenye mashamba ili nao wanufaike na mpango huu wa kuwa na hati ambazo zitawadhamini kupata mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie utawala bora. Utawala bora ni ule unaozingatia sheria, kanuni na taratibu. Tumekuwa na watumishi wengi wakilalamika kutolipwa haki zao na inapofikia hatua hii ni kuvunja utaratibu wa utawala bora. Ni uvunjaji wa haki za binadamu kwa sababu mtu unapomwajiri anategemea apate riziki kutokana na ajira yake, leo kama alivyosema msemaji aliyepita Mheshimiwa Mulyambatte, Mkoa wa Shinyanga peke yake walimu wanadai zaidi ya Shilingi bilioni moja, lakini kwa Wilaya ya Bukombe peke yake walimu wanadai Sh.320,310,450/= . Ni tatizo kubwa ambalo linawadhalilisha wataalam wetu.

Mheshimiwa Spika, utawala bora si kufuatilia mambo ya rushwa tu, ni pamoja na kuhakikisha kwamba haki inatendeka kwa Watanzania. Ninaomba kitengo hiki kifuatilie, kigundue ni wapi mapungufu haya yapo, kama Wizarani ieleweke, lakini kama ni kwenye Halmashauri vile vile ieleweke wazi na wahusika ambao kwa kweli wanahusika kutotoa haki za watendaji wetu wawajibishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna tatizo la Watendaji wa Vijiji. Watendaji wa Vijiji hawa toka Serikali ilivyosema kwamba itawachukua mpaka sasa walio wengi hawajalipwa, nalo hili ni tatizo. Mtendaji kwenye eneo la Kijiji ni mtawala, huwezi ukawa na mtawala aliye na njaa, amelala njaa unategemea atatenda haki! Ni lazima atajiingiza hata kwenye dimbwi la kuomba na kupokea rushwa. Serikali iangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii ya pekee kabisa kuitambua Wizarani ya Mawasiliano na Uchukuzi. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa jinsi alivyolivalia njuga tatizo la mawasiliano ya simu katika Wilaya ya Bukombe. Ninampongeza sana kwani hivi sasa Bukombe iko kwenye mtandao, tunawasiliana na Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nitoe wito kwamba kwa mafanikio haya sasa wenzetu wa Wizarani ya Nishati na Madini wayaangalie kwa sababu huwezi ukawa na simu bila kuwa na umeme. Hivi simu za Wanabukombe ambazo sasa wameanza kuzitumia zikiisha chaji, watazichaji kwenye maji ya moto! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi, ameshuhudia maendeleo ya Wananchi wa Bukombe alivyokuja mwezi wa tatu. Ameshuhudia jinsi Wananchi wa Wilaya ya Bukombe walivyoamua kujiletea maendeleo wao wenyewe, wamejenga Halmashauri yao kwa nguvu yao zaidi ya Shilingi milioni 200, lakini wana ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambayo tunategemea mwezi wa nane huenda ikafunguliwa. Ni juhudi za Wananchi wa Bukombe, sasa tunaomba Serikali nayo kwa yale ambayo hawana uwezo nayo kama hili la umeme, basi ihakikishe kwamba inatekeleza ahadi iliyotoa kwamba kabla ya mwaka 2005 umeme Bukombe uwafikie Wanabukombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema naipongeza sana bajeti hii nzuri pamoja na kwamba wengine wanasema inalenga uchaguzi wa mwaka 2005. Mimi nasema sawa ni ya uchaguzi wa 2005, kwani hivi kuna ubaya gani kupitisha Bajeti inayolenga uchaguzi wa 2005 lakini ni bajeti ambayo ni ya manufaa kwa Watanzania wote? Hii ni Bajeti ya Watanzania wote, imeangalia matatizo ya Watanzania, kwa hiyo inafaa kupitishwa na mimi naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuungana na wenzangu ili kuchangia hotuba iliyo mbele yetu. Lakini kabla ya kuchangia, niwape pole wale wote waliopata matatizo mbalimbali ya vifo, ya ajali na kadhalika. Haya yote yanatokana na Mwenyezi Mungu kama tulivyoambiwa kwamba *Kulamaa waqaa, wayaqaa, wasayaqaa* milki. Kwa hiyo, haya yote yanatokana na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, leo mchango wangu mkubwa utaelekeza kwenye Muungano. Lakini hata hivyo ni vizuri kutowasahau wale wote walioanzisha Muungano huu ambao ni Marehemu Abeid Amani Karume na Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere pamoja na wale viongozi wao wote waliokuwa wamekwishatangulia kwa muda huo. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, tumeachiwa hazina kubwa sana, lakini kazi tunayo kubwa sisi ambao bado tuko hai ni namna gani hazina hii tutaweza kuitumia. Wengine hufanya hadithi ya punda hata ukamvisha dhahabu atayapata kwenye dongo tu! Sasa tusifike kiwango hicho katika Muungano wetu, tujenge umoja wetu. Leo nisingesimama katika Bunge hili Tukufu kama si kwa ajili ya Muungano, lakini Muungano ndiyo ulionileta hapa na kuleta kujua na kufahamiana. Kama si Muungano huu, mimi nisingepata kutembea Mikoa mbalimbali katika nchi hii. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, penye mazuri na mabaya hayakosi, hii ni kawaida na ndivyo Mwenyezi Mungu alivyotujaalia waja wake. Yatakuwepo mazuri sana, lakini na mabaya yatajitokeza. Ikiwa kama tutanyamaza kimya yatajulikana vipi? Hayawezi kueleweka. Tuseme tujadiliane, tuzungumze na baadaye tutafute ufumbuzi. Hapo tutaweza kwenda na taratibu zetu kwa njia iliyokuwa nzuri kabisa katika chombo chetu hiki kikuu cha Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu huu kutoka Zanzibar na Tanzania Bara ni kitu kinaeleweka wazi si kitu cha kuficha. Lakini licha ya udogo wake, Zanzibar inajulikana kwamba ni nchi kamili na ilikuwa inaeleweka Kimataifa. Sasa maumbile yetu hata Mwenyezi Mungu katuumba hapa wengine wanene, wengine wadogo, lakini ni binadamu na kama mmeshaamua kwamba muwe pamoja basi tena hatutazami kwamba aah mwenzangu kiwete, mwenzangu yuko hivi, ile si mahali pake. Tutazame mwenendo uliokuwa mzuri ili kurekebisha taratibu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kitabu hiki cha bajeti cha 2004/2005 ukurasa wa 4 napenda kunukuu: “Hata hivyo, wapo baadhi ya watu wanaokerwa na Muungano. Wanajitahidi kutumia hila kutaka kutia dosari kwa malengo yao binafsi. Napenda kuwahakikishia Wananchi kuwa Muungano hauwezi kutetereka kamwe.” *Amin.* “Changamoto iliyo mbele yetu ni kuimarisha misingi imara iliyowekwa na waasisi wetu na kuutetea Muungano wetu dhidi ya maadui.”

Mheshimiwa Spika, lilemwalo lipo, kama halipo liko njiani linakuja. Lakini pia katika bajeti yetu hii ya 2003/2004 ambayo ilishapita kuna maelezo pia aliyoeleza: “Serikali zetu mbili zinaendelea kuimarisha mashirikiano na kuondoa kero mbalimbali. Baadhi ya shughuli zitatekelezwa kwa pamoja, uratibu, uboreshaji na mshikamano baina ya Wizara, Asasi na kadhalika katika mambo ya Muungano na kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu na matukio/maamuzi mbalimbali.”

Mheshimiwa Spika, sasa tuendeleo na shughuli yetu hii. Tunajua kwamba ni lazima tuwe imara kwani tulishajua kwamba huku kuna matatizo fulani kwa wale ambao ni maadui. Lakini wataondoka maadui kama kero na umoja wetu utashikamana vizuri. Hatatokea adui wala hataweza kuleta bughudha ya aina yoyote dhidi ya chombo chetu hiki tulichokiunda ambacho ndicho chenye umoja wetu.

Sasa kuna mambo ambayo kwa kweli yanaturudisha nyuma kwa upande mwingine na hapa ndipo mahali pake pa kusema. Kwanza alisimama Mjumbe mmoja hapa, lakini katika ku-*windup* kwa viongozi waliopita sikuyasikia kwa hivyo nasema tena, tuseme tumekwishakubaliana kwamba chombo chetu hiki ni kimoja, taratibu zetu ni moja, tuseme ni kwa nini mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar hulipishwa Sh.6,000/= gharama za bandari kwa tani na mzigo huo huo kwenda Mtwara au Tanga au mahali pengine ndani ya chombo hiki hulipishwa Sh.500/= Ni kwa sababu gani wakati sisi tunasema ni ndugu na tuko pamoja?

Kama unafuatana na mtoto mdogo safari zenu moja ni lazima ujue mwendo wa kwenda, kama si hivyo utamuangusha. Hii ndiyo hatua itakayofikia hapa. Unamwambia: “Hebu tazama huku.” Kumbe mwenzio kaanguka, hunaye uko peke yako mbele. Je, tumefanikisha chombo chetu hiki? Haya ni lazima tuyatazame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, kuna mizigo ambayo inatoka Zanzibar na inakuwa imekwishalipiwa shughuli zake zote, nikitaka kuuleta Bara hapa unalipia, hivyo maana

yake nini? Hata vitu vidogo vidogo! Wakati ule mwezi wa 5 tukiwa Dar es Salaam, kulikuwa na vijana wawili wamechukua *TV*.

Mheshimiwa Spika, huo ni mfano mdogo niko hai kabisa sikuhadithiwa. Walipofika wakafanyiwa *harass* wale, kwa bahati mie nipo chonjo hivi natazama. Nikawaambia: “Jamani, kwani mpya hii?” Wakasema: “Aah, si mpya.” Hii *TV* katoa nyumbani kwake, leo anasema anasafirisha anakwenda kuangalia mahali pengine nyumbani kwao, hivyo tena pia alipie? Kwa bahati vijana wale wawili wakachukua wakaenda zao.

Mheshimiwa Spika, ina maana pale palikuwa panatumika mbinu za kuwarejesha nyuma. Sasa hao watu wetu ambao tunawaweka ndiyo wataweza kuharibu Muungano wetu kwa sababu hawafuati maadili na taratibu zetu tulizoweka. Kuna vitu vya kipuuzi tu, mwanadamu anahamaki kwa jambo dogo kabisa. Ilikuwa tutoe kauli rasmi, watu wanakuja wanachukua biashara kule, lakini hali kadhalika utawakuta kila mara wanaharasiwa. Haya si mambo mazuri kusema kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tuko pamoja hata kwa shughuli za bandari, lakini utaona iko haja ya kuisaidia Zanzibar, si unajua Zanzibar hakuna wafanyabiashara, utakuta kama wawili tu. Kwa vyovyote vile, kama tunaweka *level* ya mapato sawa sawa wahakikishe kule hawezi kuja mtu. Kuna haja kidogo ya kuteremsha ili zile bidhaa ziweze kufika kwa sababu huku ni soko kubwa. Wewe utaona kwamba wote watafikia Zanzibar, si kweli! Si kweli kabisa! Lakini sasa inakuwa Wananchi wa kule wamekauka kabisa kimapato. Hata bajeti kama nilivyoisikia imepungua *five percent*, imeanguka.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo tunawajibika sisi kuwa pamoja na kuangalia vizuri kabisa kwani Wananchi wanalalamika. Leo tumetangaziwa redioni, mmesikia wanasema wanataka kupunguza wafanyakazi 27,000. Ina maana uchumi hakuna. Wakati mwingine hata kwenye nyumba tunakuwa wakali kwa kile ambacho hatujakitambua. Mtoto wako ametumwa: “Mwambie baba akanunue kitoweo.” Unakuwa mkali kwa sababu huna cha kumpa.

Kuna mambo tunawajibika kuyaangalia vizuri kabisa kwa sababu kwa jinsi ulivyoeleza Mheshimiwa Waziri ni safi kabisa, kwamba wako haya mambo hawataki tuwe pamoja. Wale wanatafuta mwanya tu wa kupita, anapita na anaeneza sumu. Kwa hiyo, ningependa hali hiyo iangaliwe ili tuweze kufanikisha mambo yetu kwa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile, hii Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, nakumbuka tulikuwa tunasema ni Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje.

Lakini leo hii imeingizwa Ushirikiano wa Kimataifa. Ilikuwa kweli ni makubaliano haya toka msingi? Ningepata hapa maelezo, kwa sababu nakumbuka mwanzo tulikuwa tunakwenda kama hivyo kwa sababu kuna mambo tukitenda tunaibana Zanzibar kwa kiasi fulani. Nataka hii mtoe maelezo huko msingi ilikuwa inatokaje, kwa



sababu hii tumekuja kujua baadaye. Kwa hiyo, hapa nataka maelezo zaidi kufahamishwa hali halisi ilivyo zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunasema tumeungana, lakini mbona hatuna kama Wizara hivi kwamba labda Wizara hii mtu anakwenda kama kule kwetu kama ana matatizo yake anakwenda na kupata ushauri kwamba ni chombo hiki nafika pale. Ukienda Wizara ya Mambo ya Nje ukifika tu hapo unaona. Lakini aah, Wizara ya Mambo ya Muungano hatuoni! Kweli tuna nia ya kuimarisha chombo hiki? Kuna mambo tusiwe kama zamani mtu akitaka taaluma anakwenda kusomea chini ya mti, wakati huo ulishapita. Tuwe na chombo maalum, jengo maalum pale tunajua kwamba hii Wizara fulani, ndiyo mahali pake. Lakini utakuta kama kisebule tu tutafika wapi?

Mheshimiwa Spika, mambo haya madogo madogo kwa kweli si mambo mazuri, kama hiki chombo chetu tunataka kuleta mafanikio, ni lazima kasoro kama hizi tuweze kuziondoa. Kuna mambo yetu haya ya Miswada, unajua iliwahi kutokea kipindi kimoja hapa, kuna Mheshimiwa fulani alieleza kitu ilikuwa habari *Deep Se a Fishing*. Sisi tulihemewa hapa kutoka Zanzibar hatujui nini!

Kwa bahati alisimama Naibu Waziri hapa, wakati ule alikuwepo Naibu Waziri Mheshimiwa Mwalimu akauliza lile suala vipi, mbona hatujui? Alijibiwa pale: “Nishaonana na Waziri wako.” Aaah, Waziri kweli katika nchi nzima aamue yeye tu! Hiyo inatosheleza kweli? (*Makofi/Kicheko*)

Kama tunavyokuja kwako Waziri Mkuu hapa na kule Dar es Salaam kuna Waziri Kiongozi, yale mambo yapite Serikalini na haya ndiyo matatizo yanayojitokeza. Tunakuja hapa sisi tunashangaa kabisa maana yake kama vinyago ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**SPIKA:** Hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia pamoja na sote afya njema tukaweza kushiriki katika shughuli hizi za Bunge asubuhi hii katika hali ya amani.

Lakini la pili, nikushukuru wewe binafsi kwa dakika za majeruhi na mimi nikaweza kupata nafasi ya kusema mambo mawili, matatu na nataka niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapa pole wale wote waliofiwa na kuwafariji wale wote waliopata ajali na matatizo mbalimbali wakati wanakuja katika kikao hiki cha Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mambo ambayo nilikusudia niyaseme mengi yamekwishazungumzwa nitabaki na machache sana. Kwanza nataka nianze na suala zima la Muungano kama alivyomaliza mwenzangu. Mimi nasema suala la Muungano

kuimarishwa au kudhalilika, basi Serikali ya Muungano yenyewe itakuwa ina sehemu kubwa sana. Kwa kuwa wao ndiyo wanaosimamia mipango yote, basi kwa kweli ni wajibu wao kuyarekebisha haya.

Mheshimiwa Spika, Muungano utaimarika kwa kuondoa hizi kasoro au kero ambazo zipo. Moja ya kero, pamoja na kuwa mmeshapitisha, lakini kwa kweli hili ni tatizo ambalo mmeupunguzia nguvu sana Muungano wetu, nalo ni suala zima la kuvunja makubaliano ya awali. Makubaliano ya awali yalisema kwamba Rais wa Zanzibar atakuwa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkafanya mabadiliko ya Katiba na kwa bahati mbaya sana ukisikia kuna mabadiliko ya Katiba, basi ujue ni kuinyang'anya uwezo Zanzibar, hakuna jingine! Ukisikia kuna mabadiliko ya 12, ya 11, hakuna la ziada hapo, isipokuwa ni kunyang'anya madaraka ya Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa makusudi kabisa mkafanya mabadiliko ya 12 ya Katiba mkamnyang'anya Rais wa Zanzibar mamlaka ya kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Kwa kuwa uwezo hatuna, lakini hilo tunasema ni tatizo na ni dosari na litaendelea kubaki kuwa ni dosari, vinginevyo lirekebishwe. Hata mkifanya vipi, hili bado ni tatizo kwa sababu mmevunja makubaliano ya msingi kabisa. Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini, kama kweli tunataka tuuimarisha huu Muungano, huu Muungano ni wa nchi mbili, haidhuru kwamba nchi moja ni ndogo, lakini tumekubaliana kuungana nchi mbili. Sasa kwa kiasi kikubwa basi tungekuwa na uwiano. Mimi nataka niulize na niweze kupewa majibu, katika suala hili la ushirikiano wa Kimataifa tuna Mabalozzi wetu ambao wanatuwakilisha Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania, ningeomba tuelezwe katika Mabalozzi wote waliopo nchi za nje Wazanzibari ni wangapi? Hilo ni suala la kwanza ambalo nilitaka niliweke wazi.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la pili ni suala uchaguzi, mwaka kesho *Inshallah* akipenda Mola kuna uchaguzi mkuu wa nchi wa mwaka 2005, uchaguzi wa Rais na Wabunge. Pia jukumu la kuhakikisha kwamba uchaguzi unakuwa huru na wa haki ni suala la Serikali. Serikali yenyewe ikiamua uchaguzi uwe huru na haki *wallahi, billahi, tallahi*, utakuwa wa huru na haki. Serikali yenyewe ikiamua kwamba uchaguzi uvurugike utavurugika. Nina mfano hai ni uchaguzi mdogo wa majimbo 15 Visiwani Pemba mwaka jana. Nataka nichukue nafasi hii kupongeza Jeshi la Polisi, rafiki yangu Naibu waziri wa Mambo ya Ndani jinsi alivyosimamia uchaguzi ule na vyombo vya dola vikatumika kwa kufuata sheria. Hakuna mtu aliyekunwa hata pele. *(Makofi)*

Hatua nyingine sisi hatukua na tatizo lolote hali kadhalika CCM tuliweza kufanya uchaguzi ule pakaandikishwa mpaka wapiga kura, matokeo yakatangazwa kila mtu akaridhika, kwa kweli uchaguzi umekwenda halali. Tunaomba kwa kuongezewa fedha Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Ni matumaini yetu kwamba fedha zile zitatumika ili kusimamia uchaguzi wa mwaka 2005 ili haki iweze kutendeka. Atakayeshindwa awe ameshindwa kihalahi taala na atakayeshinda, ameshinda kihalali taala na sisi tunawaahidi kwamba endapo tutashindwa ni *illahi taala* tutakubali matokeo na tutawapongeza usiku na mchana. *(Makofi)*

Lakini natanabahisha kwamba endapo hila zitatumika kama zilivyotumika mwaka 1995, kama zilivyotumika mwaka 2000 kwa kweli tuko tayari kupigania haki yetu mpaka tone la mwisho la damu. Hili tunasema tuko *very serious* katika uchaguzi wa mwaka 2005 kwa namna yoyote ya hila hatutakubali Serikali ya Jamhuri ya Muungano wajue kwamba tuko tayari kukubali matokeo na tunasema tutawapongeza mtakapotushinda kihalali tutakubali. (*Makofi*)

Lakini hatuko tayari kukubali tena.

**MBUNGE FULANI:** Kwenda shimoni.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Hatuko tayari tena kwenda shimoni kama mnavyosema. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli wewe ni Kiongozi Mkuu wa Serikali na ndiyo mwenye dhamana. Tunakuomba sana ukumbuke duniani, ukumbuke ahera una mamlaka makubwa na ujue kwamba kwa kweli lolote litakalotokea basi kwa kweli moja katika masuala mkubwa itakuwa ni wewe, tunatarajia wewe ni mtu wa dini kabisa, mtu wa Mungu kwa kweli utaheshimu maamuzi ya wananchi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hapo juzi tulifanya chaguzi humu ndani ya Bunge za kuchagua Wabunge wa Bunge la Afrika, nililowahi kuhudhuria ni hilo. Lakini sasa mimi niliona kitu kimoja kwamba paligawiwa hapa nafasi za Zanzibar, ziligawiwa nafasi za Bara, ziligawiwa nafasi za wanawake na nafasi za upinzani. Mimi nilikuwa nafikiria kwamba kwa kuwa tumegawiwa kwa mafungu, basi nilidhani kwamba pia na uchaguzi wenyewe utakwenda kwa mafungu, ili kuheshimu demokrasi. Lakini nadhani utaratibu huu uliotumika sidhani kama kwa kweli demokrasia hapa imepewa nafasi yake.

Kwa sababu kwa mfano kuna wanawake ambao walikuwa na nafasi yao, sasa mimi nilidhani kwamba kwa kuwa tunataka mwakilishi wa wanawake, wanawake wao wenyewe watakuwa na nafasi peke yao wachague yule mwanamke. La pili, hali kadhalika kwa upande wa Zanzibar, nilidhani Wabunge kutoka Zanzibar tutapewa nafasi tuchague wenyewe.

**WABUNGE FULANI:** Ahaa!

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, naomba utaratibu kidogo. Hali kadhalika kwa upande wa Upinzani, mimi nilidhani ili kuheshimu demokrasi kwamba Wapinzani, sisi wenyewe tutapewa nafasi kwamba tuchague mwakilishi wetu. Sasa mimi napendekeza utaratibu huu, ili kupanua wigo wa demokrasia basi chaguzi zinapokuwepo ufanyike utaratibu huu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niende katika matukio ya maafa. Kwanza nichukue nafasi hii nipongezi Ofisi ya Waziri Mkuu, wanavyokuwa makini sana katika kufuatilia masuala ya maafa upande wa Tanzania Bara. Lakini nataka nitoe masikitiko yangu ya dhati katika ofisi hii ya Waziri Mkuu, jinsi ilivyokuwa haichukui juhudi katika kufuatilia matukio ya maafa kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ni maafa ambayo hayakuwa siri ndani ya Tanzania na nje na dunia kwa ujumla yaliyotokea Kisiwani Pemba tarehe 26 na 27 Januari, 2001. Matokeo ambayo yalipelekea Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuunda Tume kwenda Pemba, kwenda kuchunguza. Tume ikaenda ikafanya kazi na ikawasilisha ripoti yake kwa Mheshimiwa Rais na mapendekezo yake. La kusikitisha kabisa hadi leo ripoti na mapendekezo ya tume ile bado hayajashughulikiwa. Tulikubaliana katika muafaka kwamba wale wote walioathirika kwa namna moja ama nyingine katika maandamano yale wangepewa kifuta machozi. Suala hili niliuliza mara baada ya kuingia Bungeni, nikapata majibu kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera kwamba suala hili linashughulikiwa na muda muafaka utakapofika mtaelezwa. Inasikitisha kuona kwamba baada ya mwaka mmoja toka niulize suala hilo, bado suala hilo halijafikia mwisho.

Nakumbuka nilimwomba Waziri wa Fedha, kwenda Pemba kuwaona hawa watu ambao wameathirika, kwa bahati mbaya alikataa. Nataka kwa mara nyingine tena nichukue nafasi hii kumwomba sasa Waziri Mkuu, mwenyewe afunge safari kwenda Pemba aende akaonane na hawa watu walioathirika. Naamini Mheshimiwa Waziri utakapokwenda Pemba ukawaona hawa viwete, yatima na akina mama walioathirika katika maandamano, ukirudi hapa naamini utatafuta fungu lolote la fedha ili uweze kuwapa angalau kifuta machozi. Hili nakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokana na utendaji wako mzuri wa kazi nadhani na naamini kwamba utafuatilia hili na tutapata muafaka.

Lakini mbali ya kuwapa fidia hawa pia suala hili litamweka Rais wetu katika *position* hili ni tatizo jamani! Kama hamkulimaliza hili nasema litakuwa ni dosari kubwa ndani ya utekelezaji na shughuli za Rais wetu Mheshimiwa Benjamin Mkapa, ambaye anamaliza muda wake. Tunataka amalize muda wake dunia imkumbatie iweze kumtumia.

Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni niliuliza swali mara moja kwamba katika kuimarisha huu Muungano na kwa kuwa hili Bunge ni la Muungano, basi kwa nini hatufikirii kwamba baadhi ya hivi vikao vya kamati vikawa vinafanyika Zanzibar? Nakumbuka Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera akajibu kwamba hili linazungumzika. Mimi nilidhani kwa jibu lile kwamba hili linazungumzika kwamba litashughulikiwa na litafanyiwa kazi. Nilidhani kwamba ndani ya kipindi hicho mwaka mmoja basi angalau japo mara moja tungeweza kukutana Zanzibar katika shughuli za kamati. Lakini hadi leo sijapata majibu yoyote. Ningeomba Mheshimiwa Waziri William Lukuvi katika hili, pia nalo atueleze limefikia hatua gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa katikati kulitokea ulipuaji wa mabomu Visiwani Zanzibar na Wizara ya Mambo ya Ndani Naibu Waziri akaenda Zanzibar kufuatilia suala hili. Lakini mara nyingi masuala kama haya yanapojitokeza mara nyingi lawana hutupiwa vyama vya upinzani na hasa *CUF* kwamba ndiyo wanaohusika kwa namna moja ama nyingine. Sasa mimi naomba niombe Ofisi ya Waziri Mkuu, kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, uweze kutueleza suala hili la mabomu hasa limefikia wapi, maana tunaona kimya hatujui kwamba waliohusika walikamatwa na wamefikishwa mahakamani,

tunaona hapa katikati ni kimya. Tunaomba lifuatiliwe na waliohusika wachukuliwe hatua madhubuti ili masuala kama haya yasisitue dosari kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala la Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Naipongeza Serikali kufikiria suala hili la uandikishaji wa Wapiga Kura katika Daftari la Kudumu. Lakini naomba nichukue tahadhari kubwa katika suala zima la Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Kwa upande wa Tanzania Bara tuhakikishe kwamba Watanzania ndiyo ambao wana haki ya kuandikishwa kwenye daftari lile na siyo Warundi, wala Wakenya, wala Waganda.

Lakini vile vile na kwa upande wa Zanzibar tuhakikishe kwamba Daftari la Wapiga Kura la Zanzibar linawahusu Wazanzibar. Hapa katikati ilitokea tuhuma kwamba Wazanzibar, wanawafukuza wabara hawawataki, dhana kwa kweli si, Wazanzibar sisi hatuna tatizo na wabara, vyama vyetu ni vya muungano tunawakaribisha. Mheshimiwa Jenista Mhagama, karibu Zanzibar tutakupokea, Mheshimiwa Grace Kiwelu, karibu, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda karibuni tutawapokea hatuna matatizo yoyote, kule ni kwenu kabisa. Lakini tunawaomba mje kwa ajili ya matembezi tutawapokea hata sisi *CUF*, mkija mimi niko tayari. Mheshimiwa Jenista Mhagama usiwe na wasiwasi nitakupokea nyumbani hamna tatizo nitakupokea, nitakuhudumia, nitakutembeza, nitakurejesha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo nakushukuru sana kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kijana aliyekuwa anachangia sasa hivi alikuwa anatekeleza Muungano kwa vitendo kwa hiyo, nampongeza kweli na aendelee na moyo huo kwamba Mwenyezi Mungu, awaongoze ili wawaongoe katika maoni na kauli ambazo zilizokuwa zinagawa Watanzania, ili waungane na Watanzania wenzao kuiongoza nchi hii, kwa sababu vyama vyetu ni vyama vya siasa hivyo tunawatekelezea siasa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo uliokuwa siyo, utangulizi nilikuwa nampongeza huyu kijana. Sasa naanza utangulizi wa kusema kwamba ada ya mja hunena muungwano ni kitendo na ningependa kuwapa pole wote waliopatwa na majanga ya kufiwa, nawapa pole wote waliopata majanga ya kuvamiwa na majambazi waliopata ajali. Kwa hiyo, Mungu atawasaidia na mtaishi katika moyo wa matumaini. Hayo ni matokeo siyo majaribu kwa sababu majaribu hujaribika na matokeo hutoweka. *(Kicheko)*

Hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni fungu namba 37. Nilipoangalia katika ukurasa ambao fungu 37 lipo nikakuta vifungu vidogo ambavyo Waziri Mkuu, anaweza akapanga fedha zake kwa utaratibu wa matumizi ya bajeti ambayo anaiomba. Lakini kwa bahati nzuri katika hotuba ambayo imetolewa kwenye kijitabu cha kueleza umma wa Tanzania ilibidi aguse sekta zote mtambuka, *cross sectoral* na Wizara nyingine. Hiyo imetupa nafasi Waheshimiwa Wabunge, kuzungumza yote, ile tabia ambayo Tanzania tunayo. Kuna kabila moja sisi kwetu linaamini sana katika miti yote ile katika pori kuna mti mkubwa kuliko yote unaitwa Mbuyu, unakwenda kwenye Mbuyu ambao kama

Waziri Mkuu, amefananishwa kama Mbuyu watu wanatambika wanaomba kila kitu pale, kila kitu kinaombwa halafu Mbuyu haujibu, unaona matokeo yake tu kwamba naomba tafadhali mvua, kila kitu kinaombwa pale. Halafu Mbuyu haujibu unaona matokeo tu yanavyotokea. Kwa hiyo, ni sawa sawa na hoja hizi zitakuwa hazijibiwi. Sasa matokeo ya hoja hizi nadhani zile Wizara za kisekta zimekaa kwa makini sana. Nilikuwa nawaaangalia nadhani mlizinakili, zinazohusu sekta ya kilimo atajibu Waziri wa Kilimo na Chakula, lakini Waziri Mkuu atatoa kama ni sera na utaratibu wa Chama chetu. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa naanza na hotuba na nchi zetu za Afrika ambazo kama Tanzania ambayo imo na nchi zingine katika dunia Afghanistan mpaka Zimbabwe, katika nchi ambazo zilipata uhuru, lakini uhuru uliopata nchi ndogo ndogo zilikuwa na tafsiri tofauti ndiyo maana kuna, migongano, vurugu, kashfa, kwa sababu watu wengine walidhani uhuru ni mapumziko, wengine wakasema uhuru ni mgao, wengine wakasema uhuru ni kutumikia. Waliosema uhuru ni mgao na waliosema uhuru ni mapumziko mara nyingi yakatokea mambo ya wimbi la uvivu, urasimu, wizi, rushwa, uharibifu wa mali ya umma na vitu vingine. Wakaleta haya manung'uniko katika taifa lao, wakaleta vurugu baridi, kashfa za kina na maisha ya kutegeana kwenye nchi zao. Kwa hiyo, matokeo yake wale waliokuwa wanasema uhuru ni kujituma wakawajibika wakajituma wakatamia ari wakawa waaminifu na wakaongeza mtaji, wakaongeza tija, mafanikio na ufanisi katika nchi zao ndiyo Tanzania leo inapeta. Najua kabisa mnaangalia kwenye tovuti kuona Tanzania na mambo ya mafanikio, lakini mnataja mambo yale ambayo ni mapungufu na kuiambia Serikali mapungufu ni wajibu kwa sababu unaiielekeza jinsi ya kuziba maeneo pamoja na haitaziba yote, lakini itakuwa inaziba maeneo ambayo ni historia.

Sasa katika wale wa kwanza niliowataja, wale wanasema tupambe halafu tusherehe, wale wavivu wanasema uhuru, halafu hata vikaharibika potelea pote. Lakini hawa wa pili mara nyingi wanakuwa wanaleta tahadhari na zile vurugu nilizozitaja na kasheshe katika Taifa lakini unakua mzigo kwa Taifa. Hawa wa pili wanaosema kwamba tunawajibika na kujituma wanasema tupambe, tusherehekee halafu tupambe tena vijana wetu wayakute mapambo hayo. Hawa wanaleta matumaini na ufumbuzi kwa taifa lao. Naomba muwashangilie hawa watu. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa Tanzania imo katika mfumo huu wa pili wa mwisho ambao unajipanga vizuri. Sasa naanza utawala bora. Utawala bora siyo utekelezaji wa mambo ya utawala yalivyo jinsi ya mpango wenyewe na mpangilio katika nchi jinsi ulivyo na huwa hauna mfume dume na unafuata mfumo shirikishi unaoanza kuanzia vitongoji, vijiji, kata, tarafa, Wilaya hadi Mkoa huwa na vyombo vya kitaifa na vyombo vingine vinakuza huko. Kuna huo utawala bora maana yake ni kuchuja baadhi ya mambo ambayo yanahusu katika ngazi yaishie kule, ndiyo maana sasa hivi Waheshimiwa Wabunge, siwezi nikasema kitongoji fulani mbona kuna matatizo kwa sababu yuko Mwenyekiti wa Kitongoji na Afisa Mtendaji wa kule.

Kwa hiyo, kuna vikao mbalimbali, tume za udhabiti na vitu vingine vinavyohusiana. Kwa hiyo, huo ndiyo utawala bora kwa mpango kwanza wa timu yenyewe kuanzia *goalkeeper* mpaka *forward line*, mpaka wafungaji. Kwa hiyo,

tunaamini kabisa wako akina Beckham wengine katika siasa katika nchi hii na ndiyo wale nimewatangaza mliofunga yale magoli matatu. Kufuta kodi goli la kwanza, kufutiwa madeni goli la pili, kuingiza wastaafu, goli la tatu, lipo la nne linakuja la kujenga uwanja wa kimataifa. Naomba mshangilie magoli hayo manne tutayatangaza wakati wa tathimini. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa kuwa watu wengi huwa hawababaiki wanapoambiwa mapungufu ya utendaji badala ya kueleza mapungufu ya wenyewe binafsi. Hivyo basi hujipanga vizuri katika kugawa mapungufu hayo. Hivyo basi mambo yaliyojitokeza kama vile kupishana mishahara, kupongeza *TRA*, uvivu, habari za matukio, wizi, kuhodhi, upendeleo, rushwa na uwajibikaji, bei ya mafuta, bei ya vitu vingine haya ni matokeo ya utekelezaji. Sasa tunasema leo vitendo, kesho ndoto, jana historia, tenda leo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba Serikali hii, kwanza utaratibu wa Bunge lako Mheshimiwa Spika, zamani tulikuwa tunastukia tu Semindu Pawa swali lako linatokea. Sasa hivi upo utaratibu huu mzuri. Napenda nipongeze Mheshimiwa Spika kwa utaratibu huu kwamba, najua kwamba wiki ijayo nina swali hii inatufanya tunajipanga vizuri kwamba unaweza ukajiandaa. *(Makofi)*

Pia utaratibu wa kujibu maswali, naambiwa swali langu namba moja, ambalo limetoa na takwimu sahihi, sasa mimi nafanya *verification*. Bahati nzuri mtoto wangu Mashishanga ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, yupo hapa sikuoni sina machoni kichogoni, lakini unasikia sauti yangu, kwamba hili jibu la takwimu ilishaletwa nakala nilipopata tu nikapeleka kwako kwa *fax* na umelipokea. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, naomba ufanye tathmini ongea na kijana wako Mkuu wa Wilaya, ambaye naye niko naye pamoja. Uongozi mnakuwa pamoja kama kuna mapungufu mtaelezana hapo hapo. Mimi nina tabia moja ya kucheza dhikiri bila dufu, ukipiga ngoma watu wasikie nje, unazipiga dhikiri kwa sababu dhikiri haiimbwi unafanya aah! Aaha! Kwa hiyo, ndani kwa ndani tu. Kwa hiyo, katika taratibu kama hizi tumezitumia Morogoro. Mfumo shirikishi unakaa *DC*, kama ana mapungufu unamwita *DC* mbele ya Mkuu wa Mkoa, mbele ya Madiwani, mnasema kuna mapungufu moja, mbili, tatu yepi ambayo unadhani unaweza ukayabadilisha na kweli yapo mabadiliko tuko pamoja kwa kazi hiyo Morogoro inasonga mbele hili maswali majibu yake piga *photocopy* peleka jimbo zima. Ahsante nashukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lingine utaratibu ambao tumeupata kuhusu malipo ya walimu, tumepata jedwali kila mkoa tunayo hapa. Msidhani tuliyozungumza haya kwamba hayapo, kila mkoa wamepewa walimu wanadai kiasi gani, kwa hiyo hili tutakabidhi. Tunakuambia Waziri Mkuu tutamkabidhi Mheshimiwa William Lukuvi ampe mtu anayehusika na hili na kufanya *verification* kama fedha hizi zilipelekwa ili kusudi tusiwindane, tutunze mambo kupata jawabu kwa sababu tunakoelekea ni karibu zaidi ambazo ndiyo kuna mazito. Tukipambana tu tutawachanganya Watanzania wanaotaka kutupa kura. Huo ndiyo utaratibu ambao tunaweza tukaufanya.

Mheshimiwa kwa hiyo, baada ya kusema hayo naingia hoja ambazo ni mahususi. Hoja ya kwanza nimesema rushwa. Hivi kwa nini rushwa izungumzwe na viongozi na mara nyingi vyombo vya habari na watu wengine huzungumza mtu anayepokea peke yake na sheria inasema rushwa ni adui wa haki, mpokeaji na mtoaji wote wana makosa. Hivi kwa nini watoaji wasisemwe nao? Kwa nini wapokeaji peke yake huandikwa? Kama alipokea peke yake aidha kaokota, au kapata bahati nasibu aliompa nani? Kwa nini wanaotoa wasitangaze? Kwa nini waache Mbunge mimi niseme kuna rushwa kwa nini yule aliyetoa ebu jitokezeni. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba watu wote waliotoa rushwa wadogo wadogo ambao wamewapa wakubwa tumieni anwani ifuatayo; Mwenyekiti Apunaki Box 941 Dodoma. Sasa haya mambo ya maneno mnajua kelele nyingi mbuzi alikosa mkia kwa sababu ya kelele. Mbuzi alikosa mkia kwa sababu ya kelele. Wakati alipangwa foleni na wanyama wengi na Mungu wapate mikia basi aliambia pateni, mikiani mbuzi akaanza kupiga kelele kwenye foleni pale pale Mungu kamwita njoo, kumwita kumwambia mbona unapiga kelele chukua mkia wako mapema, akapewa mdogo kweli kweli. Sasa kelele zina matatizo, kuna wakati mwingine wanyama waliotulia kama simba, ng'ombe mpaka tumbiri waliufuma mkia kwa sababu walinyamaza walitulia. Sasa kupiga kelele mara nyingi hakusaidii kwa sababu ya hiyo. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, rushwa haiji kwa kukemea kwa kelele kwa ushahidi maalum. Ila kuna rushwa nyingine ile ambayo wakubwa wanawapa wadogo kwa ajili ya kupata madaraka, hiyo, mnaopokea na ninyi tuambieni kwamba fulani kanipa kwa sababu ninyi tutumie kama ni mitego ili muweze mkatutambulisha kwa mambo hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, rushwa basi tunatupendekeza kuwe Muswada wa sheria uletwe kuhusu rushwa ili kusudi angalau wagodo wale wanatoa rushwa, iwe ni chambo kuwakamata wakubwa badala ya sisi kushirikishwa wakati mwingine pengine wakubwa wengine tunajihami tunakemea rushwa mbele ya umma kumbe sisi wenyewe ndiyo tunaopokea. Kwa hiyo unakuta kwamba vitu kama hivi siyo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majibu ya kujihamia yalitokea wakati nilipokuwa nafundisha civics niliuliza nani aliyekuwa anatuhumiwa katika ulipuaji mabomu Tanzania na Kenya? Sasa wanafunzi walikaa hawajui walitaka waseme Osama Bin Laden lakini hawajui, nikamteua mwanafunzi mmoja nikasema wewe, yule mwanafunzi hakusema sijui akasema siyo mimi alidhani yeye ndiyo namtuhumu. Sasa majibu kama haya hayatakiwi. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa viongozi wa aina kama hiyo wanakuwa na maneno mengi wanapokuwa wanajibu wanasema nitafanya juu chini, nitafanya kufa na kupona, fumbu fumbua, kwa makini, kwa karibu zaidi, penda usipende, tuko mbioni, nenda rudi, panga pangua, utake usitake, kila hali. Sasa majibu haya yote kwa kweli yanalenga katika kumuepusha mtu katika lawana ili kusudi asitekeleze wajibu wake. Punguza maneno fanya kazi. *(Makofi/Kicheko)*



Mheshimiwa Spika, baada ya kusema napenda kuzungumzia Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, mafanikio ya jimbo langu, yanatolewa kila wakati katika ilani ya uchaguzi ya kila mwaka na nafanya vipindi vile na vitabu vimeshatolewa. Sasa hivi tunaandaa utaratibu wa kueleza mafanikio ya jumla ya nchi yetu. Tuliwaambia kabisa uchumi wetu unakua, lakini hamuoni matokeo ya uchumi huo, ule ni uchumi jumla. Nimesema hela inachukia mifuko kuipata si rahisi lakini ukiipata inatoka. Hii kwa sababu aidha uchumi unakua au kuna walafi, badala ya kutumia vijiko kula chakula chetu cha mchana tunachokaribishana wanajilisha kwa kutumia mabeleshi. Sasa hao kwa Serikali iliyoko mbele yetu itafanya kazi ya kuwaondoa mmoja mmoja ili kusudi, sekta ziwe zinagawiwa sawa sawa. *(Makofi/Kicheko)*

Lingine barabara nashukuru zinatengenezwa barabara ya Mkulazi toka uhuru ilikuwa ina majanga mengi sana. Jana nilipiga simu greda liko Mkulazi linakuja kushughulikia. Naomba wamalize kazi ile kabla ya bodi ya barabara ya Jumamosi, Mwenyekiti, unanisikia hapo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kengele imelia?

**WABUNGE FULANI:** Bado.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Bado afadhali nashukuru. Mwisho ni kwamba Serikali kama hii ambayo iko makini katika kusimamia mambo ni kwamba mara nyingi unajitahidi kuleta takwimu, kueleza ukweli, kuwa na uwazi na mambo mengine. Sasa swali la Dodoma, kuhamia Dodoma mwakajuzi, niliseme Kinyonga mzee toka tulipohamia Dodoma angekuwa ameshafika hapa kwa kutumia miaka mitatu na nusu na angekuja kutoka Dar es Salaam kuja hapa angetumia masaa 48 kwa kila kilometa moja angetumia miaka tisa kuja Dodoma na kurudi Dar es Salaam kuchukua mkewe na kumrudisha hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala la Dodoma sasa tumefurahi kwa vile Waziri Mkuu, ameshaanza kuhamia. Ulipohama Imamu nashukuru Mashekh watakufuata. Nadhani awamu inakuja kwa sababu naona watatoa sana watakufuata. Kwa hiyo, najua kabisa atakayekuja wakati, mwingine unakuwa ukiteua unamwambia wewe uko tayari kuhamia Dodoma? Wakati mwingine hii kuhamisha Wizara nusu na nyingine nusu kubaki kule sawa sawa na nyoka mwenye vichwa viwili aliyekatawa katikati, wanasema dumila ambaye ana vichwa viwili badala ya kumuua unamkata katikati kwa hiyo, unapata gharama mbili, moja kulisha nyoka wawili badala ya mmoja, pili kutibu majereha ya nyoka wawili uliowakata. Kwa hiyo, inaleta matatizo tuchunguze haya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kuna matatizo ya *NGOs* fulani ambazo zimejitokeza ambayo kijana wangu Mashishanga aliwahi kufuatilia hili, kama nilivyosema tuko pamoja na uongozi wa Wilaya, Mkoa na hii Mungu analeta heri hawezi kuleta matatizo. Kwa hiyo, kuna *NGO* moja inafanya vurugu kule milimani, wanakata migomba yawananchi, kwa hiyo, *RAC* alitwa yupo hapa niliongea naye wanafuatilia, naomba Tume iliyofuatilia kule Vijiji vya Luholole, Changa, Kibwaya, Mfumbwe, Logo, Uponda, Mifuru, Hewe, Bagilo, Nyamigadu, Mkololo, Kumba, Amini, Ludewa, Burugi,

Lung'ala mpaka sehemu za Bamba mpaka Kilopa wale wananchi tumie Maafisa Watendaji ili kusudi waweze kufuatilia kusema ukweli Jumamosi narudi mje pale mtalipwa nauli zenu na nitawaambia kabisa kwamba tumwone nani ili tumuondoe tufute NGO ile tuunde ya kwetu. *(Kicheko)*

Watanzania tuwe pamoja tuseme macho mbele tuangalie wenzetu, tuiseme mate mbele tukaonja vitu vyao. Ahsante nashukuru.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Pamoja na kuipongeza Serikali kwa juhudi zake katika kusukuma maendeleo ya Taifa, yapo maeneo yanayohitaji kuangaliwa.

Suala la madai ya Walimu halijaonekana popote katika Hotuba ya Waziri Mkuu. Walimu ni tegemeo kwa Taifa, maana bila Walimu wanaotoa Elimu kwa moyo, tutabaki na Taifa la wajinga. Walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana Vijijini, ambako sehemu nyingine hata magari hakuna. Wanatembea kwa miguu, hawana umeme bali wanatumia vibatari tu. Njia ya kujikwamua ni wao wenyewe kujinunulia taa nzuri. Lakini Walimu wanadai arrears za mishahara (Shule za Msingi) Sh.13 bilioni, wakati Walimu wa Vyuo vya Ualimu na Sekondari wanadai Sh. 4 bilioni. Je, hii ni haki, kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa uhakika wa kulipa madeni haya ya Walimu? Kwa nini Walimu wananyaswa hivyo?

Hivi kweli Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu au Hazina wanaweza kukaa mwaka bila kulipwa? Walimu wote wanapoajiriwa mara ya kwanza hukaa mwaka mzima bila kulipwa. Walimu hawa wanaishi vipi? Je, wakiingia kwenye ukahaba mtawalaumu? Serikali itakuwa inasaidia kuzuia UKIMWI au itakuwa inawahimiza Walimu maskini wajiuze ili waweze kuishi?

Huu urasimu wa kuwaweka watoto wa watu bila mishahara, sio ukiukwaji wa haki za binadamu?

Nashauri Serikali iangalie maeneo yafuatayo na kuyafanyia kazi haraka: Walimu wapya wanapoajiriwa mishahara yao inakuwa kwenye Bajeti, walipwe haki zao bila kucheleweshwa. Urasimu uliopo kati ya Wizara ya Elimu, Idara Kuu Utumishi na Hazina ukomeshwe, Watumishi wazembe wanaochelewesha mishahara ya Walimu wachukuliwe hatua. Walimu wanadai Sh. Bilioni 17 za arrears za mishahara. Arrears hizi ni za Walimu wapya ambao hawajalipwa miezi ambayo walikaa bila kulipwa eti mishahara hiyo imeingia kwenye orodha ya madeni na pia Walimu wamepandishwa daraja lakini hawajalipwa tofauti za mishahara ya zamani na mipya.

Hii ni kero ya hali ya juu. Walimu ni Jeshi la kutegemewa. Serikali iliangalie hili na walipwe arrears za mishahara bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, madai ya uhamisho na nauli za likizo nayo ni kero kubwa, hasa kwa Walimu wa Shule za Msingi. OC inayopelekwa kila Halmashauri izingatie ulipwaji wa madeni hayo.

Nawasilisha nikitegemea kuwa Serikali sikivu ya CCM itachukua hatua haraka kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Pia Hazina kutupiwe jicho, kuna mchezo mchafu wa kula fedha za Walimu.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hoja na maswali mengi humu Bungeni kuhusu matumizi ya fedha za *STABEX*, ambazo zilitengwa kwa ajili ya kutengeneza barabara za Vijiji sehemu zinazolima kahawa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu aliliambia Bunge kuwa itatolewa Kauli ya Serikali, ambayo ilitolewa kuwa fedha zilizolengwa kujenga barabara zingefanya kazi hiyo. Tangu Bajeti ya mwaka 2003/2004 hadi sasa fedha hizo hazijatumika, huku Mawaziri mbalimbali wa Serikali wakitupiana mpira. Ni aibu kubwa kwa Serikali na Waziri Mkuu kunyamaza huku wawakilishi wa wananchi wakiendelea kulia Bungeni kama watoto wadogo kuhusu fedha za *STABEX* kutotengeneza barabara.

Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe msimamo wa Serikali kama ni kutafuna fedha za wananchi au kuacha ulaghai na kulipa fedha hizo ili zifanye kazi zilizokusudiwa. Serikali iache tabia ya kunyonya wakulima maskini.

Mheshimiwa Spika, nitaomba majibu

**MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa ninaomba na mimi kwa niaba ya wananchi wa Kitope, niungane na Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa michango yao kwenye hotuba hii nzuri sana.

Aidha, ninawapongeza Mawaziri wa Wizara hii, Ofisi ya Waziri Mkuu na wasaidizi wake wote, kwa kuandaa hotuba hii ambayo kwa kweli imesheheni sifa zote zinazohitajiwa katika kuwakomboa wananchi wa Tanzania wakati huu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa mchango wangu, naogopa kuwa mwizi wa fadhila kwa kutoipongeza CCM katika chaguzi zake za Madiwani na Ubunge kule Bariadi Mashariki. Nitalisema neno ambalo litakuwa muafaka kuashiria furaha yangu, hakuna ila kumshukuru Mola wetu kwa kukijaalia Chama cha CCM kuwa na viongozi wakweli, waadilifu na wanaotambua nini wanafanya na wananchi wake wanataka nini. Hiki ni Chama cha Ukombozi na kinajali shida za Watanzania wote bila kujali itikadi zao. Aidha, ninasema kuwa Serikali zote za CCM ni Serikali za watu kwa manufaa yao wote au yetu sote.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika hali ya siasa nchini kote Tanzania ni nzuri sana inayotokana na maadili ya chama chetu na imekuwa hivi kutokana na subira na stahimili ya viongozi wetu wakuu kutambua kuwa bila ya siasa bora yenye amani na imani hakuna maisha bora ya watu wetu. Hali hii ya usalama imekuwa haipendwi na baadhi ya

wakorofi wa nchi hii. Nasema hili kwa kuwa wapo wanaoitwa viongozi wa vyama vya siasa, wao kila siku wanaona wawe mstari wa mbele kuhubiri shari na chuki hususan kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar ni sehemu muhimu sana kwa Tanzania na haina budi kuwa salama. Sasa inakuwaje kwa hawa walioishiwa huku Bara na kukataliwa kuelekea kule Zanzibar kuhubiri shari na ugomvi na kwa sababu wanajua fika kuwa sasa ni wakati wao wa kuteleza mitini mote wanamopanda umefika na wanadhania kule Zanzibar ni mahali pa kupandikiza miongoni wetu mawazo haya na matendo haya sasa hayana nafasi kule? Kwa wakati huu ninaomba Ofisi hii ya Waziri Mkuu kuonyeshwa kuchoshwa na vitendo hivi na hatua za haraka dhidi ya hili zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama nilivyotangulia kusema, Wallahi haina cha kuongezea na kwa sababu ada ya mja ni kunena basi ninaomba kuhimiza ushirikiano wa karibu zaidi na Ofisi ya Waziri Kiongozi Zanzibar kufanya kazi kwa ukaribu zaidi. Kwa maslahi ya nchi zetu mbili na kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, wote wanaodhani siku moja Muungano huu utaleta ufa basi wajijue kuwa wameishiwa na kwa hilo ninaomba ule utaratibu ulioandaliwa wa kujenga Ofisi za Wabunge kule Zanzibar sasa utekelezwe kwa madhumuni ya kuimarisha udugu wetu wa Asili. Aidha, ninaomba sana Ofisi hii kwa kujua umuhimu wa kuwako kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kule Zanzibar basi waendeleze juhudi zao kuona Ofisi ya Makamu wa Rais kule Zanzibar inakuwepo.

Mheshimiwa Spika, nimebahatika sana kumwona Waziri Mkuu katika jimbo langu la Kitope na Majimbo mengine kule Zanzibar, akileta mambo ya manufaa na maendeleo majimboni kwetu na tunamshukuru sana na Mola atamuweka na kumpa afya njema zaidi na uwezo wa kufanya mambo ambayo Ofisi yake imeyaeleza kwa ufasaha mkubwa. Tunamhitaji sana wakati huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hotuba hii mwanana inataka kufanyiwa kazi basi naliomba Bunge letu Tukufu tumpe fedha zote alizoomba Waziri Mkuu, akafanye mambo yake mazuri na kwa maana hiyo naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa wasaidizi wako wote, kwa jinsi *Budget Speech* ilivyoandikwa kwa mtiririko. Kwangu mimi ni lazima niseme kwamba hotuba hii na muhtasari wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa kipindi hiki cha awamu ya miaka mitano ya Serikali ya CCM. Hongera sana na inafurahisha kuona jinsi ambavyo Serikali imezingatia ushauri wa Wabunge kwa kipindi chote hiki.

Awamu hii imekuwa ya mafanikio makubwa ya kutuliza na kukuza misingi ya uchumi mkubwa (*Macro-economic Fundamentals*). Baada ya mafanikio haya inabidi sasa kuwe na utekelezaji mzuri wa ujenzi wa uchumi mdogo (*Macro-economics*) na katika

hali ya Tanzania hivi sasa ni rahisi ukaelekeza kwa mafanikio ujenzi huo bila ya kupitia katika kilimo. Kwa kweli kama tunataka kuwe na impact kubwa ni lazima kiwe kilimo cha watu wa chini ambao ndiyo wanazalisha kiwango kikubwa cha mazao ya kilimo cha chakula na biashara.

Kama unavyoainisha katika hotuba yako kwamba nchi isiyojitosheleza kwa chakula haiwezi kuendelea. Ni kweli kwani nasema kuendelea kuwa na mzunguko wa njaa kila baada ya miaka kadhaa hata ujenzi na utulivu wa macro-economic fundamentals utafifia na kwa sababu *macro-economic growth* ndio kivutio kikubwa cha uwekezaji kutoka nje ya nchi itajikuta inakwama huko mbele ya safari na lengo zima la kukuza uchumi kufikia asilimia 8 au zaidi linashindikana kufikiwa. Sasa tufanye nini? Ushauri.

Kupanga ni kuchagua, kwa sababu ya uhaba wa raslimali (*Scarcity of Resources*) lazima tupange vipaumbele kwa vitendo (*priorities*). Kitu ambacho kitatusaidia ni kuhakikisha tunaipa ule mpango wa kila Wilaya kuonyesha zao lake muhimu la biashara na chakula na kuhakikisha kwamba mbolea inakuwa zero rated kikweli kweli, kumhakikishia mkulima kwamba anaipata mbolea hiyo *at cost*. Pamoja na kwamba imepanda kidogo bado mbolea kutoka Mashariki ya Kati inafika *Dar es Salaam Port (CIF value)*, kwa gharama ya wastani wa Sh. 10,000/= au kidogo kwa mfuko wa kg. 50. Inakuwaje tunaruhusu mfuko huo Tabora na Urambo kuuzwa kati ya Sh. 20,000/= mpaka Sh. 25,000/=, faida ya wafanyabiashara binafsi ni kubwa sana, lazima iratibiwe. Nchi isiruhusu faida kubwa namna hii kwa biashara mbolea matokeo yake ni njaa. Kwa sababu watu wanalima bila mbolea katika ardhi iliyochooka, wanapoteza nguvu zao bure, watu wa namna hii sio wavivu bali watahitaji msaada kuimarisha mtaji wao ambao ni nguvu zao wenyewe. Tatizo hili ni kubwa zaidi kuliko hali ya hewa kwa mfano, asilimia 40 ya wakulima wa Urambo wapo katika *category* hii. Naamini wangepatiwa msaada huu wa ziada ya chakula Urambo, ingetosheleza Mkoa mzima wa Tabora. Ninaomba mpango huu na hasa kwa Wilaya ya Urambo ifufuliwe na tupewe msaada msimu huu ili kufuta njaa.

**MOHAMED ALI SAID:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukushukuru wewe binafsi. Pili, niwashukuru Wabunge wenzangu wote waliomo humu Bungeni.

Pia napenda kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na ndugu yake, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao na hivyo hivyo ninawafariji wale Wabunge waliopata matatizo kwa kuvamiwa na majambazi ikiwa ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na matatizo ya ajali ya gari aliyoyapata Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie kuhusu uchumi wa nchi. Napenda niseme kuwa uchumi wa nchi yoyote duniani hauwezi kuwepo ikiwa nchi hiyo haina umeme.

Mheshimiwa Spika, nikueleze kuwa mpaka sasa hivi Pemba haiwezi kuendelea kutokana na ukosefu wa umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Pemba kumetengwa maeneo huru kwa ajili ya wawekezaji, lakini hadi leo hii hakuna mwekezaji yeyote aliyekuja kuwekeza. Hii ni kwa sababu ya ukosefu wa umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, ninasikitishwa sana na Shirika la Umeme (*TANESCO*), kwani lilikuwa tayari limeshaweka nyaya za umeme katika sehemu moja inayoitwa Meli Tano kwa ajili ya kutandika kwenye bahari kutoka Tanga. Lakini hilo suala lilishindikana sielewi kwa sababu gani hata zile nyaya zilichukuliwa?

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukosefu wa umeme wa uhakika, Pemba imetengwa na maendeleo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya yote haya, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, azungumze na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili Pemba tupate umeme wa uhakika wa *TANESCO*. Kwa ajili ya kuendeleza maendeleo Kisiwani Pemba.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniruhusu kutoa mchango wangu huu kwa maandishi. Ahsante sana.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza bajeti hii kwa namna ilivyoandaliwa na kuwa wazi kwa kufafanua utekelezaji wa Ilani yetu ya Uchaguzi. Naiunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha hoja hii, nitazungumzia mambo kadhaa pamoja na mapendekezo mbalimbali kama ifuatavyo:-

Upungufu wa wataalam Rukwa umo katika maeneo ya Madaktari, Walimu wa shule za sekondari na za msingi. Madaktari wamekuwa hawaendi ingawa wanapangwa. Katika hili napendekeza kuwa Serikali ifanye jitihada za makusudi kutuletea Madaktari mkoani Rukwa. Kwa kuzingatia zaidi wale ambao wamekwishaanza kazi badala ya wapya. Kwa wale wapya, Serikali irudie utaratibu wa zamani wa watumishi kufanya kazi kwa Mkataba wa miaka mitano, baada ya hapo waruhusiwe kuendelea kufanya kazi.

Sehemu nyingine ni walimu wa shule za sekondari. Mkoa wa Rukwa una upungufu wa walimu 323 wa sekondari. Hali ambayo inafanya baadhi ya shule kuwa na walimu wawili tu. Hivi hali hii itakuwaje na hivyo elimu itatolewaje? Aidha, utakuta shule inaitwa ina mchepuo wa kilimo lakini mchepuo upo mwalimu hakuna. Naomba Serikali ilianganalie.

Rukwa ina upungufu wa walimu 1624 wa shule ya msingi, hali ambayo inafanya darasa la kwanza mpaka la saba lina mwalimu mmoja tu. Hivi huyo mwalimu atafundishaje? Tunaomba Serikali iingilie kati, kurekebisha hali hii na ikiwezekana utolewe Waraka wa kurekebisha hali hii.

Kuhusu suala la mbolea ningependa kutoa mapendekezo kuwa Serikali ihakikishe mbolea inafika Mkoani Rukwa Agosti, 2004 ili kuanzia Septemba hadi Oktoba, 2004

mbolea isambazwe Vijijini, ili mkulima atakapoanza kilimo mwezi Novemba, mbolea tayari iwe imeshafika mikononi mwa wakulima. Pia Serikali ihakikishe ruzuku inayotolewa iwezeshe mkulima kupata nafuu ya bei ya mbolea. Maana hadi sasa mkulima hajaona nafuu wowote, maana sasa ruzuku yote inachukuliwa na wasafirishaji.

Kwa vile idadi ya Watanzania kufuatia sensa ya mwaka 2002, tumefikia zaidi ya milioni 30 na *SGR* yetu tuliyonayo hivi sasa ina uwezo wa kuhifadhi chakula tani 150,000. Kutokana na ongezeko hilo la Watanzania napendekeza Serikali kuwa idadi ya kuhifadhi chakula sasa itoke tani 150,000 hadi tani 300,000 mpaka 500,000. Pia fedha za kunulia chakula hicho zipelekwe mapema Mikoani hasa hasa ile Mikoa inayozalisha ziada kama vile Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Ruvuma na Iringa.

Nampongeza sana Mheshimiwa Edward Lowassa na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara ya Maji. Suala la maji katika Wilaya ya Mpanda na Sumbawanga Vijijini ni tatizo sugu na Mheshimiwa Waziri Mkuu, anakumbuka alipokuja katika ziara Mkoani Rukwa hususan Wilayani Mpanda, moja ya kero aliyoelezwa na wananchi wa Wilaya hiyo ni maji, naye aliahidi kulipatia ufumbuzi. Wananchi wana imani na kauli yake. Hivyo, kwa vile hili ni tatizo sugu, nashauri Serikali iliwekee mkakati maalum wa kulitatua. Vile vile ninapendekeza Serikali iweke mkakati maalum wa kuchimba visima vya maji katika kila Kijiji, shule za sekondari na msingi japo wapate kisima kimoja kimoja. Utaratibu huo nafikiri utasaidia sana kupunguza tatizo hili maana wananchi husumbuka sana kutafuta maji wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED JUMA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wote wa Kisiwa cha Pemba, nimshukuru sana Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza kwa kutembelea Shule ya Sekondari ya Fidel Castro huko Pemba, kujionea hali ilivyo skulini hapo lakini pili kwa mchango wake wa shilingi milioni kumi aliutoa katika kusaidia kuboresha hali ya shule hiyo ambayo yeye mwenyewe alikiri kuwa kwa Tanzania hii hajawahi kuona Shule ya Sekondari iliyo katika hali duni sana kushinda Fidel Castro. Mchango huo wa Mheshimiwa Rais ulisaidia sana kuboresha mazingira ya shule hiyo, tunashukuru sana.

Aidha, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Mkapa kwa kupevuka kisiasa. Katika kupevuka kwake huko kisiasa, siku hizi anaonekana kutofautisha shughuli za Kitaifa na zile za kisiasa. Katika majukwaa ya Kitaifa huelekeza fikra zake kwenye Utaifa zaidi kuliko kwenye ukereketwa na ushabiki wa kisiasa. Hata maamkizi yake huwa kwa wananchi na sio kwa wafuasi wa Chama chake ambao huwa wamekusanyika kwa wingi katika halfa kadhaa za Kitaifa. Kwa mfano, pale Rufiji alipokuwa anafungua Daraja la Mkapa aliamkiana na umma kwa kusema: “Tanzania Oyee!”, “Maendeleo Oyee!” na kadhalika sio “Kidumu Chama cha Mapinduzi”! kama wadogo zake wengi

walivyofanya ambapo sio ustaarabu hata kidogo kutoa maamkizi hayo katika mazingira kama yale, nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa niingie katika mjadala. Katika kufanya hivyo niseme kuwa baadhi ya wenzangu humu ndani wameeleza kuwa hali ya kiuchumi Zanzibar sio nzuri na wakaonesha wasiwasi wao kwa ustawi wa Zanzibar iwapo hali hiyo haikupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, mimi sitajikeleza kwenye uchumi bali kwenye siasa na ninasema kuwa hali ya kisiasa Zanzibar ni mbaya sana. Ukimya na utulivu unaoonekana kule hivi sasa ni wa muda mfupi sana ni sawasawa na time bomb linalosubiri wakati wake ufike lipate kupasuka au kulipuka.

Mheshimiwa Spika, licha ya kupatikana kwa Muafaka wa kisiasa baina ya Vyama vya *CUF* na *CCM*, wenye nia ya kutuliza hali iliyojitokeza baada ya uchaguzi wa mwaka 2000 na zaidi kabla na baada ya matukio ya Januari 28, 2001 ambayo yalikuwa ni ya kutisha sana. Baada ya kusainiwa kwa Muafaka na ahadi nzito za utekelezaji wa Muafaka huo mbele ya umma wa Watanzania waliohudhuria halfa hiyo muhimu na ya kihistoria zilizotolewa na Viongozi Wakuu wakiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano na Rais wa Zanzibar, ambao wao kwa nyadhifa zao hizo wakipenda wanaweza kuzuia kabisa hali iliyotokea na kusababisha kuitia doa nchi yetu hasa pale ilipozalisha wakimbizi badala ya kawaida yake ya kupokea wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, nasema pamoja na Muafaka hali ya kisiasa Zanzibar ni mbaya na kwa maoni yangu hali hiyo inasababishwa na mambo yafuatayo:-

Kwanza kukosekana kwa nia njema (*goodwill*) kwa viongozi wetu ambapo kutokana na hilo mambo kadhaa hata yale yasiyo na gharama yoyote ya fedha katika kutekelezwa kwake bado hayajatekelezwa. Mabadiliko ya mfumo wa Mahakama Zanzibar hadi leo hii hayajafanyika. Mahakama za Zanzibar hadi sasa sio huru na hazina sura ya Mahakama bali taasisi zinazolinda maslahi ya SMZ na CCM. Kesi hasa zile zenye mwelekeo wa *CUF* kushinda hazisikilizwi ila hupigwa tarehe za mbali tu. Mfano wa kesi hizi ni kama vile kesi ya kupinga kutangazwa waliokuwa wagombea na CCM kuwa washindi wa nafasi ya Uwakilishi katika Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili ni ile kesi ya kupinga kuwekewa pingamizi waliokuwa wagombea wa *CUF* kwamba haikuwa ya haki. Kesi zote mbili hizo haziendi, zimetelekezwa kabisa. Matokeo yake ni manung'uniko kuwa Mahakama sio huru na inazuia haki kupatikana. Katika Muafaka ule kuna kipengele kinachomtaka Rais wa Zanzibar kuwateua Wawakilishi wawili kutoka Chama cha *CUF* hadi leo hii amemteua mmoja tu. Aidha, Sekretarieti ya Tume ya Uchunguzi bado ni ile ile ya kabla ya Muafaka na huku yapo makubaliano katika Muafaka kuwa chombo hicho cha utendaji cha Tume kiundwe upya. Pia hadi leo uteuzi wa wafuasi wa Upinzani katika nafasi kadhaa kama vile za Ubalizi, katika bodi za Wakurugenzi na kadhalika haujafanyika. Mambo hayo yote hayana gharama yoyote katika kutekelezwa kwake, kwa nini hayajatekelezwa? Jawabu ni kukosekana kwa nia safi.



Mheshimiwa Spika, mambo mengine yanahitaji fedha lakini nayo yalitolewa ahadi na hali ikijulikana kuwa fedha zingehitajika lakini ilionekana ni vyema katika kuponya majeraha ili kuondoa chuki na hamasa. Serikali ilitoa ahadi ya kutoa kifuta machozi kwa waathirika mbalimbali wa matukio ya Januari 27, 2001. Mpaka leo vifuta machozi hivyo havijatolewa licha ya maneno na ahadi tamu zinazotolewa na Serikali zetu zote mbili.

Mheshimiwa Spika, kutokutekelezwa kwa Muafaka katika vipengele hivyo kunaonesha kuwa njia ya mazungumzo sio ya kutegemea kwani makubaliano yanayofikiwa kwa ridhaa ya yule aliye madarakani akipenda atatekeleza asipopenda hatekelezi. Jambo hili ni hatari sana kwani litokeapo tatizo lingine hatutakuwa tena na pa kukimbilia kwani mazungumzo huwa hayaaminiwi tena kutatua matatizo.

Mheshimiwa Spika, pili ni kauli mbalimbali zinazosikika kutoka kwenye vinywa vya Wazanzibari mbalimbali, wanaotawala wanasema: “Serikali hatutoi” na wanaotawaliwa (Wapinzani) wanasema “Safari hii hatukubali kwa vyovyote kuibiwa au kuporwa ushindi wetu”. Mambo hayo hayana dalili njema na yanahitaji kufanyiwa kazi kwa busara, hekima na uzalendo. Mimi kwa maoni yangu dawa ya kuzuia yasitokee tena yaliyotokea kama dhamira ya Muafaka ilivyo ni kwanza, Muafaka utekelezwe kikamilifu na pili lazima Serikali na Vyama pamoja na Tume za Uchaguzi lazima zihakikishe kuwa chaguzi zote zijazo zitakuwa huru na za haki.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. SHARIFA MBAROUK KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kuchangia, naomba kuwapa pole wale wote waliopata msiba na wote ambao wamepata matatizo wakati walipokuwa safarini kuelekea Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kwa kuanzia uvuvi wa Bahari Kuu. Katika kuimarisha na kukuza uchumi wa nchi yetu, suala la kuanzisha uvuvi wa Bahari Kuu ni muhimu uzingatiwe. Wananchi wetu ambao hujishughulisha na uvuvi kipato chao ni duni kutokana na kuwa hawana uwezo wa kuendeleza uvuvi kutokana na zana zao kutokidhi haja. Hivyo, ili kuongezea mapato naiomba Serikali hatua zichukuliwe kwa kutafuta wawekezaji wenye uwezo wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kuipongeza Serikali kwa kuiendeleza *TASAF* kwani imetusaidia kuondoa kero mbalimbali kwa wananchi wetu hasa Pemba. *TASAF* imesaidia sana kuleta ufanisi katika vijiji vingi kama vile ujenzi wa shule, zahanati, maji, madaraja na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali kwa juhudi wanazochukua kwa kutoa elimu kwa wananchi wake kuhusu masuala ya UKIMWI. Hata hivyo, naishauri Serikali kuzidi kutumia viongozi wa dini na kuelekeza nguvu zake kuhamasisha kufuata maadili yetu. Pia Serikali ipunguze semina na makongamano badala yake iendelee kuongeza fedha za kununulia dawa ambazo zitawasaidia waathirika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, kwa vile mwaka 2003/2004 hali ya chakula Wilayani Karatu haikuwa nzuri na hata msimu huu hali ya mvua nayo haikuwa nzuri na hali ya mazao katika Vijiji vya Qurus, Changarawe, Bashay, Endamagare, Laja, Kansay, Endabash na Bassodawish ni mbaya sana na hali katika Vijiji vya Kimamoja, Chemichemi, Gyekurum Lambo, Dumbechau, Makhromba, Mangola Juu na Oldeani ni chini ya wastani, yaani zaidi ya nusu ya vijiji vyote. Ni imani yangu kuwa Serikali itaweka mkakati mzuri zaidi mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karatu imekumbwa na ukame sasa kwa muda mrefu na siyo kutokana na uzembe au uvivu wa wananchi. Hivyo, tunahitaji mpango wa kuweza kuwakwamua, angalau kwa mbegu ili wananchi wajiandae vizuri zaidi kwa msimu unaokuja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za jamii. Kwa vile Wilaya ya Karatu imejitahidi katika kupunguza kwa kiwango kikubwa tatizo sugu la maji, karibu vijiji 25 kati ya 45 sasa vina miradi ya maji inayoendelea au iliyokamilika na kwa vile Sera ya Maji 2002 inatamka wazi kuwa watumia maji walipie gharama halisi ya maji ili kufanya mradi uwe endelevu na kwa kuwa mgogoro wa maji katika Vijiji vya Troma na Ayalabe unahatarisha uhai wa miradi yote ya maji Wilayani Karatu; je, Serikali iko tayari kuunda Tume huru itakayochunguza kiini hasa cha mgogoro wa maji katika Wilaya kwa nia na lengo la kuwarudishia imani wananchi na wafadhili ambao nao pia wamekatishwa tamaa na mgogoro huu?

Kwa bahati mbaya pande zote husika hazijawekwa pamoja na kusikilizwa. Ni imani yangu kuwa hatua hiyo itasaidia kuondoa mgogoro na kurudisha imani kwa wafadhili hasa wale ambao majadiliano yako hatua ya mwisho kuwekeza miradi ya maji katika vijiji vilivyobaki. Hivyo basi, kwa vile mgogoro sasa uko juu ya Wizara moja, naamini Ofisi ya Waziri Mkuu pekee ndiyo inayoweza kutatua matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ya Katiba na Sheria ilipokuwa inajadili bajeti ya Waziri Mkuu, niliuliza swali kuhusu *Contractor Epsilon*, ambaye alileta vifaa pungufu vya TVT au *sub-standard*. Kamati ilijibiwa majibu yasiyoridhisha kuwa Mkandarasi huyo alikuwa ameshaleta vifaa vyote isipokuwa havijafungwa bado. Siku mbili baadaye, Mkandarasi huyo alifikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisuti. Isitoshe, Serikali ilishindwa kutoa maelezo ya kuridhisha kwa Kamati kuhusu *Contractor* wa majengo ambayo hadi leo yamebaki magofu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaeleza nini kuhusu hali hiyo ambayo ina mwelekeo wa kuficha ukweli kama Kamati ya Bunge? Je, ukweli hasa ni nini kuhusu Mkandarasi huyo ambaye wakati anapewa *contract* hata Kampuni yake inasemekana haikuandikishwa nchini Tanzania? Wahusika na *contract* hiyo ambao wamelisababishia Taifa hasara kubwa kwa taarifa rasmi ya *CAG*, wamechukuliwa hatua gani?

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe msimamo wangu wa dhati kuwa ninaunga mkono hoja ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi za Wabunge, ni maoni yangu kuwa Ofisi za za Wabunge zisimamiwe na Ofisi ya Bunge. Fedha za ukarabati, samani za Ofisi na uendeshaji wa Ofisi za Wabunge, ziwekwe kwenye kasma ya Ofisi ya Bunge. Maafisa wa Bunge washirikiane na Ofisi za Wakuu wa Wilaya kufanikisha jukumu hili. Lakini Ofisi ya Bunge ndiyo iwajibike katika suala hili. Ikiwezesha, naamini ina uwezo wa kufanya kazi hii kwa mafanikio. Mabunge yaliyo mengi duniani hutumia utaratibu ninaopendekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa suala la rushwa, Serikali inafanya kazi kubwa kupambana na rushwa. Naipongeza Serikali kwa kufungua Ofisi za *PCB* mpaka Wilayani. Vile vile *PCB* inawezeshwa kuajiri vijana wasomi kufanya kazi za kipelelezi kama *professionals* na pia kuendesha mashtaka kwa ujuzi ufaao. Kuna suala moja ningependa nishauri kama Mwanasheria. Kumekuwepo malalamiko kwenye Vyombo vya Habari kuwa rushwa inazidi kuongezeka na inahusisha viongozi.

Mheshimiwa Spika, matamshi ya Serikali yameendelea kuwa walalamikaji walete ushahidi unaoweza kudhihirisha makosa hayo Mahakamani. Suala la rushwa ni kosa la jinai, hivyo kiwango cha kudhihirisha kosa ni kiwango cha juu sana, yaani *proof beyond all reasonable doubt*. Haiwezekani mtu binafsi aweze kukusanya ushahidi wa kiwango hicho. Kazi hiyo inaweza kufanywa na vyombo vya dola pekee kama vile *PCB*, Polisi kupitia Idara ya Kitaalam, yaani *CID* na kadhalika. Kupata ushahidi si jambo jepesi.

Mheshimiwa Spika, jukumu la mwananchi ni kutoa malalamiko rasmi Polisi, *PCB* na kadhalika kama wafanyavyo *informers* wa Polisi na walalamikaji wengine. Baada ya hapo, Polisi hufuatilia malalamiko au taarifa hizo na kupata ushahidi ufaao. Kama hakuna ushahidi, Polisi hufunga faili. Hivyo, kusema wananchi walete Ushahidi katika malalamiko ya rushwa, *is not in good taste*. Serikali iwahimize wananchi wawasilishe malalamiko rasmi *PCB* au Polisi basi.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kutoa maoni yangu kuhusu matumizi ya rushwa katika Uchaguzi wa Viongozi. Tatizo hili limeanza kuwa *out of control*. Watoa rushwa wanasifiwa na kupiganiwa mpaka vijijini. Kwa upande wa CCM kama Chama Tawala, tatizo letu kwa Uchaguzi Mkuu ujaar wa 2005 siyo suala la Vyama vya Upinzani. Tunaweza kudhibiti vishindo vyake. Lakini tatizo la rushwa ndani ya CCM ndiyo tatizo kubwa na la hatari kabisa.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili lisipodhibitiwa kikweli kweli, CCM itaanza kumomonyoka. CCM ikimomonyoka kwa wakati huu ambapo Vyama vya Upinzani ni dhaifu sana, itahatarisha usalama wa nchi. CCM ina wajibu wa kihistoria kurekebisha kwa dhati hitilafu hii. Vinginevyo tunaweza kujikuta tumepata hata Mgombea wa Urais akiteuliwa kwa kura za rushwa. Lazima tuweke vigezo vilivyo dhahiri vya uadilifu, vinavyotekelezeka na siyo vile vinavyoweza kupukutika kutokana na mawimbi yenye nguvu kubwa ya rushwa. Kiongozi anayepatikana kwa rushwa hawezi kuongoza nchi ikawa ya amani na mshikamano. CCM inao wajibu mbele ya Mwenyezi Mungu, kulilinda Taifa hili lililoasisiwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Mzee Abedi Amani Karume.

Tatizo la UKIMWI linazidi kuhatarisha uhai wa vijana wetu na wananchi kwa ujumla. Juhudi kubwa zinafanyika kupambana na janga hili. Kumekuwa na ubishani mkubwa juu ya matumizi ya kondomu kama njia mojawapo ya kupambana na maradhi haya. Kwa maoni yangu, naona ni makosa kuwataka Viongozi wa Dini wahimiza matumizi ya kondomu katika mahubiri yao. Viongozi wa Dini watatusaidia zaidi kuhimiza waumini wasifanye dhambi ya kuzini, kuwa ni machukizo mbele ya Mungu.

Mheshimiwa Spika, kuzini ni kosa, hata kama tendo hilo likiwa limefanyika kwa kutumia kondomu au bila kutumia kondomu. Hivyo, wajibu wa Viongozi wa Dini zote uwe ule wa kawaida wa kuwafanya watu wamfuate Mungu na kujikatalia. Ni katika ndoa tu tendo hili ni halali kwa Viongozi wa Dini. Baada ya hapo, wale ambao hawataki kufuata maelekezo ya Viongozi wa Dini, basi viongozi wengine wasio wa Dini, wanaweza kushauri matumizi ya kondomu. Mtumiaji wa kondomu awe *responsible* na uamuzi wa kwanza wa kufanya tendo la ngono nje ya ndoa na pili uamuzi wa kujilinda kwa kutumia kondomu. Isiwe kama vile ni lazima watu wafanye ngono.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwasilisha hotuba yake kwa utulivu na umakini. Kadhalika niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kufanikisha maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hotuba hii ninauelekeza katika mambo matatu makubwa: Maandalizi ya Daftari la Wapiga Kura, Sekta ya Habari na vita dhidi ya Ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa kwamba, Tume ya Uchaguzi ya Taifa (*NEC*), inakabiliwa na maandalizi ya Daftari la Wapiga Kura. Umuhimu wa Daftari hilo unajulikana na ndiyo maana Serikali inaviomba Vyama vya Siasa nchini kutoa elimu kwa wanachama wao kuhusu umuhimu wa Daftari la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hatukuelezwa bayana ni lini Daftari hilo litaanza kuandikishwa na iwapo litawahi kutumika au la katika chaguzi za mwaka huu za Serikali za Mitaa na Vitongoji. Tunaiomba Serikali ituwekee bayana masuala hayo mawili ili kuondoa dhana mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kutoa ushauri kwa Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuzingatia yafuatayo katika hayo maandalizi ya Daftari la Wapiga Kura: Taratibu za kujiandikisha, uteuzi wa Maafisa Uandikishaji (utaratibu wa kuwapata na sifa zao), uteuzi wa Wasaidizi Maafisa Uandikishaji (utaratibu na sifa zao), uteuzi wa Makarani Uandikishaji, wanaofaa/wasiofaa kujiandikisha (nani ata-*verify* hawa), utaratibu wa pingamizi, utaratibu wa *Appeal* kwa wale waliowekewa pingamizi, namna ya kuhamisha majina ya wale wanaohama jimbo moja kwenda jingine, uandikishaji chini ya umri wa miaka 18 na namna ya ku-*update* Buku la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa Wapiga Kura ihusishe wadau wote, kuandaa mtaala na *content* ya hiyo elimu ya Wapiga Kura na namna ya kuisambaza elimu kwa kutumia taasisi na kwa njia mbalimbali. Kuzingatia *authenticity* ya vifaa vya kujiandikisha na udhibiti na ugawaji wa vifaa vya kujiandikisha. Pia *verification of the dully filled in OMR forms* kabla ya kufanya *scanning* na kuingiza *data* hizi kwenye *data base*.

Mheshimiwa Spika, tukiweza kufanya hivyo, tutaweza kuondoa mashaka miongoni mwa wadau na kadhalika kuwa na chaguzi zilizo huru na haki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Habari. Sote tunafahamu kwamba, Kiswahili ndiyo lugha yetu ya Taifa na kwamba Tanzania ndiyo chimbuko la lugha ya Kiswahili kuenea kwake ulimwenguni. Kutokana na sababu hizi, ni wajibu wetu Watanzania kukiheshimu, kukienzi na kukiendeleza Kiswahili ili kiweze kusambaa ulimwenguni kote.

Mheshimiwa Spika, moja katika Taasisi muhimu ya kukieneza Kiswahili ni vyombo vya habari hapa nchini. La kushangaza na la kusikitisha ni ile tabia ya vyombo vya habari kuipotosha lafudhi ya maneno mbalimbali ya Kiswahili. Bali pia hata lugha sanifu haitumiki ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya hayo ni kuichafua lugha yetu wenyewe na kuwakanganya watumiaji wa lugha hiyo. Ninaiomba Serikali ichukue juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba, Kiswahili kinatumika ipasavyo katika vyombo vya habari hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vita dhidi ya Ugonjwa wa UKIMWI. Hali ya Ugonjwa wa UKIMWI hapa Tanzania bado inaonekana ni tatizo kubwa. Ni dhahiri kwamba ugonjwa huu unaendelea kusambaa kwa kasi licha ya hatua mbalimbali zinazochukuliwa kukabiliana na ugonjwa huu. Imefika mahali sasa tujiulize hasa tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, miongoni kwa hatua mbalimbali zinazochukuliwa kudhibiti UKIMWI, mimi zinanitia mashaka. Tumeshuhudia semina kadhaa, makongamano na warsha mbalimbali zikiendeshwa kuhusu namna ya kulidhibiti ugonjwa hili. Semina, warsha na makongamano haya bado hayajaleta mafanikio yoyote.

Mheshimiwa Spika, washiriki wengi wa semina hizo wanajali zaidi posho wanazopata na siyo umuhimu wa elimu inavyotolewa. Ndiyo maana elimu hiyo haisambai na kwa hiyo haikidhi haja iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari navyo hususan *ITV*, vinarusha matangazo ambayo badala ya kuelimisha jinsi ya kujikinga na UKIMWI, tangazo linatuelekeza jinsi vijana wanavyotongozana, wanavyokubaliana, hatimaye kuchezeana huku wananchi, baba na mama, dada na kaka wanaangalia *TV* zao. Matangazo hayo yanawashawishi vijana wa kike na kiume kujiongezea ufundi wa kutongozana. Hapa hatuzui UKIMWI, bali tunapalilia kuenea kwake.

Mheshimiwa Spika, wanamuziki wa kileo nao pia namna wanavyocheza miziki yao inatuchefua moyo. Mwanadada haoni vyema au muziki kunoga kama hajampakatisha matakio mchezaji wa kiume.

Mheshimiwa Spika, mitindo hii ya kucheza muziki inaongeza vitendo vya uasherati na zinaa. Kwa mtindo huu wa maisha hatutaweza kudhibiti kuenea kwa UKIMWI ikiwa hatua madhubuti hazikuchukuliwa kupiga marufuku miziki inayokwenda kinyume na mila, silka na desturi za Kitanzania. Vinginevyo juhudi zote za kupiga vita UKIMWI itakuwa ni juhudi za bure.

Mheshimiwa Spika, imefika wakati sasa lazima wananchi waelezwe ukweli kwamba matumizi ya kondomu hayaonyeshi kusaidia kupunguza maambukizi. Dawa pekee ni kuwaeleza Watanzania kuacha zinaa kama ambavyo vitabu vya dini vinatueleza. Ahsante.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Ustawishaji Makao Makuu, napenda kwa dhati kuipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali inazoendelea kuchukua juu ya suala la Ustawishaji Makao Makuu Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika suala hili pamoja na mafanikio yanayoonekana, nadhani ingewezekana tukafanya vizuri zaidi tukidhamiria na kuongeza nia yetu ambayo kwa kiasi fulani inaonekana inafifia. Kwa mfano, ingewezekana kabisa kupanga bajeti ya kuhamishia angalau Wizara moja kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma kila mwaka wa fedha. Bajeti hiyo ingejumuisha ujenzi wa majengo ya Wizara iliyopangiwa kuhama kwa mwaka unaohusika, nyumba za watumishi wa Wizara hiyo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza na kusikitisha ni kwamba, bado tunaona Serikali ikitumia mapesa mengi kujenga majengo ya Serikali Mjini Dar es Salaam. Kwa mfano, jengo kubwa na la heshima linalojengwa kwa ajili ya *BoT*, lingejengwa Dodoma lingeonyesha kweli Serikali inataka kuhamia Dodoma. Vile vile suala lingine ambalo nililisema hapa mwaka 2003 juu ya ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, ambayo pia imepangwa kujengwa Mjini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mifano hii michache inawakilisha mambo mengi ya namna hiyo yanayofifisha nia ya Serikali kuhamia Dodoma. Lakini pia inakatisha tamaa wananchi ambao tungependa kuona Serikali yote imehamia katikati ya nchi ili kurahisisha utendaji kwa wananchi nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo sasa, Serikali imejikita kupima viwanja kwa ajili ya Makazi ya watu ambao pia kasi ujenzi haiwezi kuwa kubwa sana kwa sababu matumaini yao ni madogo. Mfano mzuri, Wabunge wanao uwezo wa kujenga, lakini ni wachache tu ndio wamejenga kwenye viwanja walivyogawiwa.

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kutamka wazi kwamba, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pamoja na kuunga mkono, naomba kushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo sasa, ipo hatari kubwa sana ya kuharibu vyanzo vya mito yetu. Mito mingi, vyanzo vyake vinatoka milimani. Kazi hii inayoendelea sasa ya kukata miti ya misitu ya milimani na mbugani, itaendelea kuongezeka kila mwaka kwa sababu ongezeko la watu litapanua matumizi ya nishati ya miti. Kwa njia hii, ipo hatari kubwa miti ya misitu ya milimani kumalizika.

Mheshimiwa Spika, haitoshi kuagiza unapokata mti panda mti. Kwa sababu vyanzo vya mito yetu vinatokana na miti iliyokomaa na ya siku nyingi. Miti hii kwa ukomavu wake ina mizizi mirefu inayokua kwa kwenda chini ya ardhi na kupasua miamba na majabali na kuweka mianya inayopitisha maji kutoka ardhini na kububujika kuweka chemichemi inayopelekea kuanza kwa vyanzo vya mito.

Mheshimiwa Spika, kasi hii inayoendelea ya kukata miti ya misitu maeneo haya ya milimani, itapelekea kukosa miti yenye mizizi inayokwenda kupasua mianya ya miamba au majabali, iliyo chini ya ardhi. Miti ya misitu hiyo mizizi yake itakauka baada ya miti yake kukatwa. Kukauka kwa mizizi hiyo kutasababisha kukosa mianya ya kupitia maji kutoka chini ya ardhi kupata mibubujiko na mianya kwa sababu kukauka kwa mizizi hiyo kutapelekea mianya iliyojengeka na mizizi hiyo kuziba.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya maelezo haya, naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa, Serikali ichukue hatua madhubuti ya kulinda misitu yetu, pamoja na kuweka utaratibu mkali wa kulinda misitu yetu iliyo kwenye vyanzo vya mito yetu. Ninaishauri Serikali ianzie kufikiria kujenga mabwawa katika kila baadhi ya mito yetu inayoingia baharini, kama vile Mto Rufiji, Mto Luvu (Pangani), Mto Ruvuma, Mto Wami na Mto Ruvu. Nadhani mito hii kila sekunde moja, mita za ujazo 20,000,000 za maji zinaingia baharini kwa kila sekunde moja. Kwa hiyo, ninaposhauri ujenjaji wa mabwawa, sielekezi hoja yangu kujenga mabwawa kukidhi haja ya kupata maji ya kunyweshea mifugo yetu na kufugia samaki.

Mheshimiwa Spika, ninaposhauri Serikali ifikirie kujenga mabwawa maana yangu ni kufikiria kujenga *Big Dams* ambazo matumizi yake yatatuwezesha kupatikana ujenjaji wa nishati na hivyo kuwasitisha watu kukata miti katika vyanzo vya mito yetu.

*Big Dams* ambazo matumizi yake yatatuwezesha kupanua kilimo cha umwagiliaji na kupata maji safi na salama ya kunywa na matumizi mengine ya majumbani. *Big Dams* hizo kama nilivyosema, zitatuwezesha kusambaza maji nchi nzima na hivyo kutuwezesha kila kijiji kupata umeme na kupanua kilimo chetu cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, mimi najua ushauri huu unaweza kupata jibu la mkato ambalo litakuwa Serikali haina mtaji wa kutosha kutuwezesha kujenga *Big Dams* kwa mito yetu yenye kuingiza maji baharini kwa kila sekunde moja karibu meta za ujazo zipatazo 20,000,000.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa, ni vizuri Serikali yetu ikajifunza kutoka nchi ya Misri wakati walipoanza kufikiria kujenga Bwawa la Aswan. Nadhani inawezekana Misri walikuwa na tatizo la kupata mtaji na utaalamu wa kutosha katika ujengaji wa *Aswan Dam* na *Lake Nasser*. Lakini Mheshimiwa Marehemu Rais Nasser, alitumia matumizi ya *Suez Canal* kumwezesha kupata mtaji na wataalam wa kuwekeza katika ujengaji wa *Aswan Dam* na *Lake Nasser*. Jitihada zake Marehemu Rais Nasser ziliwezesha kujenga *Aswan Dam* mwaka 1964. *Aswan Dam* linatoa megawatts 2100. Wanatumia umeme unaozalishwa katika bwawa hili na wanapata maji ya kumwagilia. Ziada ya umeme wanauza Sudan, Libya na Jordan.

Mheshimiwa Spika, mimi nina hakika kwamba, Serikali yetu ikidhamiria kujenga *Big Dams* katika Mto Rufiji, Mto Ruvuma, Mto Luvu (Pangani), Mto Wami na Mto Ruvu, inaweza. Suala la kupata mtaji na wataalam, kama tutatumia madini yetu ambayo yana soko kubwa duniani na madini yetu mengine kama vile *Tanzanite* hayapatikani kokote kule duniani isipokuwa Tanzania tu. Kwa kutumia mbinu alizotumia Mheshimiwa Marehemu Rais Nasser, tunaweza kupata mtaji wa kutuwezesha kujenga mabwawa hayo kwa kutumia raslimali zetu tulizo nazo.

Mheshimiwa Spika, aidha, nina hakika kama tutajenga *Public Relation* nzuri na nchi zilizokuwa katika Bonded la Mto Nile, yaani kama tutajenga mahusiano na nchi za Bonde la Mto Nile kupitia *Nile Basin Initiative*, tunaweza kupata wahisani wa kutuwezesha kujenga mabwawa hayo kwa sababu matumizi ya maji ya mabwawa hayo yatasambazwa nchi nzima na hivyo maji ya Ziwa Victoria yatatusaidia katika ujenzi wa mabwawa hayo kwa hoja kwamba, mabwawa hayo yatapunguza mahitaji ya matumizi ya ndani ya Ziwa Victoria. Hivyo, nchi za Bonde la Mto Nile kupitia *Nile Basin Initiative*, watakuwa na matumizi mapana kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru kupata *response* ya Serikali katika ushauri huu. Pamoja na mimi kumwandikia barua Mheshimiwa Waziri Mkuu, bado hajanipa majibu ya barua zangu kuhusu *Dakawa Development Centre*. Kituo hiki kina historia kubwa, hivyo Serikali inapokaa kimya bila kunifahamisha kinachoendelea, kwangu mimi kitendo hicho hakinipi raha. Kwa ajili hii, natazamia Mheshimiwa Waziri Mkuu atanieleza hatma ya kituo hiki hasa akifahamu mimi nilimkabidhi barua yangu yeye mwenyewe binafsi hapana Bungeni na nyingine nilituma Ofisini kwake.



**MHE. SHAMIM PARKAR KHAN:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mikopo ya Wanawake na Wanaume, Wakurugenzi wakumbushwe kutekeleza agizo la Waziri Mkuu kutenga asilimia 10 ya mapato kwa mifuko ya mikopo ya wanawake na vijana. Wengi wameanza, lakini hawajafikisha asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *disaggregated data*, Katika suala la utekelezaji wa uwiano wa kijinsia, nashauri taarifa zetu zote zionyeshe takwimu za ME na KE na siyo jumla tu.

Naipongeza Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kufanya hivyo. *Data* ya aina hiyo itatusaidia kupanga mipango yetu kijinsia.

**MHE. PAUL E. Ntwina:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na kwa kuwa nilishachangia kwenye hotuba za Waziri wa Fedha na ile ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, niliyoitoa kwa mdomo.

Mheshimiwa Spika, nina maoni machache juu ya hotuba hii nzuri ya Waziri Mkuu. Bado inatakiwa kuwahamisha wafanyakazi waliokaa sana katika maeneo mbalimbali, kwa mfano, Ma-RAS, juzi wamehamishwa wachache tu. Ni vyema kabla ya uchaguzi, viongozi waliokaa sana maeneo mbalimbali wahamishwe. Hali ya utendaji ni mbaya sana pale ambapo watumishi wamekaa sana. Ni hulka ya binadamu kujisahau hivyo, kufanya tofauti na maelekezo yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, achukue hatua za makusudi kupata matatizo ya Wabunge kwa maana ya wananchi kuondoa matatizo yao. Kwa mfano, tangu nimeingia Bungeni nimekuwa nikiomba kujengwa kwa barabara ya Mbalizi - Galula - Namkukwe. Hii barabara ni kero kubwa kwa wananchi wanaoishi huko, kwani wananchi hutengwa wakati wa masika na maeneo mengine, hivyo, hushindwa kupata huduma muhimu na hivyo kuwa kero. Ninazo sehemu nyingine kama vile barabara ya Kapalala - Gua, ambayo nayo ni ya Wilaya ni sawa tu na hii ya Mkoa ya Galula - Namkukwe.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri Mkuu asaidie mwaka huu, barabara ijengwe. La sivyo, italetwa shida wakati wa uchaguzi. Wananchi wanaonyesha kuchoshwa na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba msaada wa kuwekewa umeme toka Mkwajuni kwenda Vijiji vya Kanga na Galula, kwani tayari nguzo zimepelekwa huko tangu mwaka 1999. Ni vitu vya kushangaza kuona kuwa licha ya Watendaji kuelewa madhara yake, wanaendelea kunyahidi na wakati unapita. Suala hili nimelipeleka kwa Waziri wa Nishati na Madini, ambaye alishawaahidi wananchi kuwa umeme ungewekwa ifikapo Desemba, 2003, ingawa tayari mwaka umepita.

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili litatuliwe vinginevyo sasa limekuwa ni la kisiasa na pia linawakatisha tamaa wananchi; wakati wanaona wilaya nyingine zikipata umeme kama vile Tukuyu na Kyela. Wala siyo eneo refu, si zaidi ya kilomita 40. Naomba msaada wako. Hivi wananchi wanajisikiaje? Je, ni vyema kuyasema hapa bila nidhamu au nifanyeje?

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine la msingi ni uhaba wa maji. Nimechimbiwa visima vitano, Galula viwili, Mbuyuni viwili na Mbangala kimoja, lakini bado hatujawekewa pampu. Suala hili pia lipo kwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Ninalo tatizo kubwa katika vijiji vifuatavyo, la ukosefu wa maji ya visima: Patamela 2, Saza 2, Namkukwe 2, Iseche 1, Mbala 1, Malangali 2, Itindi 2 na Mheza 2. Hali ya maji masafi kwa matumizi ya binadamu ni mbaya sana. Naomba sana msaada wake binafsi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, juu ya suala hili pia.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni upatikanaji wa simu walau za Kampuni ya Simu. Naomba sana tupatiwe simu pale Kijiji cha Mkwajuni. Tunayo matatizo makubwa sana ya mawasiliano, umeme umeshafika, lakini huduma hii ya simu siyo nzuri sana na ina manung'uniko sana. Amejitokeza mwanachama wa *CUF* kuleta simu ya *Cellular*. Naomba tu-*block* ile *image* mbaya kwa wananchi kuona chama kingine kinaleta huduma.

Mheshimiwa Spika, kila siku na kila mara naishukuru sana Serikali kwa yote iliyolifanyia jimbo langu na kweli bado wananchi tunaomba Wilaya yetu au tupeni Wilaya Ndogo. Tayari mji wetu ni Mji Mdogo. Majengo yapo na karibu vigezo vyote vya Wilaya vipo. Karibu sana Mkwajuni Jimbo la Songwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa ufupi kwa maandishi katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono suala zima la Serikali kuweka nguvu kubwa sana katika Elimu ya Sekondari. Baada ya kazi kubwa ya kufufua na kuimarisha Elimu ya Msingi kupitia MEM, hapakuwa na budi kwa uongozi makini kutoangalia Elimu ya Sekondari na ubora wake. Nashukuru kwa kuangalia ada na uwezekano wa kupunguza ili wengi zaidi waimudu na watu wetu wengi wasome. Hili liendane na upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada, upatikanaji wa madawa ya maabara, ajira ya Walimu wenye ujuzi ili watoto wafundishwe ili kuondoa kera ya ukosefu au upungufu wa Walimu, mishahara ya Walimu na mafao/haki zao zingine za msingi ziangaliwe na walipwe bila kusumbuliwa na ujernzi na ukamilishaji wa shule tulizonazo upewe kipaumbele ili mazingira ya shule zetu yavutie. Maabara, mabwalo na majengo ya utawala yajengwe au yakamilishwe kila shule kwa kushirikiana na wananchi, ikiwa ni pamoja na nyumba za Walimu.

Vile vile Walimu wa Shule za Msingi wapewe motisha, kwa kulipwa kwa wakati mishahara na haki zao zingine za msingi. Walimu wa Shule za Msingi wasipoangaliwa vizuri, inawezekana lengo letu la kuboresha Elimu ya Sekondari likachelewa kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie pesa za Serikali kuwafikia wakulima mmoja mmoja au katika makundi yao. Serikali imekuwa mwaka hadi mwaka inaongeza pesa za kuboresha kilimo. Tatizo limebaki pale pale ambapo mara zote fedha zetu huishia kutoa warsha na semina kwa wataalam. Ni lini wakulima wao wenyewe watapewa mafunzo, watafuatiliwa na hivyo kushiriki na kushirikishwa katika kubadili kilimo na kupata utaalamu mpya? Ninaishauri Serikali iwaangalie wakulima kuanzia wanavyoandaa mashamba, kupanda mbegu bora, wakati wa palizi, kuua wadudu na magugu, uvunaji na utunzaji katika maghala. Mwisho, liwepo soko la uhakika la mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika hoja hii napenda kuzungumzia suala la UKIMWI kwa ufupi kwamba, UKIMWI unatumaliza. Zamani tulielekeza kidole kwa wengine, lakini ukweli wenyewe UKIMWI umetugusa kila mmoja kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, dawa zinazorefusha umri ziwekwe katika Vituo vya Afya, Zahanati na Hospitali za Binafsi kwa bei ile ile (hapa Serikali ibebe gharama), Hospitali zote za Serikali. Kiwepo kitengo maalum cha kushughulikia wagonjwa wa UKIMWI. Si ushauri nasaha tu, bali pia watoe dawa za kurefusha maisha bila masharti.

Mheshimiwa Spika, kama inavyojulikana, wengi wanaofariki kwa UKIMWI ni vijana wenye umri wa miaka 13 - 49. Ni umri wa kujenga familia na Taifa. Ni umri wa kuongeza tija na watoto wa Taifa letu. Watoto wengi wanaachwa yatima. Yatima ni mzigo kwa Taifa na hasa jamii. Si yatima wote wanasaidiwa na Serikali, kwa hiyo, jamii inaendelea kushuhudia watoto wengi wakikosa huduma za msingi na mapenzi ya wazazi. Hawa yatima ndiyo Taifa la kesho.

Kwa hiyo, wazazi walioathirika wasaidiwe waishi ili walau watunze watoto wao kwa pesa na upendo. Taifa lisilo na upendo litakuwa na wingi wa ghasia na kutokufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti ya kasma ya Bunge, hakuna msaada wowote kwa Mbunge kujiendeleza kielimu. *Aspect* ya *training* kwa Wabunge haiko *ever-since*. *Why?* Wamesema sana! Naomba hili liangaliwe angalau *some assistance* kwenye *distance learning* au kodi fupi za ndani na nje ya nchi. Pia Wabunge wanahitaji kupata *Laptop Computers*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la umeme vijijini, naiomba Serikali iangalie upelekaji umeme Tarafa ya Mkoka katika Wilaya ya Kongwa kutoka pale Narco (km. 25 tu). Eneo hili ni muhimu sana kwa uzalishaji wa mahindi. Katika Mkoa wa Dodoma, hili ni eneo *potential* sana. Tafadhali tulipelekee nishati hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kongwa tumejenga Zahanati mpya 14 na Vituo vya Afya viwili kati ya mwaka 2000 - 2004. Tunaiomba Idara Kuu ya Utumishi itupatie watumishi wa afya. Zahanati nyingi kati ya hizo hazijaanza kufanya kazi hadi leo hii. Tunaomba sana hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uundaji wa Bodi za Huduma za Afya, umejaa ukiritimba. Sisi Kongwa tumeshafanya yote yanayotakiwa, lakini *Government Bureaucracy* ni kubwa sana hadi leo hatuna Bodi ya Afya wala ya Maji kwa sababu ya mlolongo. Tupunguze mlolongo hiyo na tuongeze spidi ya kuwezesha bodi za huduma kuanzishwa.

Mheshimiwa Spika, Fedha za Mfuko wa Pembejeo haziwafikii wananchi. Wilaya ya Kongwa ilikuwa na maombi mengi sana kwa mwaka 2002/2003 na mwaka 2003/2004, lakini hata mkulima mmoja hajawahi kupata mkopo huo wilaya nzima. Ni ukiritimba usio mfano. Tusiyaachie mabenki kuamua watakavyo kwa fedha za umma. Wananchi wenye nia ya kukarabati matrekta yao hawajasaidiwa. Tuone namna bora zaidi ya kuwapa misaada wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, mtambo rahisi wa umwagiliaji maji uitwao *money maker* ni ukombozi wa mkulima. Wananchi wawezeshwe kuzipata mashine hizi kwa wingi hasa kwa ajili ya umwagiliaji wa maji ya visimani Dodoma na Singida. Kweli kama umwagiliaji mdogo mdogo wa nyanya, vitunguu na kadhalika, utapewa nafasi ya mashine hizi za *money maker* vijijini, uzalishaji utaongezeka mno. Tukumbuke kuwa mashine moja na mipira yake si zaidi ya shilingi laki moja.

Mheshimiwa Spika, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu, iweke kumbukumbu kuwa msimu huu wa 2004/2005 kwa Mikoa ya Dodoma na Singida patakuwa na njaa kuanzia Desemba. Maghala ya *SGR* Dodoma, yawe na chakula cha kutosha na Kongwa isisahauliwe katika zoezi hilo. Nashauri kuwa baadhi ya maghala mapya ya *SGR* yajengwe pale Kibaigwa Wilayani Kongwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100 na naomba kutoa ushauri ufuatao katika kuboresha baadhi ya masuala:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mawaziri na Makatibu Wakuu kutojibu simu zao za mikononi. Kwa mara nyingi kuna baadhi ya Mawaziri na Makatibu Wakuu walio na simu za mikononi ukiwapigia simu hawajibu. Hii ni hatari maana unaweza kuwa na ujumbe muhimu wa kutoa hata wa kuiokoa nchi, lakini ukakosa msaada. Wengi wamekuwa wakifunga simu zao. Nashauri wajitahidi kujibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa chakula, Serikali itoe mapema fedha za kununua mahindi kwa *SGR* wakati bei ya sasa ni nzuri katika sehemu nyingi hapa nchini. Kutokana na mzunguko wa majira ya mvua, *farming season* ya mwaka 2004/2005, ambao huanza Septemba na kuendelea hadi Aprili au Mei na kadhalika, kwa uzoefu *farming season* ya mwaka 2004/2005 mvua itachelewa sana kunyesha na huenda itaanza Machi, 2005 na kusababisha shida kubwa ya chakula. Miaka mibaya huwa kama ifuatavyo:-

- Miaka mibaya (*Irregular Rain Parten*) 2000/2001, 2001/2002, 2002/2003, 2003/2004 na 2004/2005.

- Miaka mizuri (*Regular Rain Parten*) 2005/2006, 2006/2007, 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008 unategemewa kuwa na mafuriko. Kwa hiyo, ni vyema Serikali ikajiandaa kwa mafuriko. Ukitazama mzunguko huu huwa kwa miaka mitano mitano. Ni vyema sasa maandalizi ya njaa yakaandaliwa kwa kutoa fedha za kutosha *SGR* kununua chakula.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ruzuku ya Vyama vya Siasa, ninashauri fedha hizi ziongezwe kulingana na mapato ya ndani. Vyama vya Siasa vinatakiwa kuwa na zaidi ya shilingi bilioni 36 kulingana na sheria tuliyopitisha ya kulipa asilimia mbili ya mapato ya ndani. Fedha zilizotolewa Sh. 8,694,322,800/= ni ndogo sana. Naomba maelezo wakati wa majumuisho ni sababu zipi za msingi kwa Serikali kutotekeleza sheria zake, Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya uchumi na kupanda kwa bei ya mafuta, hali inaendelea kuwa mbaya sana na hasa inasababishwa na kupanda kwa bei ya mafuta. Kama fedha nyingi zinazotokana na mauzo ya madini zingelikuwa zinapitia kwenye akanti ya Serikali, *exchange rate* isingelikuwa kubwa sana kama ilivyo hivi sasa. Hivi kuna sababu zipi za msingi kwa Serikali na Benki Kuu kutodhibiti mfumuko wa *exchange rate* kama juhudi zinazofanywa katika kudhibiti mfumuko wa bei?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Habari na Utangazaji, hivi kuna sababu gani za msingi zinazofanya vyombo kama Redio Tanzania na TVT kutosikika vyema katika baadhi ya mikoa na kuzidiwa na Redio na Televisheni za watu binafsi kama *Radio One*, *Radio Free Africa* na *ITV*? Naomba sana wanaohusika wajiweke sawa waondoe aibu hii. Hivi kuna nini? Hivi watu binafsi wanazo fedha kuzidi Serikali?

Mheshimiwa Spika, Mji wa Shinyanga ulifanywa kuwa Manispaa miaka mitano iliyopita, lakini huduma zinazotolewa kwa Manispaa nyingi kama kuboresha barabara na mitaro hazifanyiki. Hivi kwa nini Serikali haitaki kuleta miradi ya kusaidia kuboresha barabara na mitaro ya Manispaa yetu?

Mheshimiwa Spika, *Library* yetu ya Bunge haipewi fedha za kutosha kununulia vitabu, *magazines* na kadhalika. Pia fedha zinazotolewa hazikidhi matumizi kwa utendaji wa Kamati za Bunge. Kama nguzo ya Bunge, ingelipewa Sh. 40b./= na Mahakama nayo ikapewa Sh. 40b./=, kuweka msukumo wa Serikali na maboresho katika utendaji wa nguzo hizi na Serikali kuonekana inafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake iliyogusa karibu kila eneo la utendaji Serikalini. Pamoja niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, kwa kuwa mihimili mikubwa ya kumsaidia Waziri Mkuu. Si hivyo tu, nichukue nafasi hii kuwapongeza Watendaji Wakuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara andamizi, pamoja na Wakurugenzi na Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii, mimi ninayo machache ya kuchangia. Kama sote tunavyokubali kuwa kilimo ni moja ya sekta inayochangia kwa kiwango kikubwa uchumi wa nchi hii. Kilimo kinaajiri asilimia kubwa ya Watanzania, kwa zaidi ya asilimia 75. Kilimo ni heshima kwa Watanzania kwani tukilima tutakuwa na uhakika wa chakula na tutaondoa fedheha ya kuwa ombaomba.

Mheshimiwa Spika, nchi isiyojitegemea kwa chakula ni rahisi kupokea amri na maelekezo kutoka kwa walio nacho. Kutojitegemea kwa chakula ni utumwa, bali kubwa zaidi ni kupoteza uhuru wa kweli kwa nchi hiyo, kutokuwa na kauli na maamuzi na zaidi kudharauliwa. Hakuna mpango wowote, wala maendeleo yoyote mbele ya njaa. Hakuna jeshi, hakuna elimu, hakuna afya, hapana maendeleo, pia hakuna usalama ndani ya nchi kama hapana chakula.

Mheshimiwa Spika, chakula ni kila kitu, chakula ni afya, usalama, elimu, maendeleo na kadhalika. Ingawa haya yote unayoyasema yanaeleweka, lakini kusema ni jambo moja na kutenda ni lingine. Kwa mawazo yangu kwa sasa na kutokana na dalili ya janga la njaa lililotukumba mwaka 2003 na kutokana na viashirio vya njaa na ukame Bara la Afrika, nadhani wakati umefika sasa kama watu wazima na viongozi msipoteze muda. Bajeti yetu na nguvu zetu zote tujielekeze katika suala la kilimo na si kilimo cha jembe la mkono, bali kilimo cha umwagiliaji na matrekta.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa na kwa haraka sana tungelianza kutumia Idara za Mageza, JKT, JKU na Wilaya mbalimbali kwa kuunda *brigade* za vijana na Serikali ikawawezesha na hata Jeshi la Wananchi, pakaandaliwa utaratibu tukafungua miradi ya kilimo. Lakini kubwa zaidi kwa nini tusiandae kongamano/semina ya Wabunge na Watendaji Wakuu Serikalini tukalizungumzia jambo hili? Hili linazungumzika.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa dhati kabisa siamini kuwa kweli Watanzania tuna matatizo ya kushindwa kujilisha. Tatizo letu tunasema sana na matendo yetu ni madogo. Ardhi yetu na hali hii tuliyonayo na umma wa watu waliopo na shida ya ajira tuliyonayo kwa Watanzania, lakini kilimo ikawa ni tegemezi bubu kwa uchumi wa nchi hii, hatuna

tena la kungojea ila tukae tutekeleze dhana ya kuinua uchumi wetu kupitia kilimo na mengine yatafuata.

Mheshimiwa Spika, mkazo mkubwa unahitaji kuwekwa kwa Daftari la Wapiga Kura na hasa Pemba na Unguja. Siku za nyuma watu kutoka Mombasa, Tanga na hata Uarabuni walikwenda Pemba kujiandikisha. Suala hili Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib alifuatilie kwa kutumia vyombo vilivyo chini yake kwa Zanzibar.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Aidha, ninaomba kumpongeza Waziri Mkuu, Mawaziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Ofisi hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya na ninawatakiwa kila la kheri kwa mwaka 2004/2005. Pamoja na yote hayo, ninaomba yafuatayo yazingatiwe:-

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kufanikisha kupatikana kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mapema iwezekanavyo, Serikali ichukue hatua za makusudi kuwaelimisha wananchi kuhusu kila kitu kitakiwacho ili Daftari likamilike. Vipindi katika Redio, Televisheni, vipeperushi na mikutano ya hadhara, vitumike kwa lengo hilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara inayotakiwa kusimamia na kuona kuwa Ofisi za Wabunge Majimboni zinakuwepo ni ya TAMISEMI na siyo Wilaya kama ilivyoandikwa katika ukurasa wa nane wa hotuba hii. Ni vyema Wizara hii ikafanya hivyo, vinginevyo suala hili litakwenda mwendo mdogo endapo litashughulikiwa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba, wapo wakimbizi ambao wana uwezo mkubwa kifedha na kutokana na hali hiyo hawakai makambini na wanaendeleza biashara zao hasa katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Hivyo, suala la Serikali kutoa vitambulisho vya Kitaifa kwa wananchi wake ni muhimu ili kuwabaini hawa na kuwapeleka makambini. Suala la vitambulisho limechukua muda mrefu sana kiasi kwamba, inashangaza na hatujui tatizo hasa ni nini.

Mheshimiwa Spika, Serikali iharakishe utaratibu wa kupima maeneo ya makazi na mashamba vijijini ili wanavijiji nao waweze kupata hati miliki zitakazoweza kuwasaidia kupata mikopo na vile vile kuwa na ushahidi wa kisheria wa kumiliki maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, elimu dhidi ya matumizi ya madawa ya kulevyaa haitoshi, Serikali ichukue hatua zaidi kuitoa. Aidha, Serikali iache mara moja kutangaza thamani ya madawa hayo yanapokuwa yamekamatwa, kwani kufanya hivyo kunawatia hamasa wahalifu kuzitafuta. Inatosha kwa Serikali kusema yamekamatwa madawa ya kulevyaa yenye uzito fulani au chupa kadhaa na wala siyo madawa yenye thamani fulani.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kusema kuwa naiunga mkono hoja hii kwa sababu inalenga kutuelekeza tunakolenga kwenda.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kuchangia mahali ambapo napenda kuisaidia Serikali yetu kurahisisha na kuboresha utendaji wake wa kazi kadri ya maoni na uzoefu wangu katika uongozi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sera ya Uzalishaji, pamoja na sisi sote kutambua kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu, Serikali yetu bado inaamini tu kuwa, pembejeo za kilimo ni mbolea (chumvi chumvi au samadi), majembe ya mkono, kemikali za kuulia wadudu waharibifu wa mimea, dawa za kuhifadhi mazao na pengine majembe ya kukokotwa na ng'ombe na mikokoteni. Hali hii inadhihirisha upungufu wetu kwa sababu hatuzingatii zaidi matumizi ya matrekta, hatujawakwamua wakulima watumiao plau kwa kulima ili wazidi pale walitumie kwa palizi, kutia mbolea na kadhalika na huduma za ugavi ni hafifu sana. Afadhali tulipokuwa na Mabwana Shamba wa Pamba, Tumbaku, Kahawa na kadhalika. Kila mmoja alijizatiti kwa zao lililomhusu.

Mheshimiwa Spika, mrabaha au *cess* kwa madini ikitolewa kwa Halmashauri husika itasaidia maendeleo ya mahali hapo. Kufuta *cess* kwa chokaa na jasi alikofanya Waziri wa Fedha siyo suluhisho lililotarajiwa na wananchi. Suluhisho sahihi na lilotarajiwa ni kutoa *cess* kwa madini ya aina zote nchini.

Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru na kuipongeza sana Serikali yetu kwa msaada wa chakula iliyotupatia mwaka huu Jimboni kwangu na Wilaya ya Nzega kwa ujumla. Tulipata chakula cha msaada na kile cha bei nafuu. Nashukuru sana kwa niaba ya wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba tu ieleweke kuwa tunapofanya tathmini ya chakula vijijini, tusiridhike kuwa kuna upungufu tu wa chakula, yaani hakuna njaa. Hali hii ni kupotosha Serikali kwa kuwa ingawa chakula kinaonekana kuwa na upungufu kaya ambazo hazina maana yake hazina hazitapewa bure na kaya zilizo na chakula hata kama ni cha ziada, anayetegemewa kusaidia ni Serikali tu. Kwa maana hiyo, kaya hiyo ina njaa haina upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, moto uliunguza Makao ya Rais, imegusa wengi na majibu ya Kamati iliyochunguza kisa na mkasa huu imegundua kuwa chanzo cha moto kilikuwa ni pasi iliyoachwa ikiwaka, nayo inanyong'nyeza mioyo. Kweli nyumbani kwa Rais hakuna usalama kiasi hicho? Lazima tushangae na kugwaya, je tuishie kustajabu?

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa Elimu ya Msingi, ninaupongeza mno na ule wa Elimu ya Sekondari utakaoanza Julai, 2004, unasubiriwa kwa hamu na shauku kubwa na Watanzania wote. Ombi, Baraza la Mitihani, Taasisi ya Elimu, Baraza la Elimu ya Juu na Baraza la Elimu ya Ufundi, wote wasitozwe kodi kwa karatasi watumiazo kwa shughuli zao za kielimu, kwani hiyo ndiyo Pembejeo ya uzalishaji wa vitabu, majarida na mitihani yote.



Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupeleka (kugawa) pesa kwenye Halmashauri kwa kuzingatia vigezo kama idadi ya watu, ukubwa wa Wilaya na maendeleo yaliyofikiwa na Wilaya ni muhimu sana na yataungwa mkono na wengi. Hii ni hali iliyotufanya wengine kulilia kupewa Wilaya kwa kuona jinsi Wilaya kubwa kubwa na zenye watu wengi lakini zilizo nyuma kimaendeleo kama Nzega, zinapewa ruzuku sawa na Wilaya ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makanga, apobaini Sheria yetu ya Uchaguzi ina kasoro nyingi ambazo pamoja na kuanzisha Daftari la Wapiga Kura, lazima sheria iweke wazi sababu za kumfukuza Ubunge mtu na za kutomfukuza ziwe bayana. Je, Mbunge akifukuzwa uanachama ikiwa ni haki atoke na Bungeni, je, yule wa Viti Maalum aliyeingia Bungeni kwa sababu ya Wabunge wa Majimbo waliofukuzwa, kwa nini yeye aendelee kudunda? Sheria inasemaje?

Mheshimiwa Spika, vilevile Mbunge wa Viti Maalum aliyeingia Bungeni kutokana na Wabunge wa Chama chake kutoka Mkoa A, Mbunge huyu anaweza kuwa Diwani halali wa Wilaya iliyo katika Mkoa B? Mbunge huyu wa Viti Maalum ikiwa aligombea Ubunge katika Jimbo la Wilaya D, akashindwa na kushika namba ya tatu au ya nne katika Jimbo hilo la Uchaguzi, lakini Chama chake kikampa Ubunge wa Viti Maalum, je, anayo haki ya kuwa Diwani halali wa Wilaya hiyo D na akaendelea kujinadi kuwa katika Baraza la Madiwani anawakilisha wapiga kura wake waliompa kura wakati wa Uchaguzi Mkuu?

Mheshimiwa Spika, kama hivyo ndivyo, ni vipi mgombea aliyeshika nafasi ya pili katika Uchaguzi Mkuu naye asidai kuwa Diwani kuwawakilisha wapiga kura waliompigia kura ambazo hazikutosha?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi wa Waziri Mkuu, Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Katibu Mkuu, Bibi Rozi Lugembe na Watendaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kuandaa hotuba nzuri, yenye ufafanuzi wa kina kuhusu masuala mbalimbali ya utendaji wa Serikali nzima. Pia pongezi ziwaendee Wana-CCM wa Jimbo la Bariadi, kwa kufanya maamuzi sahihi ya kumchagua Mwana-CCM, Mheshimiwa Danhi Makanga, kuwa mwakilishi wao Bungeni.

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepatwa na dhoruba mbalimbali, zikiwemo vifo na ajali, nikianza na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na Baba yao mzazi, Mzee Omari Kigoda. Mungu ailaze pema roho ya marehemu. Pia natoa pole kwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kupata ajali na kumshukuru Mungu kuwa amewanusuru wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi na pole zilizotangulia, naomba nichangie kama ifuatavyo: Ni ukweli usiopingika kuwa Bunge linafanya kazi nzuri ya kutunga na kupitisha sheria na mikataba, lakini tatizo ni kwamba, utekelezaji wa sheria na mikataba hiyo, unakuwa wa taratibu sana. Kwa mfano, Sheria ya Huduma kwa Jamii na zinginezo, tunaambiwa kanuni na taratibu bado zinaendelea kuandaliwa sasa. Tangu mwaka 2002 mpaka leo bado na wafungwa wanaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 26 - 27 wa hotuba limefafanuliwa suala la uvunaji wa maji ya mvua ambayo yangesaidia sana kwa matumizi hata ya umwagiliaji mashambani. Hata hivyo, nashauri taaluma hii ienezwe nchini kwa vile teknolojia hii haijaenezwa nchini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni upimaji wa ardhi, katika suala hili nashauri kuwa upimaji uhimizwe haraka kwa vile yaelekea *pace* ya upimaji na ueneaji wa *squatters* Mijini ni mkubwa na hauendi sambamba hivyo, miji kuonekana haina mipango na mandhari nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mikopo, bado kiwango kinachopeshwa ni kidogo sana kiasi kwamba, wanawake na vijana wanashindwa kukuza biashara zao. Hivi wataendelea kuwa na biashara ndogo ndogo mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ushirikiano wa Kimataifa, naipongeza Serikali yetu kwa kujenga ushirikiano mzuri na nchi jirani na duniani kwa ujumla. Hata hivyo, nasikitishwa na suala la Tanzania kutoweza kuwakilishwa kwenye mkutano uliokuwa unaandaa masuala ya *Convention* ya Watu Wenye Ulemavu Duniani huko *USA* kama Sekta ya Habari ilivyoripoti. Nafahamu kuwa kuna waliokwenda, lakini sidhani kuwa ni upande wa Serikali ambayo hatimaye ni mshauri mkuu katika masuala ya Kimataifa. Kwa msingi huo, ningepomba tu ufafanuzi ili maswali ninayoulizwa na watu wenye ulemavu niweze kuyajibu vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 57 hotuba imeelezea suala la Ripoti ya Utandawazi. Naomba kushauri kuwa ni vyema ripoti hiyo tungepatiwa Bungeni au tupewe semina juu yake, kuliko kusikia tu. Pamoja na hayo napenda kusesitiza suala la malipo ya malimbikizo ya Walimu ambao wengine wanadai haki ya marekebisho ya mishahara tangu 1998. Hali hii ilinipata hata mimi, lakini baada ya kupata nafasi hii ya Ubunge, ndipo niliposhughulikia Wizarani na malimbikizo hayo yakalipwa na Wizaru husika. Hivyo, suala hili ni kero kubwa kwa Walimu ambao ndio wengi wa kada ya wafanyakazi nchini, kwa hivyo, ni vyema kero hii ikaondoka haraka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza haya, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu umelenga katika maeneo yafuatayo ya Hotuba ya Waziri Mkuu:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hali ya Ulinzi na Usalama. Utendaji kazi na usimamizi wa Jeshi la Wananchi ni mzuri na unastahili kupongezwa. Hitilafu kubwa iko katika Jeshi la Polisi lenye dhamana ya usalama wa raia na mali zao. Hata baada ya Jeshi hili kuongezewa bajeti yake miaka miwili iliyopita, hakuna mabadiliko zaidi. Sisi tunaishi na wananchi tunaona kikwazo kikubwa cha Jeshi hilo ni kukosa nidhamu ya kazi kuanzia ngazi ya juu mpaka ya chini kabisa. Ukosaji wa nidhamu ni pamoja na vitendea kazi duni hususan magari na Vituo vya Polisi vyenye uwezo wa kuhifadhi silaha. Lingine ni mazingira mabovu/duni ya utumishi wa Serikali na tofauti kubwa mno kati ya Askari wa chini na wa juu. Tunataka majibu katika miaka mitatu ya ongezeko la bajeti, haya yametatuliwa vipi?

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula imeshindwa kumudu majukumu yake aidha kwa uwezo mdogo inayopewa na Serikali na udhaifu wa utendaji vijijini na Wizarani. Tofauti hizi tunataka kupata majibu, Serikali ina mikakati gani ya kuzidhibiti, pia ninapenda kufahamu iwapo Wizara ya Kilimo na Chakula ina *database* ya mito yote ya kudumu inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na maeneo yanayofaa kilimo cha kuvuna maji ya mvua?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Same ni kame lakini imechukua hatua gani za kukuza kilimo cha umwagiliaji katika mito yake ya kudumu ya Pangani, Sasani, Yongoma, Hingilili na Nakombo? Je, maeneo ambayo yamestawi kwa kilimo cha umwagiliaji wa kuvuna maji ya mvua kama kule Makanya na Hedaru Wilayani Same, yanafahamika na yamesaidiwa? Haya yote tunahitaji yapate majibu ili kuleta ufanisi mzuri wa uzalishaji mali na chakula katika nchi. Wananchi waelimishwe kujiweka akiba ya chakula kila msimu wa mavuno na Taifa nalo liwe na mila/utamaduni wa kuwa na hifadhi ya chakula walau ya miezi sita kwa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Programu ya Uendelezaji wa Mfuko wa Mazao ya Kilimo, moja ya maeneo yaliyokuwa yamelengwa na kutangazwa ya programme hii iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na tangu ianzishwe miaka miwili iliyopita, bado haijafika na kuanza shughuli zake Wilayani Same. Je, tunategemea ianze lini? Kuchelewa kwa programu hii kuanza, kumedhoofisha kukua na ukosefu wa maendeleo ya *SACCOS* zilizoanzishwa Wilayani Same. Katika Hotuba ya Waziri Mkuu, imethibitisha *SACCOS* za Wilayani Same kudhoofika kwa kukosa mitaji na wanachama wenye uwezo kiuchumi. Naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu inipatie majibu kuhusu maeneo ambayo nimeulizia hapa ya programu niliyoitaja.

Mheshimiwa Spika, eneo la UKIMWI ni lazima liangaliwe kwa makini kwa sababu uhibitaji wa maambukizi unahitaji kampeni kamambe kama ambavyo zinaendeshwa na *TACAIDS*, Kamati za Wizara, Mikoja, Wilaya, Tarafa, Kata, Vijiji na Vitongoji. Huu ni utaratibu mzuri na unahitaji kupongezwa. Jambo ambalo ni hitilafu kubwa ni katika maeneo mawili. Eneo la kwanza ni mgao wa fedha Wilayani. Utaratibu gani unatumika kugawa fedha hizi? Mpaka sasa tukiwa katika bajeti, Wilaya ya Same haijapata mgao wake. Sababu gani zilipelekea hili? Jedwali la Hotuba ya Waziri Mkuu ni uthibitisho. Wakati fulani niliongea hili na Kamishna Mkuu wa *TACAIDS* alinjibu

kuwa zitatumwa, ni mujda mrefu. Je, kwa nini hazijatumwa mpaka leo? Naomba kupata majibu.

Eneo la pili la mbinu za kufanikisha mapambano dhidi ya UKIMWI ni lile la upatikanaji wa dawa dhidi ya virusi geuzi (*ARVs*) kwa wagonjwa wa UKIMWI. Eneo hili inabidi liangaliwe kwa makini kwa kuwa wale waathirika wanaopewa dawa za *ARVs* watambulike katika jamii aidha kwa kuwaweka alama fulani au vinginevyo. Kinyume na hivyo, ninaogopa kuwa tutakuwa tumewapa nguvu ya kuishi na kufanya ngono na kuongeza maambukizi ya UKIMWI badala ya kuyapunguza. Tume ya *TACAIDS* inatakiwa ilianganalie hili japo siyo kwa sura ya kunyanyapaa.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Kurushia Matangazo ya TVT Arusha, katika mwaka wa fedha uliopita, kituo hiki kilipoanzishwa tulijulishwa kuwa Mkoa wa jirani wa Kilimanjaro nao utafaidika na huduma ya kituo hiki. La kushangaza ni kuwa huduma hii haipatikani mkoani kote, kwa mfano, Wilaya ya Same haipati matangazo ya TVT kabisa. Je, Ofisi ya Waziri Mkuu, ina mpango gani wa kuhakikisha huduma ya TVT ya kituo hiki cha Arusha inafika katika maeneo ya Wilaya zote za Mkoa wa Kilimanjaro?

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa ambapo vituo vingine vipya sita vitafunguliwa viko Mbeya, Tabora, Lindi, Kagera, Kigoma, Tanga na Mara ni mzuri, lakini iwapo huduma yake itakuwa finyu kama ya Kituo cha Arusha, haitakuwa na maana ya kuwa na vituo vya TVT lukuki, lakini visivyo na huduma inayokubalika katika jamii. Tunaomba Ofisi ya Waziri Mkuu ilipatie hili majibu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho katika huduma ya TVT ni kutaka kujua sababu ya ratiba/vipindi vya TVT kuanza saa 6.00 mchana badala ya asubuhi kama TV nyingine. Hii ni Televisheni ya Taifa, huduma yake inianza saa 6.00. Je, hii si kushusha hadhi yake? Tunaomba majibu kwa sababu wapenzi wa TVT wanaliuliza mno.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ndiyo kioo cha Wizara zingine zote, inategemea fedha za nje kwa asilimia 95 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, Bunge likiwepo. Je, hii si kuhatarisha Ofisi ya Waziri Mkuu na Bunge kama tukikwama kupata fedha za nje toka kwa Wafadhili? Kwa mtazamo wangu, Bunge pia linawekwa mahali pabaya kidemokrasia kwa kutegemea fedha za Wafadhili katika kazi yake. Demokrasia ya nchi ikiyumba na uhuru wetu na wa wananchi wetu utayumba. Hii ni hatari sana. Wakati ujao utegemezi huu ungehamishiwa Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, nahitimisha kwa kumpongeza Waziri Mkuu na Mawaziri wake wa Nchi, kwa kazi nzuri na hotuba iliyosheheni mwelekeo wa kazi za Serikali yetu kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, napenda kutoa shukrani zangu kwa Waziri Mkuu kwa juhudi mbalimbali kwa ajili ya kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuwashukuru watumishi wote walioko Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na kuandaa hotuba iliyo bora. Kweli, tangu nilipoingia hapa Bungeni nikiwa Mbunge, Waziri Mkuu na safu yake ya ofisini wamekuwa wakiandaa hotuba iliyokamilika.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yamekwisha ongelewa, mimi ninapenda kuzungumzia mambo mawili tu. Kwanza, ni kuhusu amani nchini. Amani si nzuri katika baadhi ya maeneo na Buchosa inaguswa sana na eneo la Ziwa Victoria, amani hakuna huko, naomba ieleweke hivyo. Pili, ni kuhusu fedha ya ukarabati au vifaa vya Ofisi ya Mbunge, ningeshauri fedha hii ibaki katika Ofisi ya Spika na utaratibu ufanyiwe hapo, kwani usumbufu uliopo hivi sasa, pesa hizi kuchuliwa kwa *RAS* ni tatizo sugu na si rahisi kuliweka sawa.

Mheshimiwa Spika, sipendi kusema mengi, kwani mengi yamekwisha zungumzwa na Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namtakia Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, apone haraka na aweze kurejea nchini ili tuwe naye karibu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa maelezo yangu kwa maandishi kama kanuni zinavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa zaidi ni juu ya majibu ya Mawaziri hapa Bungeni, ambayo aidha hayaridhishi au yanagongana na kwa maana hiyo, inaonyesha kwamba Mawaziri hawafanyi utafiti wa kutosha kabla hawajatoa majibu kwa maswali husika! Mfano ni kuhusu bomoabomoa kandokando ya barabara.

Mheshimiwa Spika, 13 Aprili, 2004, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, alitoa jibu hapa Bungeni na ipo kwenye *Hansard* ukurasa wa 12, ninanukuu: “Pia napenda niwaarifu rasmi kuwa msimamo wa Serikali kwa wale waliojenga katika *road reserve* uko pale pale kwamba, hakutakuwa na fidia”. Naibu Waziri wa Ujenzi, alijibu siku hiyo hiyo iko kwenye *Hansard*, nanukuu : “Kama mhusika anayo hati halali, hili naomba lieleweke, kama anayo hati halali anastahili kulipwa, tutazungumza naye. Kama hana hati halali, maana yake Serikali inapitisha maendeleo hapo bila malipo”. Baadaye tulipata jibu la Waziri wa Ujenzi mwenyewe kupitia magazeti kuwa wenye alama ya “X” kwenye nyumba zao, wasibomoe hadi zitakapopatikana fedha za maendeleo ya eneo husika. Mwisho ni wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu ukiwa ndani ya Bunge, kipindi cha *briffing*, ulitoa maagizo kuwa Wizara husika walete taarifa rasmi juu ya mipango ya fidia au kutofidia wenye kubomolewa na badala yake walizungumza na magazeti na siyo kuleta Bungeni.

Tunachozungumza hapa ni kwamba, mfano barabara ya Rombo inajengwa sasa na kuanzia zamani hiyo barabara iliwakuta wanaoishi hapo, leo hii unataka wabomolewe nyumba zao bila fidia yoyote! Huo siyo Utawala Bora na ni kinyume na haki za binadamu, kwani barabara na sheria yenyewe iliwakuta wananchi wamekaa. Hivyo, hatukatai barabara, lakini kama itapita kwenye eneo la mwananchi kama vile nyumba, makaburi, makanisa, misikiti, mashamba na kadhalika ni haki kabisa wafidiwe bila shida na watafutiwe maeneo ya kwenda ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hebu Serikali ifikirie ile sheria ya vijiji ya mwaka 1974 ya kusogeza wanavijiji kandokando ya barabara ili kupatiwa huduma kirahisi. Leo hii unataka waondoke bila fidia, je, hauoni kuwa huo ni usumbufu wa ubabe wa Serikali kwa wananchi wake?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni juu ya Viongozi wa CCM wanapokwenda kujinadi kwenye majimbo yaliyoshikiliwa na Wapinzani, husema kuwa Serikali haiwezi kuleta maendeleo kwenye eneo la Mbunge wa Upinzani! Sasa mambo kama haya kwa Serikali yenye mfumo wa demokrasia ya vyama vingi ni kinyuma cha Utawala Bora. Hivyo, tunaomba Serikali ikemee hilo na kwamba Serikali haina upendeleo katika kutoa maendeleo kwa wananchi wake.

Kwa mfano, Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali juu ya uamuzi wake wa kusajili Shule za Sekondari za Kata ambazo nimezihamasisha mimi mwenyewe. Shule za Sekondari saba zimepata usajili mwaka huu na ni katika Jimbo langu mimi Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na ni Mpinzani. Aidha, Halmashauri yangu ilipata cheti namba moja kwa ufanisi mzuri wa kazi. Je, hayo siyo maendeleo? Bado ujenzi wa barabara, madaraja na kadhalika. Ninashauri kuwa wakemewe sana watu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni kuhusu kilimo katika nchi hii. Serikali inafanya mchezo na jambo hili la kilimo na hasa cha umwagiliaji. Ningependa kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mtaalam katika mambo ya Kilimo, Serikali iamue kwa makusudi, kujiingiza kichwa kichwa kwenye sekta hii ya kilimo kwa kuwasaidia sana wakulima wakubwa ambao ni wazalendo ili waweze kulima zaidi na kuuza zaidi na kuweza kuzuia kushuka kwa thamani ya fedha yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu Tanzania ina uwezo wa kulima na kulisha chakula Afrika nzima, kama tutazingatia kilimo cha umwagiliaji. Hakuna mkombozi mwingine Tanzania ila ni kilimo na mifugo, basi. Tumechoka kila siku tunazungumzia pembejeo, umwagiliaji, na Serikali inaona na kutazama na kuacha kama vile halituhusu.

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 42 za *STABEX* zilizoletwa na *EU*, nakumbuka nilikuwa mmojawapo wa watu waliopigania *STABEX*, nikiwa Bukinafaso. Nilifanya mkutano na watu hao wa *EU* na wametimiza ahadi yao. Cha ajabu ni kwamba, hata hizo ambazo ni msaada kutoka kwa Wahisani hao hazijawafikia wadau, ambapo sasa ni mwaka mzima tunapigwa danadana hapa Bungeni. Naomba Serikali itoe tamko la

*breakdown* ya fedha hizo hapa Bungeni kwa uhakika na siyo kila Waziri anatoa jibu lake kama vile siyo wamoja.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni suala la umwagiliaji *Lower Moshi Irrigation*, pamoja na maswali yangu ya mara kwa mara hapa Bungeni, pamoja na ahadi ya Rais huko Mabogini Moshi Vijijini, Mawaziri husika wamekuwa wakitoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, katika *Hansard* tarehe 1 Novemba, 2001, Swali Na. 37 lilijibiwa kuwa tayari kuna kibali cha *water right* ya 3.71 na Mheshimiwa Rais alifika huko mwaka 2002 na aliahidi kuongeza idadi hiyo ya Maji. Cha kushangaza ni kwamba, wakati akijibu maswali haya Bungeni, Waziri wa Kilimo aliliambia Bunge kuwa, ahadi hiyo ya Rais imekwisha tekelezwa na akataja hiyo *water right* ya zamani wakati akijua kuwa siyo kweli. Je, wale wananchi wa Mabogini waliosikia kuwa Mheshimiwa Rais ameshatimiza ahadi yake, watatuelewaje wakati siyo kweli kwamba Rais ameshatoa kauli yoyote juu ya jambo hilo?

Mheshimiwa Spika, yanatosha kwa siku ya leo. Ahsante.

**MHE. SUMRI A.S. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kutamka kuwa naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu, kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapa pole ndugu zangu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Dada yake, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na Mzee wetu. Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amina*.

Aidha, nampa pole Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, aliyevamiwa na majambazi katika Kijiji cha Mseyu Mkoani Morogoro. Pia nampa pole Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, aliyepata ajali ya gari na kuumia na Mheshimiwa Estherina Kilasi, kwa ajali aliyopata.

Mheshimiwa Spika, vile vile nimpe pongezi ndugu yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kupata ushindi katika uchaguzi mdogo uliofanyika Jimboni kwake yeye na Madiwani wake wote waliotoka *UDP* na kurudi kwetu *CCM*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na bajeti nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Serikali kupitia Ofisi yako Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusu sehemu zifuatazo ili iweze kutusaidia kama alivyoeleza katika hotuba yake kifungu cha 12 kuhusu hali ya ulinzi na usalama. Kwa kweli napenda kufikisha ombi langu binafsi kwake kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Mpanda Magharibi kuwa, ujambazi umekithiri sana katika eneo letu la Ziwa Tanganyika hasa eneo la Kata ya Ikola na Vitongoji vyake vya Kasangantongwe, Kaselammyaga na eneo lote la ziwa upande wetu wa Tarafa ya Karema.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kuna matukio ya ujambazi kama ifuatavyo: Taarifa ya makosa ya ujambazi yaliyoripotiwa Mwambao wa Ziwa Tanganyika kwa mwaka 2000

hadi Mei, 2004, Polisi Kituo cha Karema ni 14. Watu waliotekwa ni 46, watu waliorudi salama ni 32, watu waliouawa kwa kupigwa risasi ni 4, watu 10 hawajulikani walipo hadi sasa, mali zilizoporwa ni nyavu 11, karabai zaidi ya 4 na bidhaa za dukani mbalimbali. Jumla ya thamani ya mali zote zilizoporwa ni Sh. 87,235,500/=.

Mheshimiwa Spika, matukio yaliripotiwa ni kama ifuatavyo: Tarehe 4 Mei, 2000, majambazi manne wenye silaha aina ya *SMG* walipora nyavu moja bila kuua, yenye thamani ya Sh. 145,000/=. Tarehe hiyo hiyo, majambazi hao hao walipora nyavu moja na vitu mbalimbali kwa watu bila kuua, vyenye thamani ya Sh. 717,000/=. Tarehe 19 Mei, 2000, majambazi walipora mali za duka bila kuua wala kuteka na thamani ya vitu haijulikani. Tarehe 30 Novemba, 2000, majambazi wenye silaha ya aina ya *SMG* walipora Sh. 66,000/= bila kuua. Tarehe hiyo hiyo, majambazi hao hao walipora Sh. 15,000/= bila kuteka wala kuua.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Machi, 2003, majambazi wasiojulikana idadi yao wakiwa na *SMG*, walipora wavu mmoja, karabai 4 na kamba za uvuvi 4, vyote vikiwa na thamani ya Sh. 705,000/=. Tarehe hiyo hiyo, huko Kasangantongwe, majambazi walipora mali za duka na pesa taslimu kiasi cha Sh. 1,536,000/= na kuteka watu watano ambao hadi sasa hawajulikani walipo. Tarehe hiyo hiyo tena, majambazi hao wakiwa na silaha ya *SMG* walijaribu kuteka boti, waliposhindwa walimuua mwanamke mmoja kwa risasi na kumjeruhi mwanamume mmoja na kutoweka. Tarehe 3 Agosti, 2003 majambazi kadhaa walipora mabegi ya nguo, radio moja, mtumbwi mmoja, bila kuteka wala kuua, vyote vikiwa na thamani ya Sh. 129,000/=. Tarehe 16 Desemba, 2003, majambazi wanne wenye silaha ya *SMG* walipora nyavu mbili, mtumbwi mmoja, kuteka watu sita na kuua mmoja. Mateka watano walirudi salama. Thamani ya mali hizo haikufahamika. Tarehe 20 Desemba, 2003, majambazi walipora nyavu moja na vifaa vya nyumbani na mali za dukani, vyote vikiwa na thamani ya Sh. 1,500,000/=. Watu sita walitekwa na baadaye kurudi, wote walirudi salama.

Mheshimiwa Spika, 14 Februari, 2004, huko Rwega Ikola, majambazi wasiofahamika idadi yao walipora wavu mmoja na vifaa mbalimbali, vyote vyenye thamani ya Sh. 1,715,000/= na kuteka watu watano na hadi sasa haifahamiki walipo. Tarehe 1 Machi, 2004, majambazi wasiofahamika idadi yao walipora nyavu mbili na mitumbwi miwili, vyote vikiwa na thamani ya Sh. 1,500,000/= na kuteka watu 11 na kuua mmoja. Kati ya mateka hao, walirudi 10 wakiwa salama. Tarehe 11 Mei, 2004, majambazi watano wenye silaha ya *SMG*, wawili walipora nyavu mbili na bidhaa mbalimbali zenye thamani ya Sh. 600,000/= na kuteka watu 12 na kumuua mmoja kati ya hao 12 na kurudi mateka 11 salama. Baada ya kuokolewa na Askari wa JWTZ, Polisi, pamoja na wananchi na kufanikiwa kuuwawa kwa hayo majambazi wanne na kukamata silaha za *SMG* mbili zikiwa na *magazine* nne bila risasi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ulinzi, Serikali imesikia kilio chetu na kutupa Kituo kidogo cha Jeshi (JWTZ) pale Ikola, Tarafa ya Karema. Wanajeshi wetu tunawashukuru sana kwa kazi yao nzuri, lakini pamoja na ujasiri wao, hawana vitendea kazi. Inafikia wanapotokea majambazi, inabidi wachangiwe petroli kwa ajili ya kufuatia majambazi huko ziwani na hali hiyo inafanya kazi yao kuwa ngumu sana. Ninaomba kwake



Mheshimiwa Waziri Mkuu, wale Wanajeshi wetu kule Ikola wapewe mafuta ya kutosha (petroli na dizeli). Wanalo gari, lakini pia hata pesa za matengenezo hawana.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha mafuta wanachopewa kwa sasa ni kama ifuatavyo: *Diesel* lita 290 kwa miezi mitatu, *petrol* kwa mwezi hakuna na *engine oil* hakuna.

Mheshimiwa Spika, mahitaji halisi kwa ajili ya ulinzi na utawala ni kama ifuatavyo: *Diesel* kwa mwezi lita 300, *petrol* kwa matumizi ya *boat* lita 300, *engine oil* kwa ajili ya gari na mashine ya *boat* lita 50 kwa miezi mitatu, fedha kwa ajili ya matengenezo ya gari na *engine* ya *boat* Sh. 200,000/= kwa muda wa miezi mitatu, fedha za *stationery* Sh. 50,000/=, *generator* kwa ajili ya kuchaji betri na *radio call*, kwani inabidi kufuatia chaji km. 130 wilayani na ubovu wa barabara toka Mpanda, Karema hadi Ikola, utendaji wa kazi za ulinzi unaathirika wakati wa masika, barabara hazipitiki. Tunaomba barabara hiyo ya mpakani ipewe kipaumbele kiulinzi na biashara.

Mheshimiwa Spika, bado nazidi kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, *speed boat* ya ulinzi, ambayo itakuwa eneo la uvamizi.

Mheshimiwa Spika, imebidi yote hayo niyaweke mbele yake, Mkuu wa Serikali na Wizara zote, baada ya kuona kuwa tunazidi kuelemeza na majambazi wenye silaha wakitawala mazingira ya uzalishaji mali kwa wavuvi na wakulima na kuwazidishia umaskini wananchi wetu kwa hofu ya kupoteza mali na uhai. Jeshi letu ni imara, ni simba wa kweli. Kukosa vitendea kazi, atakuwa simba asiye na meno wala kucha. Nazidi kulipongeza Jeshi letu kwa ujasiri na uvumilivu hasa katika ulinzi wa ziwani.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni uti wa mgongo wa nchi yetu. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aone maeneo yetu na kutuanzishia mabwawa ya maji kwa ajili ya tahadhari wakati wa ukame kule Kakese, Karema na Katuma. Maeneo hayo yana ardhi nzuri sana kwa kilimo chochote. Ukombozi wetu ni kilimo na maji, ndiyo uhai wa kilimo cha kweli na siyo kubahatisha mvua. Pia Tarafa ya Mwese tuna ardhi nzuri kwa kahawa, migomba na hata chai. Tunaomba barabara itengenezwe toka Mpanda hadi Mwese, ili wakulima wanufaike na kusafirisha mazao yao na wao wenyewe kwenda Wilayani.

Mheshimiwa Spika, nazidi kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, afuatilie ahadi ya Mzee wetu, Mheshimiwa John Samwel Malecela, alipotembelea Karema mwaka 1994. Aliwaahidi wananchi wa Tarafa ya Karema juu ya matengenezo ya barabara toka Mpanda hadi Karema na pia ujenzi wa gati Ziwani Karema. Wananchi wa Tarafa ya Karema wametoa salamu hizi kwako, wanauliza tamko la kiongozi wa ngazi ya juu Serikalini tangu mwaka 1994 mbona linapuuzwa? Mheshimiwa Mzee Malecela bado yupo, tunaomba tusikilizwe.

Mheshimiwa Spika, katika Tarafa ya Kabungu tuna kilimo cha mpunga, tumbaku, mahindi na muhogo. Kuna tatizo la pembejeo kutofika kwa wakati, pia bei za pembejeo hazina unafuu kwa wakulima, maana pembejeo zimekuwa ghali zaidi kuliko hata mwaka 2002. Wakulima wetu wapatiwe unafuu, kwani kilimo ni uti wa mgongo. Kuwawezesha

wakulima wetu kutanguliza umaskini, kama ilivyo katika Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii, tena na tena.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda niitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi, kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick T. Sumaye, Mawaziri wake wote wawili, Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi (Sera) na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi (Habari na Siasa), Katibu Mkuu na Watendaji wote, walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuinua uchumi wa nchi yetu na kuwaletea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vile vile nitakuwa mchoyo kama sitampongeza mwanamke mwenzetu, Mama Esther Sumaye, ambaye mara nyingi amekuwa bega kwa bega na mume wake katika kutekeleza majukumu yake kwa Taifa hili maskini, ikiwa ni pamoja na kumpa faraja pale anapoonyesha kuchukia ama kupakwa matope na wananchi bila sababu zozote za msingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi sasa kwa ridhaa yangu bila kushawishiwa na mtu, nitamke rasmi kuwa, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Mungu awatie nguvu na afya ili waweze kutekeleza azma yao kwa vitendo.

Kuhusu tahadhari ya janga la njaa. Naipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa juhudi kubwa waliyoifanya katika kuhakikisha wananchi waliokumbwa na janga la njaa, wamepata huduma. Ofisi hii ilijitahidi sana kutoa huduma ya kupeleka chakula cha msaada kwa wale wasiojiweza na chakula cha kununua kwa bei nafuu kwa wananchi wenye uwezo.

Napenda nitambue kuwa Serikali yetu katika mambo mengi mazuri kwa raia wao, kiasi kwamba nashawishika kutamka kwamba, Serikali ya CCM ni bomba. Hii imetupa faraja sana Wabunge wenye dhamana ya watu, kusimama kwenye majukwaa na kuongeza bila wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia walioshiriki kutoa takwimu sahihi za hali halisi ya janga la njaa, kuanzia Uongozi wa Mkoa wangu wa Singida na wa Wilaya, pamoja na Watendaji wote, kwani takwimu hizo ziliisaidia Serikali kufahamu na pia walifuatilia utekelezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, vile vile nitakuwa mchoyo kama sitawatambua Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Majimbo ya Mkoani kwangu, nikianza na Mheshimiwa Mgana Msindai, kwa kutoa msaada wa awali wa magunia 10 ya mahindi Jimboni kwake, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, alitoa magunia 100 katika Jimbo lake, pamona na wote kwa ushiriki wao wa namna moja ama nyingine. Mungu awabariki sana, awape nguvu, uwezo na roho ya kuendelea kuwajali wapiga kura wao.

Mheshimiwa Spika, Walimu ni watumishi wanaotegemewa sana katika Taifa hili na wenye umuhimu wa pekee. Kazi zao zinafahamika jinsi gani zilivyo ngumu na zenye hatari kwa maisha yao. Kitendea kazi chao kikubwa ni chaki na athari ya chaki inafahamika na mengine mengi. Je, Serikali ina ugumu gani wa Mwalimu kutolipwa mshahara wake, hasa wale wanaoanza kazi tena wengi wao hupangiwa vijijini ambako hawana shangazi wala mjomba wa kuwahudumia? Hivi tunategemea kumjengea maisha mazuri Mwalimu huyu au kumharibia maisha yake, kwani lazima baada ya kushindwa kuishi, atapokea hata misaada ya masharti? Hatima yake kuolewa na watu ambao siyo stahili yao. Hapo ndipo anakuwa ameharibu *future* yake yote.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali isifike mahali pa kuwashawishi Walimu kuanzisha mgogoro na Serikali yao. Suala la msingi ni kutoa kauli ya utekelezaji wa asilimia mia moja kulipa madeni yao yote ya mishahara, fedha za kujikimu kwa siku saba Walimu wanapoanza kazi, fedha za likizo, nauli, fedha za matibabu, fedha za uhamisho na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali iwe na mikakati endelevu ya kuhakikisha Mwalimu analipwa haki zake kila inapobidi. Nina hakika watarudisha imani kwa Serikali yao na kuongeza bidii zaidi kazini.

Mheshimiwa Spika, akina mama wako mbele sana katika suala zima la kuondokana na umasikini. Tangu Serikali ilipowahamasisha na kuwasaidia kupata mikopo, wanawake wa Mkoa wa Singida wametengeneza bidhaa mbalimbali ndani ya vikundi vyao. Mfano, Iramba ya Mashariki, akina mama wamesuka mapambo mengi yenye kuingia kwenye Soko la Kimataifa. Ufinyanzi Iramba ya Magharibi, kusuka mikeka, vikapu na kadhalika, Singida Vijijini na Manyoni, tatizo soko hakuna. Hapa Bungeni Serikali inasema *SIDO*, je, *SIDO* imewezeshwa kiasi gani ili inunue na wao wapeleke kwenye Masoko ya Kimataifa? Vile vile akina mama wa Shelui Sekenke, wana migodi ya dhahabu, wanapika chumvi; bali hawana mikopo mikubwa ili wanunue vitendea kazi vinavyofaa kwa kazi hii nzuri ya kuinua uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, ninatoa pongezi kwa viongozi na wake za viongozi waliosaidia akina mama wanaojitahidi kuondokana na umaskini, akiwemo Mama Anna Mkapa, Mama Shein Mama Esther Sumaye, Mawaziri Wanawake na Katibu Mkuu wa UWT, Bibi Halima Khatib, Mungu awazidishie waendeleo kutoa misaada hii. Ninaiomba Serikali iwasaidie wanawake wa Nkonkilangi Madinijoto, kwani chumvi yao ni nzuri na vifaa vya kuchimba dhahabu na dawa ya kukamatishia madini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweke kauli au mikakati ya kuzitaka Halmashauri zote nchini zitenge fedha kwenye mifuko ya akina mama kama ilivyo azma ya Serikali. Kwa kuacha kutenga fedha, ni kupuuza agizo la Serikali na kuwanyima wanawake haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002, Mkoa wa Singida ulitembelewa na Mheshimiwa Ramadhani Mapuri, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Habari na Siasa na akatoa ahadi ya kufunga TV ya Taifa na wananchi walingojea kwa

hamu sana. Sasa mbona kwenye bajeti, Singida haijatajwa? Tunaomba majibu, maana tayari ilishakuwa kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wa MMES, ninaiopongeza sana Serikali kwa kutekeleza Mpango wa MEM. Kweli huu ni mpango wa kuigwa na nchi zingine zilizochelewa kama yetu. Sasa niishukuru Serikali kwa kuhamishia juhudi zake kwenye Shule za Sekondari. Naiomba Serikali ianze kuboresha kwanza shule zilizojengwa kwa nguvu za wananchi kwa Mkoa wa Singida - Shule za Shelui, Ndago, Gumanga, Ilongelo, Salmini, Ikungi, Chikuyu, Itigi, Sanza na zingine zote za aina hiyo, ili zifanane na zile zilizojengwa na Serikali zipate Maabara, Maktaba na Walimu wa kutosha. Shule hizi zinaleta huruma sana, zimezidiwa hata na madarasa ya MEM

Ninaiopongeza Serikali kwa kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya. Huu ni ukombozi kwa watumishi wote nchini. Tatizo ambalo ni kero, bado baadhi ya watumishi kutokuwa na Kituo cha Afya ama kituo chochote cha tiba, pindi wanapoumwa. Naiomba Serikali iwape watumishi asilimia tatu kwenye mishahara yao ili na wao wapate huduma hii. Vile vile kuna dawa ambazo watumishi hawaruhusiwi kuzipata kupitia Mfuko huu wa Bima ya Afya. Je, haki iko wapi kutoa huduma nusu nusu kwa wateja? Si afadhali basi wapewe fedha za mishahara yao ili wajihudumie? Hii itaondoa utata.

Mheshimiwa Spika, ninaiopongeza sana Serikali kwa kuondoa VAT kwenye ununuzi wa Pembejeo. Sasa niulize swali. Je, Pembejeo hizi zinapatikana? Je, wakulima uwezo wa kuzinunua wanao? Nina hakika wenye uwezo wa kununua ni wachache. Naiomba Serikali iweke udhibiti wa bei za kukodi pembejeo kulimiwa, kwani wengi wao hujiweka bei za juu bila kuwahurumia wenzao. Vile vile kuwepo na mpango wa kukopeshwa wakulima wasio na uwezo ili walipe baada ya kuvuna na kuuza. Hii itawasaidia sana wakulima kulima mashamba makubwa.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali mingi ni mizuri sana, tatizo ni utekelezaji tu. Hapa naishauri Serikali iwawezeshe Maafisa Ushirika, Wachumi, ili wasimamie utekelezaji wa kuanzisha vyama hivi kutoa elimu na upatikanaji wa watumishi bora. La sivyo, vyama hivi vitapata wajanja, fedha zitaliwa na hatimaye vitakufa kama miaka iliyopita. Taaluma ni muhimu sana kwa washirika wote ili vyama hivi viimarike.

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Spika, Serikali imeonyesha nia nzuri ya kufanya uchaguzi kuwa wa haki na huru kwa kuanzisha Daftari la Wapiga Kura. Tunaomba Daftari hili liwe wazi na kila mwenye haki ya kuandikishwa aandikishwe. Uwakala wa Vyama vya Siasa uwepo wakati wa kuandikisha Daftari hilo.

Pili, ni kuhusu Tume ya Uchaguzi. Serikali ilishauriwa kwamba, Tume iwe ya uwakilishi wa Vyama vya Siasa, imeshindikana. Sijui kuna siri gani mpaka mkakataa ushauri huu. Lakini tunachoomba, Tume iwe huru, isiingiliwe kati na Serikali au na vyombo vya dola. Isimamie uchaguzi kwa mujibu wa sheria na mshindi atangazwe bila mizengwe. Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ajue kwamba, amani na usalama wa nchi, umo ndani ya mikono na mdomo wake. Ahakikishe anachunga haki na endapo

atavurunda na kupinda uamuzi wa wapiga kura, basi atasababisha maafa makubwa ambayo hata yeye hatakuwa salama. Hawezi kusababisha vurugu na watu wakauana na yeye akaachwa adunde barabarani akiwa mzima. Kama Mwenyekiti wa Tume hawezi kuacha kuwa wakala wa CCM, kuwa na wagombea mfukoni, kuwa lazima chama fulani kishinde, basi namshauri ajiuzulu mara moja kabla ya kumfika haya ambayo nayatabiri.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni ya amani na ni kimbilio la raia wa nchi nyingi ambazo hazina amani. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi yetu imejaa dhuluma na dhuluma iko ya aina tatu: Dhuluma ya rushwa, dhuluma ya uchaguzi na dhuluma ya kugawa maendeleo sawa.

Mheshimiwa Spika, dhuluma ya rushwa imejaa nchini na hupati haki yako bila kutoa chochote. Dhuluma ya uchaguzi ni mbaya zaidi kuliko dhuluma zote. Kuitumia Tume ya Uchaguzi kuharibu uchaguzi na kuweka viongozi ambao hawakuchaguliwa na wananchi, kutumia vyombo vya dola kusaidia hilo. Dhuluma ya kugawa maendeleo sawa ni kutokugawa maendeleo (keki ya nchi) sawasawa, mikoa mingine kuendelea zaidi na mingine kudumaa, mfano ni Mikoa ya Kusini na Kaskazini mwa nchi yetu. Dhuluma hizi tatu zikitimia katika nchi ni hatari. Turudi katika Dini, imani zetu (Kurani na Biblia), vitabu vyote hivi vimelaani dhuluma na Mungu atahukumu hapa hapa duniani kwa mwenye kudhulumu, hata kama kilichodulumuwa kina uzito wa mzigu wa mdudu chungu (sisimizi).

Mheshimiwa Spika, kuna aya katika Biblia zimekataza dhuluma. Pia kuna aya tatu katika Kurani, zilizokataza dhuluma. Hakuna kitakachozidi kwa mwenye kudhulumu ila hasara. Hakuna kitakachozidi kwa mwenye kudhulumu ila *dhalala*. Hakuna kitakachozidi kwa mwenye kudhulumu ila *tabara*. Aya ya kwanza inaonyesha hasara kwa mwenye kudhulumu, mfano, ajali za kila siku za barabarani, magari, treni, meli na moto katika benki na Ikulu, matetemeko na kadhalika. Aya ya pili (*dhalala*) ni kudhalilika kila uchao, mfano, njaa inasumbua kwa nini na tuna raslimali za kutosha za kukuza uchumi, madini tunayo lakini tumewaachia watu wanachimba, wanachukua kwa ndege kupeleka kwao na sisi tunawatazama tu.

Mkaa wa Mawe Mchuchuma, tunautazama tu, wenzetu nchi za nje wanauchimba mkaa huu mita 20 - 30, sisi wetu upo juu kabisa. Wataalam wapo, lakini ni nini kinatuzuia! Chuma - Liganga, tunakiangalia tu. Samaki na mazao ya baharini, tumewapa watu leseni wanavua na wanauza nje bila sisi kujua. Samaki wanakwisha, sisi tunakunywa pombe. Vile vile wanyamapori, Waarabu wamepewa leseni wanaua tu. Mito na maziwa, maji yanatiririka baharini bila kutumika na sasa tunaomba chakula kwenye nchi ambazo zinaishi majangwani. Aya ya tatu (*tabara*), ni ukame ambao Mungu huutia katika nchi yenye dhuluma. Mungu ameondoa mvua yake. Nashauri kwamba, ili Mungu arudishe mema yake kwetu, tuondoe dhuluma katika nchi yetu, dhuluma ya rushwa, uchaguzi na haki sawa.

Mheshimiwa Spika, kuna uwanja mmoja wa ndege ambao kuna ndege ya Shirika moja la kigeni, huingia nchini mwetu kila wiki, tena mchana, kuna mtu mmoja mashuhuri sana, kesho yake ndege ikishakuja, huenda uwanjani hapo na kufanya biashara ya

madawa ya kulevywa. Ikifika ndege, huwa kuna vijana watatu ambao hushuka kwenye ndege hiyo bila kupekuliwa mizigo yao na aghalabu hupitia *VIP* na mara nyingine hupanda ndege hiyo bila kupekuliwa mizigo yao. Je, kulikoni, huo hauwezi kuwa mwanya wa kuingiza madawa ya kulevywa? Siko tayari kutoa maelezo zaidi ya haya, nahofia usalama wangu. Serikali ina mkono mrefu, ichunguze na itagundua.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Spika, naomba niwasilishe mchango wangu wa maandishi kwa hotuba ya Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, ningependa kwa kuanza kuipongeza Serikali kwa namna ilivyoshughulikia kwa umakini wa hali juu, pale tatizo la njaa lilipoikumba nchi yetu. Nawapongeza viongozi na Watendaji wote waliohusika kwa namna moja au nyingine katika utekelezaji wa zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu hivi sasa ipo katika mapambano makubwa ya kuondoa umaskini. Mipango, Sera, Makongamano, Warsha na Semina nyingi zinazoendeshwa hivi sasa, kwa sehemu kubwa zinalenga katika kupanga mbinu na mikakati kutokomeza umaskini.

Mheshimiwa Spika, takriban viongozi wote kwa umoja wetu, Tumekuwa tukitilia mkazo uimarishwaji wa shughuli mbalimbali za uzalishaji wa miundombinu ili kurahisisha mapambano hayo. Tunazungumzia kuimarisha kilimo chetu, ikiwa ni pamoja na kutilia mkazo kilimo cha umwagiliaji, tunaelekeza ufugaji wetu uwe wa kisasa ili tufuge kibiashara, utalii na biashara na hata uvuvi na uwekezaji tunaowavutia wawekezaji ili tuweze kufanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo langu ni kwamba pamoja na ukweli huo kuhusu umuhimu wa biashara katika mapambano dhidi ya umaskini, Wizara ya Viwanda na Biashara bado inaonekana kuwa si Wizara ya kipaumbele. Nadhani uamuzi wa kuitenga Wizara ya Viwanda na Biashara kutoka katika Wizara za kipaumbele, haukuwa uamuzi sahihi. Ningependa kushauri sasa kuwa wakati umefika wa kuzungumza na wahisani wetu ili wakubali kuiingiza Wizara hii katika orodha ya Wizara za Kipaumbele. Hii itasaidia kuiwezesha Wizara hiyo kupata fedha za kutosha na kuweza kuimarisha mifuko ya mikopo iliyopo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo sasa, viwango vinavyotolewa kwa wafanyabiashara ndogo ndogo ni vidogo sana na inakuwa vigumu kuweza kuwaendeleza. Ningependa kuishauri Serikali kutafuta mbinu za kuweza kupata fedha za kutosha ili iweze kukopesha wafanye biashara ndogo ndogo mitaji mikubwa kidogo.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kujua ukweli kuhusu agizo la Serikali kuwa michango na ushuru unaotozwa kwa wakulima kutokana na mazao yao ya asili usizidi asilimia 5. Ningependa kufahamishwa kama agizo hilo bado lipo au limefutwa. Hii inatokana na maelekezo waliyopewa wanunuzi wa zao la ufuta, katika Mkoa wa Lindi ambao wametakiwa kutoa ushuru wa zaidi ya 18% hadi 23%. Kama agizo hilo bado lipo,

naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anajibu hoja anijulishe na ikiwezekana arudie tena kuwakumbusha Watendaji wake kuhusu umuhimu wa kutekeleza agizo hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningependa kutoa pongezi zangu kwa Watendaji wa Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya kwa kazi yao nzuri, isipokuwa nashauri, kitengo hicho kipewe fedha za kutosha kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya dawa za kulevya. Hali ilivyo sasa ni kwamba kitengo hicho kinategemea sana vyombo vya habari kwa maana ya Redio na Magazeti katika kutangaza madhara ya dawa za kulevya na kwa kweli vyombo hivyo vya Redio na Magazeti vimefanya kazi nzuri. Lakini wakati umefika sasa wa Tume kuendesha semina na makongamano katika nchi nzima ikianzia na mikoa ile ambayo tatizo hili ni kubwa. Aidha, wananchi waelimishwe kuhusu umuhimu wa kuvisaidia vyombo vya dola katika mapambano dhidi ya dawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Spika, nimeona inafaa na mimi nichangie mawazo yangu machache huku nikimpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na ya kina. Naiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Uzalishaji Mali, kazi kubwa iliyo mbele yetu ni kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Maeneo yanayostahili kupewa kipaumbele kukuza uchumi na kuwatoa katika umaskini wananchi walio wengi ni Kilimo, Mifugo na Uvuvi, viwanda hasa viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao ya kilimo, ushirika, uchimbaji wa madini na utalii, ujenzi na ukarabati wa barabara na ukuaji wa biashara ya nje. Maeneo yote hayo yana mchango mkubwa katika kuwapunguzia wananchi umaskini na kipato.

Mheshimiwa Spika, lazima juhudi zilizokwisha kuanza kututoa katika kilimo duni cha jembe la mkono kwenda kwenye kilimo cha kisasa chenye kutumia ujuzi na maarifa, ziendelee. Ukame na upungufu wa chakula mara kwa mara umeonyesha wazi kuwa lazima sasa juhudi kubwa ielekezwe kwenye kilimo cha umwagiliaji mashamba. Mpaka sasa tumeshindwa kutafsiri azma yetu ya kuimarisha na kuendeleza mbele kwa ufanisi mkubwa kilimo cha umwagiliaji maji mashamba.

Mheshimiwa Spika, lazima sasa tuamue kuyaendeleza mabonde ya mito yote mikubwa nchini kama Ruaha, Kilombero, Rufiji, Wami, Pangani, Malagarasi, Ruvuma na mengine, kama maeneo tarajiwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji. Wakati huo huo *scheme* ndogo za umwagiliaji zinazojulikana zifufuliwe na kuendelezwa na *scheme* mpya zianzishwe kutoka Wilaya ya Kilosa, *scheme* hizo ndogo ziko Malolo, Kilangali, Mvumi, Likandu, Lumuma na Munisagara.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika kupambana na upungufu wa chakula, lazima sasa hatua zichukuliwe kujiwekea akiba ya chakula katika kila Kaya na katika kila Kijiji. Katika Jimbo langu la Uchaguzi (Gairo), upo mfano hai wa vijiji viwili vya Mkalama na

Majawanga katika Tarafa ya Gairo ambako wananchi wameweka utaratibu madhubuti wa kujiwekea akiba ya chakula na akiba ya mbegu za mahindi na mtama katika ghala ya kijiji kwa kila kijiji, ghala ambazo wamezijinga wao wenyewe kwa kusaidiwa na Shirika la Misaada la *AFREDA*.

Mheshimiwa Spika, hivi ni vijiji viwili vilivyokuwa na akiba ya kutosha ya chakula kiasi kwamba hawakuhitaji msaada wowote wa chakula Serikalini wakati wa upungufu wa chakula. Inafaa sasa huo ndiyo uwe utaratibu mahsusi wa vijiji vyote nchini kuwa na ghala za kuhifadhi chakula cha akiba na mbegu za mazao mbalimbali. Hili linawezekana.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kukuza uchumi, tunahitaji pia kuzingatia suala uwekezaji katika sekta ya uzalishaji mali na kukuza uchumi. Kama ibara ya 46 ya Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000 hadi 2010 inavyosema: “Uchumi wa kisasa, pamoja na kwamba unategemea kazi na maarifa, lakini unachochewa sana na mitaji ...”

Sera yetu ya uwekezaji imeiwezesha nchi yetu kuvutia mitaji. Tunahitaji pia kuimarisha utalii na kuwekeza katika shughuli za utalii. Tuchukulie kwamba Bodi ya Biashara ya Nje na Bodi ya Utalii ni vyombo vya umma vilivyopewa jukumu mahsusi la kuvutia uwekezaji kutoka nje na kukuza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, njia mojawapo ya kuwezesha kukuza mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi ni kushiriki kwa Bodi ya Biashara ya Nje katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa nje ya nchi. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati kuwezesha Bodi ya Biashara ya Nje (*Board of External Trade*) ishiriki katika Maonyesho ya Biashara ya *EXPO 2005* huko Japan. Ushiriki wa Tanzania katika *EXPO 2005* umomashakani kutokana na *BET* kukosa fedha walizozomba Serikalini katika Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ya mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Huduma za Kiuchumi, kinachohitajika hapa ni kuongeza nguvu katika ujenzi na ukarabati wa barabara. Juhudi kubwa na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika ujenzi wa barabara kuu za lami chini ya uongozi wa Wizara ya Ujenzi na barabara za mikoa chini ya *Regional Road Boards*, zinaonekana wazi na zinastahili kupongezwa. Lakini kwa kuinua uchumi vijijini, juhudi zaidi ielekezwe katika utengenezaji na ukarabati wa barabara vijijini. Iko haja ya kuwatumia Wahandisi wa Ujenzi wa Mikoa kusaidia na kufuatilia ujenzi wa barabara vijijini. Wahandisi wa Halmashauri wanahitaji kusimamiwa kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Huduma za Jamii, katika kuondoa umaskini usio wa kipato, mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utaratibu shirikishi wa uandaaji wa mipango ya elimu na utekelezaji wa MEM, yameonyesha mikakati sahihi kabisa ya kuwashirikisha wananchi kujipatia maendeleo kwa haraka. Utaratibu huo unafaa kuigwa na sekta zote zenye lengo la kuboresha maisha na kuinua uwezo wa wananchi kujiondoa katika lindi la umaskini. Mpango wa Maendeleo ya Shule za



Sekondari ambao unatarajiwa kuanza rasmi Julai, 2004 nao unastahili utekelezwe kwa ari ile ile iliyoonyeshwa kwenye MEMEM.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Huduma za Afya, utaratibu shirikishi wa Mfuko wa Afya ya Jamii, inafaa sasa uendelezwe katika Wilaya zote nchini. Hii ni pamoja na Bodi za Huduma za Afya katika Halmashauri na Kamati mbalimbali za vituo vya kutolea huduma za afya. Mafanikio tuliyoyapata katika uimarishaji wa Afya ya Msingi yalituwekea msingi ambao unastahili kuendelea kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zote zinazoonekana kuchukuliwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI, bado hali ya UKIMWI nchini ni mbaya. Ipo haja ya kutazama upya utaratibu tuliojiwekea, la muhimu kabisa ni kuwa na uongozi imara katika ngazi ya Taifa ambao wakati wote utekelezaji na kufuatilia juhudi zote zinazochukuliwa kupambana na janga la UKIMWI. Hali ilivyo sasa tuna utitiri wa vyombo mbalimbali, mashirika mengi yasiyo ya Serikali na hata vikundi vya familia vimejitokeza kujihusisha katika kupambana na UKIMWI. Utaratibu wa hali ya juu unahitajika. Nina mapendekezo ambayo mimi naamini yatasaidia katika kuleta mafanikio.

Kwanza, sekta ya afya ndiyo inayostahili kuwa Sekta Kiongozi katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

Pili, ipo haja ya kuwa na Waziri Maalum atakayepewa dhamana na madaraka ya kuongoza mapambano dhidi ya UKIMWI, awe ni Waziri atakayewajibika Bungeni kwa ukamilifu. Hivyo katika utaratibu wa sasa, mmoja katika Mawaziri wawili wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu apewe dhamana hiyo au Waziri wa Afya apewe jukumu hilo.

Tatu, Kamati shirikishi za kudhibiti UKIMWI za Halmashauri za Wilaya ziwezeshe kifedha na zisimamiwe kwa ukamilifu. Zilivyo hivi sasa hazifanyi kazi inavyostahili. Muundo wake pia urekebishwe, aingizwe Mwakilishi wa Sekta ya Afya kama Mjumbe katika Kamati. Hivi sasa ameachwa nje, si Mjumbe wa Kamati yoyote. Hii siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, katika mapambano dhidi ya UKIMWI, nipendekeza Sekta ya Afya iwe Sekta Kiongozi kwa kuwa shughuli nyingi za kupambana na UKIMWI zinatekelezwa na na Sekta ya Afya. Huduma za Maabara na Wataalam wa Maabara ndio wanaogundua watu walioambukizwa na wenye virusi vya UKIMWI. Ushauri nasaha ni sehemu tu ya Elimu ya Afya. Bila kuwa na ujuzi wa Elimu ya Afya ya Jamii, huwezi kutoa huduma za ushauri nasaha kwa ufanisi. Utoaji wa Elimu wa Afya ni kazi ya kawaida ya Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, tiba sahihi na ujuzi wa matumizi sahihi ya dawa za kurefusha maisha ya wagonjwa wa UKIMWI, wanaoelewa ni wataalam wa tiba na hata tiba ya magonjwa nyemelezi yanayoambatana na UKIMWI, hutolewa na Madaktari. Huduma za kuwatunza wagonjwa, zinawategemea sana Wauguzi. Hata huduma za wagonjwa wa UKIMWI majumbani wanakoishi wagonjwa zinawategemea sana Wauguzi kutoa ushauri

kwa ndugu wa mgonjwa na hata kusaidia kuuguza. Uongozi wa *TACAIDS* peke yake hautoshi kusimamia mapambano dhidi ya UKIMWI. Lazima usimamiwe kwa ukamilifu na Waziri mwenye dhamana na jukumu la kusimamia huduma za Afya nchini, kwani UKIMWI ni ugonjwa. Hakuna ugonjwa ambao si ugonjwa wa jamii na huduma za afya ni huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, mwisho tuzingatie mwongozo uliotolewa na Rais wetu mpandwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapu katika hotuba yake kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 12 Februari, 2004 ukiwa ni mwongozo wa Kanuni tatu kuu za maisha katika kupambana na UKIMWI.

- Kama hujaambukizwa, hakikisha huambukizwi;
- Kama umeambukizwa, hakikisha humwambukizi mwingine na ujitunze (na kujipatia lishe bora) ili uishi muda mrefu iwezekanavyo; na
- Unyanyapaa uwe mwisho.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu yenye kurasa takriban 68, haikutaja mradi wa Taifa na mkubwa sana wa *Mtwara Development Corridor* wala sehemu mojawapo kama barabara ya *Mtwara - Mbamba Bay* na *Mchuchuma Coal for Electricity*. Je, nitafsiri kuwa ilikuwa *omission* au Waziri Mkuu haupendi na hautaki mradi huo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkoa na Wilaya ya Songea, Jimbo la Peramiho limepata miradi mingi na sehemu kubwa imetekelezwa vizuri. Wajibu wangu ni kutoa shukrani nyingi sana kwa niaba ya wapiga kura wangu. Kuna miradi mitatu imetolewa na Serikali Kuu:-

(i) Barabara ya Songea - Mitomoni pamoja na daraja lake kuvukia Mozambique.

(ii) Barabara ya kutoka Wino kwenda Ifinga, mradi ulipata fedha toka Ujenzi. Kazi ikafanyika hadi kufika Ifinga. Kabla ya kumaliza marekebisho ya *finishing*, Serikali Kuu ikarudisha *cattepillar* na fedha walikopa kuipeleka barabara ya Songea - Tunduru. Sasa *Tanroads* wanaikataa barabara hiyo na kumtupia *District Engineer*. Uwezo wa *District Engineer* ni mdogo sana.

(iii) Umeme wa kutoka Songea kwenda Peramiho, *TANESCO* walianza kazi ya *survey* ili umeme upelekwe Peramiho. *TANESCO* Makao Makuu wakasitisha mradi huo *until further notice*.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati kurudisha miradi hiyo na kuagizwa itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umaskini wa Wilaya fulani, nia ya Serikali ya kupeleka kazi Wilayani ni nzuri. Lakini nia haioani na uwezo. Kuna Halmashauri zinazopata mapato mengi na ziko ambazo hata zingefanyaje hazitapata mapato ya kutosha. Songea ni Halmashauri ambayo haina mapato ya kutosha na baada ya kufuta kodi, hali imekuwa mbaya zaidi. Nashauri tuwe na *National HIPC* yaani tuzitazame Halmashauri zile maskini kabisa zipewe ruzuku nzito toka Serikali Kuu. Ruzuku za upendeleo, kuliko sasa Halmashauri zenye fedha zinapewa fedha zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme Ruvuma, Serikali imejitahidi kufikiria nini la kufanya walifikiria *Nakatuta Hydro* ikawa ngumu. Wakasema Mchuchuma ikiwa tayari, ipate umeme toka Mchuchuma. Lini kitendawili Waziri Daniel Yona, anashughulikia sasa kupeleka umeme wa gridi toka Makambaku. Naomba muunge mkono katika juhudi hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Walimu, tafadhali walipwe madai yao. Tafadhali sana.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii iliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake iliyoandaliwa kwa uhakika na umahari mkubwa sana. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Habari na Sera, pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia kwa kutaka ufafanuzi katika ukurasa wa 39 *para* ya 53. Mstari wa mwisho unazungumzia maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi ya *Mnazi Bay* kwa ajili ya Mkoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma yataanza. Lakini wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anasoma hotuba yake, hakutamka Ruvuma, badala yake aliruka.

Mheshimiwa Spika, maelezo yanahitajika kwa sababu suala la umeme Mkoa wa Ruvuma ni kufa na kupona na kama aliacha kutamka kwa sababu hotuba ilikosewa, basi naomba awaeleze wananchi wa Mkoa wa Ruvuma hasa Mji wa Mbinga kuhusu kupatikana kwa umeme katika wilaya hiyo kongwe yenye utajiri mkubwa. Lakini wakazi wake wanatumia vibatari na kuni kama njia pekee ya nishati.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Mratibu na *think tank* wa maendeleo ya nchi hii hasa katika medani ya mipango. Kupanga ni kuchagua. Sisi tumechagua kutumia maji yetu kuzalisha umeme. Kwa kufanya hivyo, inamaanisha kwamba kilimo chetu itabidi kitegemee mvua ambayo hatuna uhakika nayo. Matokeo ya maamuzi hayo yanatuletea aibu ya njaa pale wakati mvua hainyeshi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine tukiamua kutumia maji yetu ya Mito kuzalisha chakula na mazao mengine ya kilimo ikiwemo mifugo pamoja na matumizi viwandani na mijini, basi itabidi nchi iamue kisera na ni jukumu la Waziri Mkuu kuelekeza sekta hizo ili zikubaliane kuwa na matumizi endelevu ya raslimali zetu adimu kama maji. Hata hivyo, uamuzi wa kutumia maji kama ya Mto Ruvu, Mto Rufiji na kadhalika kwa shughuli za kilimo badala ya umeme, inabidi kupata njia mbadala ya kupata umeme hususan mkaa wa mawe, kinyesi (*biogas*) au kutokana na jua (*solar energy*).

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itathmini upya utaratibu wake wa kupanga ili mipango hiyo iwe na matokeo endelevu na yenye *multiplier effects*. Umeme ukipelekwa nchi nzima na hasa yale maeneo ambayo yamejiandaa kwa maendeleo kama Mbinga, hapatakuwa na sababu ya kuwapa chakula cha njaa au mambo madogo madogo, wao wenyewe watayafanya.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme lisipochukuliwa hatua za haraka litaigawa nchi hii kimaendeleo kati ya mikoa teule kama vile Kilimanjaro, Arusha, Dar es Salaam, Manyara na kadhalika dhidi ya mikoa inayoonewa kama Ruvuma, Kigoma, Lindi na Mtwara ni mikoa ambayo inao utajiri mkubwa. Wananchi wake ni wafanyakazi hodari, lakini wanashindwa kusindika mazao yao au kuvutia wawekezaji kwa sababu ya kukosekana miundombinu hii ya umeme. Kama Serikali haioni umuhimu wa kutimiza ahadi yake ya kupeleka umeme Wilaya ya Mbinga, basi ijue kuwa wananchi wa Mbinga nao wana uchungu kama wenzao wa Mikoa ya Kilimanjaro au Arusha na wana uwezo wa kujenga chuki dhidi ya viongozi hasa pale wanapoona Serikali haiwatendei haki.

Mheshimiwa Spika, mwisho nimalizie mchango wangu kwa hitimisho kwamba rushwa ya nchi hii ambayo wananchi wake wamegawanyika katika makundi mawili, lile linaloona kuwa rushwa imekithiri hasa katika ngazi nyeti na lile linaloona rushwa hata kama ipo, siyo tatizo. Ni jambo la hatari sana kwa maendeleo ya kijamii na uchumi wa nchi. Mbunge anapotamka Bungeni kuwa atatumia *Albadri* kuondoa rushwa miongoni mwa jamii hasa viongozi na watendaji wakuu wala rushwa, budi tafakuri ya kina ifanyike.

Mheshimiwa Spika, kwa lugha nyingine, rushwa ipo na imekithiri. Lakini haiendeshwi na binadamu wa kawaida, labda maruhani kama wale waliopiga kura Pemba. Ikiwa kama maruhani wamevamia mfumo wetu, basi Serikali iangalie upya mfumo wetu wa kisheria na utawala kama unaweza kudhibiti rushwa. Vinginevyo, kila mtu atakuwa anamwonyesha mwenzake kidole nyakati za mchana na kupokea au kutoa rushwa kwa njia nyepesi nyepesi ya takrima. Naomba ushauri huu utendewe kazi. Naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyojieleza mbele ya Bunge, naomba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Ulanga Mashariki, kuunga mkono hotuba yake kwa umakini

alioonyesha. Nampongeza yeye mwenyewe, Mawaziri wa Nchi katika Ofisi yake, Katibu Mkuu na Wataalam wote katika Ofisi yake.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwa Watanzania kwamba Waziri Mkuu katika vipindi vyake vyote viwili vya kumsaidia Rais wetu, kama Waziri Mkuu amefanya kazi nzuri sana. Hii inatokana zaidi na kujituma kwake, yapo mambo ambayo tunatakiwa kujifunza kutoka kwake, hasa ya uchapaji kazi, umakini katika majukumu aliyo nayo, ukaribu na Kiongozi wake wa juu na mwisho umakini wa kuhimili vishindo.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 35 wa hotuba yake, Waziri Mkuu amezungumzia utekelezaji wa miaka kumi kuendeleza Mtandao wa Barabara (2001 - 2010). Katika mafanikio ya suala hili kukamilisha Daraja la Mto Rufiji na kufunguliwa na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, mafuriko ya Mto Rufiji, ujaaji wa maji Mto Rufiji na matokeo ya maji kutoka Mto Kilombero kule Mahenge/Ifakara. Sisi hupata mafuriko ya Mto Kilombero. Hivi Waziri Mkuu kwa umuhimu wa kumalizika Daraja la Rufiji, wakati umefika sasa Serikali kutamka ujenzi wa Daraja la Mto Kilombero? Kutamka tu katika mipango yake ya baadaye, ili awamu zitakazokuja zianze kufuatilia tamko hilo!

Mheshimiwa Spika, kuhusu waliostaafu, pamoja na mapendekezo aliyotoa Waziri wa Fedha kwamba wastaafu hao wataanza kulipwa mwezi Januari, 2005 (wale waliochukua kwa mkupuo), mimi naendelea kushauri kwamba wastaafu hao ni wenzetu, walifanya kazi nzuri katika nchi yetu. Muda huu ni mrefu mno, Wizara inayohusika iteue maafisa kama kikundi cha kushughulikia wastaafu hao na walipwe kabla ya Desemba, 2004 na mwezi wa mwisho uwe ni Januari, 2005.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii awali ya yote kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo sahihi wa kutia matumaini kwa kule tuendako kuhusu ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ulinzi na Usalama. Kimsingi naamini kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vinajitahidi kufanyakazi nzuri. Hali ya nchi kwa ujumla wake imetulia. Lakini upo upungufu kadhaa ambao ni muhimu ufanyiwe kazi. Vitendo vya wananchi kuchukua sheria/hatua mikononi siyo tu kwamba ni vitendo vya uvunjaji sheria, isipokuwa vinaonyesha pia kwa upande mwingine kuwa mahusiano ya vyombo vya ulinzi hususan Polisi na wananchi siyo mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa ulinzi wa umma/wananchi ni suala muhimu lisilo la kupuuzwa. Lakini wananchi wanapogeuzwa miradi ya Polisi, hapo ndipo mgogoro unapoanzia. Kama Askari wetu wangekabidhiwa wahalifu na wananchi wakachukua hatua madhubuti za kisheria kwao, wananchi wangejenga imani kubwa kwao na hivyo kutoingia katika matendo ya kuwaadhibu wahalifu. Kwa hiyo, bado juhudi ya kuhimiza ulinzi wa pamoja kati ya wananchi na vyombo vya dola vya ulinzi, zinahitajika kutiliwa mkazo na kuendelezwa ili waweze kushirikiana pamoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala bora. Pamoja na juhudi na kazi nzuri inayofanywa na Serikali yetu juu ya kuona kwamba kunakuwepo utawala wa sheria, bado tafsiri hii inapotoshwa na Watendaji waovu na walafi walioko katika chombo cha Mahakama ambao hutumia nafasi zao kupotosha haki za raia wema kwa kutumia dhama zao.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu kumetokea kuwapo kesi nyingi za ardhi ambapo wananchi kadhaa wamenyang'anywa mashamba yao ambayo wameyamiliki kwa kipindi cha zaidi ya miaka 30 na baadaye wajanja wachache wamewapeleka Mahakamani kwa kisingizio cha kwamba ni mashamba yao ya ukoo. Kwa hiyo, pamoja na kwamba walihama, lakini sasa wamerudi kuyamiliki na Mahakama ya Mwanzo ikawapa.

Mheshimiwa Spika, sina hakika ni sheria gani ilitumika kuhalalisha maonevu haya. Nilikwisha mwandikia Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba na Mkuu wa Mkoa wangu kumpa nakala pamoja Mkuu wa Wilaya, lakini leo ni mwaka wa pili ufumbuzi haujapatikana. Aidha, suala la rushwa bado ni kikwazo kikubwa katika azma ya Serikali kutekeleza utawala bora. Polisi na Mahakama, vinaendelea kuongoza katika kutuchafulia mazuri yafanywayo na Serikali yetu. Tujipange vizuri Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maafa, napenda kumpongeza Waziri Mkuu na kupitia kwake kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera). Katika kipindi cha janga la njaa lililoathiri sana wananchi, juhudi za dhati zenye utu, zimedhihirika na hivyo kero na adha hiyo ilipunguzwa makali sana na Serikali kupitia kwenu. Nashauri juu ya umuhimu wa kuwepo tahadhari ya mapema juu ya maafa mbalimbali nchini na naipongeza Ofisi yako kuandaa na kuzindua rasmi sera ya maafa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, ubinafsishaji na uwekezaji katika sekta hii ya madini ni jambo zuri sana. Ni matumaini yangu kuwa raslimali hii tukiitumia vyema tunaweza kujikwamua na umaskini uliokithiri nchini. Hata hivyo, mgao wa mapato yatokanayo na sekta ya madini ni vyema ukatazamwa upya na kwa kweli kwa ujumla nashauri yafuatayo katika hili:-

(i) Kuwepo mrabaha unaotolewa moja kwa moja katika Halmashauri/maeneo ambayo migodi hii ipo ili kuwafanya wananchi waone mabadiliko ya haraka ya kiuchumi na kijamii badala ya kupitishia mrabaha katika Serikali Kuu ambapo mapato hayo hulazimika kuingia katika mfuko wa Taifa zima. Naipongeza Serikali kwa kuamua kuunda Tume juu ya utafiti wa namna ya kutatua tatizo hili la Sekta ya Madini.

(ii) Mikataba iliyowekwa baina ya Serikali na wawekezaji wa sekta ya madini ni vyema ikafanyiwa mapitio upya (*review*) kama *option* hiyo ilikuwepo. Hii ni kwa kuwa hali inayoonekana kwa sasa ni kwamba yaelekea kama mapato ya Serikali (mrabaha) tuupatao ni kidogo mno!

(iii) Wananchi wazalendo waliojikita katika sekta hii wawezeshwe na Serikali ili baadaye watoke katika uchimbaji mdogo waingie kwenye uchimbaji mkubwa baada ya kupata uzoefu na nyenzo za kisasa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, pamoja na kuipongeza Serikali kwa hatua inazoanza kuchukua katika eneo hili muhimu, kwa kweli tulichelewa mno kuliona na kuchukua hatua madhubuti juu ya kuinua kilimo chetu kutoka hali ya nyenzo za ujima hadi kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Spika, umwagiliaji na nyenzo bora za kazi ya kilimo pamoja na pembejeo, anuwai ndilo jibu sahihi la kuboresha kilimo chetu. Kinachohitajika ni kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika kilimo. Kwa hiyo, maeneo kama ya Kanda ya Ziwa kupata njaa ni aibu kwa uongozi wetu. Bajeti ijayo, nashauri tufanye Mapinduzi ya kilimo maana Mapinduzi ya viwanda yatafuatia baadaye.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji, naipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kimapinduzi wa kuanza kazi ya ujenzi wa bomba la maji toka Ziwa Victoria kwenda Kahama na Shinyanga. Kimsingi, ili mradi huu uwe endelevu na wenye manufaa kwa wananchi wengi, nashauri maeneo yote ambayo yatapitiwa na bomba hili, vijiji na miji midogo husika iwekewe vituo vya kuchotea maji hayo. Matoleo ambayo yataruhusu vijiji vingine vilivyo umbali wa kilometa 30 na kuendelea kutoka lilipopitia bomba hilo, viweze kupata maji kwa kujitolea wenyewe kuchangia kwa hali na mali wakishirikisha Halmashauri zao ili mradi huu ulete manufaa kwa watu wengi kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kupitisha bomba katikati ya vijiji/miji midogo bila kuwapa huduma kama ambavyo umeme wa gridi ya Taifa ulivyopita katika maeneo kadhaa yakiwemo ya Shinyanga, hususan Jimbo la Solwa, siyo jambo la kiuungwana na utu kwani linachochea moyo wa chuki na hujuma. Aidha, ni udhalilishaji kwa sababu sisi Watanzania wote tunaamini kwamba binadamu wote ni sawa. Haya si maji ya watu wa Mijini tu.

Mheshimiwa Spika, bado naendelea kuamini kuwa nchi yetu itajengwa na Watanzania wenyewe na kwamba ushirikishwaji wa jamii katika kila jambo la ujenzi wa Taifa, kutaendelea kuwepo na moyo wa umoja wa wananchi na kutumia vipaji vyao kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuhimiza suala la kuhamia Makao Makuu Dodoma. Bado upo upungufu kadhaa unaojionyesha Serikalini juu ya umakini wa kutekeleza azma hii. Ni vyema kigugumizi kinachoonekana kijibiwe kwa kufanya maamuzi ya kimapinduzi na hasa kuamua Wizara ya Fedha iwe Dodoma. Maana kiini kikubwa cha uendeshaji kikiwa hapa Dodoma, wengi watalazimika kuishi hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nimekwisha changia kwa kusema ndani ya Bunge hili kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, bado naendelea kuunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda mfupi tuliopewa wa kujadili hoja yoyote kwa kusema, nimeona ni vizuri nichangie kwa maandishi pia ili kuisisitiza yale nionayo kuwa ni muhimu kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuyazingatia.

Mheshimiwa Spika, mtandao wowote wa barabara lazima uwe kamili usiishie katikati. Mfano, tukitaka barabara ya Tunduma - Sumbawanga iwe na manufaa zaidi, lazima iunganishe barabara ya Sumbawanga hadi Mpanda, Uvinza, Kasulu, Kibondo hadi Bukoba ili biashara ya wenzetu na Uganda ishamiri na itoe matunda mazuri. Lakini pia, ili tuweze kutumia nafasi ya hali ya biashara na nchi jirani ya Kongo (*DRC*) ni budi barabara iunganishwe pia toka Sumbawanga hadi *Kasanga Port* ili usafiri wa bidhaa kwenda Kongo, Rwanda na Burundi kupitia Ziwa Tanganyika, ulete mafanikio kwa wakazi wetu. Pamoja na hilo, huu ndiyo wakati muafaka wa kuimarisha Reli ya *TAZARA* ifanye kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, wakati pia umefika wa kuimarisha mpango wa zamani wa *Uhuru Corridor* ambayo ilitarajiwa kuwa chachu ya uzalishaji chakula na mazao ya biashara ili kuwezesha *TAZARA* kuendesha shughuli zake kibiashara. Mheshimiwa Waziri Mkuu azitake Wizara husika kuandaa mikakati wa jinsi ya kutumia maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na uhakika kuwa sera zote zilizopitishwa, Ofisi ya Waziri Mkuu, izitake Wizara zote ziandae mikakati ya utekelezaji wa sera zao na ziletwe kwenye kikao cha Aprili, 2005 kabla ya kikao cha Bajeti, ili tuone kama kweli yaliyomo ndani ya sera mbalimbali yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM, bado kuna haja ya kuangalia upya utaratibu mzima wa uingizaji na uagizaji wa Pembejeo. Mimi nina uhakika, bei ya mbolea katika Soko la Dunia, bado ni ndogo. Bei ya mbolea ikiwemo *Urea, DAP, CAN* bado tunaweza kuipata kwa shilingi 12,000/= kwa mfuko kwa nchi nzima bila hata ya Serikali kulipia ruzuku ya usafiri. Nimekwisha mwandikia Waziri wa Kilimo na Chakula kuhusu uwezekano huo na kupeleka nakala kwa Waziri wa Fedha ili kutuwezesha kutokana na kidogo tulicho nacho, tuagize tani zaidi ya 12,500 za *Urea* msimu huu na kuzisambaza kupitia baadhi ya mawakala waaminifu.

Mheshimiwa Spika, suala hili linahitaji maamuzi ya haraka na ya kukubalika pande zote ili tuone kama hatuwezi kweli kuvunja mtandao wa wafanyabiashara ambao wanakimbilia faida kubwa sana na kuumumiza mkulima. Ombi ni sasa hivi, Uchaguzi ukuta tunasambaza mbolea ya bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia ombi langu kwa Waziri Mkuu kuhusu *SGR* kupewa fedha mapema ili tuwahi ununuzi wa mahindi kwa ajili ya hifadhi yetu kabla ya



walanguzi hawajapita na kuwarubuni watu wetu vijijini. Tuanze kuwawekea viwango vya bei ili wasiwaumize wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe agizo kwa mikoa ile ambayo haitakuwa na minara ya TVT, katika awamu hii, basi Serikali ikubali mitambo ya Halmashauri za Miji na Wilaya, yenye kurusha matangazo kwenye miji yao, iunganishwe na mitambo hiyo ya TVT bila gharama yoyote au usumbufu wa kutakiwa kuwa na leseni ya kuunganishwa na mitambo hiyo. Mkoa wa Rukwa pia tunaomba uingizwe kwenye awamu hii kutokana na upembazoni pamoja na matukio mengi ya kiusalama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, inayohusu Mapitio na Mwelekeo wa kazi za Serikali na Madirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi yake na Taasisi nyingine kwa mwaka 2004/2005. Hotuba ni nzuri, imechambua kwa makini na wazi wazi kazi za Serikali zilizofanywa mwaka 2003/2004 na zinazotarajiwa kufanywa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ina mwelekeo mzuri wa kuleta maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa nchini, mimi kwanza nampongeza yeye pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri na pili, kwa niaba yangu mwenyewe na wananchi wa Jimbo la Mbinga Mashariki, naunga mkono hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda niyafikishe maombi yangu mawili kupitia meza yako Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni juu ya kilimo:-

(a) Naomba mpango wa kufidia gharama ya usafirishaji wa mbolea kwa wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, uendelee. Pia fidia hiyo isitolewe hadi ngazi ya mkoa, bali ingefaa sana ikatolewa hadi ngazi ya Makao Makuu ya Wilaya au ikiwa uwezo unaruhusu, ikatolewa hadi vijijini

(b) Kwa lengo la kuongeza uzalishaji mazao ya kilimo, Serikali ishirikiane na wananchi kujenga mabwawa ya uhakika kwa nchi nzima ili yatumike kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji. Tukiendelea kulima kutegemea mvua tu hii inamfanya mkulima afanye kazi kwa muda wa miezi mitatu na miezi tisa kwa mwaka akae tu bila kazi ya kuzalisha. Katika hali ya namna hii, mkulima itamwia vigumu sana kuondokana na umaskini.

(c) Katika Bajeti ya mwaka 2003/2004, ilitamka kuwa kila Wilaya ichague mazao mawili, moja la chakula na lingine la biashara na Serikali ingesaidia. Kwa kuwa ni

jambo zuri halijafanyika mwaka 2003/2004, basi tunaomba sana lifanyike mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, la pili ni juu ya umeme:-

(a) Makao Makuu ya Wilaya ya Mbinga ni mojawapo kati ya Makao Makuu za Wilaya 13 zisizo na umeme. Wananchi wa Mji wa Mbinga wanaomba kufahamu umeme Mbinga utafika lini? Cha ajabu, mipango ya umeme kwa ajili ya Wilaya zingine inaelezwa, lakini kwa ajili ya Wilaya ya Mbinga, hakuna maelezo na mambo ni kimya.

(b) Umeme unaozalishwa kwa kutumia mkaa wa mawe ni wa uhakika, hautegemei hali ya hewa kama umeme wa maji. Mwaka huu tunaambiwa kuwa mabwawa mengi yanayotumika kuzalisha 70% ya umeme nchini, hali ya maji si nzuri kutokana na uhaba wa mvua katika maeneo hayo. Tunaomba kufahamu ni lini Serikali, *TANESCO* na Mwekezaji wa Mradi wa Mchuchuma wa kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe, mtafikia makubaliano?

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake, kwa kutuletea Bajeti nzuri na makini yenye kuzingatia kuondoa kero na kupunguza umaskini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuchangia mawazo yangu namna ya kuimarisha Muungano, sababu kubwa za kuenzi Muungano wetu, ukiacha usalama na udugu uliopo, ni maslahi hasa ya kiuchumi. Haiwezekani mfanyabiashara makini kuleta biashara zake kupitia bandarini, aache kupitishia Dar es Salaam kama hakuna maslahi.

Mheshimiwa Spika, suala la kodi na tozo/ushuru mbalimbali zinazotowazwa katika bandari zetu lazima ziwe na malengo ya kuhamasisha biashara na siyo kuuu. Kila bandari hasa ya Zanzibar na Dar es Salaam, lazima zifanyiwe uchambuzi yakinifu ili kubaini aina ya mizigo ambayo itakuwea ni kwa maslahi kwa pande zote mbili ili kila mtu afaidike (*win-win situation*).

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Wizara za Fedha za pande zote mbili za Muungano, Wizara za Biashara na Viwanda na *TRA* pamoja na Bodi ya Mapato Zanzibar, kukutana haraka sana kuondoa malalamiko hayo. Vile vile nashauri *TCCIA* na *Chambers of Commerce (ZCC)*, zishirikishwe kikamilifu na baadhi ya Wabunge wa Zanzibar. Tumechoka na kero hii.

Mheshimiwa Spika, suala la mishahara na hasa ya wafanyakazi wa ngazi za chini kutolewa kwa wakati muafaka ni nyeti sana. Haiwezekani mishahara ya Walimu au ya Waganga na Wauguzi isitolewe kwa miezi miwili mpaka mitano, halafu wahusika wasiwajibishwe. Ndugu zetu hawa wanafanyakazi za utume, kazi takatifu za kuwalea vijana wetu na wananchi kwa jumla. Hivyo na sisi tuwaheshimu na kuwaenzi. Mishahara yao iwe ya kwanza kutolewa na isiwe na usumbufu hata kidogo. Sambamba na hilo, naipongeza Serikali kwa kurejesha pesa za wastaafu, lakini naomba kima hiki kihuishwe ili kiweze kuwanufaisha.

Mheshimiwa Spika, tunaelekea kwenye harakati a Uchaguzi, mwaka huu na mwakani. Mimi nawaomba sana viongozi wa kisiasa wa vyama vyote kutumia majukwaa kwa nidhamu na heshima. Tuache kabisa mtindo huu unaoelekea kujikita ndani ya vyama kwa kutumia matusi mengine ya nguoni, kashfa na lugha zingine zisizofaa. Lazima turithishe vizazi vyetu utamaduni mzuri na endelevu uliojaa ustaarabu na adabu ili tuendelee kuwa Taifa la kuheshimika na kudumisha demokrasia. Vyombo husika kama Polisi, Tume ya Uchaguzi na Msajili wa Vyama vya Siasa washiriki kikamilifu katika kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Spika, UKIMWI na utandawazi ni suala linalogusa sana maisha ya Watanzania na Waafrika kwa ujumla. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali, vyama visivyo vya kiserikali na wananchi, bado napendekeza yafuatayo yafanyiwe kazi:-

(i) Vipindi vya TV vimulikwe sana kwa vile vipo ambavyo vinachochea kufanya ngono kuliko elimu ya kuzuia na/au kujikinga yaani maadili mema.

(ii) Wataalam wa Mawasiliano Tanzania na Afrika, wajitahidi kuzuia na/au kudhibiti picha mbaya na vipindi visivyo na maadili katika *internet* vinavyomulikwa katika Bara hili letu kwa nia ya kupotosha utamaduni, silka na adabu za kiasili kwa Waafrika hasa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza hotuba pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anazozifanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kupendekeza suala la uimarishaji wa Muungano wetu wa Tanzania, kwa kuwa kuna watu wabaya ambao hawaupendi Muungano wetu hasa kwa wale wa Vyama vya Upinzani wa Zanzibar. Hupenda kutumia kila njia wanazozoweza ili Muungano wetu uvunjike na kueneza kwa watu kuwa kuwepo na Serikali tatu. Hilo ni suala litakaloigawa nchi yetu. Kwa hiyo, viongozi au watu kama hao wasidharauliwe na badala yake wafuatiliwe na kuchukuliwa hatua kali pale wanapopatikana na hatia na wasiruhusiwe kufanya mikutano yenye matusi dhidi ya viongozi wa Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, napendekeza matangazo mengine ya uhamasishaji wa kupambana na UKIMWI yanayotolewa kwenye TV hasa ITV, yaweze kufanyiwa uchunguzi baada ya kuonyeshwa. Kwa sababu matangazo mengine yanahamasisha ngono badala ya kukemea ngono. Kama lile suala la wapenzi wawili wanapokunana kwa

miguu na muda si mrefu wakaondoka kwenda kufanya hicho kitendo cha ngono. Ni kweli tunaelimishwa juu ya matumizi ya kondomu, lakini imekuwa mno.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kwa sababu nchi yetu ni ya Muungano, basi katika kuondoa umaskini au kupambana na umaskini kuwe Kimuungano. Kwa sababu miradi mingi ya mikopo au ile ya misaada inaishia Tanzania Bara tu, haifiki Zanzibar. Kwa hiyo, umaskini ukiondoka Tanzania Bara na kubakia Zanzibar na kwamba ni Muungano, ina maana bado umaskini utakuwepo na hatutakuwa tumepunguza. Kwa hiyo, ni vizuri Zanzibar itazamwe na kupewa kipaumbele kwa miradi yote inayoingia Tanzania, kwa sababu inakuwa ni maskini mno.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya Ulinzi na Usalama, naipongeza Serikali kwa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya shughuli za ulinzi na usalama. Katika Jimbo la Lushoto na Wilaya kwa ujumla, ujambazi umekithiri katika maeneo ya misitu na njia kuu ya lami kutoka Mombo hadi Lushoto.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali izidishe juhudi kuongeza *patrol* katika maeneo hayo. Polisi wapewe nyenzo za kufanyia doria saa za usiku. Pia Polisi wanaohusishwa kushirikiana na majambazi waondolewe kazini mara moja. Wananchi wanawajua wanahofia kuwataja kwa kuogopa usalama wao. Kura za maoni kwa ajili ya kuwataja wahusika zinaweza kusaidia kuwapata wahusika. Kura hizo ni budi zifanyike kwa siri na wahusika wathibitishiwe usalama wao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, malipo ya haki stahili kwa Walimu ni muhimu sana hasa katika kipindi hiki tunapoelekea kwenye uchaguzi. Walimu ni kiungo muhimu sana kati ya Wabunge na Wapiga Kura. Serikali isipowapatia haki zao wakiendelea kunyanyasika, watajenga chuki kwa Serikali yao. Jambo hili ni nyeti, lipewe kipaumbele. Ziko fedha nyingi za kulipia madai ya Walimu na wafanyakazi wengine, lakini zinatumiwa vibaya katika Halmashauri za Manispaa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, wizi umekithiri katika Halmashauri, fedha za miradi zinateketea. Nashauri hatua mahsusi zichukuliwe. Ipo dhana ya kuhusisha matumizi mabaya ya fedha za miradi, hususan ya barabara za Halmashauri na watumishi wa Makao Makuu ya TAMISEMI. Suala hilo lichunguzwe kwa undani, wahusika wachukuliwe hatua, wakibainika. Wabunge wasikilizwe wanapowataja watumishi wakorofi.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri na yenye mwelekeo wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu kwa kazi nzuri aliyoifanya katika kipindi cha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kudumisha amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda sasa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Desemba, 2001, wananchi wa Nyamuma, Wilayani Serengeti, familia zipatazo 135 walichomewa nyumba kwa amri ya Mkuu wa Wilaya, Ndugu Thomas Ole Sabaya, akisaidiwa na *OCD* wa Wilaya ya Serengeti Ndugu Alexander Lyimo.

Mheshimiwa Spika, katika tukio hilo, jumla ya nyumba 540 zilichomwa moto, mali zote za wananchi hawa ziliporwa, mifugo yao ilipotea na vijana wapato wanne walipoteza maisha yao mara tu baada ya tukio hili. Vile vile kuna watu ambao hawajulikani walipo tangu tukio hili lilipotokea.

Mheshimiwa Spika, ingawa mimi kama mwakilishi wao, nilileta malalamiko katika vyombo vya Serikali, Wizara ya Mambo ya Ndani, TAMISEMI na Mkuu wa Mkoa wa Mara. Watuhumiwa walikana kabisa kuwa hamna nyumba zilizochomwa wala mali zilizopotea.

Mheshimiwa Spika, baada ya watuhumiwa kufikishwa mbele ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, walikiri mbele ya Tume kuwa walichoma nyumba za wananchi wa Nyamuma. Vile vile mbele ya Tume, walishindwa kueleza mali za wananchi hao walizipeleka wapi. Vile vile mbele ya Tume hiyo, wananchi walionyesha kipigo walichopata na kuna mama mmoja alipigwa na *OCD* hadi mimba yake kutoka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa watuhumiwa wamekiri mbele ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuwa walitenda makosa, naomba Serikali itoe maelezo ni hatua gani inatarajia kuzichukua dhidi ya watuhumiwa na ni hatua gani inatarajia kuchukua kuhakikisha kuwa wananchi wanalipwa mali zao zilizopotea na kuporwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba Serikali ichukue hatua za haraka za kuwapatia wananchi waliochomewa nyumba, mahali pa kuishi kwani hadi sasa wanatangatanga Mjini Mugumu. Naomba vigogo Serikalini wasiwalinde wahalifu hawa kwani watakuwa hawawatendei haki wananchi wa Serengeti.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa mategemeo kuwa Serikali italitilia maanani suala hili.

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na Mheshimiwa William Lukuvi, kwa kujitahidi kuendesha Wizara hii. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utalii. Utalii ni sekta ya pili ambayo inategemewa kuongeza Pato la Taifa. Ikiwa hivyo ndivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, mbona fedha iliyotengwa kwa Sekta ya Utalii ni ndogo ukilinganisha na jirani zetu?

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwako ni kwamba zitafutwe mbinu za kuwapatia fedha ili waweze kutangaza kwa nguvu vivutio vyetu vya ndani ya nchi. Pia zinahitajika fedha za kuelimisha wananchi wetu ili waweze kusaidia Usalama wa Watalii.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe binafsi pamoja na Tume ya Huduma za Bunge kwa kusimamia kuweza kuanza Ofisi ya Bunge Zanzibar. Hii ni hatua kubwa kwa Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar na pia itatuongezea heshima kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imetenga fedha za kutosha kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama hasa kwa wakati wa Uchaguzi. Ombi ni kwamba Mlandege tusaidiwe kupanua na kukiimarisha kituo chetu cha Polisi cha Mlandege.

Pili, kwa kuwa fujo za kisiasa zote huanzia Darajani na Vikokotoni kwenye Jimbo la Mlandege, naomba tujengewe Kituo cha Polisi eneo la Vikokotoni, sehemu kwa ajili ya ujenzi ipo tayari na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, anaielewa vizuri sehemu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa, tuitwe Mbunge mmoja mmoja atoe uzoefu na ushahidi kuhusu rushwa.

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wasaidizi wake wakuu, ikiwa ni pamoja na Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Wiliam Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na watendaji wakuu wa Ofisi yake, wanaojumuisha Katibu Mkuu, Bibi Rose Lugembe na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali, kwa kazi nzuri ya matayarisho ya hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo imeweka wazi hali ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2003/2004 na mpango wa mwaka 2004/2005. Yako mafanikio makubwa yanayoendelea kuwafikia wananchi katika sekta za huduma za kijamii na miundombinu. Mafanikio haya yanatokana na juhudi za Serikali na mwitikio wa wananchi katika kutekeleza Ilani makini ya sera za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuchangia maeneo mawili katika hotuba hii. Kwanza ni kuhusu sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi.

Kwanza naipongeza Serikali kwa kuleta sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Sera hii imetayarishwa kwa umakini mkubwa na mwelekeo wa kiutekelezaji. Mimi naitafsiri sera kama sera mama ya sera zote za kisékta. Sera inatoa mwongozo wa jinsi gani kila sekta kwa kutumia mfumo wa sera hii mama, sekta itatayarisha mpango wa utekelezaji wa kuwawezesha wananchi katika sekta husika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali sasa ihuishe sera za sekta zote na mwelekeo unaowiana na sera hii mama ya uwezeshaji ili sera hizo nazo zionyeshe wazi changamoto au hoja iliyopo au inayozungumziwa, tamko la sera kisékta, mikakati ya utekelezaji na programu za kutekeleza sera hiyo. Endapo sera za kisékta zitahuishwa ili ziweke wazi mpango na utekelezaji sekta mbalimbali zitatoa mchango dhahiri katika kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ubinafsishaji, naipongeza Serikali kwa kutekeleza sera ya ubinafsishaji kwa umakini mkubwa bila kutetereka pamoja na kelele nyingi za baadhi ya watu ambao wamesita kuelewa mtazamo na mwelekeo huu wa kunusuru mashirika ya umma kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naishauri Serikali ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kuwa mashirika nyeti bado yanabakia kwa njia moja au nyingine katika mkono wa Serikali, ili Serikali iweze kuyadhibiti hasa pale yanapoelekea kukwaza shughuli za kijamii na kiuchumi. Mfano ni Shirika la Reli, Bandari, Benki za Taifa ya Biashara, Mawasiliano yaani Simu na Posta na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifuatilie tatizo la mafao ya wafanyakazi wa mashamba ya mkonge yaliyobinafsishwa ambao mpaka leo bado hawajalipwa na Serikali haitoi kauli yoyote. Inasemekana kwa mashamba yaliyochukuliwa na *Katani Ltd.*, Serikali ilitoa fedha hizo kupitia *Katani Ltd.* Naomba kauli ya Serikali juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, vile vile yapo mashamba ya chai. Mfano Ambangulu, Dindira na Balangai, Wilayani Korogwe na Lushoto yanayomilikiwa na wafanyabiashara binafsi ambao wana malimbikizo ya mishahara kwa muda mrefu. Naomba Serikali ichukue hatua madhubuti ili wafanyakazi walipwe.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naungana na wenzangu kuwapa pole wale wote waliopata matatizo ya kufiwa, akiwemo Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda. Pia nampa pole Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa ajali walizopata.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri na yenye upembuzi wa kina. Napenda pia kumpongeza kwa utekelezaji na usimamizi mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa chakula, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi alivyoshughulikia tatizo la upungufu wa chakula. Kwa kweli Ofisi ya Waziri Mkuu hasa Waziri wa Nchi (Sera), Mheshimiwa William Lukuvi, alitembelea kila mahali na kuhakikisha kwamba wananchi wenye upungufu wa chakula wanapatiwa msaada. Nawapongeza pia Wakuu wa Mikoa na Wilaya zilizokubwa na upungufu huo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali sasa iainishe Kaya zenye upungufu wa chakula kila mwaka hasa kaya zinazoongozwa na wanawake, watoto na wazee ili kuweza kuweka mikakati ya kuwasaidia kupata pembejeo ili kuhakikisha wanajitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Huduma za Jamii, napongeza kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Elimu na Utamaduni chini ya mpango wa MEM na sasa mpango wa MMES unaotegemea kuanza mwezi Julai. Napongeza kupunguza ada za Shule za Sekondari, lakini bado kuna kero kwa watoto yatima ambao wanatakiwa kuchangia michango ya majengo na michango mingine iliyowekwa na shule. Kibaya zaidi, Walimu Wakuu wanangoja wakati wa kufanya mitihani ndipo wanawafukuza kuleta michango hiyo. Hii tabia siyo nzuri. Naomba Walimu Wakuu wapewe mwongozo kuhusu kunyanyasa watoto hawa na michango hii yote iondolewe. Serikali igharamie kwa watoto yatima na ambao wazazi hawana uwezo.

Mheshimiwa Spika, ni wakati mwafaka sasa kuhakikisha wasichana waliopata mimba au walioacha shule kwa sababu yoyote, wapewe nafasi ya kujiendeleza hata kama ni nje ya mfumo wa kawaida wa Serikali. Serikali ishirikiane na Taasisi zisizokuwa za Serikali kufanikisha suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapambano dhidi ya UKIMWI. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jitihada na ujasiri mkubwa wa kushughulikia tatizo hili. Napongeza kazi nzuri inayofanywa na *TACAIDS* pamoja na Taasisi mbalimbali, yakiwemo mashirika ya Dini, *NGOs* na *CBOs* mbalimbali, hii ni pamoja na *TAPAC* kwa kuonyesha utashi wa kisiasa barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, elimu ya UKIMWI bado inahitajika vijijini. Elimu itasaidia kupunguza unyanyapaa na kujali wagonjwa, watoto yatima na familia zilizoathirika. Kama elimu ya UKIMWI haitaendelea kutolewa, wananchi hawatakuwa tayari kujitokeza kupimwa na hatimaye kuingia kwenye mpango wa kupewa dawa hasa kwa wale wanaohitaji. Suala kwamba elimu kwa njia ya semina, sasa basi, siyo sahihi kuwepo. Semina zinatakiwa kwenda ngazi za chini vijijini na zifikie makundi yote kama ya wanawake, vijana, wazazi, viongozi wa dini na makundi mengine muhimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.



**MHE: AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Frederick Sumaye, kwa hotuba yake nzuri na ya kusisimua ambayo ilitoa tathmini vizuri kwa kipindi kilichopita na kuweka bayana malengo ya kipindi kinachokuja na namna yatakavyotekelezwa. Hotuba hii ni ya hali ya juu na yenye kuwatia moyo Watanzania wote. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukumbushia suala la kutoa ruzuku ya mbolea kwa mikoa yote hasa tukizingatia kwamba Tanzania ni nchi ya kilimo.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kuwapa pole wale wote waliopata misiba kwa kufiwa na mzee wao na wale waliopata ajali wakati wanakuja Dodoma kwa shughuli zao za Kibunge.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze mchango wangu katika suala zima la Daftari la Uchaguzi kwa Tanzania Bara. Kutayarisha Daftari la Wapiga Kura ni jambo linalogharimu mabilioni ya fedha. Kwa hiyo, ni jambo la busara sana pawepo na matayarisho ya kutosha pamoja na kuwashirikisha wadau wote kama vile viongozi wa vyama na kuwaelimisha wananchi ili wote wapate haki ya kujiandikisha muda utakapowadia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushirikishwa wadau wote, lazima utekelezaji wa matayarisho ya Daftari hili kwa wazi kabisa ili kupunguza manung'uniko ambayo yanaweza kuleta matokeo yasiyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la vyombo vya ulinzi kuongezewa fedha katika Bajeti ya 2004/2005, mimi binafsi nimefarijika sana kwa hili maana askari wetu wanaishi na kufanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini hofu yangu isije ikaonekana kwamba nia njema ya kuongeza fedha kwa vyombo hivi, ikageuka kuboresha zogo na vurugu wakati wa Uchaguzi Mkuu ujao mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, ni jambo lisilofichika kwamba uchumi wa Zanzibar ni duni sana. Hii ni kutokana na pato lake ni dogo sana kutokana na kuanguka kwa sekta ya biashara. Inakadiriwa kwamba mara hii katika Bajeti ya Zanzibar kuna upungufu wa zaidi ya 4%.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ipo haja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuliona hili na kuweza kusaidia kunusuru hiyo hali.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuchangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera), Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Habari na Siasa), pamoja na Katibu

Mkuu, Bibi Rose Lugembe na Watendaji wake wote kwenye kuandaa hotuba na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Wote nawapa hongera.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwenye Bajeti nzima ya nchi, imefurahisha kutambuliwa kwa mara nyingine tena umuhimu wa sekta ya kilimo. Kutambua huko ni kukiri kabisa umaskini halisi wa nchi yetu. Kazi moja ya Serikali ni kutoa ajira kwa wananchi wake. Lakini kukiri huko kwa kutoa 80% ya ajira kwenye sekta ya kilimo kwa watu wake, ni kuelekeza uzito wa sera ya nchi ya kupunguza umaskini ifikapo mwaka 2025 pamoja na utekelezaji wa *millennium goals*. Hapa ndipo pawe mahali pa kuanzia kwenye kurekebisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na *2025 vision* kama nilivyosema hapo awali, ni shida tu inayoifanya nchi hii iwe na 80% ya watu wake waajiriwe na sekta ya kilimo. Hivyo basi, Serikali ina jukumu la kuhakikisha ina mikakati ya kupunguza tegemezi ya ajira ya watu wake kwenye sekta ya kilimo. Nchi zote zilizoendelea kiuchumi, ajira ya watu wake iko kwenye takriban 2%. Hivyo Tanzania itakuwa inajidanganya kabisa eti ikifikiria kuungana kwenye *Global Village* na kutekeleza *millennium gloals* kwa ushindani fasaha. Pamoja na mikakati ya kuboresha sekta zingine zenye kuchangia Pato la Taifa, mikakati mahsusi iwe ni kupunguza ajira kwenye sekta ya kilimo ili watu waajiriwe kwenye sekta zingine.

Mheshimiwa Spika, hilo halitawezekana bila kupanua na kuendeleza kiteknolojia kilimo (*large scale farming modernized*) na kuwapa wakulima wa sasa nyenzo za zana na pembejeo na huduma zingine za ugavi (*machinery, farm inputs and extension services*).

Mheshimiwa Spika, hatua hizi nilizotaja ni muhimu. Ingewezekana basi ongezeko la Pato la Taifa, tija kutoka sekta zote, mafanikio ya tija, kipato kikubwa kielekezwe kwenye sekta ya kilimo. Baada ya mafanikio na kufanikisha miundombinu, hasa barabara, hakuna sababu ya kupuuzia kilimo tena. Sekta zingine ziendelezwe pia kwa kasi ndogo ukilinganisha na kazi inayo/itakayo amuliwa kwenye sekta ya kilimo. Nina imani mchango wa sekta ya kilimo kwenye Pato la Taifa, utakapofikia angalau 70%, basi Bajeti yetu itakuwa tegemezi tu kwa kukopa na siyo kwa kutegemea misaada.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia picha ya Bajeti yetu ya mwaka 2004/2005, ni kama ifuatavyo takriban kwa haraka:-

	Asilimia
(a) Misaada ya <i>HIPC</i> Trilioni 1.3	39
(b) Mapato ya ndani Trilioni 1.6	48
(c) Mikopo Trilioni 0.4	14
<i>Total Budget</i> Trilioni 3.3	100

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, kwa sababu mchango wa Pato la Taifa kutoka sekta ya kilimo ni 45% mapato ya ndani, mchango wa sekta ya kilimo ni takriban unatarajiwa kuwa shilingi trilioni 0.700/= . Hivyo basi, tutakapofikisha mchango kwenye kiwango cha kati ya 60% hadi 70% kama mchango wa sekta ya kilimo, shida

itakayobakia kwenye Bajeti ni kuongezea Bajeti ya nchi kwa kukopa kwenye Taasisi za fedha za ndani na nje. Hapo angalau tutakuwa na mantiki ya kuungana na wenzetu duniani, angalau kwenye utandawazi, *the global village*.

Baada ya kusema hilo, naomba niunge mkono na hotuba ya Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri Mkuu, hususan kwenye hoja zote kwenye ibara 36, 37, 38, 39, 40 na 41. Ni muhimu sana kabla ya kuwezesha *large scale farming*, kuwawezesha wakulima (*peasants*) wadogo wadogo kupitia SACCOS kama ilivyoainishwa kwenye ibara ya 39.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, wananchi wetu kiufupi wapatiwe na wawezeshwe mapema iwezekanavyo kwa matrekta, pembejeo, huduma za ugavi na kilimo cha umwagiliaji.

Pia wawezeshwe hivi vigezo kwa kupitia taasisi zetu za fedha kwa kupitia SACCOS kwa mategemeo ya kupanua kilimo.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanyika jimboni kwangu Kilombero, inaonyesha kuwa mkulima anayeweza kulima ekari moja ya mahindi, kipato chake kwa mwaka ni shilingi 210,417/= tu. Kipato hiki ni kidogo kukidhi mahitaji ya mwananchi, lakini ifikapo kuwawezesha kulima ekari 10, basi angalau atakuwa na pato lisilopungua la shilingi milioni 2 kwa mwaka. Kwa kifupi, takwimu ni kama zifuatazo:-

*Total yield per hectore, 3500 kg., Net farm income shillings 252,500*  
*Average Farm gate price shillings 130/=*  
*Gross output per hectare shillings 455,000*  
*Monthly income per hectare shillings 21,042/=*

<i>Variable costs</i>	
<i>Seed and chemicals</i>	<i>shillings 20,000</i>
<i>Fertilizers (urea, TSP)</i>	<i>“ 70,000</i>
<i>Total valuable cost</i>	<i>“ 90,000</i>
<i>Labour costs/machinery</i>	
<i>Ploughing</i>	<i>“ 25,000</i>
<i>Harrowing</i>	<i>“ 20,000</i>
<i>Planting</i>	<i>“ 17,500</i>
<i>Herbicide application</i>	<i>“ 17,000</i>
<i>Weeding</i>	<i>“ 20,000</i>
<i>Transport</i>	<i>“ 12,000</i>
<i>TOTAL</i>	<i>“ 112,500</i>

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya yote, naomba kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu moja kwa moja. Ahsante.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, mimi napenda nichangie sehemu tatu katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nikianzia la kwanza, napenda kuimbusha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa sisi ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa inakuwaje au kuna mantiki gani ya kuwa tujengewa Ofisi na Ofisi ya Waziri Kiongozi? Waziri Kiongozi anatumia fungu gani la kutujengea Ofisi sisi? Ana ubavu huo? Kwanza asingewajengea hao Wawakilishi wake.

Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali itujengee Ofisi kama wenzetu. Iache kutupiga chenga kwa kutupeleka kwa Waziri Kiongozi. Sisi fungu letu liko Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu kuhamia Dodoma. Kuhusu kuhamia Dodoma siyo mbaya, lakini hivi ndiyo tuko tayari kweli kweli? Mbona mimi sioni kuwa tayari na kuhamia? Hebu kwanza tujenge nyumba za wafanyakazi pamoja na Maofisa, ndiyo tuanze kutaka kuhamia. Lakini hivi sasa sioni tutahamia wapi.

Tatu, ni kuhusu chaguzi za mwaka 2004/2005. Ningependa kuziomba Serikali zote mbili sikivu kuwa zitutayarishie uchaguzi ambao utakuwa wa huru na haki.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, alipotuhutubia hapa Bungeni, alisema anakerwa na udhaifu wa Vyama vya Upinzani. Kwa hiyo, tunamwomba aweke chaguzi zilizo huru na haki na sisi tunamwahidi kuwa udhaifu huu utaondoka.

Mheshimiwa Spika, tunaziomba Serikali zisiingilie kwenye chaguzi hizo na mara baada ya uchaguzi tu, matokeo yatolewe, yasicheleweshwe, kwani kuna tabia ya wagombea wengine wakishashindwa, hawakubali na wanakwenda kuitishia Tume ya Uchaguzi. Nayo Tume kwa vile hawajiamini, huwa wanakubali kuvuruga matokeo. Ninayo mifano mingi, nitataja miwili.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995, haukuwa na sababu ya kukaa siku tano, ila ni baada ya mgombea wa CCM kuona kashindwa na kupika matokeo.

Pili, uchaguzi wa mwaka 2000, baada ya wagombea wa CCM kuona wameshashindwa, waliikoromea Tume ya Uchaguzi na kukubali kuvuruga matokeo yote ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. Kwa vile Serikali za CCM ni sikivu kama ninavyosema, basi itutayarishie uchaguzi mzuri na wakubali matokeo wanaposhindwa.

Mheshimiwa Spika, hii ni nchi yetu sote. Zile kauli za kuwa fulani hatawali nchi hii, ziondoke. Nchi hii haiwezi kutawaliwa na vyama viwili au Serikali haitolewi kwa vikaratasi vya kura. Haya yote ni maneno yanayosemwa na watu wa Chama Tawala na yanaashiria uvunjwaji wa amani, lakini Serikali zote mbili ziko kimya.

Mheshimiwa Spika, mimi namwomba Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa vile mwakani anategemea kustaafu na tayari amejitokea historia nzuri, kwa hiyo, ajitahidi. Chaguzi hizi ziwe nzuri, huru na za haki ili akabidhi madaraka kwa walioshinda bila kigugumizi, ili asichafue historia yake nzuri ambayo ameshajiwekea.

Kwa hiyo, isichafuliwe na watu ambao hawapendi kukabidhi madaraka baada ya kushindwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda nizungumzie kuhusu Muungano. Wabunge wengi wa kutoka Unguja wanapochangia kuhusu Muungano huwa wanasema kuwa kuna maadui wa Muungano. Hao maadui wa Muungano ni nani katika nchi hii? Maana sisi *CUF* ndiyo tunaonekana hatupendi Muungano, jambo ambalo siyo kweli. Sisi tunaupenda Muungano, isipokuwa tu tunataka uboreshwe zaidi. Sisi *CUF* tuna mtandao mkubwa wa Chama Tanzania nzima. Kwa hiyo, hatuna haja ya kuvunja Muungano wetu na tunataka kukiendeleza chama chetu. Ahsante.

**MHE. ADELASTELA E. MKILINDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pole kwa Waheshimiwa waliopata matatizo wakati wakiwa safarini kuja Dodoma na pia nitoe pole nyingi kwa familia ya Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mpendwa.

Mheshimiwa Spika, pia nitoe pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa katika nyadhifa mbalimbali za Kitaifa. Zaidi nimpongeze Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuleta sifa kwa nchi yetu, kwa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ina upungufu na wote wanaochangia wanabainisha haya. Inapotokea Mbunge kutoa mawazo yake na Mbunge mwingine kuona mawazo yale hayafai, siyo jukumu la Mbunge aonaye hayafai kusema kwamba Mbunge amesema hivi na hivi na siyo sahihi, si kweli, ni unafiki na kadhalika. Tabia hii ni ukosefu wa nidhamu na uvunjaji wa maadili yetu kwamba hotuba inayochangiwa na iliyo mezani na siyo maoni ya Mbunge mwingine yeyote. Mbali na hivyo, yatakuwepo malumbano ya kisiasa. Je, unafiki uko wapi kwa yule anayeunga mkono na huku analaumu au anayelaumu au kukosoa na kutounga mkono?

Mheshimiwa Spika, nathubutu kusema kuwa hotuba hii ina aina ya maneno yanayotia matumaini, lakini ukweli ni kwamba hakuna hata ukweli wa kuaminika. Mfano, ameeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa hali ya chakula ni nzuri. Hivi hali ya chakula ni nzuri wapi? Hivi hatutasikia misaada ya chakula ikihitajika ndani ya mikoa yetu? Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha, naamini haina chakula cha kutosha. Wawekezaji katika kilimo mbona hakuna? Kiko wapi kilimo cha umwagiliaji? Chakula kitatoshelezaje bila hayo?

Mheshimiwa Spika, rushwa ni ugonjwa ambao CCM imeshindwa kuutibu. Wapo watu wasomi wanaofanya tafiti na kuishauri Serikali kuhusu nini kifanyike juu ya suala la kuondoa rushwa nchini. Lakini Serikali hii haifanyi lolote isipokuwa kukanusha kwamba rushwa haipo na zaidi kutaka ushahidi. Je, kitabu kinachoeleza kuhusu rushwa na uchaguzi wa mwaka 2000, kiko wapi? Uchaguzi uliohusisha vyama vingi ulitawaliwa na rushwa mwaka 2000 na watu wengi walilalamika hadi watafiti hao toka Chuo Kikuu wamawezeshwa na *PCB* kufanya utafiti na walipoibuka na kijitabu hicho, haieleweki kimeigusa nini Serikali hadi kutoruhusu Watanzania kukiona. Naomba Wabunge

tupatiwe nakala ya kitabu hicho kabla hatujamaliza kipindi hiki cha Bunge mwezi wa nane. Kitabu kinaitwa *Multi- Party Elections Corruption in Tanzania*.

Mheshimiwa Spika, Dr. Sinda na Prince Bagenda, wanakifahamu sana kitabu hiki na wameshiriki. Naomba Watanzania pia wakione. Ahsante sana.

**MHE. SALAMA KHAMIS ISLAM:** Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri na watendaji wote wa Ofisi yake.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichangie hoja kuhusu kilimo. Nchi yetu ni nchi nzuri, yenye hali ya hewa nzuri na yenye rutuba. Tatizo kubwa ni kwamba wananchi wetu wanasumbuliwa na zana za kisasa za kilimo, mbolea hawapati kwa wakati na vile vile kukosa maji kwa sehemu zenye ukame. Ni vyema Serikali ikaandaa mpango wa kilimo cha umwagiliaji ili wananchi waweze kupata mavuno mengi na ya uhakika.

La pili, nchi yetu ni nchi ya amani na watu wake wanaishi kwa hali ya usalama. Raia wanaotoka nchi za jirani wanakuja nchini kwetu na kufanya vitendo vya uhalifu na kurudi nchini kwao. Raia hawa huja nchini kwa njia isiyo halali. Naomba sana Serikali idumishe ulinzi zaidi sehemu za mipakani na visiwani pia. Lingine ni kwamba Serikali izingatie kuona ipo haja ya raia wa nchi nyingine kuweza kupatiwa vitambulisho vya uraia.

La tatu, ni kuhusu Utalii. Utalii ni chanzo cha Pato la Taifa. Naomba sana Serikali iitangaze nchi yetu kwenye masuala ya utalii. Tunazo sehemu nyingi za kuweza kutembelewa na watalii, wanyamapori, maeneo ya *Eastern Mountain Arc*, Mapango ya Kilwa, Njombe, Bagamoyo na Kondo. Vile vile tunazo fukwe nzuri zenye mandhari nzuri. Serikali ishawishi wawekezaji waje wawekeze hasa kwenye sehemu za fukwe ili tuweze kupata pato kwa Serikali na wananchi wapate sehemu za kupumzikia.

Mheshimiwa Spika, la nne ni pongezi kwa Serikali kupunguza kodi na nyingine kuzifuta kabisa. Lakini kuna kodi ambazo bado ni kero kwa wananchi na wanalalamika. Kuna kodi wanatozwa wananchi wenye nyumba, ambazo wanazikodisha nyumba ikiwa kodi yake inafikia shilingi 500,000/= na zaidi. Inabidi mwenye nyumba atozwe 15% ya kodi anayoipata katika nyumba ile.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali ifikirie upya suala hili kwa sababu kuna baadhi ya wananchi wanajenga nyumba hizo kwa taabu sana. Inabidi afanye biashara ndogo ndogo au kapata fedha zake za kuacha kazi. Ipo kodi ya majengo, kodi ya ardhi. Naomba sana Serikali iwaonee huruma wananchi hawa ambao wanaotegemea kupata pesa kutokana na kodi ya nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa kupata nafasi hii kuchangia. Kabla ya yote, naunga mkono hoja 100%.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri yenye maono, Mheshimiwa Frederick Sumaye, akisaidiana na Mawaziri wake, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na Mheshimiwa William Lukuvi. Vile vile, pongezi kwa Watendaji wote chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Bibi Rose Lugembe.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nachangia kifupi kama ifuatavyo kuhusu Taasisi ya Utangazaji Tanzania (*TUT*), naipongeza Serikali kwa kujitahidi ili wananchi wengi waweze kupata taarifa muhimu nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuendeleza TVT iweze kuonekana nchi nzima, ukizingatia ni *Television* pekee ya Taifa kati ya vituo vyote vilivyopo nchini. Ushauri ni kwamba, kwa vile TVT huonekana hasa katika baadhi ya maeneo mengi mpaka vijinini, ni vyema matangazo ya TVT yaanze mapema, kwa mfano, asubuhi badala ya mchana saa nane, ili waweze kuwa na *coverage* nzuri kama wanavyofanya *ITV*, *Channel Ten*, *Star TV* na kadhalika.

Pia TVT inayo *bank* kubwa na habari za matukio yaliyopita kihistora tangu tunapata Uhuru hadi miaka ya 1970 na kuendelea. Kwa nini hazina hii inaonyeshwa kwa uchache wakati watu wengi wanakuwa bado hawajarudi makazini?

Mheshimiwa Spika, nashauri wapange programu zao ili wananchi wengi waweze kuona tulikotoka na tulipofika na hii itasaidia kuionyesha Serikali yetu juhudi zake za kuwahudumia wananchi tangu enzi za uhuru. Hii itasaidia kuwaelimisha wananchi na kutilia mkazo utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Spika, kuhusu UKIMWI, naipongeza Serikali kwa jinsi inavyopiga vita janga la UKIMWI kwa juhudi zote Kitaifa na Kimatiafa. Tatizo kubwa sasa si uelewa wa wananchi kuhusu suala la UKIMWI, tatizo ni jinsi ya kutumia *resources* hasa kuwafikia ngazi za vijijini. Usimamizi bado hairidhishi katika baadhi ya Halmashauri na hakuna ushirikishwaji wa wananchi, hivyo kuwepo na matumizi mabaya.

Mheshimiwa Spika, idadi ya waathirika na yatima ni kubwa. Bado dawa hazijawafikia vijijini, pamoja na ughali wa dawa za kurefusha maisha, tunaiomba Serikali iwe makini sana katika upatikanaji wa dawa hizi kwa walengwa. Vinginevyo, jitihada kubwa inayofanya na kutenga fedha nyingi, watafaidika wachache wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Rushwa. Serikali inajitahidi sana katika suala hili. Rushwa nyingi inayozungumziwa hapa ni kule katika sehemu za kupatia huduma muhimu za wananchi. Visingizio ni hali ngumu ya watoa huduma. Tunashukuru kuwepo na mtandao wa *PCB* mpaka Wilayani. Bado kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kuwafichua wahalifu, badala ya Watendaji wa Ofisi za *PCB* Wilayani kuwa tishio kwa wananchi, hivyo kukosa ushirikiano.

Kuhusu ukame na upungufu wa chakula, kama tunavyofahamu, hali ya chakula haikuwa ya kuridhisha kutokana na ukame katika kipindi cha mwaka 2003/2004.

Serikali imejitahidi kuwapatia chakula wananchi kutoka hifadhi ya chakula ya Taifa. Lakini kulikuwa na mapungufu mengi katika ugawaji wa chakula kutoka ngazi za Wilaya kwenda kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, malalamiko mengi ni dhahiri yameifikia Serikali. Hatuombi njaa tena itokee, lakini pale kwenye malalamiko yaliyojitokeza, kama chakula cha njaa kupewa baadhi ya wafanyabiashara na wao kusimamia uuzaji wa chakula na kusababisha kuuza chakula kwa bei kubwa badala ya ile ya shilingi 50/= kwa kilo. Hivyo, pale kwenye malalamiko, Serikali kupitia Halmashauri, iwachukulie hatua watendaji ili kuisafisha Serikali yetu na vile vile kupunguza malalamiko ambayo yanaleta doa katika Chama chetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho pamoja na mengi yaliyozungumzwa, ni vema yakatekelezwa kwa kadri ya uwezo. Tatizo siyo *budget*. Tatizo ni watendaji wasio waaminifu. Serikali inao uwezo na inawafahamu kutokana na taarifa mbalimbali zinazowafikia. *It can be done, play your part.*

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sikupata fursa ya kuchangia kwa kauli na kwa kuwa naenda safari uliyonituma, naomba uniruhusu nichangie hoja hii nzito kwa maandishi kwa urefu zaidi ya kurasa mbili.

Mheshimiwa Spika, ningependa awali ya yote kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wake wa Nchi, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa hotuba hii nzuri sana na kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia hoja iliyopo mezani, naomba uniruhusu nitoe pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba wa kufiwa na baba yao mzazi. Naomba pia kumpa pole Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na binti yake. Naomba Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi na awape subira wafiwa. Naomba pia uniruhusu kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge wote waliopata ajali na kuvamiwa na majambazi walipokuwa safarini kuja Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nyadhifa mbalimbali hivi karibuni, pongezi maalum zikiwa kwa Mheshimiwa Balozzi Getrude Mongella na Mheshimiwa Danhi Makanga kwa ushindi mkubwa waliopata wao binafsi na heshima kubwa iliyopata CCM. Zaidi ya yote, ni jambo la furaha na faraja kubwa kufahamu kwamba Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa amepata afueni kutokana na operesheni aliyopata na yuko njiani kurudi nyumbani. Ninamwombea Mwenyezi Mungu ampe nguvu na uwezo zaidi wa kuliongoza Taifa letu.



Mheshimiwa Spika, nikirejea hoja, nafarijika sana kwa hotuba nzuri sana, fasaha, inayotoa muhtasari wa mafanikio yaliyopatikana na miongozo thabiti katika jitihada za Serikali ya awamu ya tatu katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, uboreshaji wa huduma za jamii na kupambana na umaskini kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 na Dira ya Taifa ya mwaka 2025. Ni hotuba inayotoa msisimko na matumaini mapya kwa wote wanaoitakia kheri Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana na yanayotarajiwa katika sekta mbalimbali za huduma za jamii, huduma za uchumi, sekta za uzalishaji na ukuaji wa uchumi kwa jumla ni makubwa. Anayesema kwamba CCM haijafanya lolote ama anadhamiria kupotosha kwa makusudi au yuko katika usingizi mzito na ndogo kubwa. Hivi wapotoshaji hao hawaoni maendeleo makubwa ya miundombinu, majengo na huduma mbalimbali zikiwemo elimu, afya, maji, barabara, mawasiliano, uchukuzi na sekta za uzalishaji kama vile kilimo, viwanda, madini, maliasili, utalii, ushirika na huduma za Taasisi za fedha na nyinginezo, achilia mbali takwimu na ripoti mbalimbali zinazothibitisha ukweli huo? Hatua hizo za maendeleo zimewekewa uzito zaidi na sera mpya za uwezeshaji na maafa. Ninaipongeza sana Serikali kwa haya.

Mheshimiwa Spika, maendeleo yote hayo yanatokana na sera nzuri za CCM pamoja na umakini na umahiri katika kuandaa mikakati na mipango thabiti ya utekelezaji wa sera na mipango hiyo, pamoja na ushirikishi wa kiwango cha juu wa wananchi katika ngazi zote za upangaji na utekelezaji. Mafanikio haya pia yanatokana na uimarishaji wa utawala bora, demokrasia, mshikamano wa Kitaifa, ulinzi, usalama na amani. Kwa sehemu kubwa, mafanikio haya yametokana na uongozi bora wa Viongozi Wakuu wa Kitaifa akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Msaidizi Mkuu wa Mheshimiwa Rais katika kuongeza na kuratibu shughuli za kila siku za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu siku zote amekuwa mstari wa mbele, tokea apewe dhamana ya kuongoza Serikali kwa wadhifa alio nao, Mheshimiwa Frederick Sumaye siku zote amekuwa katika mstari wa mbele katika kuhamasisha na kuhakikisha kwamba mafanikio na maendeleo zaidi yanapatikana kwa mujibu wa sera, mipango na ubunifu unaoambatana na sera na mipango iliyopo.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mkinga lilibahatika kutembelewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi wengine wakiwemo Mawaziri na Manaibu Waziri katika mwaka wa fedha wa 2003/2004. Katika ziara yake Jimboni Mkinga, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipata taarifa na kujionea hali halisi ya Jimbo hilo na Wilaya ya Muheza kwa jumla, wakati akizindua Kituo cha Afya cha Mkinga.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mkinga linaloanzia baharini na kuishia katika Milima ya Usambara Mashariki, lina hali zote za hewa na pia lina miti mingi na raslimali nyingine nyingi yakiwemo madini. Hivyo, Jimbo la Mkinga limebahatika kuwa na uwezo wa kuzalisha aina nyingi za mazao na bidhaa mbalimbali. Bahati mbaya, wananchi na wawekezaji hawawezi kutumia nafasi hizi nzuri zilizopo kutokana na mapungufu mengi. Pamoja na mafanikio mengi yaliyopatikana, bado yapo mengi yanayostahili kuendelezwa takriban katika sekta zote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu, Afya, Maji, Mawasiliano, Umeme na Barabara, bado zipo kero nyingi kuhusu majengo, vitendea kazi na watumishi. Wananchi wa Mkinga wanashukuru sana kwa ujenzi wa madaraja saba katika barabara ya Tanga - Horohoro. Hata hivyo, ni matarajio yao kwamba madaraja matatu yaliyosalia yatajengwa na barabara hiyo kuu na muhimu kujengwa kwa kiwango cha lami haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kilimo, Ufugaji, Uvuvi, Misitu, Nyuki, Wanyamapori, Madini, Viwanda na Ushirika, bado kuna udhaifu mkubwa wa huduma za ugani, mafunzo, taarifa za masoko na upatikanaji masoko. Nafarijika kwamba hotuba ya Waziri Mkuu imebainisha haya pamoja na hatua za ufumbuzi. Ni matumaini yangu kwamba Jimbo la Mkinga lililo pembezoni litapewa kipaumbele maalum katika kuondoa kero hizi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa 100%. Ahsante.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, suala la Muungano wa Tanzania ni nyeti sana. Serikali yenyewe ina sehemu kubwa ya ama kuimarisha au kudhoofisha Muungano huu na ili kuimarisha Muungano huu, ni lazima Serikali kuondoa kero zote za Muungano.

Moja ya kero kubwa ni kutoshirikishwa kwa Wazanzibari katika masuala mengi ya nchi hii na pili, ni suala la mapato (*TRA*) kwa Serikali ya Zanzibar. Utaratibu ulipo wa ukusanyaji mapato haukidhi haja na hivyo kuiacha Zanzibar katika hali ya umaskini wa kutupwa. Utaratibu wa Rais wa Zanzibar kutokuwa Makamu wa Rais ni tatizo kubwa na kasoro kubwa ya Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli za uchaguzi. Uchaguzi huru na wa haki hufanywa na kusimamiwa na Serikali iliyopo madarakani. Hivyo, ni wajibu wa Serikali iliyopo kuhakikisha kuwa chaguzi zote za nchi hii zinakuwa huru na za haki. Mfano hai wa hoja yangu ni uchaguzi mdogo wa majimbo 15 Pemba, uliofanyika Mei, 2003. Serikali kupitia vyombo vyake vya dola, vilisimamia kwa uadilifu mkubwa uchaguzi huo na ukaenda salama kabisa. Hivyo, tunatoa wito maalum kwa Tume ya Uchaguzi ya Taifa na ile ya Zanzibar kwa upande mmoja na vyombo vya dola kwa upande mwingine kusimamia kwa haki na uadilifu wa hali ya juu uchaguzi wa Vitongoji/Vijiji kwa mwaka 2004 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 ili nchi yetu isijekuingia katika vurugu za wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchaguzi ndani ya Bunge, utaratibu wa sasa wa chaguzi mbalimbali ndani ya Bunge si wa kidemokrasia. Nashauri kwa nafasi za Zanzibar, basi ni vyema Wabunge wa Zanzibar wakapewa nafasi ya kuchagua mwakilishi wao. Vivyo hivyo kwa nafasi za wanawake, ni vyema wakaachiwa wanawake wenyewe wachague mwakilishi wao. Hali kadhalika Kambi ya Upinzani, iachiwe wapinzani wachague atakayewawakilisha. Hili likitendeka, litapanua wigo wa demokrasia nchini kuliko utaratibu ulipo sasa wa Bunge zima kuwapigia kura wagombewa wa nafasi zote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ulipuaji wa mabomu Zanzibar. Siku chache zilizopita, kulitokea mtafaruku wa ulipuaji mabomu kule Zanzibar na mara nyingi matukio kama haya yanapotokea, hushukiwa Vyama vya Upinzani hasa CUF kuwa wanahusika kwa namna moja ama nyingine na Serikali hadi leo haijatoa taarifa rasmi ya matukio hayo. Tunaiomba Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, itoe taarifa rasmi ya nani alihusika na ulipuaji ule na hatua gani zimechukuliwa kwa waliohusika?

Mheshimiwa Spika, kuhusu matukio ya maafa, inasikitisha sana kuona kwamba hadi leo Serikali imeshindwa kuwapa kifuta machozi wale wote walioathirika katika maandamano ya Januari 26 hadi 27, 2001 licha ya kuwa tulikubaliana katika muafaka kuwa wote walioathirika katika maandamano hayo wangepewa hicho kifuta machozi si zaidi ya tarehe 30 Desemba, 2002. Tunaiomba Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kutoa tamko rasmi humu Bungeni kuhusu hatma ya walioathirika katika maandamano ya mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, kuhusu baadhi ya vikao vya Kamati kufanyika Zanzibar. Kwa kuwa Bunge hili ni la Muungano wa nchi mbili yaani Tanganyika na Zanzibar, ni vyema kufanya shughuli za Kimuungano. Niliuliza humu Bungeni juu ya utaratibu wa baadhi ya vikao vya Kamati za Bunge kufanyika kule Zanzibar. Waziri alijibu kuwa hili linazungumzika. Lakini bado hadi leo hatujaona utekelezaji wake. Tunaomba Ofisi ya Waziri Mkuu itupe maelezo kwa nini suala hili linaonekana ni kikwazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya TVT, pamoja na huduma nzuri za TVT, bado sehemu kadhaa Kisiwani Pemba, TVT haionekani. Tunaomba Serikali iboreshe mitambo ya TVT ili na sisi tulioko Pemba tuweze kufaidi huduma hii muhimu ya habari.

Mheshimiwa Spika, tunasikitika sana juu ya utendaji kazi wa *ITV*. Mara zote *ITV* huwa haonyeshi Msemaji wa Upinzani, tunaomba suala hili lirekebishwe.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nasikitika kwa kukosa nafasi ya kuchangia kwa mdomo ili walionichagua wanisikie. Napenda kuchangia hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bado kilimo kinazungumziwa tu. Nina wasiwasi hata mwaka 2004, mambo yatakuwa kama miaka iliyopita. Nashauri kwamba wakulima wana uwezo wa kupata mikopo kwenye Benki na hata hivyo Benki itakayoanzishwa itawashughulikia hawa tu na siyo wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji *Affirmative Loans* kwa wakulima wadogo. Nchi kama Namibia, wanayo mifuko kama hiyo. Hata *Pride Tanzania Ltd.*, inaweza kutumika kama chombo cha kuwafikia hao wakulima kutokana na mtandao wake mkubwa na *experience* waliyapata kushughulikia mikopo midogo ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu, wakati umefika sasa wa kutumia *experience* tuliopata katika miradi ya UPE, MEM na sasa MMES, kufikiria sasa *Universal Secondary Education*. Tuachane kabisa na mambo ya Shule za Msingi. Hatuwezi

kukabiliana na utandawazi tukiwa na elimu duni. Pia *English* iwe sasa lugha ya kufundishia. Tusibabaishane na mijadala ya ubinafsi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya walimu, ni ukiukwaji wa Katiba kutowalipa walimu mishahara yao kwa visingizio mbalimbali. Walimu wanafunzi wamekuwa wanafanyakazi toka Januari, 2004 na hadi sasa hawajalipwa mishahara yao yaani 80% ya mishahara wa Mwalimu wa Daraja la IIIA. Hivi huu ni ubinadamu kweli? Wanaohusika wachukuliwe hatua. Hapa Bungeni tunashangazwa na majibu ya Mawaziri, wanatupiana mpira. Wizara tatu, Wizara ya Elimu na Utamaduni wanasema TAMISEMI na TAMISEMI wanasema Utumishi.

Mheshimiwa Spika, walimu wanadai jumla ya shilingi bilioni 12, lakini Serikali imetenga shilingi bilioni 9 tu kwa madeni sugu yote. Hii ina maana kwamba walimu wajitegemee kabisa. Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe tamko kuhusu madeni haya ya Walimu.

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waairi Mkuu - Frederick Sumaye, Mawaziri wa Nchi, Mheshimiwa William Lukuvi na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Katibu Mkuu na wataalam wake wote kwa umahiri wao mkubwa katika kuandaa na kuwasilisha hotuba nzuri. *Really it is open, clear and comprehensive budget.*

Mheshimiwa Spika, ukame unaoendelea kuikumba Tanzania unasababishwa na mambo mengi, lakini baadhi ya hayo ni wimbi la ukataji miti hovyoyote na utaratibu. Miti mingi inatoweka kwa lengo la uchomaji wa mkaa, lakini baya zaidi na cha kushangaza ni kwamba wakati uharibifu huu ukitekelezwa, watendaji wa kijiji wanashuhudia na hawakemei. Watendaji wa Kata wanashuhudia, Wakuu wa Wilaya na Watendaji wao wanashuhudia na hawakei. Je, tabia ya kulindana itatufikisha wapi? Hii ni hatari na kuna uwezekano wa kukosa mvua zaidi Tanzania na kukaribisha jangwa katika maeneo kadhaa kama jitihada za makusudi hazikuchuliwa na Serikali kuweza kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini baya zaidi ni ile tabia mbaya iliyojitokeza ya ukataji wa miti katika vyanzo vya maji. Hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, kama chakula tulichovuna hakitatumika vizuri, basi ni dhahiri kwamba njaa haitamalizika.

Mheshimiwa Spika, kumezuka tabia ya kutumia chakula hicho kwa kutengeneza pombe ya kienyeji na baya zaidi ni kule kuzuka kwa tabia ya uuzaji wa chakula hicho kwa wafanyabiashara bila kuzingatia uwekaji wa akiba kwa wakulima wenyewe. Hivyo, ninaiomba Serikali kwa kushirikiana na ngazi za watendaji wa vijiji, kutoa taaluma kwa wakulima juu ya matumizi bora ya chakula.

Mheshimiwa Spika, UKIMWI bado ni janga la Kitaifa na pamoja na jihitihada za Serikali za kupambana na janga hili kwa njia mbalimbali, bado idadi ya wanaoathirika

inaongezeka siku hadi siku. Sasa ni vyema tukafanya utafiti kwa nini waathirika wanaongezeka.

Mheshimiwa Spika, *TACAIDS* inafanya kazi nzuri juu ya kutoa elimu juu ya janga hili. Lakini uchunguzi wa kina ambao watumiaji wa kondomu wamechunguza kwamba kondomu hizo ni hafifu, si madhubuti na mara nyingine huchanika/kupasuka wakati tendo la ngono linapoendelea. Hivyo, Serikali iangalie upya juu ya kuhakikisha kondomu zinazotolewa ziwe madhubuti zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali imedhamiria kwa dhati kupambana na UKIMWI, basi ni vyema kwa namna ya pekee ikarekebisha mienendo ya mavazi ya akina mama, ambayo mavazi hayo yanachochea ngono na hatimaye UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, mashindano ya urembo katika maeneo kadhaa yanaonyesha dalili za wazi kwamba mavazi yao warembo hao ni kinyume na maadili ya Watanzania. Ni nusu uchi, na Serikali ikalifahamu hii, lakini hawakemei. Hii ni tabia iliyozeleka kwa wasichana wengi kujiingiza kwenye mashindano ya warembo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ikaangalia upya namna ya kuendeleza mashindano ya warembo. Ni vyema tuangalie mila, silka, desturi na utamaduni kwa jumla wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ya kuendeleza kuwapatia dawa za kurefusha maisha ni jambo zuri, lakini ni vyema waathirika hao baada ya hali zao za viwiliwili kuboreka, ni vyema wapewe taaluma ya kutoambukiza wengine. Kwani kuna wasiwasi kwa waathirika hao kuendelea kutesa baada ya kujisikia afya zao ziko nzuri.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba waathirika hawa baada ya kupatiwa dawa za kurefusha maisha, wapangiwe mikakati maalum wa kudhibitiwa. Vinginevyo, faraja hii itapelekea vilio na vifo zaidi. Hatutawanyanyapaa, lakini na wao wasiambukize wengine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTH M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza hotuba hii na ninaiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, pamoja na maeneo ya kilimo kutengwa, naishauri Serikali sasa ibadili mtazamo wa kilimo na iendelee na uwekezaji.

Pia itenge maeneo iwape sasa wanawake, wapewe nyenzo kama trekta, mbegu, mahema, usafiri, fedha za kujikimu na kadhalika kama ilivyogawa maeneo na nyenzo kwa vijana wa Dar es Salaam kule Gezaule na wakashindwa. Nina hakika hapa tunaweza kupiga hatua na pia dawa za kutunzia chakula ziongezwe.

Kuhusu njaa, sasa chakula kimepatikana kwa baadhi ya mikoa hapa nchini. Naishauri Serikali itoe fedha za kutosha, ikusanye chakula kwa wingi kwa bei nafuu kuliko kungojea kuagiza nje ya nchi na kwa bei kubwa.

Kuhusu mikoa ya chakula, ipigwe marufuku kwa wenye tabia ya kupika pombe na viongozi wa Serikali ya Kijiji na Chama wawajibike.

Kuhusu trekta, nashauri Serikali inunue trekta, iwagawie Magereza ili irudie hali yake ya zamani ya uzalishaji chakula ambao ulisaidia sana Kitaifa. Pia nashauri Halmashauri zishauriwe kununua matrekta kwa ajili ya kuwakodisha wananchi kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zishauriwe, ziwe na mashamba ya chakula na wafanyakazi wao wawe na urahisi wa kupata chakula na mashamba pia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gonjwa la UKIMWI, nashauri Serikali izidi kusaidia kupiga marufuku picha ambazo zinakiuka utamaduni wa Mtanzania. Hata muziki unaoonyesha watu nusu uchi, wanatuharibia maadili ya watoto wetu. Ifanyike kama kwa kipindi cha *Passion*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyombo vya habari. *RTD*, inasikitisha kuona mtumishi wa miaka mingi ametumikia Taifa hadi akawa Kaimu wa *RTD*, leo anahamishiwa Wizara nyingine kwa ajili ya uonevu (wivu), kijicho cha mtu bila kujali utumishi wa mtu au kwa kuwa alikuwa mwanamke? Mbona mwanaume alikaimu miaka mingi, hakuondolewa hadi siku ya kustaafu kwake? Uonevu huu utaisha lini? Naomba jibu wakati unapotoa hoja tafadhali.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana leo tunazungumza wazi, tunaonekana kwa wapiga kura wetu. Ndani ya Bunge, hawaonyeshwi watu walioko nyuma upande wa Upinzani. Ila upande wa Mawaziri na Wabunge, wanaonekana wote hadi nyuma. Je, sisi Wabunge wa wa nyuma upande wa Upinzani hatuna wapiga kura wala familia, ambao wangependa kutuona tumo Bungeni? Waongeze teknolojia yao zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano kwa Mawaziri na Wabunge, mawaziri wana simu, lakini simu zao hazipatikani. Kila unapopiga hupati. Tunaomba Serikali iwaongeze dola ili wawe wazi kwa Wabunge wenzao kuwasiliana nao. Wengine ukienda kwao huwapati bila simu, inakuwa shida kuwasiliana na baadhi yao. Wengine wazuri sana, wako radhi hata kama wamepumzika, wako radhi kuinua na kukusikiliza. Tunaomba utusaidie hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabenki, kwa kuwa wanawake wanahitaji kujiendeleza kuondoa umaskini, tunaomba Serikali iongeze sauti juu ya riba, bado kubwa sana. Naomba tusaidiwe.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa fursa hii adimu ya kuchangia hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Awali ya yote,

napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake iliyojaa mantiki na dira ya maendeleo ya nchi yetu. Serikali yetu imefanya mengi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba kuishauri Serikali katika mambo yafuatayo:-

Kwa kuwa Serikali ilibuni programu maalum ya kusambaza umeme kwa kuanzia kwenye Makao Makuu ya kila Wilaya, Ofisi ya Waziri Mkuu isimamie vizuri mpango ambao kwa sasa hivi Wizara husika imeanza kutekeleza bila kuonyesha ratibu ya utekelezaji. Inashauriwa Wizara inayohusika ingetoa ratiba na vigezo vya vipaumbele vinavyotumika hivi sasa kuliko utekelezaji wa siri iliyopo sasa ambao inategemeana tu mahusiano yaliyopo kati ya Wizara na Wilaya husika.

Aidha, kutokana na kutokuwepo na uwazi katika ratiba ya utekelezaji, baadhi ya Wilaya zinajisikia kusahuliwa. Kuna ubaya gani licha ya ukosefu wa fedha uliopo, Wizara hiyo ikatueleza orodha kamili ya mpango wa utekelezaji ili kufahamu mpangilio wa Wilaya kama zilivyopangwa, ikiwemo na Wilaya ya Ludewa. Wilaya gani inaanza, ipi itafuata, uwazi na ukweli.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo kubwa la wakulima wetu kuendeleza kilimo ni mtaji katika uzalishaji wa mazao, kwa nini Serikali kwa makusudi ikatenga fedha kwa ajili ya kuanzisha na ku-*support* Vyama vya Akiba na Mikopo vijijini ili wakulima waweze kupata mikopo ya uzalishaji?

Aidha, Serikali ingeweza kuchangia *initial capital* kwa Vyama vya Ushirika vinavyoonyesha mwelekeo mzuri licha ya utaratibu wa sasa wa *Export Credit Guarantee Scheme* ambayo huvifanya vyama viendeleo kujiendesha kwa kutegemea, mikopo dumu daima.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine la mkulima ni bei duni za mazao wanayozalisha, haziwezi kurudisha hata gharama ya uzalishaji. Hivyo, kufanya mkulima kukata tamaa na umaskini kuongezeka. Je, haiwezekani kuanzisha mfuko wa kufidia wakulima pale bei ya mazao yao inapoporomoka kadi kufikia chini ya gharama ya uzalishaji wa mazao hayo?

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, na mimi ninawapa pole wale wote waliofiwa na wale waliopata matatizo mbalimbali, na waliokufa Mungu azilaze pema roho zao. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naipongeza hotuba hii kwa dhati jinsi ilivyo nzuri. Mchango wangu nianze kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni uti wa mgongo katika nchi yetu. Kwa hiyo, tuwape elimu wananchi wetu, tuwape pembejeo mapema ili tuweze kulima kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, wanawake walio wengi wameshahamasika na vikundi vya ushirika. Kwa hiyo, Serikali sasa iwape mikopo ya matrekta ili waweze kujikwamua na umaskini, kwani ukimwondoa mwanamke kwenye umaskini, basi familia hiyo itaondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, sasa elimu ni muhimu sana. Mimi naishauri Serikali iangalie sana zile Wilaya ambazo hazina sekondari za kutosha na watoto wanafaulu vizuri toka Shule ya Msingi kwenda Sekondari na wanabakia majumbani eti hawana madarasa ya kusomea. Hii ni unyonge kwa wale watoto wanaofuatia nyuma kuvunjika moyo wa elimu. Kwa hiyo, Serikali isaidie hizo Wilaya ambazo zina upungufu wa sekondari.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza hotuba hii sana kwa kuona umuhimu wa wanawake na kuwatengea fedha zaidi za mikopo ili wajikwamue na umaskini. Kwa hayo machache, ninaiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mia kwa mia.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kikatiba Waziri Mkuu ndiye msimamizi mkuu wa shughuli zote za Serikali, kuna mpango gani wa ujenzi wa barabara kutoka Nzega - Tabora - Mbeya, Manyoni - Kigoma, Ipole - Mpanda?

Pia kuna utaratibu gani wa kumtumia Mhakiki Mali Mkuu wa Serikali kukagua mali ya Halmashauri?

Kuna mpango gani wa ujenzi wa *Mwanza Airport* hasa *Cargo, Terminal* na egesho la Ndege na fedha kiasi gani zimetengwa?

Napongeza juhudi za Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kujenga malambo na suala la maji kutoka Ziwa Victoria, lengo ni kwenda Kahama na Shinyanga. Naomba lengo liwe hadi Mkoa wa Tabora, hususan Nzega.

Mheshimiwa Waziri Mkuu uliambia Bunge utahamishia Ofisi yako Chimwaga. Je, ni fedha kiasi gani zilizotumika na tayari umeshahamia?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mrabaha katika hotuba ya Waziri wa Fedha, alisema anakusudia *cess* badala ya mrabaha na akadiriki kusema alikosea. Mimi naamini Serikali haikukosea. Hata alipoelezea badala ya mrabaha iwe *cess* ni sahihi. Madini yote kuanzia sasa yalipwe *cess*. Kufuta siyo ufumbuzi. Je, wale waliokula fedha za wananchi Geita wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Fedha za Walimu, malalamiko ya malipo ya Walimu kuanzia mwaka 2001/2002 hadi Desemba, 2003 yamefikia :-

- Walimu TAMISEMI 13,041,961,860/=
- Walimu Wizara ya Elimu na Utamaduni 4,063,804,096/=

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii Serikali inatenga shilingi bilioni 9 tu kwa watumishi wote.



(a) Je, hizo fedha zilizotumwa kwenye Halmashauri ya Wilaya (OC) zimekwenda wapi?

(b) Ni mipango gani imewekwa kuhakikisha deni hili lote limelipwa kabla ya 2005?

(c) Hatua gani zitachukuliwa na wewe kuwaadhibu waliozitemia vibaya fedha hizo? Kuna danadana za kusumbuliwa Walimu hawa hasa Wizara za Elimu, Utumishi na TAMISEMI. Walimu walipwe mara moja.

**MHE TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, nachangia moja kutokana na hotuba ya Bajeti iliyosomwa na Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha, nalo ni kuhusu ongezeko la kodi katika *soft drinks* na hasa soda.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia vinywaji vyote vikali kama bia, *wine*, *whisky* ni vya ndani na kutoka nje ya nchi, vimewekwa kodi ya 5%. La ajabu, soda ambayo ni kinywaji cha mtu wa kawaida na hata kule vijijini, imepandishwa hadi kufikia 6.7%. Naomba Serikali iwafikirie wananchi wa chini, ikiwezekana bia, *wine* na *whisky* ndizo zipandishwe kodi au soda ishushwe kodi ili vinywaji vyote iwe 5%.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia vinywaji vyenye kilevi (*alcohol*), kwa namna fulani vina madhara kwa jamii, tofauti na soda ambayo haina madhara yoyote kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. SHAIKU AHMADA AMEIR:** Mheshimiwa Spika na mimi nitaungana na wenzangu kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wake wawili wanaohusika na Sera na Habari. Hotuba hii ni nzuri na italeti mafanikio makubwa kwa mwaka wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, sasa nachukua nafasi ya kukupongeza wewe kwa jinsi kazi za Bunge letu unavyozifanya. Uzoefu wako wa siku nyingi pamoja na elimu yako, unakufanya ufanye kazi bila kutetereka na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, pia tuko zaidi ya Wabunge mia mbili humu Bungeni, lakini kila Mbunge unamtendea haki na unatuongoza kwa usawa kabisa bila ya kutumia dini, uzawa wala ukabila. Sisi sote kwako ni sawa.

Mheshimiwa Spika, pia tunakupongeza kwa kusimamia majengo ya Ofisi Ndogo huko Dar es Salaam na Zanzibar. Ukakamavu wako ndiyo uliosababisha kujengwa Ofisi

hizi. Kwetu Wabunge kutoka Zanzibar tunaona utakuwa umefungua ukurasa mpya wa maendeleo Visiwani. Sifa nyingi zitakumiminikia kutoka kwa Wazanzibari.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa matajiri wenye kuagiza bidhaa mbalimbali toka nje wameacha kuteremsha mizigo yao kupitia Bandari ya Zanzibar kutokana na kuwa kiwango kimoja cha ushuru kwa bandari zote za Tanzania. Kitendo hichi kimesababisha mapato kupungua kwa Serikali ya Zanzibar. Hivyo basi, tunaomba suala hili lizungumzwe na Serikali zote mbili au hali ya Zanzibar itazidi kuwa mbaya.

Mheshimiwa Spika tunampongeza Rais Benjamin William Mkapa kwa kuanzisha mradi wa *TASAF*. Mradi huu umeenea nchi nzima. Hivi sasa mradi huu umeenea katika mikoa yote mitano Zanzibar. Maendeleo makubwa ya kupigia mfano yamepatikana, lakini hivi sasa pesa za awamu hii zimemalizika na kwa hivyo baadhi ya miradi imesimama kwa kungojea pesa wa kukwamulia miradi hiyo. Tunaomba wahusika wa *TASAF*, suala hili walishughulikie ili kuliendeleza suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uharibifu wa mazingira ni jambo linalotaka uenezi wa taaluma ya uhifadhi wa mazingira pamoja na usimamizi kwa kushirikisha wadau. Mazingira yanaharibika hasa kwa kukata kuni na uchomaji mkaa. Sote tunajua kuwa hakuna nishati mbadala isipokuwa mkaa, maana ndiyo nishati ya bei nafuu. Ili kuzuia kupungua kukatwa kwa kuni, basi nishati ya umeme ipunguzwe bei.

Mheshimiwa Spika, pia uchomaji wa misitu husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na husababisha vifo kwa viumbe wengi. Kwa ujumla uharibifu wa mazingira husababisha uharibifu wa vyanzo vya maji na hatimaye sehemu hizo kupata ukame.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuwakumbuka ndugu zetu walioathirika kwa UKIMWI kwa kuwapatia dawa za kupunguza makali ya maradhi hayo. Kitendo hichi kinastahili kupongezwa sana. Waathirika wengi watapata matumaini na wataishukuru Serikali yao kwa kitendo hiki. Tunaomba wasimamizi wa watendaji wa shughuli hii ya tiba, waifanye kwa umakini na uadilifu.

Mheshimiwa Spika, mwisho na mimi naiunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kupata nafasi ya kuchangia machache katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Pili, nampongeza sana kwa hotuba yake, nzuri sana, imejaa busara na hekima nyingi, imejumlisha na kugusa pembe zote kwa maendeleo ya nchi yetu. Nionavyo mimi, imekamilika na ina sifa zote. Kwa maana hiyo, nampongeza sana yeye binafsi, Mawaziri wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba uniruhusu nichangie maeneo machache yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya kisiasa. Ninakipongeza Chama cha CCM na Serikali zake kwa busara zake na kukomaa kisiasa kwa kuiweka nchi yetu katika hali ya salama, amani na utulivu kwa zaidi ya miaka arobaini hivi sasa. Watanzania wanafurahia amani hii na utulivu uliopo, kwani naamini kwamba katika karne hii hakuna Chama zaidi ya CCM kinachoweza kuweka amani na utulivu kama huu tulioupata kwa wakati wote huu.

Mheshimiwa Spika, nakipongeza Chama cha CCM na Serikali zake kwa juhudi hizo na kuziomba zikamate bidii hiyo hiyo na kupata ushindi mkuu zaidi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2005. Mimi ninaamini kabisa uwezo huo wa ushindi upo.

Mheshimiwa Spika, utitiri wa Vyama vya Siasa, umekuwa mkubwa mno. Ninakubali kwamba tunakuza demokrasia. Lakini hakuna fursa isiyo na mipaka. Vyama vingine havina lengo jema, kazi yake ni kuongeza vurugu na kusababisha chusha za kisiasa zisizo na maana.

Vyama havina hata sera na vinapokwenda kuomba kura kwa wananchi vinakosa hata Udiwani, matokeo yake vinatoa maneno ovyo na pengine kusababisha kuvunja amani katika baadhi ya maeneo. Naomba sana suala hili iliangaliwe vizuri na kuna haja ya kufikiriwa tena.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Daftari la Wapiga kura, naipongeza Serikali kwa matayarisho ya Daftari hilo, limedaiwa na Wapinzani. Lakini kwa busara za Chama cha CCM na Serikali zake zimekubali na Daftari litakuwepo. Kwa hiyo, ninavieleza Vyama vya Upinzani, vikubali matokeo vikishindwa vikubali na vishirikiane na Chama Tawala pamoja na Serikali zake katika kujenga na kustawisha maendeleo ya Taifa letu. Waache *sabotage* na majungu mengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya Ulinzi na Usalama, naunga mkono juu ya taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba hali ya Ulinzi na Usalama ni nzuri. Nafikiri hali ya amani na utulivu katika nchi yetu na mipaka yake yote ni nzuri, amani inapatikana. Lakini kazi kubwa sasa ni kupambana na majambazi. Naomba sana, umefika wakati wa kupanga nguvu zetu na kupambana na majambazi ambao wanatumia silaha. Nashauri zipangwe operesheni maalum.

Mheshimiwa Spika, mwisho nampongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kutuletea ushindi mkuu kwa CCM na sasa kuwa ni Mbunge wa CCM.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naunga mkono hotuba na Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi nikupongeze wewe mwenyewe binafsi kwa kipaji ulicho nacho cha kuongeza vikao hivi vya Bunge kwa umakini na ufanisi mzuri. Hongera.

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wake wote wawili, pamoja na wataalam wao wote kwa kuwasilisha kwa umakini Bajeti yao ya mwaka 2004 kwa kuainisha kwa uwazi nia na dhamiri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya kuwaondolea shida Watanzania ambao ndio wapiga kura kwa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004 nchi yetu ilikumbwa na uhaba wa chakula kutokana na ukame ulioikumba nchi yetu ambalo hilo ni jambo la wazi kwa watu wote. Lakini la kufikiria zaidi, hilo tayari limeshachukuliwa hatua za dharura na kwa bahati nzuri tumefanikiwa. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, hilo tayari limemalizika, jambo la kujiuliza ni kwamba je, huko tunakoendelea, nchi yetu imejitayarisha vipi kuanzisha kilimo cha umwagiliaji, ambacho hakiangalii msimu ila kinaangalia namna gani mazao yatapata maji ili yaweze kukua?

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali ya ulinzi na usalama wa nchi yetu, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuweka bayana hatua zote za Serikali za kupambana na aina zote zinazoweza kusababisha uvunjaji wa amani katika nchi hii. Serikali itatumia nguvu zake zote kuhakikisha inayazima yale yote ambayo yanaweza kuhatarisha usalama wa raia wake.

Mheshimiwa Spika, suala la kupambana na maradhi hasa UKIMWI ni vyema Wizara husika kwa kushirikiana na wananchi, wazidi kutoa elimu na kueleza kwa uwazi zaidi kuhusu UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, hali ya rushwa katika nchi yetu hivi sasa imekuwa midomoni mwa wananchi wote kutokana na kazi inayoongezeka siku hadi siku kwa kasi kubwa. Ningeiomba Serikali pamoja na juhudi zake zote iongeze makali katika kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, napenda kutamka wazi kwamba naunga mkono hoja hii kwa 100%. Ahsante.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kusimamia shughuli za Serikali kwa ufanisi mzuri. Aidha, nawapongeza wafuatao Waziri wa Nchi, Sera, Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, Habari na Siasa, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bibi Rose Lugembe na wataalam na Watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, hawa wote ninawapongeza kwa mambo yafuatayo:-

Kwa kutoa ushauri mzuri na kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika usimamizi na uendeshaji vizuri wa shughuli zote za Serikali kwa kipindi cha 2003/2004.

Kwa kutengeneza hotuba nzuri yenye kuonyesha bayana mafanikio ya Serikali katika utekelezaji wa Sera za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imeuthibitishia umma wa Tanzania kwamba Chama cha Mapinduzi kupitia Serikali yake, kinatekeleza sera zake kwa vitendo na siyo porojo kama wanavyodai baadhi ya Wapinzani. Mafanikio haya yanaonekana wazi hususan katika sekta ya elimu, afya, ujenzi, miundombinu na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba suala la rushwa limepungua na siyo kubwa kama linavyozungumziwa. Viashirio vya kupungua kwa rushwa ni kuongezeka kwa makusanyo ya kodi na Bodi ya TRA. Kwa hili, ningependa kumpongeza Waziri wa Fedha na Mamlaka ya TRA na ajira ya Walimu wa Daraja la A mwaka huu. Zoezi hili limefanyika bila manung'uniko. Pia ugawaji wa chakula cha njaa, kwa kiwango kikubwa mgao huu umezingatia sana mwongozo na taratibu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni uboreshwaji wa huduma za mawasiliano hapa Tanzania. Kwa kiwango kikubwa Watanzania wanawasiliana kwa urahisi sana. Juhudi hizi ziendele kwenye maeneo ambayo bado hayajafikiwa. Pamoja na mafanikio yote, kuna maeneo machache ambayo ningependa kuyatolea maoni kwa nia ya kuboresha. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya Ulinzi na Usalama. Kumekuwepo na matukio ya ujambazi hapa na pale. Ningependa kushauri kwamba mfumo wa kuwastaafisha wanajeshi na maaskari polisi vijana uangaliwe upya. Hawa kwa sababu wanazo nguvu na mbinu za kupanga matukio yasiyo mazuri, basi wanaweza wakawa tishio kwa usalama kwa mali za raia. Wengi wao wanastaafu kwa kipato kidogo sana. Hawa waangaliwe vizuri. Naomba Serikali iangalie namna ya kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ya Askari polisi, hususan Ofisi za Polisi Mkoa wa Morogoro. Hata mahabusu yao ni kama pango la panya. Hata vitendea kazi kama karatasi hazipo. Sasa hawa watafanya kazi kwa raha gani? Lingine ni jinsi askari wa Jeshi la Wananchi wanavyochukua sheria mkononi na kuwaadhibu raia wasio na hatia pale wanapokwaruzana na raia. Ninaomba tabia hii ikomeshwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala bora, kuna Mahakimu wachache hususan wale wa Mahakama ya Mwanzo wanaowanyanyasa raia kwa mtindo ambao unaashiria mazingira ya rushwa. Kama inawezekana, je, Hakimku akasikiliza kesi na kutoa maamuzi/hukumu siku ya Jumamosi bila kuwepo mlalamikiwa? Hii kada ya Mahakimu bado ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukame na upungufu wa chakula. Naomba kusema kwa sauti kubwa kwamba Mkoa wa Morogoro unao uwezo wa kulima chakula cha kutosha kwa nchi nzima. Tunaomba kuwezesha kiteknolojia na kwa upatikanaji wa pembejeo kama walivyofanyiwa wenzetu wa Nyanda za Juu Kusini. Aidha, tunaomba daraja katika Mto Kilombero ili Wilaya ya Ulanga iweze kufikiwa kwa urahisi na usalama. Ulanga kuna chakula kingi, lakini matatizo usafiri.

Kuhusu sekta ya nishati pamoja na matukio makubwa katika sekta ya madini, ningependa kutoa rai moja nayo ni ile ya kutokuwepo na uthibiti wa uchimbaji hovyoy wa madini. Kwa mfano, hivi karibuni katika eneo la Bwawa la Mindu Morogoro, wachimbaji wadogo wamevamia na kusababisha uharibifu mkubwa sana katika eneo hili ambalo ndiyo chanzo pekee kwa Manispaa ya Morogoro. Mkuu wetu wa Mkoa na Wilaya, wanatumia nguvu zao zote kudhibiti hali hii, lakini bado wachimbaji wanarudi kuendelea na shughuli zao, *despite the fact* kwamba kuna walinzi (Polisi) katika eneo hilo. Athari za vitendo hivi ni kubwa sana. Bwawa sasa limechafuka na kujaa mchanga pamoja na uchafu wa zebaki. Hali hii isipodhibitiwa, hali ya upatikanaji wa maji katika Manispaa ya Morogoro tayari upo mashakani.

Pia napenda kuiomba Serikali iangalie uwezekano wa kutoa elimu ya mazingira, UKIMWI, umuhimu wa kutunza mazingira katika maeneo ya machimbo, umuhimu wa kuanzisha Vyama vya Kuweka na Kukopa kama njia ya kujiwekea mitaji endelevu. Kuhusu UKIMWI, ni faraja kubwa kwa Serikali, imeonyesha kujali kulinda na kuboresha afya ya waathirika wa janga la UKIMWI kwa kuanza maandalizi ya upatikanaji wa dawa za kuboresha afya ya waathirika wa UKIMWI. Naomba yafuatayo, pamoja na upatikanaji wa *ARVs*, Serikali iangalie upatikanaji wa tiba ya magonjwa nyemelezi ambayo ndiyo yanayosababisha kifo kwa ugonjwa wa UKIMWI. Magonjwa hayo ni malaria, homa ya matumbo, vichomi, *diagnosis ya TB (X-ray, kupima makohozi)*, vifanyike bure.

Mheshimiwa Spika, lische inachangia kwa asilimia zaidi ya 80 kwa wagonjwa. Wengi wao wanayo matatizo ya utapiamlo. Naomba sambamba na *ARVs*, Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia hawa wagonjwa chakula cha kutosha au mlo ulio kamili. Wengi wao hawana nguvu ya kujitafutia chakula kwa ajili ya udhaifu. Shughuli hii ya kuwapa waathirika, ninashauri apewe Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa William Lukuvi, kwani uzoefu wa kugawa chakula anao tena sana. Hizi dawa zisiwafaidi watu wa Mijini tu. Ikiwezekana hizi dawa zipelekwe hadi vijijini kwenye Vituo vya Afya. Zaidi nashauri kwamba upatikanaji uwe endelevu kwani kila anayeanza kutumia *ARVs*, ijulikane kwamba ni tiba ya maisha. Ningependa kushauri kwamba Serikali iangalie *NGOs* zinazotoa *counseling* na *home based care* kwa wagonjwa wa UKIMWI, kwani wanao uzoefu mkubwa sana wa kutoa tiba na huduma nyingine muhimu kwa wagonjwa UKIMWI. Kuhusu huduma kwa yatima. Ni faraja kubwa sana kuona jinsi ambavyo Serikali inasaidia kuchangia elimu ya watoto yatima. Lakini tatizo ni mahitaji mengine muhimu kama nguo, *pocket money*, madaftari, matibabu na ada za mitihani. Naomba haya yaangaliwe.

Mheshimiwa Spika, sekta ya elimu imeonyesha mafanikio makubwa hususan Elimu ya Msingi. Lakini tatizo ni vijana wengi wanaishia Darasa la Saba, wengi wao ni watoto bado. Ningependa kuishauri Serikali iangalie namna ya kuhamasisha wananchi kuanzisha Shule za Ufundi wa *TASAF*. Mpango huu utasaidia sana kuwawezesha hawa vijana kujiajiri wenyewe pamoja na kusaidia maendeleo ya vijiji katika sekta nyingi.

Kuhusu ubinafsishaji, mpango huu umekwenda vizuri, ila kwetu Morogoro kuna kiwanda cha viatu ambacho kilibinafsishwa mapema sana. Lakini baada ya muda mfupi,

kiwanda kiliungua na mwekezaji akaingia katika biashara ya mahoteli. Cha kusikitisha ni kuona uharibifu mkubwa wa kiwanda hiki ambacho kilikuwa kikubwa kuliko viwanda vyote vya viatu Afrika - *South of the Sahara*. Je, hatima ya kiwanda hiki ni nini? Aidha, ningependa *SIDO* ipeleke huduma zake vijijini kama njia pekee ya kuinua kipato cha wananchi wa vijijini na pia kupunguza wimbi la vijana kuhama vijijini kwena Mijini. Nampongeza tena Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri na kwa Ofisi yake kuwa mfano mzuri wa *Team work* katika kutekeleza sera za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia na nakutakia afya njema.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha asubuhi kinaishia hapo, tutakaporejea saa 11.00 jioni watoa hoja wataanza kujibu mambo yaliyozungumzwa hapa ndani kwa mpangilio kwamba Mawaziri wawili wa Nchi wataanza kwanza wao, halafu ndiyo atakuja mtoa hoja mwenyewe, halafu tutaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima ya kupitia kifungu kupitisha kifungu kimoja kimoja. Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Dua.

**WABUNGE FULANI:** *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kikao kilichoanza asubuhi kinaendelea. Namwita Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, mwenye dhamana ya Habari na Siasa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa dua yako jioni hii. Umenisaidia nafikiri mambo yatakuwa mazuri hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi napenda nichangie hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ameitoa tokea Jumatatu na leo kufikia sehemu ya mwisho, kwanza ningependa niseme kwamba tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, tunaposikia pongezi nyingi sana kwa Waziri Mkuu wetu, sisi wasaidizi wake tunafarijika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana Mbunge mmoja alisema kwamba kuna Mawaziri wawili wa miamvuli wamekwama juu ya mbuyu. Nikafikiri mimi na mwenzangu, hapana sisi tuko *fit*. Kwa hiyo, nashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa shukrani kwa *boss* wetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia maeneo mawili makubwa, kwanza ni eneo la Habari ambayo inahusiana na *Television*, Redio, Magazeti na vyombo vya Habari kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, waliochangia hoja hii ni Waheshimiwa tisa, nao ni Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la *Television* kulikuwa na maelezo kwamba kuwepo na mkakati maalumu wa kumaliza jengo lile pale la Makao Makuu ya TVT ambalo lilikuwa *Audio Visual Institute (AVI)* na tumesikia na tutajitahidi kuharakisha kulimaliza kadri ya uwezo wa fedha utakavyopatikana. Suala la pili, limezungumzwa kwamba wangependa waone kwamba *Television* yetu ya Taifa na Redio Tanzania inafika nchi nzima ili tuweze kushindana na watu binafsi na pia tufanye wajibu wetu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuenea redio na *Television* nchini, tunajibu kwamba mpaka sasa hivi tunatarajia kwamba katika muda mfupi kiasi cha Mikoa 18 itaona *Television* ya Taifa katika kipindi kijacho. Kwa sasa hivi inaonekana Mikoa ya Unguja na Pemba ni Mikoa mitano na Dar es Salaam, Pwani, Dodoma, Arusha na Mwanza. Kuanzia mwezi ujao vitajengwa vituo vingine nane ambavyo ni vya Lindi ambacho kitahudumia Lindi na Mtwara, Tabora, Mbeya, Musoma, Tanga, Kigoma na Bukoba. Nataraji katika muda mfupi tutaweza kuzima kiu ya wananchi wetu kuwafikia huduma hii muhimu katika Mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na hoja ya kwamba Mkandarasi aliyejenga TVT bado hakuwasilisha vifaa katika mtambo ule. Lakini sasa nina taarifa kwamba Mkandarasi huyu ametekeleza wajibu wake na sasa vipo katika Makao Makuu ya TVT. Kwa hiyo, ugomvi naye kwa suala hilo haupo.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na hoja kwamba Mkandarasi huyu hakusajili kwenye Bodi ya Wakandarasi kwa mujibu wa Sheria. Jambo hili pia liko Mahakamani, kwa sababu Bodi hii imewashitaki. Tungeomba sisi Wabunge tuachie Mahakama ifuate mkondo wake ili iende kwa mujibu wa Sheria na Katiba yetu.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na hoja kwamba ukarabati ufanyike kwenye Redio Tanzania (*RTD*). Hilo tumesikia na katika Bajeti ya mwaka huu mtaona mle kwamba kuna fedha maalumu zimetengwa kwenye ukarabati Redio Tanzania, Dar es Salaam. Lngine katika eneo hili kuna kilio kikubwa kwamba wanataka wananchi wa Tanzania, Redio yetu ya Tanzania hasa wakati wa Taarifa ya Habari itumie lugha kwa uangalifu na fasaha kwani iwe mfano kwa redio nyingine na nchi nyingine za nje. Hili tumelisikia na tumewaeleza Wahariri wetu kwamba wajitahidi sana kuboresha uwezo wao ili waweze kutoa habari hizi kwa kutumia Kiswahili fasaha na sanifu, tutajitahidi sana, tusiwe kama Msemaji wa Upinzani hapa aliboronga boronga



hapa akasema, tujione kama mbuzi kwenye gunia sijui, wakamvisha kaptura ya jela. Maneno mithili akaandika mithiri yaani vurugu tupu.

Mheshimiwa Spika, tutajitahidi, sisi kama Serikali, tutarekebisha hali hiyo. Kulikuwa na hoja nyingine ya maslahi ya wafanya kazi wa *RTD* yaboreshwe na kwa mujibu wa muundo mpya. Sasa hivi wa Redio Tanzania na *Television* ya Taifa. Maslahi ya wafanyakazi wa Redio Tanzania yameboreshwa sana na kwamba tutawapa *arreas* zao wafanyakazi wa Redio Tanzania za mwezi wa Aprili, Mei na Juni. Huu ni ushahidi kwamba Serikali imejitahidi kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Lakini haitoshi, lakini itakuwa hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kwamba tuwaondolee kodi wamiliki wa vyombo vya habari hasa magezeti, ni jambo zuri. Lakini kwa hali yetu sasa hivi tunafikiri kwamba kuna maeneo muhimu zaidi ya kuondoa kodi hasa kwa sababu watu wenyewe pia wanafanyakazi ya kibiashara. Kwa hiyo, kwa sasa hivi tungeomba Waheshimiwa Wabunge mtuachie tupate fedha hizi zisaidie maeneo mengine ya kuondoa umaskini, kwenye hospitali, afya, shule na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na hoja kwamba ushauri kwamba wamiliki wa vyombo vya habari wajitahidi kipindi hiki cha uchaguzi, mwaka 2004 na mwaka 2005 basi wasiwe na upendeleo kwa wanasiasa maalumu.

Mimi nafikiri wamesikia na sisi kama wamiliki au wadhibiti wa vyombo hivi tutaelekeza wamiliki wa vyombo vya habari, Redio na *Television* watende haki na uadilifu kwenye kazi zao. Mimi naamini kwamba wanaelewa kwa sababu Sera yetu ya Habari imeelekeza hivyo kwamba wafanye kazi kwa uadilifu na haki na usawa. Hayo nafikiri wamesikia na sisi tutasimamia kama wasimamizi wakubwa wa eneo hili.

Mheshimiwa Spika, lingine ni upande wa Siasa. Eneo hili limechangiwa pia Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Kamati ya Bunge ya Sheria, Katiba na Utawala, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir na Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha. Katika eneo hili tunazungumza kwanza eneo la Tume ya Uchaguzi, Daftari la Wapiga Kura na Majimbo ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja hapa kwamba inafaa Tume yetu ya Uchaguzi iwe na muundo mpya. Ni jambo jema na Serikali hatupingi hilo. Lakini tunasema Waheshimiwa Wabunge, muwe na subira. Kwa sababu waamuzi wa mwisho nni ninyi Wabunge Watukufu.

Kwa hiyo, Serikali inaandaa mabadiliko ya Katiba, yatakuja Bungeni hapa na bila shaka kila mmoja atapata nafasi ya kutoa maoni yake juu ya muundo bora na kurekebisha hapa na pale ili tufanikishe demokrasia katika nchi yetu na hii pia itawapa nafasi kwa wadau wa nje ambao ni sisi Wabunge, wanaweza wakapata nafasi ya kutoa maoni yao jinsi ya muundo gani uwe ili tufanikishe malengo yetu. Kwa hiyo, Serikali haina pingamizi nalo lakini nafikiri tsubiri wakati ufike ili kila mmoja apate nafasi ya

kuchangia na ninyi Waheshimiwa Wabunge ndio watu wa mwisho wa kuamua juu ya hatima ya muundo wa Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, pia lilizungumzwa juu ya Daftari la Kudumu la Wapiga kura, litayarishwe kwa msingi ya uwazi. Hili tumesema wakati nawasilisha Muswada wa Sheria hii kwamba Serikali haina cha kuficha, tutapewa nafasi, watu watoe maoni yao. Tutashirikisha, ndiyo maana tumekuwa na Semina mbalimbali na ninakusudia kwamba wakati wa Kikao hiki cha Bunge tufanye semina moja hapa ya Wabunge wote ili kuwaelimisheni namna ya Daftari la Wapiga kura litakavyotayarishwa na ninyi mtoe maoni yenu ili tuweze kuboresha hali halisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naahidi kwamba semina hiyo mtapata nafasi ya kutoa maoni yenu na viongozi wa Tume ya Uchaguzi watakuwepo hapa ili nao wasikie yale maoni yenu kwa ajili ya kufanikisha demokrasia ndani ya nchi yetu.

Pia ilitolewa hoja kwamba uandikishaji wa Daftari la Kudumu la wapiga kura uzingatie shughuli na amali na kazi za watu mbalimbali hasa Mheshimiwa Benedict Losurutia, alisema kwamba wapiga kura wake wengi ni wachungaji. Kwa hiyo, ni vizuri tukaangalia hayo.

Kuna wachungaji, wafugaji, wavuvi na kuna wakulima. Tutajitahidi wakati tunaandaa Daftari hili na wakati wa kuandikisha tujaribu kuwafikia wengi zaidi ili kila mmoja apate haki ya kupiga kura mwaka 2005. Kwa hiyo, hili tumelisikia na Tume ya Uchaguzi itajitahidi kufanya hivyo ili kila mmoja apate haki ya kuwapata wote hao, ili kila mmoja apige kura.

Mheshimiwa Spika, pia kuna hoja kwamba ZEC ya Zanzibar na NEC ya Muungano zishirikiane katika kuandaa Daftari la Kudumu la Wapiga kura. Kila mmoja ana taratibu zake na kanuni zake, washauriane na kushirikiana kwa sababu jambo hili kila mmoja inabidi afuate Katiba yake na maelekezo yake. Lakini mashauriano yapo na nia yetu wote ni kwamba kufanya uchaguzi huu uwe wa haki na huru kwa Bara na Visiwani. Hiyo ndiyo nia yetu kubwa sana.

Kuna hoja nyingine ya elimu ya uraia. Elimu ya uraia itolewe na kwamba Serikali ichukue jukumu lake la kuwaelimisha watu na pia tutawashirikisha NGOs na pia wadau wenyewe wa Vyama vya Siasa wana wajibu wa kuwaelimisha watu wao namna bora ya kujua jambo hili. Na ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu mtapata semina hapa bila shaka mtakuwa wasimamizi wakubwa wa jambo hili na msaidie. Kwa sababu nia yetu wote ni kwamba tunataka kufanya uchaguzi uwe wa haki na huru.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine inayosema kwamba siku 21 za kuandikisha zinatoshwa? Zinatoshwa, kwa sababu miaka yote hiyo ya uhai wetu uchaguzi wanaandikisha watu katika muda wa wiki tatu zinatoshwa. Muhimu ni kwamba vituo vya uandikishaji tuwafikie wananchi kwa sehemu kubwa sana. Muhimu wananchi wenyewe wahamasishwe, wajue kwamba ni wakati wa kujiandikisha. Muhimu pia viongozi wa Vyama vya Siasa pia wafanye wanachama wao na wapenzi wao ili wajiandikishe. Kwa

hiyo, inawezekana kabisa hili. Muhimu kwamba wote kwa pamoja tufanye kazi ya kuwahamasisha watu wetu na isiachiwe Serikali peke yake.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilizungumziwa ni je, kwamba Daftari hili la Wapiga kura litatumika pia kwa uchaguzi huu wa mwaka 2004 wa Serikali za Mitaa? Hapana! Hatukuamua hivyo, tutaanza mwakani. Lakini tunasisitiza jambo hili, maana yake haiwezekani, tumechelewa sasa hivi. Kwa hiyo, tutaanza uchaguzi wa mwakani wa Madiwani, Wabunge, Rais na pia Baraza la Wawakilishi kwa kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kulikuwa na hoja hapa kwamba viongozi wa Vyama vya Siasa walitoa mapendekezo yao hapa Dodoma kuhusu jambo hili. Lakini suala la kutoa maoni ni lingine na uamuzi ni lingine, Serikali ndiyo yenye uamuzi. Tunatoa maoni tu basi ya kwamba watachukua, mengine wataacha si lazima. Hatulazimiki jambo hilo. Lakini kama jambo jema tutachukua, tunasema kwamba uchaguzi huu utakuwepo mwakani. Lakini tulifikiri mwakani tutaangalia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lingine Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, alisema kwamba anafikiri kwamba kuna haja ya kugawa Majimbo upya. Ni jambo jema, lakini tuna taratibu zake. Kwanza lazima vipindi vya miaka 10 kwanza itokee ndiyo Majimbo yanagaiwa upya. Tume ndiyo yenye mamlaka ya kugawa na baadaye Rais anaamua.

Kwa hiyo, tunasema kwamba bado muda upo, tuangalie lakini maamuzi Serikali ikashatoa mtaambiwa kwamba Majimbo yatagawiwa au hayagawiwi. Kwa hiyo, kwa sasa hivi hatuna maamuzi yoyote kwa sasa hivi tusebiri mpaka Serikali itakapoamua tuone kwamba inawezekana au haiwezekani. Lakini masharti hayo kwamba lazima miaka 10 ipite kwanza lazima Tume ya Uchaguzi ipendekeze na pia lazima Rais aamue. Mtu mwingine yoyote hawezi kuamua majimbo haiwezekani. Ni makosa ya kisheria. Kwa hiyo, msijiamulie huko, kugawa majimbo huko wakati hamna mamlaka hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo wa Vyama vya Siasa walichangia ni Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga na Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo. Kulikuwa na hoja kwamba Sheria ya Vyama vya Siasa ifanyiwe marekebicho. Ni jambo jipya, vyema tutafanya hivyo. Lakini tatizo siyo vyama vya siasa, siyo Msajili. Tatizo ni vyama vya siasa vyenye ndani ya vyama vyenu kwamba lazima mwendeshe vyama kwa kufuata demokrasia, mwache udikteta na uachwe uimla. Huo ni ukweli na hoja ya Mheshimiwa Makanga amethibitisha hapa juzi kwamba kuna uimla katika vyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo kasema pale, kuna uimla katika Vyama vya Siasa. Kwa hiyo, katika vyama vinne ambavyo vimo ndani ya Bunge hili, viwili viongozi wao wamekiri kwamba kuna udikteta ndani ya Vyama. Kuna vyama vinne ndani humu. Viwili viongozi wao wote madikteta, vimebakia viwili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, la msingi ni kwamba tujitahidi Vyama vya Siasa viwe na demokrasia na si wanachama na viongozi tuwasindikize viongozi wetu

demokrasia wawe nayo. Kulikuwa na hoja nyingine kwamba Msajili wa Vyama afanye uhakiki wa Vyama vya Siasa vya upinzani kwamba vingine ni vyama hewa. Huu ni wajibu wa Msajili na atafanya hivyo. Pia kulikuwa na hoja kwamba baadhi ya viongozi wanatoa kauli za uchochezi katika majukwaa ya siasa na la msingi hapa na sisi ni wajibu kwenda kuwaelimisha, kuwafahamisha na wamejifunza hatua kwa hatua. Lakini kama watakuwa hawasikii basi Serikali itachukua hatua kuwaadhibu wale wote ambao wanaleta uchochezi katika nchi yetu.

Kulikuwa na hoja nyingine hapa ya matumizi mabaya ya ruzuku kwamba baadhi ya viongozi wa Vyama vya Siasa wanachukua hela za ruzuku, wananunua nyumba ya milioni 50, wanachukua hela wanaolea, wanafanya harusi kwa ruzuku ya chama. Haya kwa kweli ni kinyume cha taratibu za maadili ya uongozi na taratibu za Vyama vya Siasa. Kwa hiyo, nashauri wale wote ambao wamefanya hivyo Msajili wa Vyama atafanya utafiti na kuchunguza na wale wote ambao wataonekana kwamba wamefanya makosa yataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria ya nchi yetu. *(Makofi)*

Kulikuwa na hoja nyingine kwamba mwanachama akifukuzwa katika chama basi anapoteza Ubunge wake. Hiyo ni kwa mujibu wa sheria kwamba huwezi kuwa Mbunge mpaka uweke mdhamini wa chama chako. Kwa hiyo, mpaka hapo tutakapoondoa dhamana hiyo ndipo jambo hili litamalizika. Lakini sasa haiwezekani kufukuzwa uanachama na mtu akabaki kuwa Mbunge.

Kuna suala lingine la fidia ya waathirika wa matokeo ya Januari 26 kule Zanzibar ambayo wanasema kwamba inafaa wapewe fidia. Serikali imesema haitoi fidia, itatoa kifuta machozi na hayo maamuzi yamekubaliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumekubaliana kwamba tutajitahidi kutafuta fedha ili iwasaidie wale ambao walipata athari hizo kule Zanzibar wakati wa Uchaguzi Mkuu uliopita, mbali ya kuwaonya na kuwatahadharisha, Waziri Mkuu ingawa kawatahadharisha, Marehemu Makamu wa Rais, Dr. Omar Ali Juma, kawatahadharisha, bado walikuwa ngangari, basi matokeo yake ndiyo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kustaajabu ni kwamba hata kwenye hotuba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani amesema kwamba wako tayari kuondoana shingo, amesema humu. Sasa hii maana yake nini? Wakati tunasubiri kutoa fidia hii, wanasubiri kutoa shingo. Sasa ni bora tusembiri mpaka Uchaguzi Mkuu upite mara ya pili tujue namna ya kutoa fidia zote mbili. *(Kicheko)*

Ningeshauri Waheshimiwa Wabunge, tuache jazba na tufanye kazi kwa mujibu wa taratibu zetu. Eneo la pili ninalotaka kuzungumzia na maeneo mawili ya mwisho, kulikuwa na hoja hapa ya Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu alizungumzia kwamba hata Chama Cha Mapinduzi pia kimewafukuza wanachama wake na viongozi wake. Iweje washtuke kwa chama cha UDP, ni kweli, lakini mfano wake si kweli. Amesema kwamba Ndugu Aboud Jumbe kafukuzwa na Maalim Seif Shariff Hamad kafukuzwa.

Mheshimiwa Spika, mimi ninao ushahidi hapa, nitakusomeeni, na mimi nilikuwa Mjumbe wa *NEC* na nilikuwepo Dodoma hapa. *(Makofi)*

*(Hapa kielelezo husika kilionyeshwa Bungeni)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mimi nimekuwepo katika kikao kile cha Dodoma hapa CBE, tarehe 24 hadi 30 Januari, 1988. Nilikuwa Mjumbe wa Kikao hicho. Lakini nasoma kitabu ambacho ameandika Mheshimiwa Aboud Jumbe hiki. Mheshimiwa Andrew Chenge, hiki kitabu kinasema nini? *Conjecture Vs Truth* au siyo?

*Conjecture* sijui kutamka Kiingereza mie, maana ile ni uzushi dhidi ya ukweli, amesema hapa. Sasa nitaelezea kinasema nini?

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya nilitaka nitafsiri kwa Kiswahili lakini nimeshindwa.

Anasema: *“Twenty years ago to the surprise and unexpectation of most if not all who were at CCM Meeting of Central Committee, I requested to be allowed to vacate all the Posts I then held; of President of Zanzibar, Chairman of Revolutionary Council, Vice President of Tanzania and Vice Chairman of CCM. Despite all available evidence including minutes of the meeting concerned, a handful of people outside the meeting either knowingly or unknowingly prefer to embark on a wagon of conjecture hence they conveyed false obviously unchecked information to their unsuspecting audiences listeners, readers. The purpose of this booklet is to reveal and undeniable truth to those who have been deliberately mistakenly, wrongly informed.”* Page one. (Makofi)

Kwa hiyo, taarifa hii pia itakwambia nini madhumuni ya kitabu hiki kwa wasomaji wale ambao hawajui. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naendelea. Kwenye kumbukumbu za Mkutano huo, nina-*quote* hivi: *“At the end of speech the Vice Chairman, Jumbe said the allegations made are revealing and if the Central Committee thinks that I myself or the Central Government or the Revolutionary Government of Zanzibar are involved in way or another even if by the slightest doubt, I give you the benefit of doubt. In that case the great favour you can grant me is to allow me to hand over back to you whatever responsibilities. I had in all the positions you vested on me. I am making this clean and pure statement, without a grain of arrogance, but with humility; without a sting of anger or trace of pleasure.”* Page six. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hizi ni kumbukumbu. Kumbukumbu za CCM hizi. Naenda mbele, potelea mbali kwamba Kiingereza hawajui. (Kicheko)

*“At the end of Central Committee Meeting is reported in the same minutes that, while closing the session, the Chairman of CCM, Julius Kambarage Nyerere requested the Central Committee to thank Ndugu Aboud Jumbe for his contribution which helped the meeting to arrive at a commendable resolution. He further stated that, Ndugu Jumbe has also served the Party for a long time and very much assisted to strengthen the*

*Union in the 12 years he was Vice Chairman of the Party, Vice President of the Union and President of Zanzibar. He therefore recommended Ndugu Aboud Jumbe to be honoured and given the respect he deserves, the Party to instruct the Union and the Zanzibar governments to look after him and his family. Page seven. (Makofi)*

Hiyo ndiyo heshima aliyopewa Ndugu Aboud Jumbe Mwinyi. Kwa hiyo, alijiuzuru, hakufukuzwa. Sasa tuangalie sakata la wengine. Tuangalie kundi lingine lilivyofukuzwa wanachama, hili genge la Maalim Seif Shariff Hamad na wenzake. Kinasema hivi: *“The CCM Central Committee received and discussed the report by Party’s Principal Secretary Ndugu Rashid Kawawa, of his April, 1988 visit in the Zanzibar regions. The purpose of this visit was to assess the condition state of the organization’s life. The report showed that the political situation in Zanzibar particularly in the north and the South of the islands was not satisfactory. This state was caused by the following:-*

- (i) Assault against the Party;*
- (ii) Invasion into the Party by opponents; and*
- (iii) Campaign against the Party founders.*

Mheshimiwa Spika, hayo ni maneno yanayoonekana kwenye ziara ya Katibu Mkuu wa Chama. *“The report then submitted the names of Party and Government leaders, disclosed by the Party Members and Elders, disclosed in creating discord and political confusion in Zanzibar. The Leaders involved were Ndugu Rashid Hamad Hamad, Ndugu Seif Sharif Hamad, Ndugu Soud Yussuf Mgeni, Ndugu Hamad Rashid Mohammed, Ndugu Suleiman Seif Hamad na Ndugu Khatib Hassan Khatib.*

*Other accused were Shaaban Mloo and Ali Haji Pandu. Hizo ni kumbukumbu za CCM. Naendelea mbele, Central Committee during the discussion of the subject used the opportunity to remind itself what had happened in 1985 namely:-*

*(i) Creations of discord and political confusion in Zanzibar prior to the election of Idris Abdul Wakil to the post of President of Zanzibar.*

*(ii) Despite the warning the group continued its acts of antagonism, persuasion, discord and creation of confusion till in October, 1987 they became bold and open.*

*(iii) In those activities, the group formed affiliations with external enemies centred in London. Dubai and Denmark.*

*(iv) This antagonistic group is committed to using Zanzibar as a focal point of disrupting peace and stability in the whole of Tanzania.*

*(v) Central Committee after careful consideration of the said activities conclude the plea was serious problem for which the following partisan were accountable, Seif Sharif Hamad, Rashid Hamad Hamad, Seleiman Hamad, Hamad Rashid Mohamed, Soud Yussuf Mgeni, Khatib Hassan Khatib, Ndugu Shaaban Mloo and Ali Haji Pandu. They*

*were all given the opportunity to defend themselves against their accusation. After a careful examination of their defence, the meeting came to the following decision:-*

*(a) They were all guilty of undermining the Party with the object of turning the people against the Union;*

*(b) Though they had been warned since 1985 yet they continued over years in their untoward the activities towards the Party, thus derving punishment concurrent with the weight of their guilty.*

*(c) The accused have been so engrossed in their selfish crave for power, to the extent that they were able to be used by external enemies in their campaign to sabotage the Party and undermine the Union.*

*(d) Through all these activities of theirs, they have revealed that we are not with us. They have deserted us to join the enemy with object of enhancing their opposition to the Party and through in the Union.*

*(e) In consideration of these findings, the Central Committee is convinced that the following are guilty of consipracy against the solidarity of the Pary and the peace and stability of , the Committee therefore, anonymously agreed to expell them from the Party. Page 21 - 22.(Makofi)*

*Naomba nirejee tena sentensi hii, The Committee therefore anonymouly agreed to expell them from the Party. Wamefukuzwa.*

*Mheshimiwa Spika, basi na hayo sasa nimalizie mstari wa mwisho, ni kikao si mtu, siyo out, ni Chama kimeamua. Mjifunze kutoka CCM jamani, namna ya kuongoza Chama. (Makofi)*

*Pia kulikuwa na hoja nyingine ya Kiongozi wa Upinzani kuhusu Mzee Thabit Kombo. Mmesoma pale, aseziita Riwaya za Thabit Kombo, sasa bahati mbaya nimekuja nacho, ninayo hapa Riwaya yake. Nitakusomeeni. (Makofi)*

*Mheshimiwa Spika, Watanzania tuna tabia ya kuheshimu wazee, ni desturi yetu na mila yetu, tunaheshimu hivyo. Lakini Mheshimiwa Mkuu wa Upinzani hakumheshimu Mzee Thabiti Kombo, sioni ajabu, kwa sababu hamjui. (Makofi)*

*Mheshimiwa Spika, hamjui na siasa kwake ni ngeni na kaparamia behewa la siasa mwisho mwisho huku. Lakini mimi nafikiri haikuwa haki kabisa kumsema vibaya Mzee huyu hasa kwa sababu ni marehemu, amefariki. Ni marehemu tunatakiwa tumrehemu badala ya kumsema vibaya na katika mazingira yetu ya Waafrika nafikiri ni utovu wa adabu sana kumsema marehemu na mtu mzima. (Makofi)*

*Sisi tunajua kwamba Mzee Thabiti Kombo ni mkongwe wa siasa nchi hii, hakuna asiyejua. Mimi namjua, nimemwona, nilikuwa naye katika Afro Shiraz Youth League, katika Chama namjua. Ni mkongwe wa siasa hakuna anayempata hapa. Lakini la msingi*

ni kwamba yeye ni mmoja katika waasisi wa Chama Cha *Afro Shiraz* kule Zanzibar, chama cha Waafrika.

Mheshimiwa Spika, yeye ni mwasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar. Yeye ni mwasisi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Yeye ni mwamzilishi wa Chama Cha Mapinduzi. Kwa hiyo, jeuri yetu yote hii hapa leo ni sehemu ya mchango wa Mzee Thabit Kombo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ningepomba Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani, tuwaheshimu wazee wetu. Tuache kazi ya ukasuku. Unapewa nyimbo unaimba tu hujui kitu ni gani. Huyu mtu muhimu sana. Thabit Kombo ni mtu muhimu sana katika maisha ya nchi hii. Lakini nampa pole sana Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, si makosa yake. Mambo huyajui, umefikia juu tu, lakini nataka niseme Thabit Kombo kwamba ametunga Riwaya, naomba nitoe baadhi ya *chapter* za Riwaya za Bwana huyu, tuone je, kwamba huyu ni Riwaya kweli au vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 92 anazungumza Thabit Kombo jinsi ushirikiano uliokuwepo kati ya *TANU* na *ASP*. Anasema hivi, “Siku yenyewe iliyofanyika kule Zanzibar, Mkutano wa Hadhara uliohudhuriwa na watu wapatao elfu kumi na Msemaji Mkuu akawa Bibi Titi Mohamed na Saadani Kandoro. Bibi Titi alitoa hotuba kali sana, inayosisimua, kushawishi wananchi wa Zanzibar kufanya kitendo cha ujasiri. Alisema mwanamke huyu, tunasema bila woga, “Lazima muondoe kibendera kile cha Kijogoo pale.” Ndipo tutambue kuwa ninyi ni wanaume kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, hamjui jogoo. Jogoo ni alama ya Chama cha *HIZIB* kule Zanzibar Maskani, hata hajui yeye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, alichokuwa anasema Bibi Titi ni kwamba: “Ondoeni jogoo yule pale,” anawaambia viongozi wa *Afro-Shiraz Party* kule Zanzibar, anasema Thabit Kombo. Je, Riwaya hii?

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 95 kuna picha hapa ya Thabit Kombo wako Mbale, Uganda mwaka 1960 na viongozi wengine chungu mzima katika mkutano wa *PAFMECA*.

**WABUNGE FULANI:** Inatosha!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Haitoshi bado.

Mheshimiwa Spika, Thabit Kombo alipewa Nishani ya Ushujaa na Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, Mwalimu Julius Nyerere anamwambia Thabit Kombo toka mwaka 1953 hadi sasa umekuwa kiongozi shujaa na mwenye uthabiti wa moyo katika ngazi ya juu katika Chama na katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano. Umewahi kushika nyadhifa mbalimbali na kutekeleza pasipo ubinafsi, kwa uhodari usio na kifani. Umewahi kuwa Mkuu wa *Shiraz Association*, Katibu Mkuu wa *Afro-Shiraz Party*, kiongozi mmojawapo wa Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964,



Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Waziri wa Afya wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Waziri wa Biashara. Kwa hiyo, nakutunukia nishani hii tarehe 26 Aprili, 1985. Huyu ni mtu wa kumdharua huyu?

**WABUNGE FULANI:** Hata kidogo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Nyimbo za kutunga tu za kasuku hawajui kwa hiyo, ingefaa usome.

Mheshimiwa Spika, nimesema haya kwa sababu ya kuweka rekodi sawa tu, wao wameanza, mimi namaliza. Wenyewe wameanza wanasema huyu bwana riwaya hii ndiyo riwaya yenyewe, riwaya ya mtu ambaye amesaidia tukafika hapa leo. Wamezungumza juu ya Ndugu Abdu Jumbe, nimejibu. La msingi hizi sio fitina bali najibu hoja ambazo ninyi Wapinzani wenyewe mmetoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUWI):** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, naomba nitoe pole kwa Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mpendwa.

Pia napenda kutoa pole kwa wenzetu waliokumbwa na maafa mbalimbali nikianzia na Mheshimiwa Anne Malecela, kwa kuvamiwa na majambazi na mwenzetu Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere pamoja na Mheshimiwa Estherina Kilasi, wote nawapa pole sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia jana wakati tukiwa humu, nimeelezwa kwamba Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, alipigwa naye nampa pole kwa kupigwa ingawa sijui nani alimpiga, ataniambia baadaye. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa hii ilikuwa ni hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kama tunavyojua Kikatiba Waziri Mkuu ni mratibu wa shughuli zote za Serikali, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia masuala yote ya Serikali. Isingewezekana kwetu sisi kugusia yote lakini kama mnavyojua mlikuwa mnasema nafikiri hamkuwa mnamwambia Waziri Mkuu peke yake, lakini wote kwa ujumla wetu. Kwa kuwa tumeanza tu mchakato wa Bajeti, yaliyo mengi yamenukuliwa na Waheshimiwa Mawaziri wenyewe, wasaidizi wao na *Hansard* zipo yatatolewa majibu kwenye hotuba zao. Tutakachokifanya sisi tutamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kujibu machache lakini sisi ni miongoni mwa wasaidizi wengi waliopo hapa ambao nao watafanya kazi kama yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na hoja ya kwanza ambayo imetolewa na Mheshimiwa George Mlawa, juu ya uendeshaji wa ofisi za Wabunge uwe chini ya Ofisi ya Bunge. Utaratibu uliopo hivi sasa unawezesha usimamizi na ufuatiliaji wa karibu zaidi kwa kuwatumia Makatibu Tawala wa Mikoa, labda hapo baadaye wakati ambapo tunajua

kwamba ofisi yetu kupitia Tume imeandaa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano utakapoteklezwa kikamilifu, pengine jambo hili linaweza kutekelezeka lakini kwa sasa kwa sababu hatuna mtandao huo, nafikiri tuendelee na utaratibu huu ambao unawezesha ofisi za Wabunge kuratibiwa au kusimamiwa na Ofisi za Ma-RAS.

Mheshimiwa Spika, najua tatizo, kuna wengine wamezungumzia jambo hili kwamba ofisi hizi zimekuwa hazipewi huduma, hazikarabatiwi na haziangaliwi. Leo sitoa maelezo mengi kwa sababu najua ipo taarifa ya Kamati ya Huduma za Bunge itakuja hapa ambayo imetembelea Mikoa kadhaa na tutajadili.

Mheshimiwa Spika, ninachojua kwa taarifa ndogo niliyonayo ambayo wenzangu wa TAMISEMI wameiunganisha hapa Mikoa mingi sana katika Bajeti hii wamejitahidi angalau kukarabati au kuziweka sawa ofisi za Waheshimiwa Wabunge. Kwa mwaka huu wa fedha, Mikoa mingi sana imetenga fedha kwa ajili ya huduma mbalimbali za Wabunge katika maeneo yao. Naomba nihitimishe hili kwa kusema tusubiri hiyo taarifa ya Kamati ya Huduma za Bunge na kwa kuwa wote tumepitishiwa fomu na tumejaza, bila shaka baadaye tutakapojadili tutajua tunaazimia nini.

Mheshimiwa Spika, pia imezungumzwa sana habari ya vita dhidi ya UKIMWI. Jambo hili limezungumzwa sana na Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha; Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali.

Mheshimiwa Spika, hoja zilikuwa viongozi wa dini wasitakiwe kuhimiza matumizi ya *condom*. Sisi tunafikiri viongozi wa dini wana hiari ya kuhubiri na kuhimiza yale wanayoona yanafaa katika vita dhidi ya UKIMWI. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, fedha za mapambano dhidi ya UKIMWI zielekezwe kwa waathirika wa UKIMWI na yatima. Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuwasaidia waathirika wa UKIMWI na watoto yatima. Baadhi ya mambo yaliyofanyika ni kuanzishwa kwa Baraza la Waathirika ambalo litaratibu shughuli zao na kutolewa kwa mwongozo wa yatima. Vile vile Tume imekuwa ikitoa msaada kwa yatima kupitia Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wajumbe wanawake katika Kamati ya Kudhibiti Ukimwi ngazi ya Halmashauri iongezwe. Sheria Na.7 na 8 ya mwaka 1982 inaainisha idadi ya wajumbe kwenye Kamati mbalimbali ngazi ya Halmashauri. Hata hivyo, Halmashauri hazizuiliwi kuwaalika wananchi wowote wale katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya iongezwe fedha ili kukidhi mahitaji ya dawa kwa ajili ya waathirika wa UKIMWI. Serikali imeshaanza mpango wa kuhakikisha upatikanaji wa dawa hizi za virusi geuzi. Kwa kuanzia, kama mlivyosikia kwenye Bajeti zetu, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 2 kwa ajili ya kununua dawa. Mpango wa Serikali wa kutoa dawa za bure kwa wagonjwa wa UKIMWI walio katika hatua za

kuanzishiwa dawa hizo unaanza mwaka huu wa fedha na Mheshimiwa Waziri mhusika wa sekta hii atatoa ufafanuzi wakati wa Bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, pia imeelezwa yatolewe maelezo kuhusu vitabu vya UKIMWI vilivyochapishwa na kuonekana havifai. Hili lilielezwa kwa tafsiri kwamba vitabu hivi vililenga tu shule za msingi. Ukweli ni kwamba vitabu hivyo vilikuwa kwa ajili ya kuelimisha watu wa rika zote kuhusu vita dhidi ya UKIMWI zikiwemo shule za msingi. Kwa kuwa lengo halikuwa shule za msingi peke yake na kwa kuwa ilionekana kwamba havipendezi sana katika shule za msingi vitabu hivi vimepelekwa kwa walengwa wa makundi mengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wagonjwa na waathirika wa UKIMWI wasaidiwe kwa kupatiwa lishe ya bure. Jukumu la kuwasaidia waathirika ni la jamii nzima. Serikali itashirikiana na makundi mbalimbali ya jamii zikiwemo asasi zisizo za Kiserikali kadri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la elimu ya UKIMWI kutolewa hadi vijijini. Elimu dhidi ya UKIMWI inatolewa kwa makundi yote ya jamii.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazotumika kwa semina, warsha zipunguzwe na zielekezwe kwa waathirika wa UKIMWI. Mapambano dhidi ya UKIMWI yanahusisha vipengele vingi sana. Serikali itahakikisha mgawanyo wa fedha kwenye vipengele hivi unazingatia vipaumbele tulivyonavyo katika vita dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa John Singo, hii ni maalum amesema Wilaya ya Same haijapata mgao wa fedha za UKIMWI kama ilivyo kwenye jedwali la hotuba ya Waziri Mkuu. Naomba radhi Wilaya ya Same haikuonekana haikuchapwa kwa makosa, lakini imepatiwa shilingi 20,450,000/= katika mpango huo.

Mheshimiwa Spika, nataka nijumlishe hapo hapo na hoja ya Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, aliyesema fedha za uhamasishaji kuhusu UKIMWI zitolewe kwa uwiano kwa Wilaya zote. Upo utaratibu ambao umetumika, Halmashauri zilikuwa zinaandaa miradi hii na fedha zimekuwa zinatolewa kutokana na maombi ya Halmashauri zenyewe kwa kuzingatia ubora wa miradi na uwezo wa kutekeleza. Sasa kwa sababu taarifa zote za Halmashauri naweza kuzipata, Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye ana matatizo ya kujua Halmashauri yake iliandika nini ili alinganishe na fedha ambazo ameziona kwenye jedwali na hizi nitakazosisoma, tuko tayari kushauriana naye kwa sababu kuna Halmashauri nyingine waliomba pesa nyingi lakini hazikidhi vigezo vya kupatikana kwa fedha hizi au maombi yale yamekwenda nje kabisa ya utaratibu. Watu wameomba magari matano, sita, wameomba *music instruments, computer* lakini malengo ya fedha hizi hayakuwa hayo. Kwa hiyo, wale wote ambao wanafikiri wana matatizo ya uwiano wa fedha hizi tuko tayari kukaa hapa na wataalam wa *TACAIDS* wako hapa watawaelimisha. Tuna nia ya makusudi kuziita zile Halmashauri ambazo hazikuandika vizuri kabisa ili tukae nazo tuwaeleze namna ya kuandika vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya wakati tunachapisha vitabu hivi taarifa nyingine hazikuwepo, nataka kusema pamoja na hii Same ziko Wilaya nyingine ambazo hivi sasa zitapewa fedha na michangunuo yao imeshapitishwa. Wilaya hizo ni za Bagamoyo, Mafia, Manispaa ya Dodoma, Makete, Biharamulo, Kibondo, Same, Bunda, Kwimba, Ukerewe, Mpanda, Kahama, Meatu, Manyoni, Singida, Igunga na Korogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi Halmashauri ambazo baada ya hapo Wilaya zake zinachambuliwa karibuni nazo zitapatiwa fedha, hizi nilizosisoma zinapatiwa sasa hivi, Wilaya ambazo miradi yake inachambuliwa ni Wilaya za Bukombe, Magu, Morogoro, Muheza, Sikonge na Tabora. Lakini ziko Wilaya nyingine 23 ambazo hizo ndio nimesema mipango yake inahitaji kuboreshwa kabla ya kupatiwa fedha. Tutawasiliana na Wakurugenzi ili tuwaeleze namna ya kuboresha hii.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa ni la madini, hili limeongelewa na Waheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Stephen Kahumbi. Kwa ujumla wamezungumzia habari ya mrabaha na wamependekeza na viwango na wengine wamesema Serikali ianze utaratibu wa kutoa mrabaha huo, mengi yamezungumzwa lakini yanahusiana na mrabaha.

Mheshimiwa Spika, jibu la Serikali ni kwamba hivi karibuni mmesikia hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Serikali imeshateua Kamati Maalum ya Kuchunguza na Kuchambua Matatizo ya Sekta ya Madini. Nafikiri ni busara tusubiri tuone matokeo ya Kamati hiyo kwa sababu inapita nchi nzima, inahoji kila mtu na pengine hata Waheshimiwa Wabunge tutafikiwa na tumeambiwa Mheshimiwa Mbunge mmoja ambaye anatoka kwenye eneo lenye madini mengi ya dhahabu yumo kwenye Kamati hiyo ni mwakilishi wetu, naomba tuvute subira. Pia Serikali katika Bajeti yake imeelekeza kwa kina mchango wa sekta ya madini katika maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuchangia linahusu maafa hili limezungumzwa sana na Mheshimiwa Wilferd Lwakatare na Mheshimiwa Stephen Kahumbi. Hoja ya kwanza inasema fedha zinazotengwa kwa ajili ya maafa ziwekewe utaratibu na hoja ya pili inasema fedha za maafa ziwafikie walengwa na hoja ya tatu inasema maelezo kuhusu kuungua nyumba ya Rais hayaridhishi.

Mheshimiwa Spika, maelezo ni kwamba fedha za maafa ziko chini ya utaratibu wa Serikali kama fedha nyingine. Kwa sheria ya zamani tunayoitumia sasa kila maafa yanapotokea huwa kuna Kamati ya Makatibu Wakuu inakaa, wanaijadili tukio lile, wanapendekiza kiwango cha fedha ndipo zinatolewa na Hazina, zinakwenda kutumika kule ambapo maafa yametokea. Lakini sasa kwa sera hii ambayo tumezindua juzi ambayo Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mmesoma, utaratibu mpya utabuniwa na ambao utatungiwa sheria na itakuja hapa Bungeni. Kwa kuwa mmeshapata sera hizo, naomba tuvute subira baada ya sera hiyo yatakuja marekebisho ya sheria ile ya mwaka 1990 ili tuweke sheria nzuri zaidi ya kudhibiti maafa nchini.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ya ustawishaji Makao Makuu. Mambo haya ya ustawishaji Makao Makuu yamezungumzwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma na Kamati yetu ya Bunge ya Katiba, Sheria, Utawala imetupa ushauri juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, hoja zenyewe zinasema Serikali itunge sera na sheria ya kuwezesha kuhamia Dodoma. Pili, kuwe na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zote za kuhamia Dodoma awamu kwa awamu, ratiba iwe wazi ikionyesha Wizara, Taasisi zinazohamia Dodoma na lini. Tatu, inasema taasisi zilizokwishaamia Dodoma kama Bunge ziimarishwe.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Makao Makuu mapya wa nchi yetu ni mchakato wa muda mrefu unaotegemea uwezo wa Serikali na wadau wengine. Aidha, uamuzi wa kujenga Makao Makuu ni wa Serikali na kwa kweli ni wa hiari kwa wadau wote. Azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma iko pale pale na inafanyika kwa awamu kulingana na uwezo wa Serikali. Hili linathibitishwa na nguvu kubwa na jitihada za Serikali ambazo zinaonekana hivi sasa za kuimarisha miundombinu na huduma muhimu ambazo Waheshimiwa Wabunge wote mmeziona zimeimarishwa hapa Dodoma kama maji sasa tatizo imekuwa historia hapa Dodoma, nyumba za wafanyakazi zinajengwa pale mnaona haya yote yanaendelea kwa sababu jambo hili bado linaendelea na malengo yetu yapo pale pale.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililozungumzwa linahusu Kanuni zetu za Bunge na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, yeye anasema kwamba uwepo utaratibu wa siri wa kupiga kura Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, maelezo ni kwamba taratibu za uendeshaji wa shughuli za Bunge zinatawaliwa na Kanuni za Bunge za Kudumu ambapo sote Waheshimiwa Wabunge tunazipitisha. Endapo Kiongozi wa Upinzani ana hoja ya msingi aiwasilishe kwenye Kamati husika na endapo itaonekana inafaa iwasilishwe kwenye Bunge ili iweze kutolewa uamuzi. Ingawa kwa mawazo yangu utaratibu wa sasa ni mzuri sana kwa sababu kama wote tunavyojua kwamba Bunge hili ni la wazi ni vizuri wananchi wakajua Mbunge wao amewawakilisha namna gani hapa Bungeni, utafichaje kura wakati mambo yote yako wazi?

Hivi sasa hizi *television* zote tunayoyafanya hapa yako wazi kabisa. Hiki ni chombo cha wazi, hakuna sababu ya kufanya siri kama nia yako ni hapana, sema hapana tu kama nia yako ni ndio sema ndio tu ili wananchi wako wajue kwa nini unasema hapana na kwa nini unasema ndio. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililozungumzwa hapa ni hali ya chakula. Imesemwa hapa hali ya upatikanaji wa chakula Wilayani Karatu na Serikali ifanye tathmini ya kaya zenye upungufu wa chakula na zile zinazoendeshwa na wanawake hili limesemwa na Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o. Lingine limesemwa na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, waliokiuka taratibu za kusambaza chakula cha njaa wachukuliwe

hatua. Lngine limezungumzwa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, hali ya upatikanaji wa chakula Wilayani Karatu kwa mwaka 2003/2004 haikuwa nzuri hivyo Serikali itoe mbegu ili wajiandae kwa msimu ujao. Maelezo ni kwamba Serikali itazingatia mahitaji ya mbegu kama alivyopendekeza Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwa maeneo yote yaliyoathirika kwa ukame na mafuriko ikiwemo Karatu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, amesema Serikali isimamie na kudhibiti uagizaji wa chakula nje na ihimize kilimo cha muhogo. Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha upatikanaji wa chakula nchini. Hatua hizi ni pamoja na kuhimiza hifadhi ya chakula katika ngazi ya kaya, kutoa mbegu kwa waathirika wasio na uwezo na kuhimiza kilimo cha mazao yanayostahimili ukame. Hoja nyingine ilikuwa ya Mheshimiwa Benedict Losurutia na Mheshimiwa Paul Makolo, kwamba Serikali iendelee kupeleka chakula kwenye maeneo ambayo bado yana uhaba wa chakula. Maelezo ni kwamba Serikali itashirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha upatikanaji wa chakula kwenye maeneo yenye upungufu.

Hoja nyingine inasema Serikali iwe na mpango wa kuondokana na tatizo la njaa. Hii imetolewa na Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Hamisi Jumanne Nguli, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Adelastela Mkilindi. Serikali ina mpango au mikakati mbalimbali ya kuinua tija katika kilimo ambayo itaongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Baadhi ya mikakati hiyo ni programu ya kuendeleza kilimo, mradi wa umwagiliaji maeneo yenye ukame, mpango kabambe wa umwagiliaji na ruzuku ya pembejeo.

Hoja nyingine inasema Serikali ijizatiti kununua chakula kutoka kwenye maeneo yenye ziada kwa ajili ya *SGR*. Hii imetolewa na Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Leonard Derefa. Katika mwaka huu wa fedha, Serikali kupitia *SGR* imeipa uwezo wa kununua na kuongeza akiba ya Taifa ya chakula. Kwa mwaka huu wa fedha Serikali imejiandaa kununua kupitia *SGR* tani 100,000 za mahindi na tani 1,000 za mtama kwa bei ambazo zitatangazwa na *SGR* hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wanasubiri tu unyevunyevu kwenye mahindi yale upungue, mahindi yakauke vizuri, halafu waanze kununua lakini tumejiandaa na ununuzi huu ni mkubwa sana ukilinganisha na ununuzi uliofanywa katika miaka mitatu, minne, iliyopita. Vituo vimeshapangwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, ataeleza vituo na Kanda ambazo zitatumika kununua mazao haya.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine imezungumzwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kwamba tuwahimiza wananchi watunze chakula lakini tuhimize mihogo, hii ni hoja ya msingi. Serikali imekuwa inahimiza watu wajiwekee chakula lakini pia tumehimiza sana kilimo cha muhogo na mtama sio kama chakula cha njaa ila kama mazao yanayostahili ukame. Kwa kweli Mikoa imejitahidi sana na kwa sababu hiyo ndio maana Serikali mwaka huu tulitoa zaidi ya zile fedha ambazo mmeziona zimetolewa na *FAO*, Serikali yenyewe ilitoa shilingi milioni 120 kwa Mikoa fulani fulani kwa ajili ya kununua mbegu hizi za mtama na mihogo ili kuimarisha kilimo hiki. Ufafanuzi wa ziada utatolewa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililozungumzwa hapa ni vita dhidi ya dawa za kulevya. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Esha Stima na Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala na Mheshimiwa Frank Mussati. Hoja zenyewe ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali iweke mikakati ya kushughulikia waathirika wa dawa za kulevya. Pili, ukarabati wa jengo la Ofisi ya Tume ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya ukamilishwe. Tatu, dawa za kulevya zikamatwe na zitangazwe uzito wake tu na sio thamani. Nne, Tume ya Taifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya ipatiwe fedha za kuelimisha wananchi kupitia vyombo vya habari.

Kwa kifupi maelezo ni kama ifuatavyo, Serikali inashirikiana na wadau mbalimbali kutoa elimu kwa umma, tiba na watumiaji wa dawa za kulevya kwa kutekeleza mikakati ya Kikanda na Kimataifa kudhibiti dawa hizo.

Mheshimiwa Spika, hoja juu ya ukarabati wa jengo hoja ambayo imetolewa na Kamati yetu, ushauri umepokelewa, tutazingatia katika Bajeti ijayo.

Hoja ya dawa za kulevya zikamatwe na sio kutangaza thamani yake, lengo la Serikali katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya ni kuelimisha jamii juu ya madhara ya dawa za kulevya kiafya na mapato haramu yanayopatikana toka kwenye dawa hizo kwani zinachangia katika kuharibu uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, kwenye Bajeti ya Tume zimetengwa fedha za kuelimisha na kuhamasisha jamii dhidi ya dawa za kulevya kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz.

Mwisho, kwa kuwa sisi kama viongozi wa Bunge tumeshiriki sana katika kampeni za dawa za kulevya, napenda kuwapongeza sana viongozi wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Mkoa na Wilaya ambao wameshiriki kikamilifu katika mikakati ya kupambana na dawa za kulevya. Tarehe 26 Juni, 2004 itakuwa ni siku yetu ya Kimataifa ya kuadhimisha Siku ya Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya. Sherehe hizi zinafanyika Mwanza na mgeni rasmi atakuwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Anna Abdallah. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie jambo lingine juu ya *Dakawa Development Center*, jambo hili limeandikwa sana na Mheshimiwa Shaweji Abdallah huyu ni Mbunge wa eneo hilo, najua wako wadau wengine walishawahi kuja kuniona juu ya jambo hili, tumeshughulikia sana. Najua Mwenyekiti wa Wazazi wa Mkoa wa Tanga kwa jina simtaji ameshughulikia sana jambo hili na hivi sasa Serikali inashughulikia mapendekezo mbalimbali kuhusu muundo na mamlaka ya uendeshaji wa kituo hicho ili kuwe na mpango endelevu wa kuendeleza huduma mbalimbali ndani ya kituo hicho cha *DAKAWA*.

Mheshimiwa Spika, wakati tukisubiri maandalizi haya mapya ya Serikali, huduma zilizopo hivi sasa pale ndani pana Shule ya Sekondari (*high school*) inayoendeshwa na

Wizara ya Elimu na Utamaduni itaendelea, kuna Chuo cha Ufundi kinachosimamiwa na *VETA* kinaendelea na Shule ya Msingi ambayo inaendeshwa na Halmashauri ya Wilaya itaendelea. Makatibu Wakuu hawa watatu wanaosimamia sekta hizi wamekubaliana kwa mara ya kwanza kuchangia gharama hizi ili shughuli hizi ziendeshwe bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, lingine imezungumzwa habari ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, Mheshimiwa Paul Kimiti amezungumzia jambo hili, Serikali iharakishe hatua za kuleta Muswada wa Uwezeshaji Bungeni. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Paul Kimiti kwamba Muswada huu utawasilishwa katika Bunge lako Tukufu na kwa kuwa Sera imeshapita na tumeiona, litakalofuata sasa ni Muswada, hilo litafanyika. Chombo kitakachoundwa kusimamia uwezeshaji kipewe madaraka ya kufanya kazi zake, suala hili litazingatiwa wakati Muswada utakapokuja na kujadiliwa mbele yenu Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, lingine lililozungumzwa na Mheshimiwa Paul Kimiti kwamba muundo wa Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu, vitengo vipunguzwe.

Mheshimiwa Paul Kimiti amefanya kazi sana katika Wizara hii, anaijua sana. Kwa kweli majukumu yaliyopo hapa ni ya uratibu ratibu tu, ukizungumzia Kitengo cha Maafa kwa kweli ni uratibu maana shughuli hizi zinafanyika kila mahali. Ukizungumzia kazi ya msingi ya Waziri Mkuu ya uratibu wa shughuli za Serikali lazima ikae hapa. Kwa hiyo, mambo mengi yaliyopo na vitengo vilivyopo pale Waziri Mkuu kwa kweli vinahusisha shughuli ya uratibu hakuna kitu ambacho kinafanyika pekee katika eneo lile. Yapo mengine yanafanywa pale vitengo hivi vinaonekana vingi lakini kwa kweli ni vitengo ambavyo vinaambatana sana na mamlaka aliyopewa Waziri Mkuu ya uratibu wa shughuli za Serikali kwa mfano shughuli za Maafa, UKIMWI, Ustawishaji wa Makao Mkuu haya ni mambo ya uratibu tu yanagusa zaidi ya Wizara moja.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine imetolewa na Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Wizara ya Viwanda na Biashara iwekwe kwenye orodha ya Wizara muhimu. Ingawa sijui Wizara muhimu ni nini, lakini sisi tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz ndani ya Serikali tutauangalia ili tuweze kuona mapendekezo ya Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz.

Maswali ya Waheshimiwa Wabunge yanayopelekwa kwenye Wizara hayajibiwi haraka, hili limeulizwa na Mheshimiwa Abdallah. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba maswali yenu yote yaliyoulizwa mpaka Mkutano wa Kumi na Tano yameshajibiwa na Serikali hata leo ukiniambia leta jibu langu kwa maandishi nitakupa kila Wizara imeshajibu. Hapa hakuna tatizo isipokuwa tunapambana na muda, muda tulionao na maswali tunayouliza haufanani maswali ni mengi muda wa kuuliza hapa kwa sababu tuna aina moja tu ya kujibu maswali ya kusema ni mchache. Lakini pia Ofisi ya Spika imeweka uwiano ambao unafuatwa katika kupanga ratiba ya maswali ili kila Mbunge apate haki yake. Wako mafundi hapa wanaandika maswali 100 na wapo wengine sio mafundi sana wanaandika mawili lakini kila mmoja lazima apate haki yake. Kwa hiyo, sio kweli kwamba Serikali inachelewesha majibu, majibu yapo ila lazima tufuate utaratibu wa namna ya kuyajibu ili kila Mbunge anufaike na ratiba inayopangwa hapa.



Kuhusu huduma kwa Waheshimiwa Wabunge, masuala ya Wabunge wa Muungano wanaoishi Zanzibar washughulikiwe moja kwa moja na Ofisi ya Waziri Mkuu, jambo hili limeelezwa kwenye hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Ali Said Salim, aliyechangia mwishoni anasema uchaguzi wa ndani ya Bunge uwe kwa mafungu yaani wanawake wajichague wenyewe, Wapinzani wenyewe. Haiwezekani kwa sababu hawa wanawakilisha Bunge zima na wanapokwenda kule kwenye Bunge la Afrika, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, haendi kuwakilisha wanawake, anawakilisha Bunge hili, hilo moja kwa moja haliwezekani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Bakari Mbonde, amezungumza kwa uchungu sana juu ya taarifa ile ya Mkaguzi. Ninachotaka tu kumwambia Mheshimiwa Bakari Mbonde, usishikilie shilingi yetu jambo hili lipo kwenye vyombo vya Serikali vya uchunguzi linafanyiwa kazi. Kwa hiyo, shilingi yetu baadaye usiishike. *(Makofi/Kicheko)*

Kuhusu mgawanyo wa mamlaka za dola, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa wamesema kwamba Bunge na Mahakama ziwe huru kuandaa na kusimamia Bajeti zao. Hoja ilikuwa inasemekana Katiba Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu ndio mkubwa wa Bunge, sio kweli.

Mheshimiwa Spika, Afisa Mhasibu wa Akaunti ya Ofisi yetu ni Katibu wa Bunge sio Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu na Bunge lina *vote* yake ninyi wote mnajua na Mtendaji Mkuu kama nilivyosema ni Katibu Mkuu na Bajeti yetu inapitishwa na Tume yetu wenyewe sio Ofisi ya Waziri Mkuu, Tume yetu ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Spika. Haya mambo lazima yafahamike, haya mambo tunafanya wenyewe hapa, Bajeti tunapanga wenyewe kwa uwiano kutokana na fedha ambazo zimetengwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ziko hoja nyingine ambazo zinasema baadhi ya vikao vya Kamati ya Bunge zifanyike Zanzibar. Hili ni jambo linalokwenda na Bajeti kwa sasa kwa kweli kwa Bajeti hii hatuna uwezo kwa sababu gharama zake hatukuziweka tuendelee na utaratibu huu tutaangalia kama uwezo wa Serikali utakuwepo, baadaye tutafanya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paul Kimiti amependekeza kwamba sera za Serikali ziandaliwe mikakati ya utekelezaji. Nakubaliana naye, sera zote zinawekewa mikakati ya utekelezaji na juzi tumewapeni Kamusi ya Sera ili angalau Waheshimiwa Wabunge mjue hata sera zenyewe zipo ngapi zinazotumika hivi sasa. Kwa hiyo, hata ninyi kwa sababu mnakutana na Mawaziri mbalimbali katika Kamati mtawauliza juu ya mikakati hiyo ambayo ipo tayari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi za Mawaziri wanapotembelea Majimbo ya Vijiji zitekelezwe. Haya yalisemwa na Mheshimiwa Alhaj Ahamadi Mpeme. Mawaziri wote wamepewa maelekezo kuhakikisha kuwa wanatekeleza ahadi zao kwa wananchi kama ilivyo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kadri uwezo unavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoweza kusema mwanzo michango ya Waheshimiwa Wabunge ni mingi, lakini nimeainisha mambo machache ambayo ningeweza kuchangia yaliyo ndani ya uwezo wa Ofisi ya Waziri Mkuu

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema machache ambayo yamesemwa na Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, suala la Wabunge wanaoteuliwa na Rais halipanui demokrasia. Nataka tu kumwambia rafiki yangu kwamba suala hili la Rais kuwateua Wabunge ni la Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, anasema tabia ya kupingana pingana kwa Wabunge ndani ya Bunge isiruhusiwe. Nafikiri anawapa *message* wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba tena kurudia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mbalimbali na naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani nyingi sana kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia kwa njia yoyote ile. Lakini pia na wale ambao hawakupata nafasi kwa sababu nina hakika muda haukutosha, kama tungekuwa na siku nyingi zaidi, nina hakika wengi zaidi wangechangia.

Mheshimiwa Spika, waliopata nafasi ya kuchangia hapa Bungeni kwa kusema ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa George Lubeleje ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia hoja hii, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Methew Ole-Timan, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Profesa David Mwakyyusa, Mheshimiwa Hamisi Jumanne Nguli, Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Kidawa Hamisi Saleh, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo na Mheshimiwa Grace Kiwelu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Teddy Kassela-Bantu, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Alhaj Ahamadi Mpeme, Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Khadija Kusaga, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Omar

Mwenda, Mheshimiwa Robert Mashalla, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Semindu Pawa na wawili wa mwisho ni Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Habari na Siasa) na Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao na naomba niwataje kuwa ni Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Alhaj Shawaji Abdallah, Mheshimiwa Shamim Parkan Khan, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura na Mheshimiwa Captain Theodos Kasapira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, Mheshimiwa Mussa Lupatu, Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Martha Wejja, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Kanali Feteah Saad Mgeni, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Sumri Mohammed, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mheshimiwa Mohammed Ali Said, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Sharifa Mbaruk Khamis, Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Ali Karavina, Mheshimiwa Sijamini Mohammed Shaame na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa yote ambayo yameshauriwa na Waheshimiwa Wabunge na kama walivyoeleza Mawaziri waliosaidia kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge yatafanyiwa kazi na Serikali, ofisi yangu itayaratibu, lakini kila Waziri hapa alipo pia amekuwa akichukua *notes* za yale mambo ambayo yanahusu sekta yake ili wayajibu baadaye katika hotuba zao zinazokuja.

Napenda niwashukuru sana Mawaziri wawili Mawaziri wa Nchi, katika Ofisi yangu ambao wametoa majibu ya kina. Naamini baada ya majibu hayo wamenirahisishia sana kazi yangu na napenda niwashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo napenda nisemee maeneo machache yaliyobaki, lakini hata hivyo nina hakika hatutaweza kumaliza yote kama nilivyosema kwa hiyo, mengine itabidi bado Mawaziri waendeleo kuyatolea maelezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Mtwara Corridor*, kwanza napenda nikubaliane kabisa na Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia juu ya *Mtwara Corridor* wakiongozwa kabisa na Msemaji wa kwanza Mheshimiwa Thomas Nyimbo. Serikali inakubaliana kabisa na umuhimu wa *Mtwara Corridor* na kwa kweli ni *corridor* muhimu si kwa nchi yetu tu lakini inaunganisha na nchi zingine ambazo tunapakana nazo katika eneo hilo na ni *corridor* au ukanda ambao nchi hizo zingine pia zinakubali ni muhimu sana kwa maendeleo ya haraka ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa upande wa suala la mkaa wa mawe wa Mchuchuma, kama Wizara ya Nishati na Madini ilivyoeleza na nina hakika wataendelea kutoa taarifa ya maendeleo labda wakati wa hoja yao. Wizara inaendelea kujadiliana na wawekezaji wahusika kwa sababu kama tulivyoelezwa ni vema tukawa waangalifu ili tusije kuweka mradi ambao utakuwa mzigo sana kwenye uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, walikuwa wanaendelea kushauriana na kama alivyosema Waziri wakati ule inaonekana kwamba kuna maelewano mazuri yanaelekea kufikiwa. Kwa hiyo, hilo litakapofikiwa kwa kweli miradi ya *Mtwara Corridor* itatekelezwa lakini bado miradi mingine ingeweza kuanza kutekelezwa ingawa wahusika wao wangependa waanze na huu wa umeme ambao ndiyo tunajadiliana nao. Kwa mfano, moja ambalo wanajadiliana nao ni uwezekano wa kuanzisha kutoa umeme kwa awamu badala ya kutoa *megawatt 400* zote kwa mara moja waweze kutoa labda 200 kwa mara moja na jinsi matumizi yanavyopanuka halafu waongeze hizo zingine. Sasa haya ndiyo baadhi ya mambo ambayo wanajadiliana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme Kusini, pia taarifa hii ilikwishatolewa na Wizara husika katika Bunge hili hili wakati wakijibu maswali na mradi wa *Mnazi Bay*, majadiliano kwa kweli ni kama yamekamilika na Serikali na wahusika wanaanza kujenga wakati wowote ili kuweza kupata umeme wa uhakika kwa upande wa Kusini.

Kwa suala la Songo Songo nalo pia lilielezwa na Wizara wakati walipokuwa wakijibu maswali kwamba kweli kwa *design* ya ule mradi umeme ambao unapatikana katika ule mradi ni ule ambao utatolewa katika vituo vile vya njiani. Gesi nyingine inakuja Dar es Salaam kwa ajili ya shughuli hizi zingine kama kutumia kwenye viwanda, kwenye nyumba na hata pia kuzalisha umeme, ndivyo mradi ulivyobuniwa tangu mwanzo.

Kwa hiyo, nadhani la msingi kama bado gesi hiyo ni kubwa kama inabidi kuelekezwa Kusini basi inabidi kutengeneza mradi mwingine upya. Lakini kwa mradi wa *Mnazi Bay*, mimi nina hakika ukikamilika na *Inshallah* na huu wa Mchuchuma ukafanya kazi hata huu wa Songo Songo kwamba uelekee Kusini itakuwa haina umuhimu. Lakini Wizara yetu ya Nishati na Madini itaendelea kutoa taarifa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ubinafsishaji, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia vipengele mbalimbali katika ubinafsishaji. Moja, ni kwamba Watanzania wameenguliwa, ndiyo lugha iliyotumika katika ubinafsishaji.

Jambo ambalo nina hakika Waheshimiwa Wabunge wanalijua, tulipewa taarifa hapa Bungeni ya makampuni mangapi ya umma yamebinafsishwa kwa Watanzania na kama tunakumbuka takwimu zile sehemu kubwa za makampuni mengi yamebinafsishwa kwa Watanzania wenyewe, sehemu kubwa zaidi imebinafsishwa kwa Watanzania ama Serikali kwa ubia na watu wa nje, sehemu kidogo ndiyo ambayo imebinafsishwa moja kwa moja kwa maana ya asilimia mia moja kwa watu wa nje na kwa kumbukumbu zangu kiwango kilikuwa kama asilimia sita.

Kwa hiyo hayo mengine yote ama tuko pamoja na watu wa nje ama ni sisi Watanzania wenyewe. Hiyo ni njia mojawapo ya kuonyesha kwamba Watanzania hatukuachwa pembeni.

Mheshimiwa Spika, njia ya pili, ni kwamba kwa yale makampuni ambayo labda yanaonekana ni makubwa na Watanzania uwezo wetu sisi wenyewe usingeweza kumudu kuyaendesha, Serikali ingeweza kutenga baadhi ya hisa kwa ajili ya Watanzania. Leo katika kampuni na mashirika ambapo Watanzania wana hisa kuna Watanzania kama laki moja hivi ambao wana hisa katika makampuni mbalimbali na hili nalo kwa kweli ni namna nzuri ya kuwahusisha Watanzania katika ubinafsishaji na pia kuwaingiza katika uchumi wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lilikuwa ni namna gani wafanyakazi wanapata haki zao katika mashirika haya yanayobinafsishwa na watu wamezungumzia sana hasa suala la *Tanzania Elimu Supply* (Shirika la Elimu....

**MBUNGE FULANI:** Vifaa vya Elimu.

**WAZIRI MKUU:** Shirika la Vifaa vya Elimu. Nataka niwaelezeni kwamba msimamo au utaratibu wa Serikali uko nyuma kwa makampuni ambayo yalikuwa yanafilisika. Utaratibu wa kisheria unaeleza kwamba madai ya mabenki kwanza yanalipwa na wenye hisa kama wapo na kadhalika, halafu watumishi wanakuwa mwisho.

Katika utaratibu ule unasema mtumishi anapata shilingi elfu nne, ndiyo anaondoka nazo lakini baada ya Serikali kuliangalia hilo pamoja na kwamba sheria yetu inasema hivyo Serikali iliamua kwamba hata kwa yale mashirika au makampuni ambayo yamefilisika angalau watu wapewe zile haki zao za msingi (*Statutory Benefits*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa mashirika yote kama 280 ambayo tumebinafsisha ukiacha mashirika machache ambayo hata hayafiki matano ambayo yalikuwa na Mikataba yao ya hiari, wote wamekuwa wakilipwa *statutory benefits* au haki zao za msingi zile ambazo mnapoingia Mkataba wa kazi ndiyo unasema nikikuachisha kazi au ukiacha kazi utalipwa haki hizi. Kwa hiyo, zile hata kwa mashirika ambayo yamefilisika imebidi Serikali itafute fedha kuwalipa wafanyakazi. Mashirika mengi

yamekuwa yakipata matatizo kwa sababu kama tunavyojua katika mashirika na wao wana utaratibu wa pensheni katika mashirika ya pensheni kama *PPF* na *NSSF*. Mashirika mengi sana yalikuwa hayalipi makato yale ya wafanyakazi, wafanyakazi wanakatwa fedha lakini fedha zile hazipelekwi. Fedha zile zisipopelekwa mnachajiwa riba na adhabu, Serikali imejikuta ili hao wafanyakazi wapate haki zao inatakiwa ilipe nadhani kitu kama bilioni 17. Hizo ni fedha ambazo ilibidi Serikali itafute.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili la *TES*, tangu mwaka 1992 lilikuwa halijapeleka hata shilingi kwenye vyombo hivyo vya pensheni ya wafanyakazi. Wafanyakazi wanakatwa lakini fedha zao hazikupelekwa huko. Kwa hiyo, inabidi Serikali itafute hizo fedha ambazo pamoja na adhabu na riba ilikuwa inavuka kama bilioni moja na laki sita hivi, lakini tumezungumza nao wametupunguzia punguzia nadhani itakuwa kwenye milioni kama mia tisa au bilioni moja. Lakini shirika hilo pia lina madai mengine, lina madeni yaliyolimbikizwa yanayozidi zaidi ya shilingi milioni mia nane na sitini na tano, lina hasara iliyolimbikizwa ya zaidi ya shilingi milioni mia nane na nne, lina madai yaliyoko kortini ya zaidi ya shilingi milioni mia tano. Serikali imelipa fidia kwa wafanyakazi walioachishwa bila utaratibu zaidi ya shilingi milioni 746, imelipa pia *PPF* zaidi ya shilingi milioni 700 kwa watu ambao wameachishwa pia bila utaratibu na imelipa shilingi milioni 60 kama malimbikizo ya mishahara.

Kwa mwaka mmoja uliopita shirika hilo wala lilikuwa halilipi mishahara ya wafanyakazi wake, ilikuwa ni *PSRC* inalipa. Kwa hiyo, eti hilo shirika ni safi sana, lina faida kubwa, kwa nini wafanyakazi wake hivi na hivi, hii ndiyo hali yenyewe. Lakini tumesema wote watapata haki zao za msingi (*Statutory Benefits*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, katika nyumba zilizouzwa wala hakuna zilizouzwa kwa magendo au kwa namna yoyote ya kinyume. Nyumba zao zote, kwanza nyingi sana zimepata bei kubwa sana kuliko zile bei za tathmini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo niseme kidogo juu ya uimarishaji wa majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama. Huu ni wajibu wa Serikali na ni lazima utekelezwe, tutaendelea kuimarisha majeshi yetu kadri uwezo wetu utakavyoruhusu. (*Makofi*)

Jeshi letu la Polisi ni Jeshi makini sana. Leo Tanzania katika Afrika tunajivuna kwamba ni Kisiwa cha amani, lakini sehemu mojawapo kubwa ni kwa sababu tuna Jeshi la Polisi linalofanya kazi yake vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jeshi hili halitumiki na Chama chochote wala haliwezi kufanya shughuli za kuonea mtu. Sasa nilifikiri pale walipoona kwamba Bajeti ya Jeshi hili imeongezwa wangepurahi, lakini kwa wale waliosikitika na kuwa na wasiwasi na mimi naanza kuwa na wasiwasi nao labda wana wasiwasi wa kwamba labda wao ni wahalifu wahalifu. Jeshi la Polisi wewe liachie lifanye kazi yake, wewe usiwe mhalifu, tii tu sheria za nchi, utaona ni Jeshi zuri ajabu. Wala hutapambana nalo, wala hutakaruzana nalo na litakulinda wala haliangalii wewe unatoka Chama gani, una rangi gani, una shughuli gani, mradi ni raia mwema. Lakini kama ukifanya vurugu, Jeshi la Polisi litakushughulikia bila kujali wewe unatoka wapi, una itikadi gani, una cheo gani au una umri gani.

Kwa hiyo, tafadhali sana naomba tushukuru kwamba angalau tunajitahidi kuboresha uwezo wa vyombo vyetu hivi vya dola ili vitusaidie na tutaendelea kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mbolea ni ....

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika siyo Mwenyekiti.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru Mama Anna Abdallah kwa kunisahihisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kilimo kimezungumzwa sana na kwa kweli mimi nakubaliana kwamba kilimo ni sehemu muhimu mno ya maisha yetu na jambo lolote likitokea katika kilimo ni lazima Waheshimiwa Wabunge washtuke. Kwa hiyo, huku kushtuka kwenu mimi sioni tatizo na nakubaliana na ninyi, lakini tatizo kubwa la kilimo chetu ni kwamba kinategemea mazingira ambayo hatuna uwezo nayo wa kuyadhibiti. Kilimo hiki kinategemea mvua tu kwa sehemu kubwa.

Mimi nina hakika kwa Waziri huyu huyu kama mwaka huu tutapata mvua nzuri mwakani tukikutana kwenye Bunge hapa tutampongeza sana kama tulivyowapongeza Mawaziri wengine kwa sababu kutakuwa na mazao ya kutosha. Lakini kama mvua haitanyesha kwa kweli ni vigumu sana Waziri wa Kilimo na Chakula upate sifa, lazima utasemwa. Lakini nina hakika tunafanya kila ambalo tunaweza ili kuendelea kuboresha kilimo chetu.

Kwa miaka miwili hivi sasa tumejitahidi sana kuelekeza raslimali kwenye kilimo, lakini hazijatoshwa kwa sababu kilimo kinahitaji raslimali nyingi sana. Umwagiliaji tu wenyewe ukisema kwamba tumwagilie kwa kiwango tunachokihitaji ni fedha nyingi ambazo hatuwezi kuwa nazo.

Mheshimiwa Spika, nina hakika Waziri atakuja kueleza mipango aliyonayo ya kilimo, mipango ya mbolea, Mikoa itakayopata mbolea na kadhalika. Lakini kwa ile mbolea ya mwaka 2003, mimi nakubaliana kabisa na aliyoyasema Mheshimiwa Anne Makinda wala siyo mageni, hili tulilizungumza hata hapa Bungeni kwamba mbolea ile ingechelewa, tulijua kabisa lakini tuliona jambo hili tusipolianza hatutalianza kwa sababu ni jambo gumu. Tulidhani ni vema tulianze ili mwaka unaofuata sasa tuwe tunaendelea kuliboresha kuliko kila mwaka tungekuwa tunaogopa.

Kwa hiyo, tulilianza kwa kweli tukijua bado lina matatizo na hata sasa bado tutaendelea kuwa na matatizo lakini tuna hakika kabisa mwaka huu yatapungua kuliko mwaka jana. Hapa nataka niwaambie lengo letu baadaye kwa mambo muhimu kama mbolea na vitu kama hivi *Sulphur* angalau tuwe na ruzuku hata kama ni ndogo kwa nchi nzima. Kwa hiyo, huku tunakoanza kwa Mikoa michache ni ili tuanze kupata ujuzi kwa sababu hebu fikiria kwa Mikoa minne tumepata matatizo hivyo je, tungefanya nchi nzima si tungepata matatizo makubwa zaidi? Kwa hiyo, tunataka tupate ujuzi ili jinsi

tunavyopanua polepole basi mpaka tutakapomaliza kwa nchi nzima tuwe na uwezo wa kuweza kulifanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo, pia inahudumiwa kama mazao, wala hakuna ubaguzi hasa kama ulivyohisiwa. Kwa mfano, madawa yote ya magonjwa ya milipuko huwa tunatoa bure, kama kuna magonjwa ya milipuko kama *CDPP* hata *Foot and Mouth Disease* au *Lack Water* na kadhalika ikilipuka kwa kweli Serikali inajitahidi kutafuta fedha ili kutoa dawa ili mifugo yetu isiungamie. Lakini kwa mwaka huu na bila shaka miaka inayoendelea tutaendelea kujitahidi hivyo hivyo. Katika Mfuko wa Pembejeo kuna kiwango ambacho kitatumika kwa upande wa dawa za mifugo ili kupunguza makali ya dawa za mifugo hasa za uogeshaji. Kwa hiyo, Mfuko huu pia utahudumia mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu, Mpango wa Elimu ya Sekondari (MMES) Waziri wa Elimu na Utamaduni, atakuja kutoa maelezo mazuri zaidi lakini kama tulivyosema nataka tu nisisitize lengo letu ni kuhakikisha kwamba angalau asilimia hamsini ya watoto wa *primary school* wanapata nafasi ya kwenda sekondari. Sasa hii umuhimu wake ni nini? Umuhimu wake ni kwamba hata yale maeneo ambayo hayana sekondari sasa yatapata umuhimu wa kujengewa sekondari kwa kushirikiana na wananchi. Kwa hiyo, mambo mawili hapa ni muhimu sana, nataka Waheshimiwa Wabunge kila mtu akienda kwenye Jimbo lake aende nalo.

La kwanza, ili kupata sekondari nyingi kwa sababu tunalenga asilimia ya watoto waliopo shule za msingi ni lazima watoto wetu wote waende shule za msingi. Kama una watoto wachache wanaokwenda shule za msingi maana yake na sekondari zitakuwa chache. Kwa hiyo, tupeleke hasa sisi wafugaji, tupeleke watoto wote shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi zamani tulipokwenda shule tulikamatwa. Sasa kama inabidi utaratibu huo uendelezwe kukamata watoto wenye umri wa kwenda shule waende shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni wananchi kushiriki kwa sababu MMES hauwezi kujenga sekondari kuanzia mwanzo mpaka mwisho, wananchi lazima tushiriki.

Napenda nishukuru sana wananchi ambao wameshiriki katika ujenzi wa shule za msingi katika Mpango wa MEM. Sasa naomba uzoefu ule ambao tumeupata katika MEM tupeleke kwenye MMES. Wale ambao walitumia vizuri sana zile fedha kwa kushirikiana na nguvu za wananchi walijenga madarasa mengi, wengine mara mbili, wengine mara mbili na nusu, wengine hata mara tatu. Lakini wale waliong'ang'ania tu ile tarakimu waliyopewa kutoka Wizarani wamejenga idadi ile ile ya madarasa, sasa leo bado wana upungufu mkubwa. Sasa kwenye sekondari naomba tutumie uzoefu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo ya utendaji na mahusiano ambayo yameelezwa hapa. Haya hayawezi kujibiwa hapa ila Serikali itayafanyia uchunguzi. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, mgao wa fedha Kimkoa nataka tu nirudie tena hili jambo, haiwezekani kukawa na Serikali ambayo inataka kuonea sehemu fulani ya nchi. Tunagawa fedha, tatizo ni kwamba tu hazitoshi, lakini kwa kweli tunajaribu kuzigawa kwa mahitaji ambayo mengine ni ya wazi. Kwa mfano, nilikuwa naangalia Mkoa wa Mwanza ulitolewa kama mfano kwa sababu unaonekana una fedha nyingi, lakini Mkoa wa Mwanza fedha za ndani za maendeleo zilizotengewa ni shilingi milioni 664 tu, bilioni 4.5 ni fedha za nje kwa miradi ambayo iko pale.

Kwa hiyo, mara nyingine hizi takwimu zinaweza zikatudanganya. Lakini pia tusiangalie tu zile takwimu zilizoko kwenye Mkoa tuangalie pia ujumla, maana zote ni fedha za wanalipa kodi tuangalie tu katika ujumla wake.

Niseme tu Mkoa wa Shinyanga kwa mfano, kwa sababu tu ulitolewa mfano hapa iko mifano mingi tu ningeweza nikasema. Mkoa wa Shinyanga kwa mfano, kuna miradi ya maji ambayo inagharimiwa na Waholanzi shilingi bilioni 53, lakini kuna nyingine bilioni 42 nadhani ndiyo pamoja na hizo za Waholanzi. Kuna miradi ya umwagiliaji zaidi bilioni moja, kuna miradi ya UKIMWI karibu milioni 380. Kwa hiyo, ukiangalia tunaweza tukachukua tu zile tarakimu zinazoonekana chini ya Mkoa lakini ukiziangalia katika upana wake utaona kwamba tumejitahidi sana kutawanya rasilimali kadri inavyowezekana. Lakini lengo langu hapa nataka kuwambieni hakuna ambaye anataka kuona kwamba kuna mahali panaonewa kwa sababu wote ni Watanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la mrabaha namshukuru sana Mheshimiwa Waziri amelijibu kwamba tunayo ile Kamati inayoshughulikia jambo hilo. Lakini katika mrabaha kwa wale ambao wanajua Kiswahili ni mrabaha wale ambao hawajui Kiswahili ni mrahaba. Kwa mrabaha nataka niseme mambo mawili.

Jambo la kwanza ambalo nina hakika jawabu lake tatalipata katika Kamati ni kama tunapata kwa kweli halali yetu katika madini haya sasa Kamati ile inafanya kazi vizuri nadhani tuwasubiri. *(Kicheko)*

Jambo la pili, ambalo mimi ningependa sana tuliendee kwa uangalifu ni hili la kusema hivi sisi Wapare tunapata nini? Sasa mimi nasema tujifunze pia kutoka katika nchi zingine hili jambo ni la siku nyingi, wala si la leo wamejaribu kuliangalia huko nyuma wakaona wasilichokoze. Tukianza na rasilimali hizi kwamba zinapotoka kwangu mimi ninapata nini, msidhani ni dhahabu tu peke yake, wa gesi watakuja wadai chao, wa maji huu umeme wote tunaotumia katika nchi hii ni wa maji na wao watadai, wa samaki watadai, wenye Mlima Kilimanjaro watadai, wenye bahari watadai samaki zao, kwa hiyo tutaifikisha nchi mahali ambapo tutakuwa na ugomvi wenyewe ndani kwa ndani. Kwa hiyo, ndiyo nasema hili jambo lazima liendewe kwa uangalifu mkubwa. Tujifunze yanayotokea Nigeria, Nigeria kuna mapambano yasiyoisha Kaskazini na Kusini kwa sababu hizo. Mimi ningeomba sana haya mambo tuyaendee kwa uangalifu unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru sana yule bwana aliyetusaidia kufunga valve ya mafuta wakati tulipopata tatizo la moto pale Ubungo. Yale yaliyoelezwa kwamba amepata shilingi 200,000/= si kweli, mpaka sasa hajapewa chochote, lakini

hajapewa chochote si kwa sababu hapewi, *TANESCO* walishajiandaa siku nyingi lakini Wizara kwa kushauriana na watu wengine waliona jambo hilo lifanyike kwa njia nzuri zaidi na fedha atakazopewa ni nzuri tu ni milioni kadhaa kwa hiyo, si mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije suala la Muungano. Nashukuru sana kwamba wote hapa tunazungumza kwamba Muungano ni muhimu. Muungano ni muhimu na Muungano lazima tuulinde na kuulinda Muungano ni pamoja na kuyatukuza Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, hapo lazima tukubaliane, bila kutambua hilo maana yake unataka kuweka dosari kwenye Muungano.

Nataka kusema tu kwa kifupi yapo matatizo ndani ya Muungano wetu tumejitahidi kuyatatua mengi sana na mengine bado yapo na hata hayo mnayoyaona nyie tukiyatatua yataokea mengine hata tusingekuwa na Muungano hata katika nchi si kuna matatizo. Kwa hiyo, hayo matatizo ni maisha tu ya kawaida jinsi hali za maisha zinavyobadilika matatizo yataendelea kujitokeza. Kubwa linalotakiwa ni utaratibu wa kuyatatua.

Mheshimiwa Spika, tuna Tume yetu sasa ya pamoja ya fedha itasimamia mengi ya matatizo hayo. Tatizo letu kubwa ni la umaskini wala si nani anamwonea nani, ni tatizo tu la umaskini. Kwa hiyo, tupigane kupambana na umaskini pande zote za Muungano na mimi nina hakika kama tutaendelea vizuri jinsi uchumi wetu unavyokua mengi ya haya yatakuwa ni historia tu yatafutika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la Utawala Bora. La kwanza katika Utawala Bora ni rushwa, katika Serikali hii sijawahi kusikia hata siku moja kwa mtu yeyote kuanzia Mheshimiwa Rais na kuteremka chini kwamba hakuna rushwa nchini, hatujawahi kusema hivyo na wala sijawahi kusikia hata zile nchi ambazo wanasema zina zile alama karibu na kumi maana yake hata hiyo Finland rushwa ipo kidogo.

Kwa hiyo, hatujawahi kusema hakuna rushwa tunachosema ziko jitihada za wazi za kupambana na rushwa. Tunachosema ziko juhudi za wazi zimeonyesha matunda za kuelimisha wananchi juu ya haki zao na juu ya rushwa. Tutaendelea na kazi hiyo na wala hiyo kazi haina mwisho tutaendelea nayo wala hatutarajii kwamba kuna siku eti nchi hii au dunia hii kuna nchi itafikia mahali kwamba hakuna rushwa hata kidogo haiwezekani.

Kwa hiyo, naomba sana wananchi tuendeleo kupambana na rushwa. Utawala wote utaendeleo kupambana na rushwa popote pale tutakapopata uthibitisho wa rushwa hatua zinazopaswa zitachukuliwa na viongozi wetu hasa Wakuu wa Wilaya wataendeleo na taratibu zao zile katika kila Wilaya za kupambana na rushwa na wataendeleo na Kamati zao za kudhibiti matatizo haya. Ubadhirifu nashukuru sana kuna sehemu hapa zimezungumzwa kuna ubadhirifu zitafuatiliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutii sheria maana tunazungumza Utawala Bora. Utawala Bora siyo Serikali tu inayohusika hata wananchi na hata sisi viongozi na sisi tutii sheria, usipotii sheria utapambana na tatizo sasa na ile nayo inaharibu Utawala Bora. Sisi tungependa mambo yaende vizuri kwa hiyo kila mmoja atii sheria. Ukisikia mtu anasema nimepigwa na Polisi sasa kuna wakati Polisi nao wanavunja Utawala Bora,

lakini kuna wakati ambapo mwananchi naye au kiongozi au mtu yeyote naye anaharibu Utawala Bora, sasa katika hali ile lazima kunakurekebishana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utendaji wa Serikali. Utendaji wa Serikali nao lazima utii Utawala Bora. Serikali ni chombo ambacho kina vyombo ambavyo vina mabavu lakini ni lazima itumie vyombo vyake kwa *style* ambapo inalinda Utawala Bora. Namshukuru sana hata na *IGP* amewaeleza Polisi wake kwamba lazima watumie nguvu ile ambayo inaruhusiwa katika kazi zao siyo nguvu ya ziada. Lakini usije ukatarajia kwamba eti Polisi anakwambia simama, husimami, unadhani atageuka aondoke zake, hapana, akikwambia simama na wewe simama maana huo nao ni Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Utawala Bora timu hii ya Mawaziri hapa nataka tu niseme ni timu moja kama timu ya mpira. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge karibu wote mliochangia mmesifu juhudi mbalimbali ambazo zinafanywa na Serikali kwa kweli zimefanywa na timu hii chini ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa.

Mimi Waziri Mkuu kama ingekuwa timu basi ni *team manager* wao. Kwa hiyo, kama kuna mafanikio yameonekana ni kwa sababu tuko kama timu moja. Sasa katika timu moja kila mtu ana eneo lake, tumecheza na nadhani mafanikio haya yametokana na kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa wako Mawaziri ambao tumesema wamefanya vizuri wengine hatukuwataja lakini nataka tu niseme kwa kweli kazi yote ni ya timu moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaelezeni kilichotokea ni kwamba tulipofanikiwa kuingia kwenye *HIPC* kwa sababu raslimali zetu hazitoshi tuliama maeneo fulani ndiyo tuyape kipaumbele, Huduma za Jamii, Elimu, Afya, Maji na barabara. Kwa hiyo, maeneo hayo tuhakikishe ndiyo yanapata uwezo zaidi kuliko yale maeneo mengine. Kwa hiyo, wote tunafanya kazi kwa pamoja kama timu moja.

Mheshimiwa Spika, siku moja nilisoma nadhani ilikuwa Katuni ya Chezo, alirudi nyumbani anasikitika sana, mke wake akamuuliza vipi leo mbona unasikitika sana, akasema nimetolewa kwenye timu yaani ameondolewa kwenye timu, akamwambia kwa nini, akasema kocha alikuwa anachukua tu wale ambao walikuwa wanafunga magoli na mimi nilikuwa golikipa. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, yule kocha alishindwa kutambua kwamba huyu golikipa hawezi kwenda kufunga goli kule kwenye upande wa pili. Lakini kumbe mchango wake ni mkubwa katika ushindi. Kwa hiyo, sisi wote hapa tunacheza kwa pamoja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu sasa juu ya madai ya watumishi mbalimbali hii nayo ni sehemu ya Utawala Bora. Hapa niseme huko nyuma tulikuwa na madai mengi sana ya Polisi, ya walimu, ya wanajeshi, ya watumishi wengine na hata watu ambao walikuwa wametoa huduma nyingi sana kwenye Serikali. Mtakumbuka tulikuwa na

madai nadhani ya ndani kama bilioni 600 hivi tumejitahidi sana kuyalipa madeni haya. Kabla ya mwaka 2000 walimu tulikuwa tumbakiza shilingi bilioni moja na kitu kidogo na mimi walikuja kuniona *CWT* tuhakikishe zile fedha zimelipwa. Kwa hiyo, kwa kweli si kwamba madai haya ya walimu yamepuuzwa muda wote tumejitahidi sana kuyalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa bahati mbaya imetokea sasa kuna madai mengine makubwa. Sasa nataka niyasemee haya yametokana na sababu moja kubwa ni sababu ya mafanikio ya MEMEM. Katika MEMEM tumeajiri walimu karibu 28,000 katika miaka miwili na nusu hivi na mwaka huu tutaajiri zaidi ya walimu 15,500 sasa huku kuajiri kwa mara moja nako kumesababisha tatizo, lakini hii ni sehemu ya mafanikio. Hiyo ni sababu moja tu, sababu ya pili, inawezekana pia kuna uzembe katika kuhakikisha walimu wanapata haki zao na sababu ya tatu, inawezekana hata kukawa na ubadhirifu na wizi katika fedha zinazokwenda. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hizi sababu zote tatu itabidi zifanyiwe kazi. Kwa sababu ya hili la kwanza sasa nataka niwaambieni Wizara ya Fedha imetenga fedha shilingi bilioni 9 kwa ajili ya madai haya ya walimu. Fedha hizi zilitengwa kwa sababu hiki ndicho kiwango ambacho kimehakikiwa na nataka kuwahakikishieni kwamba fedha hizi zatalipwa mara moja katika mwezi Julai, 2004.

Kwa hiyo, Waziri wa Fedha ninakuagiza pamoja na Waziri wa TAMISEMI, mhakikishie fedha hizo walimu wanazozidai ambazo zimehakikiwa wanazipata pamoja na mishahara yao ya mwezi Julai, 2004. Dalili ni kwamba kuna madai zaidi. Madai haya zaidi yaanze kuhakikiwa mara moja na yale yatakayohakikiwa yatalipwa kutokana na *contingency fund* ya Hazina. Kwa hiyo, tunataka kwa kweli tuhakikishe madai hayo ya walimu tumeyamaliza. *(Makofi)*

Jambo la pili, ambalo Serikali inafanya hivi sasa ajira ya ualimu ina mlolongo mrefu sana. Wizara ya Elimu na Utamaduni inawaajiri inawapeleka TUMITAA, TUMITAA inawapeleka kwenye Halmashauri, Halmashauri inapeleka walimu kwenye kila shule, Mwalimu Mkuu anatoa ripoti kwamba mwalimu aliyeletwa amefika anarudisha habari kwenye Halmashauri, Halmashauri inapeleka TAMISEMI waliofika ni hawa, TAMISEMI inapeleka Utumishi, Utumishi ndiyo inapeleka Hazina. Sasa jambo la pili tutakalofanya tutafanyia kazi mlolongo huu tuone namna ya kuufupisha. *(Makofi)*

Jambo la tatu, kwa yale maeneo mawili mengine niliyosema Wakuu wa Mikoa wako hapa, ninatoa agizo wakahakikishe wanakwenda kupeleka timu za kuchunguza katika Halmashauri za Mikoa yao kwanza kwa kuchukua *Warrant of Funds* fedha zote ambazo zimepeleka wakasema ni malipo ya walimu kama zililipa walimu na waliolipwa tunawataka kwa majina. Tarehe 31 Julai, 2004 taarifa hizo zifike kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kama kweli kuna watu ambao wamekula hizo fedha za walimu mimi nasema afadhali wajisalimishe mapema. Kama Halmashauri zimetumia hizo fedha kwa shughuli za Halmashauri siyo za kuwalipa walimu, Mkurugenzi na Afisa

Elimu watachukuliwa hatua na Halmashauri husika itakatwa hizo fedha na Hazina. (Makofi)

La nne, katika jambo hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu naye anaunda Tume yake ya kuchunguza jambo hili na Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa taarifa ndani ya Bunge hili katika Bunge la mwezi Oktoba na Novemba, 2004. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nizungumze jambo moja la mwisho. Nataka nigusie sasa hotuba ya rafiki yangu Kiongozi wa Upinzani hapa Bungeni, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare.

Mimi na yeye ndiye tulitoa hotuba, hotuba yangu ilikuwa inaonyesha Serikali imefanya nini na tutafanya nini katika mwaka unaokuja. Kwa wale waliosikiliza hotuba yake sijui kama ilieleza kama wao Wapinzani wangepata Serikali wangepanya nini, mimi sijui kama ilikuwepo. Hotuba yake ilikuwa tu inalaumu Serikali na kwamba haikufanya jambo lolote na kwamba Bajeti aliyotoa Mheshimiwa Waziri Fedha haitekelezeki ni porojo tu ni kuwauzia wananchi mbuzi kwenye gunia.

Sasa mimi nataka kumhakikishia rafiki yangu Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, kwa sababu wakati mwingine huwa anajiita Waziri Mkuu Kivuli hata ungekuwa kivuli kwa kweli hiyo hotuba yako haifanani na ya kivuli cha Waziri Mkuu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka tu kumwonyesha kwamba nini tumefanya kwa sababu alikuwa anatuponda kwamba hatujafanya lolote. Nataka tu nimpe mifano michache ya pale kwake Bukoba. Nitoe mfano tu kwa mfano, MEM baada ya uchaguzi wala sisemi ya kabla ya uchaguzi, kwa hiyo, tangu mwaka 2001 na kuja mpaka sasa mwaka 2004. Kwa upande wa MEM, Mkoa wa Kagera umepata shilingi bilioni 12.3. Halmashauri ya Bukoba imepata shilingi milioni 477, Road Fund Mkoa wa Kagera umepata shilingi bilioni 2.8, Halmashauri imepata shilingi milioni 483 na zaidi Basket Fund Mkoa wa Kagera umepata ziadi ya shilingi bilioni 2.5, Halmashauri ya Bukoba imepata shilingi milioni 785 na zaidi hizi ni fedha ambazo zimeenda kwenye Halmashauri hatuzungumzi zilikwenda Mkoani kwa miradi mingine. Iko miradi mingine tu mikubwa ya barabara, iko Miradi ya KAEP inasaidia shughuli mbalimbali za wananchi.

Sasa akisema Serikali haijafanya lolote sijui alitaka ifanyeje. Kijijini kwake anakotoka katika Kata ya Kibeta ndiyo anatoka huyu Mheshimiwa Mbunge, shule ya Msingi ya Kibeta mwaka 2002 imejengewa madarasa matatu na MEM na mwaka 2003 imejengewa madarasa mawili ya MEM, *capitation* wamepokea zaidi ya shilingi milioni 11 hiyo ni shule moja nampa ile shule yake ya pale kijijini kwake, kuna wanafunzi 10 pale wanasomesha kwa utaratibu huu wa Serikali Elimu ya Sekondari kutoka kwenye hiyo kata yake.

Sasa akisema kwa kweli Serikali haijafanya lolote tunapata matatizo sana kukuelewa Mheshimiwa Mbunge. Inawezekana barabara kubwa kama ya Mtukula-Muhutwe- Kigoma hata hii kweli haionekani barabara ya lami inakata kabisa Mkoa ule

katikati! Sasa haya yote kweli ukizungumza hotuba ya namna ile kwa kweli hutaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nadhani inawezekana tatizo ni lile alilolisema kwamba anakimbia watu ambao wanakwenda nyumbani kwake sasa haoni haya.

Kwa hiyo, mimi ningekuomba sana Mheshimiwa Mbunge wewe fika tu kule Jimboni mpaka kijijini, sisi tunaendelea kuchapa kazi na tutaendelea kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi na Serikali hii ni sikivu, yote mliyotushauri tumeyapokea na tutayafanyia kazi na tutajitahidi kabisa kutoa huduma kwa wananchi kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, walisema hii ni Bajeti ya uchaguzi, lakini Bajeti zetu mbona zote ziko hivi hivi, zote ni nzuri tu zinahudumia wananchi vizuri na mimi nina hakika tutakapofika kwenye uchaguzi mambo haya yatatuvusha *inshallah*. Naomba Waheshimiwa Wabunge watupe hizo fedha tukazifanyie kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mjadala sasa wa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu umekamilika. Katibu atatusomea *agenda* inayofuata. Lakini namna ya kuidhinisha maombi yake ni kwamba tukimaliza kupitisha kifungu kimoja kimoja tukiwa katika Kamati, Bunge litarudia halafu Mheshimiwa Waziri Mkuu au mmojawapo wa Mawaziri wake atatoa taarifa kwamba Kamati imepitia vifungu vyote na imevipitisha. Halafu ndiyo ataomba Bunge liidhinisha Makadirio ya Wizara hiyo, hapo ndiyo tutapiga kura ya kukubali au kukataa. Kwa hiyo, sasa hivi tuendeleo kama nilivyoeleza. Katibu hatua inayofuata.

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **Matumizi ya Kawaida**

#### **Fungu 25 - Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... .. 1,160, 772,800/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kitabu kimeandikwa kwa Kiingereza, Kanuni zetu zimeandikiwa Kiswahili, kwa hiyo, tunachofanya *Sub Vote* ndiyo maana yake kifungu kwa maana ya Kanuni. Kwa hiyo, tunapitisha kila *Sub Vote* peke yake. Sasa nawahoji wanaoafiki *Sub vVote* 1001 ipitishwe. Hapana, Mheshimiwa Bakari Mbonde. Kama kuna mwingine naye ajitokeze ili ...

Eeh Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi na Mheshimiwa Lucas Selelii, nafikiri. Sawa anza Mheshimiwa Bakari Mbonde.

Nikumbushe taratibu za Kamati msemaji hawezi kuzidi dakika 5, mwisho dakika 5. Endelea.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitarajii kutoa shilingi. Kifungu cha 1001 Mshahara wa Waziri Mkuu. Sitarajii kutoa shilingi ila ile sindano ya ganzi aliyonipiga Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera) Mheshimiwa William Lukuvi, inanipa matatizo kidogo kuhusiana na suala nililolizungumza asubuhi.

Nilikuwa naomba tu anisaidie kwamba suala lile la ubadhirifu wa fedha za umma lipo Serikalini ngazi gani? Ofisi ya Rais, PCB au kwa Adadi Rajabu au Ofisi ya Waziri wa Nchi, Sera? Kwa sababu hata aliyefuja hizo fedha alikuwepo Serikalini.

Lakini vile vile kama taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilikuwa sio sahihi, je, kiongozi huyo atapelekwa mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili aweze kushughulikiwa kisheria? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Hoja aliyoitoe asubuhi Mheshimiwa Bakari Mbonde, tunaifahamu na ilifikishwa kwenye vyombo vya dola kati ya PCB na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiko jambo hili liliko likichambuliwa ili kuthibitisha mashtaka au vinginevyo.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anataja waliochangia. Nilichangia kwa maandishi na hoja yangu ilikuwa kwa sababu yeye ni msimamizi wa shughuli za Serikali humu ndani na uko nje kwamba kuna wakulima ambao wamedhulumiwa fedha yao ya STABEX. Najua lile la walimu ameshughulikia kama ambavyo anahusika na nina uhakika hata hili liko chini ya uwezo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka tumekuwa tukileta hoja hapa na maelezo binafsi na Serikali ilikuwa ikitoa kauli. Katika Bajeti iliyopita tuliambiwa kwamba wakulima hawawezi kupewa fedha mkononi kwa vile watalewa. Kwa hiyo, kinyume chake fedha zile zikatumika kujenga barabara katika maeneo ambayo yalikuwa yanahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa asubuhi lilikuweco swali na unavyokumbuka alivyouliza ilitokea kwenye semina na Mawaziri wale wale wakawa wanatupiana mpira. Sasa mimi nina uhakika kwa sababu Waziri Mkuu yuko hapa na namshukuru kwa jinsi ambavyo amezungumzia lile la elimu na hili akitupatia ufumbuzi na mwelekeo nadhani inaweza ikatusaidia. Sasa kabla hatujasema na yeye achukue mshahara labda pengine na

yeye aonje uchungu kwa kupunguziwa mshahara kama wakulima walivyonyimwa halafu wakanyimwa na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kwa maelezo hayo mafupi Waziri Mkuu atusaidie fedha zile ziko wapi, kwa sababu aliyekuwa anajibu swali hapa asubuhi ameeleza kwamba fedha sijui kuna watu wanazunguka Wilayani. Mimi nimefika Wilayani jana, hakuna mtu anazunguka kule na fedha zile haziko, Ujenzi na watu wa Ujenzi wako hapa tunataka msimamo wa Serikali fedha zile ziko wapi? Vinginevyo tuunde Kamati hapa twende tuone ziko kwenye mfuko, nani anazikwamisha? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala ambalo tumelizungumza mara nyingi sana hapa Bungeni. Kama alivyoeleza mwenyewe tumelitolea hata tamko rasmi. Naomba kwa ufupi sana nirudie baadhi ya yale niliyosema asubuhi na kuyapanua kidogo. Napenda nimhakikishie kwamba katika hotuba yangu ya Bajeti ni moja ya masuala ambayo nimeyashughulikia pia kutokana na Wabunge wengi sana kulizungumzia suala hilo.

Kuna mkataba kati ya Serikali ya Tanzania uliotiwa saina kati ya Wizara ya Fedha na Jumuiya ya Ulaya juu ya fedha hizi. Katika mkataba ule kuna kifungu chenye *Euro* milioni 10 ambacho kitatumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Kwa wakati huu fedha zile hazijawa *dispersed* bado ziko Benki. Lakini ameteuliwa *consultant* kuandaa mapendekezo ya barabara zitakazofaidika na fedha zile. *Consultant* yule bado yuko kazini hajaleta taarifa Serikalini. Tunatarajia kwamba ataleta taarifa Serikalini mwisho wa mwezi huu au mwanzo wa mwezi Julai.

Sasa kwa hiyo, hata mimi sina hakika ni barabara zipi zilizoingizwa. Mimi sina hakika kama mtaalamu huyu angekwenda Jimboni kwa Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, kwa njia ambayo pengine angeonekana akirandaranda barabarani. Kwa hiyo, mimi naomba hebu tupewe muda tulieleze tena suala hili katika Bajeti. Fedha zile zipo hakuna hata senti moja iliyotetereka na zitatumika kuanzia mwaka huu kutengeneza barabara hizo. (*Makofi*)

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nadhani kama alivyosema tumelizungumza mara nyingi. Mimi sio mwendawazimu wa kutaka kuchelewesha Bunge na shughuli zake, sasa hiyo ni mara nyingi. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari tuunde Kamati hapa mimi nitajisafirisha twende tukaangalie pale anaposema ili tuje tuelezane Wabunge kwamba Kamati hii ilichunguza fedha zile zote zipo? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani umenisikia, wale ambao hawana Kahawa ndio wanao-shout. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sidhani kama ni jambo la kuundia Kamati. Kwa sababu kumbukumbu zote zipo. Lakini Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi kama anataka kuthibitisha maelezo haya aende



Wizara ya Fedha, *EU*, aje Wizara ya Kilimo na Chakula watamwonyesha makabrasha yaliyopo. Sio jambo la kuundia Kamati.

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kifungu hicho cha 1001 Mshahara wa Waziri.

Nataka kupata maelezo katika hotuba ya Bajeti na hata katika hotuba yake yeye Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza namna ya hatua ambazo zitafanyika kwa ajili ya kuinua kilimo na hasa ameelezea juu ya mbolea namna gani ambavyo kodi imeondolewa kwenye mbolea na vitu vingine vya kilimo.

Lakini nimemsikiliza sana Waziri wa Fedha, nimemsikiliza hata yeye Mheshimiwa Waziri Mkuu hajagusia hata kidogo juu ya mbegu bora. Kama tutatoa mbolea, tutatoa vyote bila ya mbegu bora basi tutakuwa tunajidanganya hasa juu ya kuondoa kodi kwenye hizi mbegu. Mbegu hizi bado ni bei kubwa sana hasa ukiangalia jinsi wananchi wanavyoshindwa kuzinunua hasa hizi mbegu bora, *cagri* na zingine.

Sasa mimi naomba kama katika orodha hiyo mbegu haimo ya kuondolewa kodi. Mimi ningeomba Serikali iondoe kodi na itaje kabisa mbegu bora iondolewe kodi kama ambavyo mbolea imeondolewa kodi. Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kwamba mwaka 2003 kwa mara ya kwanza kwa miaka mingi sana ndipo Serikali ilipoamua tena kwa kuthubutu kweli kweli kutoa ruzuku katika mbolea. Tunaji-*restrict* katika mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini kwa sababu tulikuwa tunataka tujaribu kuangalia hivi tukitoka hii ruzuku itatusaidia vipi kuongeza upatikanaji wa chakula na kupunguza matatizo ya chakula yaliyokuwepo nchini na kuongeza uzalishaji katika kilimo. Tulifanikiwa kwa kiasi kikubwa sana kama nitakavyoeleza baadaye. Lakini tulipata matatizo pia katika utekelezaji wa kazi ile. Mwaka huu tunapanua sana utoaji huo wa mbolea kwenda kwenye mikoa mingine tunafikiri tukienda kwa uangalifu tunaweza hata ku-*cover* nchi nzima kwa hiyo kila mkulima akapata unafuu huo wa mbolea. Kwa hiyo, tunajua hili tunaliweza.

Kwa upande wa kodi hakuna kodi yoyote inayotozwa mbegu ama pembejeo za kilimo ama zana za kilimo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha alilieleza hili vizuri kabisa tena akaongeza kwamba kama tutagundua mahali popote penye tatizo ambalo halikushughulikiwa likifikishwa kwake atachukua hatua za kulirekebisha. (*Makofi*)

Kuna miradi miwili ambayo nitaizungumzia kwa undani zaidi wakati wa kuwasilisha *speech* yangu hapa ambayo moja ya mambo inashughulikia ni mbegu, pembejeo na zana za kilimo na inampa mkulima nusu ya bei atakayoingia kununua vitu hivi. Kwa hiyo, kuna mambo mengi ambayo yanatokea, yanayotaribu kurekebisha haya mapungufu yaliyoko katika kilimo ili kumwezesha mkulima kuzalisha kwa tija kubwa zaidi. (*Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 27 - Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... .. 8,694,322,800/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... .. 1,344,984,800/=

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuulizia mambo mawili.

Kwanza fedha za madawa ya mifugo, ndiyo nataka kuulizia kwa nini hizi fedha zinawekwa kwenye pembejeo. Kwa sababu hizi fedha zinamezwa kila siku na pembejeo inawekwa tu kwamba iko pale lakini haionekani. Kwa nini isiondolewe kabisa iwe peke yake ijulikane kwamba ni ya madawa ya mifugo? Kwa sababu naona ni pembejeo ndiyo inazingatiwa zaidi ya madawa. Lingine ...

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa Lekule, haturudii tena mjadala, hapa unatafuta ufafanuzi tu wa *item* fulani katika kifungu hiki.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ufafanuzi huo. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Sawa, basi namwita Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia Mifugo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha? Aah, Waziri Mkuu mwenyewe kumbe anataka kujibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba kama anavyofahamu Mheshimiwa kwamba huko nyuma Wizara hizo zilikuwa pamoja ndiyo maana vilikuwa pamoja. Lakini mwaka 2004 wameweka utaratibu maalum ambapo fedha kwa ajili ya mifugo zitakuwa zimekwishatengwa katika mfuko huo, kwa hiyo, watu wa pembejeo hawatazigua, zitakuwa ni kwa ajili ya mifugo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ..175,173,100/=

Kifungu 2002 - *Civil Affairs and Contingencies* ... ..222,147,800/=

Kifungu 3001 - *Parliamentary and Political Affairs* ... .. 227,759,300/=

Kifungu 5001 - *Coordination of Government Business*... .. 1,430,961,400/=

Kifungu 7001 - *Government Printer* ... .. 3,637,898,800/=  
Kifungu 7003 - *Information Services* ... .. 7,528,539,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi  
bila ya mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 42 - Ofisi ya Bunge**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... .. 2,764,334,600/=  
Kifungu 2001 - *National Assembly* ... .. 13,875,724,100/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi  
bila ya mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 61 - Tume ya Uchaguzi**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... .. 30,135,736,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi  
bila ya mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 91 - Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... .. 638,627,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi  
bila ya mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti Ukimwi**

Kifungu 1001 - *Policy, Planning and National Response*... ..330,735,000/=  
Kifungu 1002 - *Finance, Administration and Resource  
Mobilization* ... .. 2,302,864,200/=  
Kifungu 1003 - *Monitoring, Evaluation, Research  
and Mis.* ... .. 401,329,500/=  
Kifungu 1004 - *Advocacy Information and  
Education and Comm.* ... .. 498,432,000/=  
Kifungu 1005 - *District and Community Response* ... ..814,135,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi  
bila ya mabadiliko yoyote)*

#### **Mipango ya Maendeleo**

#### **Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 - *Administration and General*... ..500,000,000/=

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri na pia nashukuru kwamba *speech* yangu imemfanya Waziri Mkuu ametembelea Kibeta leo.

Lakini nilikuwa naomba kufahamishwa na kutolewa ufafanuzi thabiti kwamba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Sera) anieleze kwa ufasaha kabisa kwa mwendo huu. Waziri Mkuu anieleze kwa ufasaha kwamba fedha zinazotengwa ndani ya *Development* itatuchukua muda gani *calculation* za Kisayansi kwa kweli kuhamia hapa Makao Makuu pamoja na umaskini wetu na kama anaona kama vile kazi hii itakuwa kubwa si ni bora Serikali ikaufuta mpango huu?

**MWENYEKITI:** Hizi fedha za ukarabati wa Chimwaga, jengo moja hazihusiani na uhamishaji Makao Makuu. Basi ameshaelewa sasa.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa hii *development fund* kuna mambo ya *agriculture*. Nilitoa mchango wa maandishi nikidai kwamba kulikuwa na ahadi ya Rais kuhusu *Lower Moshi Irrigation*. Sasa nilivyojibiwa hapa Bungeni kwamba ahadi hiyo imetekelezeka. Ilikuwa haijatekelezeka kwa sababu hiyo *Water Right* ilipatikana mwaka 2001 na tulijibiwa hapa Bungeni tarehe 1 Novemba, 2001. Kwa hiyo, hiyo ahadi ya Rais ilikuwa haijatekelezeka na kwa kuwa bado tunaulizwa huko vipi ile ahadi na kwa kuwa Waziri Mkuu ndio mkubwa naamini anaweza akanipatia jibu tukawajibu nini kule na bado haijatekelezeka mpaka sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Jicho la Spika litakuona litakapoitwa kifungu kinachofuata. Sasa hivi tuko 1001 unayozungumzia hapa 5001.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001-*Coordination of Government Business...* .... 10,815,010,000/=

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tu tumejibu swali hapa Bungeni tukampa Mheshimiwa Thomas Ngawaiya maelezo marefu kabisa juu ya suala hili. *Lower Moshi* tuna matatizo mawili, tatizo la kwanza linatokana na kwamba yale maji yanayokwenda kwenye Mradi wa Umwagiliaji uliojengwa hayatoshelezi mahitaji kwa sababu kuna watu wameyachukua yale maji kabla hayajafika kwenye mradi. Kutokana na tatizo hili iliamuliwa kwamba yachukuliwe maji kutoka Mto Kikuletwa ili yaende yakaongeze maji kwenye sehemu hii ya umwagiliaji. Lakini tukawa tuna matatizo mawili. Tuna tatizo la kumwagilia maji *Lower Moshi* lakini tuna tatizo la kuzalisha umeme *downstream at the same time* Nyumba ya Mungu na Mabwawa yanaendelea na Pangani.

Kwa hiyo, ikabidi kukaa na kukubaliana na ku-*compromise situation* ambayo ingetuwezesha kupata yote mawili. Ikakubalika kwa huo kwamba Mradi wa *Lower Moshi* upewe maji *3.71 cusecs* nafikiri ili uweze kupanua eneo lake la kilimo na wakati huo huo tuendelee kuzalisha umeme.

Hiyo kazi imefanyika na mimi nafikiri Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, *in all due respects* tatizo lingekuwa ni kuimarisha mradi, sio kutekelezwa kwa ahadi ama jambo lingine lolote mradi yale mahitaji yanayohitajika yameshapatikana. Jambo tunalotakiwa kufanya sasa ni kutafuta raslimali za kutekeleza mradi huo. Lakini tunaweza kukaa hapa tunababaishana tu na maneno tuliahidiana tuliahidiana lakini watu hawatalima mpunga bila maji kupatikana. Mimi nafikiri hilo ndilo suala la msingi na hilo nitashirikiana naye kuhakikisha linatekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilitaka kujua hii *Agricultural Marketing System Development Programme* ambayo ina shilingi bilioni 7 imepelekwa hapa kwa Waziri Mkuu kwa sababu mimi nilitegemea itakuwa kwa Waziri wa Ushirika na Masoko ili ninapowaeleza wapiga kura na wananchi wajue ni wapi pa kutafuta. Sasa nataka kueleza tu utaratibu unaotumika kuziweka huku na zikanyimwa kupelekwa kule.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE WILLIAM V. LUKUWI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa natoa maelezo juu ya hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Paul Kimiti ya majukumu ya Waziri Mkuu.

Mpango huu unatekelezwa na mradi huu unahusisha mikoa mingi na Wizara nyingi zinahusika katika kutekeleza mpango huu. Isingekuwa rahisi Wizara moja ku-*coordinate* Wizara zingine. Ndiyo maana mpango huu kwa Waziri Mkuu lakini fedha hizi haziji ziko kwenye mradi moja kwa moja. Hizi ni fedha za msaada kwa wafadhili zinatolewa na *IFAD*. Kwa hiyo, Waziri Mkuu ni kama *coordinating agent* na huu ndio utaratibu wa maandalizi wa miradi ambayo inayohusika zaidi ya Wizara moja.

Kwa mfano hata ule mradi wa MEM. Mradi wa MEM unahusisha TAMISEMI na sehemu nyingine. Ukiangalia Kamati ya wataalam, Mwenyekiti wake ni Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Ni utaratibu tu wa utendaji wa Serikali. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sikuelewa, mimi labda kama wengine wameelewa. Hajatuambia wanachokwenda kufanya, ametoa mifano ya MEM akarukia huku na huku. Nilitaka kujua *specifically* ni vipi ili nielewe vizuri ni kitu zinakwenda kufanya hizo ambazo haziwezi kwenda kwenye ile Wizara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hapana uliuliza kwa nini zimewekwa hapa kwa Waziri Mkuu badala ya kule. Umeshajibiwa kwa nini kwamba ni *coordinating function*. Nafikiri maelezo yanaridhisha. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 7003 - *Information Services* ... .. 1,004,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 - Ofisi ya Bunge**

Kifungu 2001 - *National Assembly*... .. 1,899,913,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu - 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

Kifungu 1001 - *Adminstration and General*... .. 6,317,700,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti Ukimwi**

Kifungu 1001 - *Policy, Planning and National Responds*...5,186,600,400/=

Kifungu 1002 - *Finance, Admin and Resource*

*Mobilization*... .. 1,270,835,000/=

Kifungu 1003 - *Monitoring , Evaluation, Research*

*and Mis.* ... .. 1,002,345,000/=

Kifungu 1004 - *Advocacy Information and*

*Education and Comm* ... ..1,092,149,000/=

Kifungu 1005 - *District and Community Response* ... ..13,889,739,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makisio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na mengine yanayowasilishwa na Waziri Mkuu yameidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2004/2005.

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kufikia hapo ndio tunafikia mwisho wa shughuli zilizopangwa kwa siku ya leo. Kwa hiyo, kwa mamlaka niliyopewa, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho asubuhi saa 3.00.

*(Saa 01.28 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi tarehe 24 Juni, 2004 saa tatu asubuhi)*